




KIDOKEZO

Ni nani hasa anayewaua viongozi wa wapigania uhuru? Kwa nini viongozi hawa wameuawa wengi zaidi Kinshasa kuliko mahali pengine popote katika Afrika? Je, hatua gani zichukuliwe ili kupambana na kukomesha uhalifu huu usiokuwa na kifani?.

Naam. Umoja wa Nchi Huru za Afrika umepata jibu la masuala yote hayo na mengine. Ni Willy Gamba tena. Nyota ya Afrika na mpelelezi maarufu asiyekubali kushindwa - katika mapambano ya kutisha na kumwaga damu.

Safari hii Willy hakupambana na vikundi vya wanafunzi wa ujasusi bali ni miamba kamambe iliyojidhatiti kutenda uovu bila kujulikana. Ni mapambano ya mafahali, maana Willy naye si mchezo, na vurumai iliyotokea iliukumba mji wa Kinshasa katika wimbi la misukosuko ambayo kamwe haitasahaulika.

Usalama wa viongozi wa wapigania uhuru Kusini mwa Afrika ulikuwa umetishiwa, kwani kulikuwa kumetokea mauaji ya viongozi hawa katika nchi mbalimbali za Afrika. Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika (OAU) haukuweza kuvumilia hali hii, hivyo ulikata kauli kuwasaka wapinga mapinduzi hawa na kuwafagilia mbali ili kukomesha vitendo hivi vya kijahili.

Willy Gamba mpelelezi maarufu wa Afrika alijikuta amechaguliwa na OAU kuongoza kikundi cha wapelelezi wa Kiafrika cha kuwasaka na kuwatokomeza majahili hawa.

Kinshasa mji mkuu wa Zaire na mji unaosifika kwa starehe zake katika Afrika ulijikuta ni uwanja wa mapambano kati ya vijana wapiganaji shupavu wa Kiafrika wakiongozwa na Willy Gamba na wapinga mapinduzi wa Afrika wakiongozwa na Kaburu Pierre Simonard. Ndipo patashika ambalo halijawahi kutokea katika Afrika liliwaka moto katika mji huu ambalo halijatokea lisahaulike katika historia ya mapambano dhidi ya wapinga mapinduzi wa Afrika

SURA YA KWANZA

LUSAKA

“Tafadhali sikilizeni, huyu ni rubani Mwanakatwe ninafurahi kuwafahamisheni kuwa tunakaribia uwanja wa ndege wa Lusaka ambapo ndipo patakuwa mwisho wa safari yetu, Ni matumaini yangu pamoja na wafanyakazi wenzangu kuwa mmefurahia safari yetu mliyosafiri na Shirika la ndege la Zambia, na tunawakaribisheni tena kusafiri nasi mpatapo safari. Sasa fungeni mikanda yenu tayari kwa kutua, asanteni,”

Abiria wote ndani ya ndege hii walifunga mikanda yao tayari kwa kutua. Wale waliokuwa karibu na madirisha waliangalia chini kuiona Lusaka ilivyo kwa juu. Kweli ilitoa picha ya kupendeza sana. Wakati abiria wengine wakijishughulisha na mambo hayo kulikuwa na abiria wanne ambao mara kwa mara walikuwa wanaziangalia saa zao kana kwamba wanachelewa kitu fulani. Mara tu rubani alipotoa taarifa wawili wao waliangaliana. Ingawa abiria hawa walikuwa hawakupandia sehemu moja lakini wawili wao walikuwa wakifahamiana. Wawili walikuwa wamepandia Khartoum Sudan na wawili Dar es Salaam Tanzania. Wawili kati ya watu hawa wanne walikuwa Mawaziri wa Ulinzi kutokana katika nchi hizi mbili na walikuwa wakifahamiana vizuri sana. Ingawaje walikuwa bado hawajapata fursa ya kuzungumza lakini kila mmoja wao alihisi sababu ya kuwepo kwa mwenzake katika safari hii. Watu waliokuwa wameandamana na Mawaziri hawa ni Wakurugenzi wa Upelelezi wa nchi zao.

Abiria hawa ambao walitegemewa kusafiri katika daraja la kwanza, walikuwa wamesafiri katika daraja la kawaida na hakuna abiria wenziwe wala wafanyakazi wa ndani ya ndege waliowatambua kuwa ni akina nani kwani hata hati zao za kusafiria (passport) walizokuwa wakitumia zilikuwa za kawaida tu.

Ndege ilipokuwa imetua abiria waliteremka na kuelekea ofisi za uhamiaji na ushuru wa forodha. Hawa watu wanne walipita sehemu hizi bila matatizo, ingawaje mara kwa mara waliziangalia saa zao kwa wasiwasi kidogo kana kwamba wanazidi kuchelewa kitu. Waliweza kupita kwa urahisi zaidi kwa sababu hawakuwa na mizigo mingi ila mikoba tu ya kawaida.

Walipotokeza nje ya jengo la Uwanja wa ndege walipokelewa na madereva wa teksi waliokuwa tayari kupata abiria wa kupeleka mjini. Hawa watu wanne waliingia ndani ya teksi iliyokuwa karibu na mmoja kati yao akaamru.

“Mjini haraka sana”.

“Mpita kuti amadala?” aliuliza dereva teksi katika lugha ya Kinyanja.

“Hatujui kilugha sisi,” alijibu mmoja wa watu hawa.

“Nyinyi ni wageni?”.

“Ndiyo”.

“Nilikuwa na maana mjini niwapeleke sehemu gani?”.

“Kwacha House”.

Ajabu ni kwamba muda wote huo hawa watu walikuwa hawajasalimiana wala kusemeshana. Kutokana na ukimya na namna ya watu hawa walikuwa na haraka isiyo kifani, kwa hiyo dereva alivuta kasi ili kusudi aweze kuwaridhisha abiria wake. Sharti kama angejuwa ni watu gani aliowabeba asingekubali kwenda mwendo aliokuwa akienda. Maana hawa Mawaziri wawili wa Ulinzi walikuwa ni wanakamati wa kamati ndogo ya usalama ya Kamati ya Ukombozi ya Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika.

Hii kamati ndogo ya usalama ilikuwa na wanakamati kutoka nchi nane na mara hii wanakamati hawa walikuwa wameitwa kwenye mkutano wa dharura na wa siri mjini Lusaka, ambako Mwenyekiti wa kamati hii ndiko alikuwa anatoka. Habari walizokuwa wamepelekewa wanakamati hawa kwa njia ya simu zilikuwa zimewataka wanakamati hawa wafike Lusaka kwenye kikao hicho cha dharura ambacho kingefanyika Jumamosi saa kumi jioni wakiwa pamoja na Wakurugenzi wa upelelezi wa nchi zao kwa sababu ya tatizo la mawasiliano wanakamati hawa ndio walikuwa wa mwisho kufika mjini Lusaka. Wanakamati kutoka nchi nyingine walikuwa tayari wamewasili.

Wakati dereva wa teksi anaegisha gari, kwenye maegesho ya Kwacha House ilikuwa yapata saa kumi unusu mchana ambayo ilikuwa inamaana walikuwa wameisha chelewa muda wa nusu saa. Mmoja alimlipa dereva na wao nusu wakikimbia walielekea mlango wa mbele wa Kwacha House.

Kwa mara ya kwanza toka wakutane ndipo waziri wa ulinzi wa Tanzania aliwasalimu, “Habari zenu, poleni na safari tumechelewa lakini si sana, Sisi salama, natumaini watakuwa wanatungoja, hata hivyo sisi tumejitahidi sana kufika kama walivyopanga,” Alijibu Waziri wa Ulinzi wa Sudan huku wakiwa wamefika meza ya mapokezi ya Kwacha House. Kabla hata hawajazungumza na msichana aliyekuwa amekaa kwenye hiyo meza alitokea kijana mmoja bila hata kuwauliza akawaambia “Wazee twendenui huku,” Na wao bila kuuliza walimfuata, “Mmekuwa mnangojewa kwa hamu sana mkutano bado haujaanza,” Huyu kijana aliwaeleza huku akipanda ngazi za ghorofa ya kwanza. Walimfuatana wakiwa bado na hiyo hali yao ya wasiwasi maana walikuwa hawajui mkutano huu ulioitwa kiajabu ulikuwa wa nini.

“Chumba hiki ndicho cha mkutano,” aliwaeleza yule kijana huku akifungua na wao bila kusita wakaingia ndani. Ndani ya chumba hiki cha mkutano mlikuwa na meza kubwa ya mkutano ambayo tayari watu kumi na wawili walikuwa wamekaa huku wakiizunguka meza. Mtu mmoja ambaye alikuwa anafanya idadi ndani ya hiki chumba cha mkutano kuwa kumi na tatu alikuwa amesimama dirishani akiangalia chini barabarani. Kanakwamba alikuwa akihesabu magari yaliyokuwa yakipita hapo chini. Hata walipokuwa wakiingia hawa wanakamati wengine, bado aliendelea kuangalia, huko chini kanakwamba alikuwa hakisikia kishindo cha kuingia kwao.

Hawa wanakamati walioingia walikaa kwenye nafasi zao na kushiriki katika kilichokuwepo ndani ya chumba hiki, huku kila mtu akionekana kuwa mwenye mawazo mengi sana. Baada ya kupita kama dakika tano hivi, huyu mtu aliyekuwa amesimama kwenye dirisha aligeuka na kuangalia chumbani. Huyu alikuwa ndiye Mwenyekiti wa kamati ya Ukombozi ya Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika. Alienda mpaka kwenye meza akavuta kiti akakaa, kisha akavunja kimya kilichokuwamo chumbani kwa kusema, “Ndugu Wanakamati, inabidi nitoe shukrani zangu kwenu nyote kwa kuweza kuitikia mwito wa kuhudhuria hiki kakao cha dharura cha kamati ya usalama ambacho kimeitishwa kinamna yake. Nilikuwa na wasiwasi mwingi kuwa huenda wanakamati wengine wangeshindwa kufika kwa muda uliopangwa. Hii inazidi kutudhihirishia kuwa Afrika ni moja na umoja wa Afrika unazidi kukomaa siku hadi siku” Alinyamaza kido kiasi cha kupitisha mate, halafu akaendelea “Vile vile ningependa kuwakaribisha Wakurugenzi wa Upelelezi ambao kwa kawaida si wanakamati wa kamati hii, kuwa mtakuwa na haki ya kupiga kura kama wanakamati wa kawaida. Nafikiri tumeelewana mpaka hapo.”

“Tumeelewa,” walijibu wanakamati kwa pamoja. Kila mtu alionyesha sura ya uchu wa kutaka kujua hasa ajenda ya mkutano huu. Huku akiwa amekunja uso aliendelea. “Ndugu wanakamati, nasikitika kuwaeleza kuwa hiki kikao chetu si cha kawaida na ndiyo sababu kimeitishwa kwa siri kwa maana haikutakiwa ijulikane kuwa kikao hiki kimeitishwa kutokana na jambo lenyewe ambalo limefanya kikao hiki kiwepo kutokana na jamno lenyewe ambalo limefanya kikao hiki kiwepo. Ni jinsi hii mhitasari wa maneno yatakayoamjadiliwa na kuamriwa katika mkutano huu hautachukuliwa.

Hii ina maana itabidi sisi wote tusikilize kwa makini na yote tutakayoyasikia tuyaweke moyoni mwetu, yawe siri yetu,” Chumba cha mkutano kilikuwa kimya kabisa isipokuwa sauti ya Mwenyekiti peke yake. Alipokuwa amefikia hapa sura ya kila mtu alionyesha mshangao wa jinsi mkutano ulivyokuwa ukiendeshwa huku wengine mioyo yao ikipiga haraka haraka kwa shauku ya kutaka kujua jambo lenyewe.

“Ndugu wanakamati.” Mwenyekiti aliendelea kwa sauti ya huzuni. “Naamini mmesikia tukio lililotokea mjini Kinshasa Zaire juzi usiku na kutangazwa jana,” aliwaangalia huku baadhi yao wakitingisha vichwa kuonyesha kuwa walikuwa na habari kisha akaendelea, “Tumepata habari kuwa aliyekuwa rais wa shirikisho la vyama vya wapigania uhuru Kusini mwa Afrika ndugu Edward Mongo ameuawa huko mjini Kinshasa Zaire baada ya gari alilokuwa akitembelea kutegwa bomu ndani ya mtambo wake na kuripuka. Yeye alikuwa ametokea Libreville Gabon ambako alikuwa akihudhuria mkutano wa umoja wa Matafa kuhusu kuzuia Ufaransa kuiuzia Afrika Kusini dhana za kivita na kuisaidia kutengeneza silaha za Nyuklia. Na alikuwa amepita mjini Kinshasa kwa mazungumzo na serikali ya Zaire kuhusu hali iliyoko Kusini mwa Afrika, Na kabla ya kufanya mazungumzo hayo, ndugu Mongo alikufa juzi usiku kwa mripuko wa bomu lililotegwa ndani ya injini ya gari aliyokuwa amepewa kutembelea. Jambo hili limesikitisha wakuu wa nchi huru za Afrika, kwa maana kifo cha ndugu Mongo kina maana ya pigo kubwa kwa ushirikiano wa vyama vya wapigania uhuru Kusini mwa Afrika! Hii inaonyesha waziwazi kuwa ni njama za makaburu na vibaraka wao kutaka kuvunja harakati za ukombozi zinazofanywa na wapigania uhuru Kusini mwa Afrika. Ni dhahiri kuwa kumuua ndugu Mongo wamejipalia mkaa, lakini kitendo kama hiki hatuwezi kukiruhusu kiendele.

Kwa jinsi hii ndugu wanakamati, kikao hiki cha dharura kimeitishwa kusudi kitafute dawa ya kukomesha vitendo kama hivi na vile vile kutafuta jinsi gani

tunaweza kuwapa fundisho hawa wanaohusika na kitendo kama hiki kuwa sasa Afrika iko macho na haitaki kuchezeza. Hili ndilo jukumu tumepewa na wakuu wa nchi huru za Afrika na hatuna budi kulitekeleza,” alimaliza huku akiwatazama wajumbe kikamilifu.

“Ndugu Mwenyekiti, bado haijaeleweka sawasawa hasa kuhusu inatakiwa tufanye nini?. Kwa kweli jambo hili ni la kusikitisha sana na hata wakati natoka nyumbani niliacha baraza la mawaziri limekutana kuzungumzia tukio hili. Kwa hivi jambo tutakalozunguzia au kuamua hapa lina maana kuwa ndiyo utakuwa msimamo wa nchi huru za Afrika. Kwa jinsi hii, ndugu Mwenyekiti, tunaomba utueleze suala hili kinaganaga kusudi tuweze kulielewa sawasawa na pindi tutakapotoa maamzi yalingane na matakwa ya nchi huru za Afrika”, alitoa rai mjumbe kutoka Kenya.

Wajumbe wengine walitingisha vichwa, kuonyesha kuwa na wao walihitaji ufafanuzi zaidi. Akijibu hoja hiyo, Mwenyekiti alisema, “Ndugu wanakamati, nadhani itabidi nifafanue jambo hili kwa kutoa historia fupi juu ya matukio ya namna hii na nini kimefanyika katika jitihada za kuyazuia.

“Miaka mitatu iliyopita kumetokea matukio ya mauaji kwa viongozi wa wapigania uhuru na tukio hili la juzi linakuwa la sita kwa muda wa miaka mitatu. Tukio la kwanza ambalo lilitokea mwaka juzi lilitokea mjini Dar es Salaam ambapo Mkuu wa ofisi wa Wapigania Uhuru iliyoko mjini hapo ndugu Leon Fadaka aliuawa kwa bomu baada ya kupokea kifurushi kilichokuwa kimetumwa kwake kwa njia ya posta na wakati alipokuwa akikifungua kililipuka kwani ndani yake kuliwa na bomu na alikufa pale pale. Uchunguzi ulifanyika ikabainika kuwa kifurushi hili kilikuwa kimetumwa kwake kwa njia ya posta kutoka mjini Kinshasa. Serikali ya Zaire ilijaribu kuchunguza jambo hili lakini bila ya mafanikio. Mwaka huo huo wa juzi baada ya miezi sita tangu kuuawa kwa ndugu Fadaka, kulitokea tukio lingine la namna hiyo hiyo hapa mjini Lusaka, baada ya Mkuu wa ofisi ya wapigania Uhuru ya hapa naye kupata barua kutoka mjini Paris Ufaransa na mara alipokuwa akifungua bahasha, kukatokea mripuko ambao ulimua papo hapo.

Tukio hili lililaaniwa vikali kote Ulimwenguni lakini hakuna mtu wala kikundi cha watu kilichokamatwa bali lawama ziliwaangukia makaburu na vibaraka wao kuwa ndiyo tu wangeweza kuhusika na vitendo hivi. Matukio mengine matatu yametokea mwaka jana. Tukio la kwanza mwaka jana lilitokea mjini Lagos Nigeria, wakati ndugu Nelson Chikwanda ambaye alikuwa mwakilishi wa wapigania uhuru katika ofisi njema za Umoja wa nchi huru za Afrika iliyoko mjini

hapo alipigwa risasi na mtu asiyejulikana. Uchunguzi mkali ulifanyika lakini hakuna lolote lililotambulika.

Miezi mitatu baada ya tukio hili huko Lagos, ofisi ya wapigania uhuru iliyoko mjini Nairobi ililipuliwa na wafanyakazi watatu akiwemo ndugu Nene ofisa wa juu katika ofisi hiyo aliuawa. Tukio la mwisho mwaka jana lilitokea tena mjini Kinshasa wakati Afisa wa juu katika Jeshi la wapigania uhuru Meja Komba Matengo alipokutwa ameawa ndani ya Hoteli Tiptop chumbani mwake. Yeye alikuwa amewasili mjini hapo kuhudhuria kikao cha kamati ya ukombozi ya nchi huru za Afrika kilichokuwa kikizunguzia kuunganishwa majeshi ya wapigania uhuru Kusini mwa Afrika. Na ndugu wanakamati tukio la mwisho kufikia sasa ni hili ambalo limetokea juzi. Naamini nyote mnakumbuka hatua ambazo zimechukuliwa kujaribu kuhakikisha usalama wa ndugu hawa wapigania uhuru. Mpaka sasa tumefaulu kutegua mabomu kadhaa yaliyokuwa yametumwa kwa wapigania uhuru kadhaa kwa njia ya barua ama vifurushi jambo hili tumeweza kufuzu kwa sababu barua zote au vifurushi vinavyotumwa kwa watu hawa vinafunguliwa kwanza na wataalam kutoka idara ya usalama ya kila nchi ambapo ofisi hizi zilizopo. Lakini jinsi ya kuzuia matukio mengine kama lilile lililotokea Lagos, Kinshasa, TipTop Hoteli na hili la juzi inakuwa vigumu sana kuyazuia.

Hata hivyo, hatuna budi kujihami, kwani hatuwezi kukaa tu huku ndugu zetu wakiuawa huku na kule ili kusudi harakati za ukombozi wa Kusini mwa Afrika ziweze kusimama. Kwa hivi, ndugu wanakamati, tuko hapa ili tujadiliane ni njia gani tuzitumie katika kujihami. nafikiri nimeeleweka vya kutosha,” alimalizia Mwenyekiti.

Mkutano ulishikwa na ukimya wa kama dakika tano hivi huku kila mjumbe akizingatia mambo yote yaliyokuwa yameelezwa. Mjumbe wa Zambia ambaye kwa kawaida huwa ndiye Mwenyekiti wa kamati hii ndiye alikuwa wa kwanza kuvunja kimya hiki kwa kusema, “Ndugu Mwenyekiti na ndugu wanakamati wenzangu, kusema ukweli jukumu hili tulilopewa ni jukumu gumu sana. Ni gumu kwa sababu inabidi kikao hiki kiamue nini kitu gani kitendeke dhidi ya mauaji haya ambayo yanatokea kwa ndugu zetu wapigania uhuru. Ingawaje suala hili ni gumu lakini hatuna budi kulitatua maana tumeaminiwa na viongozi wa nchi zetu na ni matumaini yangu lolote tutakaloliamua hapa ndiyo utakuwa uamzi wa Afrika. Ndugu wanakamati, matukio haya kama yalivyoelezwa na ndugu Mwenyekiti, Utaona ya kwanza yanatokea katika nchi zetu zilizo huru. Ingekuwa habari nyingine kama matukio haya yangetokea kwenye uwanja wa mapambano

kwani jambo kama hili lingeweza kueleweka. Lakini utaona kuwa tunapigwa vita nyumbani kwetu. Hii ina maana tumeshindwa kuwalinda hawa ndugu zetu? Suala sasa ni tufanye nini? Kwa upande wangu naonelea ya kwamba inabidi tutafute kiini cha matukio haya, kwani tukishapata kiini chake itakuwa rahisi kupata ufumbuzi. Mpaka sasa hivi tumefahamishwa kuwa matukio mawili yametokea mjini Kinshasa, moja Dar es Salaam, moja hapa Lusaka, moja Nairobi na moja Lagos. Tukio la mjini Dar es Salaam linasemekana limetokana na kifurushi kilichokuwa kimetumwa kwa njia ya posta kutoka mjini Kinshasa, Zaire. Uchunguzi huu unatuonyesha wazi wazi kuwa tukio la Dar es Salaam kilikuwa mjini Kinshasa, kwa hiyo hii inatupa idadi ya matukio matatu kati ya sita yakiwa yametokea mjini Kinshasa Zaire. Ndugu wanakamati, kutokana na hali hii, inaonekana waziwazi kuwa mjini Kinshasa kuna mambo na kama uchunguzi halisi ukifanywa mjini hapo huenda tukapata kiini hasa cha mauaji haya. Kwa hivi ni rai yangu kuwa utumwe ujumbe kutoka kwenye kamati hii ukaonane na wakuu wa serikali ya Zaire, uzungumzie juu ya jambo hili, ukiwa unaomba serikali ya Zaire ifanye upelelezi kabambe juu ya matukio hayo. Ni imani yangu kuwa kwa kufanya hivi tutapata ufumbuzi wa jambo hili. Sijui wanakamati wenzangu mnasemaje,” alimaliza.

Mjumbe wa Sudan aliinua kichwa na kwamwangualia Mwenyekiti akionyesha sura ya kutaka kusema kitu. Mwenyekiti ambaye naye alikuwa akimwangualia alimtingishia kichwa kumuashiria aendele. Hivyo alianza kwa kusema, “Ndugu Mwenyekiti na ndugu wajumbe, kusema kweli mzigo tuliopewa ni mzigo mzito lakini kama walivyokwisha sema walionitangulia hatuna budi kuubeba. Ningependa kuunga mkono maelezo ya ndugu mjumbe aliyemaliza kusema kabla yangu, maelezo ambayo nisingependa kuyarudia kwani naamini yameeleweka vizuri sana. Kweli mtu yeyote anaweza kuona mjini Kinshasa kuna matatizo na ingefaa zaidi uchunguzi ufanyike mjini hapo juu ya matukio haya. Ingawa makubaliano ya suala hili inabidi uchunguxi ufanyike lakini namna alivyotoa maoni ndugu mjumbe mimi nina maoni tofauti na yeye jinsi ambavyo uchunguzi huu ungefaa ufanyike. Ndugu wajumbe ni matumaini yangu kuwa mtakubaliana na mimi kila tukio la namna hii linalotokea katika nchi yoyote lazima upelelezi wa hali ya juu ufanyike kusudi yeyote anayehusika aweze kukamatwa na kutiwa hatiani. Hivi ndivyo nchi zote zilizopatwa na baraa la aina hii zimejitahidi kufanya, ingawaje bila mafanikio maalumu. Mwisho wa kila upelelezi umekuwa ni lawama tu kwa Afrika Kusini na vibaraka wake. Kwa jinsi hii ndugu wajumbe kutuma ujumbe ukazungumze na serikali ya Zaire ili kuongeza jitihada katika upelelezi

wake kuhusu matukio haya, itakuwa sawa na kuiomba kufanya kitu ambacho imekwisha kifanya, kwani mimi naamini kwa dhati kuwa Zaire imekuwa ikifanya kila iwezavyo kusudi iweze kuwakamata hawa wauaji, ingawaje bila mafanikio. Kwa hivi naonelea kuwa Zaire inahitaji msaada katika upelelezi wake msaada ambao unabidi utoke nje ili kuimarisha nguvu za wapelelezi wa nchi hiyo.

Kwa hiyo nato oni kuwa kiundwe kikosi cha wapepezi kitakachotoka katika Nchi Huru za Kiafrika ambacho kitaenda Zaire kikasaidiane na wapelelezi wa Zaire ni bahati nzuri kuona kuwa katika mkutano huu, wakurugenzi wa upelelezi wa nchi huru nane za Kiafrika wako hapa na wanaweza kutusaidia kitaalam jinsi ya kuunda kikosi hiki,” alimaliza huku akipigiwa makofi ya kumpongeza kwa maoni yake, vile vile ikionyesha wajumbe wengi waliafiki maoni yake. Kwa mara ya kwanza minong'ono ilisikika katika chumba hiki, Mwenyekiti aliikataisha minong'ono hii kwa kusema.

“Ndugu wajumbe mnanipa moyo kwa kuona kuwa jambo ambalo limekuwa nikilifikiria siku nyingi na kunisumbua rohoni siku nyingi leo limeweza kusemwa na nyinyi kabla hata mimi mwenyewe sijalisema. Nilikuwa nachelea kulisema awali nikiwa na mawazo kuwa huenda lingeweza kupingwa, lakini ni furaha iliyoje kuona jambo hili limeshangiliwa na wajumbe wote, ni kweli kabisa ya kuwa wakurugenzi wa upelelezi mmeitwa katika mkutano huu ili muweze kutusaidia kitaalam ni jinsi gani tunaweza kuunda “Kikosi cha Kisasi” kikosi kidogo na chenye kufaa. Kabla sijasema mengi naonelea niwaachie uwanja wataalam waweze kutushauri kabla hatujafikia uamzi kamili,”

Mkurugenzi wa Upelelezi wa Nigeria ndiye alikuwa wa kwanza kusema, “Asante sana ndugu Mwenyekiti na ndugu wajumbe. Kikao hiki mimi ni mara yangu ya kwanza kuhudhuria na, nakihudhuria wakati hasa ambapo nahitajika kukihudhuria kikamilifu katika matatizo yanayoikabili Afrika kwa wakati huu. Ni wazo zuri sana kuunda “Kikosi cha Kisasi” ambacho kitasaidia katika kutafuta na kukipiga vita kikosi kingine cha maadui wa Afrika. Mawazo yaliyokwisha tolewa kuwa baada ya kikosi hiki kuundwa kiende Kinshasa kikasaidiane na idara ya usalama ni jambo la busara. Lakini kwa upande wangu kutokana na ujuzi wangu katika mambo ya upelelezi, mimi naonelea kuwa baada ya kuunda kikosi hiki si vizuri kikasaidiane na idara ya usalama ya Zaire bali kiende huko kikijitegemea na wala kisijulikane kabisa na mtu yeyote nchini Zaire kama kuna kikosi kama hiki. Nikisema hivi sina maana kuwa siamini sserikali ya Zaire, bali ni kufuatana na hali yenyewe ya kazi ya kipelelezi ilivyo. Jinsi watu wachache Afrika watakavyoweza kufahamu

kuwepo kwa kikosi hicho ndivyo kitakavyokuwa na nafasi nzuri ya kuweza kufanikiwa. Kwa maana inabidi ieleweke wazi kuwa adui tunayepigana nae ana nguvu na ujuzi wa hali ya juu na ndiyo sababu watu maarufu sita wameweza kuuawa bila kushika au kuawa mtu hata mmoja kwa upande wa wauaji. Kutokana na tukio lililotokea mjini Lagos nimejifunza mengi kwani upelelezi wa tukio lote ulifanyika chini yangu. Kwa hivyo nathubutu kusema kuwa hili ni kundi la wauaji wa hali ya juu sana na wana mipango ya hali ya juu sana. Kiupelelezi hata mimi nahisi mjini Kinshasa kuna mizizi ya matukio haya. Kwa kifupi basi ni maoni yangu kuwa kwanza lazima tuunde kikosi cha wapelelezi wa hali ya juu sana katika Afrika, pili kikosi hiki kiwe na watu wachache sana, tatu kitakapokwenda Zaire kiingie kisirisiri na kifanye kazi zake kwa siri kama kikundi cha maadui kinavyofanya kazi kisiri, na serikali ya Zaire isijulishwe kabisa juu ya kikosi hiki kwa sasa huenda mpaka hapo baadaye itakapokuwa lazima (Zaire haikuwa mojawapo katika nchi nane za kamati ya usalama) na mwisho lazima kikosi hiki kiundwe haraka iwezekanavyo na kiwe kimefika Zaire wakati bado kuna moto wa kifo cha ndugu Mongo,' alimalizia.

Wakurugenzi wengine wote wa usalama kutoka katika nchini nyingine walikubaliana na maoni hayo yote ya mwenzao. Lililokuwa limebaki sasa juu ya kikao kuzungumzia uundwaji wa kikosi chenyewe. “Ndugu wanakamati, inaonekana tumepiga hatua za haraka sana katika kutafuta ufumbuzi wa tatizo hili,” alisema Mwenyekiti. “Lilopo sasa ni kuzingatia maoni yaliyotolewa na kuyashughulikia kikamilifu kufuatana na vile mkutano utakavyokubaliana na maoni hayo. Kwa sababu tumekubaliana kuwa lazima kikosi kiwe tayari wakati bado kuna moto wa kifo cha ndugu Mongo huko Zaire, hii ina maana hatuna nafasi ya kuchagua watu ili tukawafundishe waje waunde kikosi hiki, bali inatubidi tupate watu ambao tayari yamekwisha pata ujuzi wa juu katika upelelezi, kutoka katika nchi mojawapo za Kiafrika na kuunda kikosi hiki kutokana nao. Suala sasa ni kwamba je, tunao watu kama hawa Afrika. Ikiwa suala hili litajibiwa sina shaka tatizo letu litakuwa limekwisha,” alimaliza Mwenyekiti huku akiwaangalia wanakamati mmoja baada ya mwingine.

Mkutano kwa mara nyingine uliingiwa na minong'ono kati ya kila Waziri na Mkurugenzi wake wa Upelelezi mingong'ono hii iliendelea karibu nusu saa, ubishi ukizuka hapa na pale kati ya Waziri na Mkurugenzi wake. Kisha mjumbe wa Tanzania aliinua kichwa na kutoa kohozi la kujitayarisha kusema. Wengine waliposikia ishara hii walinyamaza na kumwangalia wakingojea kusikia atasema nini, naye alianza, “Ndugu wajumbe, sina budi kutoa shukrani zangu kwenu nyinyi

kwa kuwa tayari kunisikiliza. Vilevile ningependa kutoa furaha yangu jinsi mkutano huu unavyoendeshwa na jinsi ambavyo wajumbe waliowahi kusema, wameweza kusema kwa moyo wa Afrika moja na wala si kwa nchi binafsi kwa sababu hii hata mimi nasikia mori na ninathubutu kuwaeleza kuwa serikali ya Tanzania inaye mtu ambaye akipata msaada wa mtu mmoja au wawili pamoja na baraka za Afrika Huru anaweza kuitekeleza kazi hii kwa kiasi kikubwa sana. Mtu huyu amewahi kufanya shughuli za namna hii kubwa kubwa, na kama ndugu wajumbe mnakumbuka juu ya karatasi za wapigania uhuru zilizoibiwa jijini Dar es Salaam na kuweza kukamatwa mjini Nairobi mtu aliyewezesha jambo hili lifanikiwe ndiye ninayemwelezea. Ujuzi wake ni wa hali ya juu sana na ni imani yangu kuwa anaeleweka vizuri kwa wakurugenzi wa upelelezi, hasa kwa jina.

“Ndiyo tunamfahamu sana, hata sisi tulikuwa tunamzungumzia huyo huyo,” alidakia Mkurugenzi wa Upelelezi wa Kenya.

“Sina shaka ni Willy Gamba,” alitamka Mkurugenzi wa Upelelezi wa Ghana.

“Ndiye hasa nilikuwa namzungumzia,” alijibu mjumbe wa Tanzania.

Mkutano ulinza kumzungumzia huyu mtu aitwaye Willy Gamba, sifa zake zote zilielezwa mbele ya mkutano na Mkurugenzi wa Upelelezi wa Tanzania na mkutano kwa ujumla ulikubaliana kuwa mtu huyu angefaa apewe jukumu hili.

“Nafikiri ndugu wanakamati tumefikia uamzi juu ya suala hili kwa sasa mimi naonelea jambo hili tunawaachia Wakurugenzi wa Upelelezi wakae na walishughulikie. Huyu mtu Willy Gamba tumeamua ndiye ataongoza “Kikosi Cha Kisasi” na mambo mengine yote yatatengenezwa na hawa wakurugenzi ambao ni wataalam, itabidi tuonane tena kesho saa kumi na mbili jioni hapa hapa. Hii itawapa nafasi nyinyi wataalam kutayarisha mambo yote na kuhakikisha kuwa tuonanapo kesho Willy Gamba nae awe amefika hapa. Kwa sasa hivi tufunge mkutano, nyinyi mtapanga muda wenu wa kukutana, nafasi zenu za kulala zimetayarishwa, kila mtu aondokapo hapa apite mapokezi kuna dereva na ofisa usalama kwa kila mwanakamati. Ni matumaini yangu kuwa tuonanapo kesho jioni mambo yatakuwa yameshughulikiwa kikamilifu. Itakuwa tu kupokea taarifa kamili na mambo ya kuanza. Asante sana.”

Mwenyekiti alifunga mkutano na kuangalia saa yake ambayo ilionyesha ni saa mbili unusu za usiku wa siku hii ya Jumamosi.

SURA YA PILI

DAR ES SALAAM

Mjini Dar es Salaam, kama ilivyo katika miji mingine yoyote Ulimwenguni, kulikuwa kumejaa pilikapilika siku hii ya jumamosi usiku. Saa tano hizi za usiku pilikapilika zilikuwa bado nyingi sana. Watu wengi waliokuwa wameanza starehe za Jumamosi mapema mchana walikuwa wanarejea nyumbani kupumzika, wakati wengine waliokuwa wameanza starehe jioni, walikuwa wamo katikati ya sherehe na wakati ule ule walikuwa na kundi jingine ambalo ndipo lilikuwa linaanza pilikapilika za sherehe saa tano hizi.

Katika msululu wa magari yaliyokuwa kwenye barabara ya Morogoro yakitokea mjini kuelekea sehemu ya Ubungo, mlikuwa na gari moja aina ya 'Colt Gallat Coupe' nambari TZ 300130 ambayo ndani yake mlikuwa na kijana mmoja nadhifu sana na msichana mmoja mrembo sana, ambao walikuwa katikati ya ubishi.

“Mimi nakwambia twende Mlimani Park,” alisema yule kijana.

“Nieleze kwa nini tusiende Safari Resort?” Aliuliza yule msichana.

“Bendi mpya ipo pale ya Zaire.”

Yaani wewe unafuata upya wa bendi au bendi yenyewe ilivyo.”

“Basi Lolita mpenzi, tutakwenda Safari Resort,” alijibu yule kijana huku akiongeza mwendo wa gari.

“Lakini usije ukawa umeudhika, ee Willy mpenzi.”

“La hashu, ningekuwa sikuridhika ningekuambia, bila kusita.” Kusema kweli magari mengi yalikuwa yakielekea kwenye klabu moja maarufu sana iitwayo Resort iliyoko sehemu ya Kimara. Kwa hivi baada ya watu hawa kukubaliana kwenda kustarehe usiku huu huko Safari Resort walielekea moja kwa moja mpaka kwenye klabu hiyo. Walipoingia ndani ya klabu hii walikuta watu tayari walikuwa wamejaa. Muziki ulikuwa ndipo umepamba moto.

“Loo Willy rekodi hiyo mimi naipenda,” alisema Lolita mara tu walipoingia ndani,

“Twende tukacheze alijibu Willy. Bila hata kutafuta mahala pa kukaa kwanza waliingia kwenye uwanja wa kucheza na kuanza kulisakata rumba.

Baada ya rekodi hii kwisha, walitoka na kuanza kutafuta mahala pa kukaa.

“Willy karibu huku,” Meneja wa klabu alimkaribisha. Meneja wa klabu hii alikuwa amemwona Willy wakati akiingia, na kwa sababu alikuwa akimheshimu sana, alimtafutia mahala pa kukaa ili asipate taabu kutafuta.

“Asante sana Rajabu, hujambo lakini?”

“Mimi sijambo, je wewe?”

“Alhamdulillah Mungu anasaidia”.

“Oh, samahani bibie tabia yangu inataka kuwa mbaya kwa kutokusabahi kwanza, hujambo?”

Rajabu alimsalimia Lolita huku akiwakalisha kwenye meza aliyokuwa amewatayarishia.

“Sijambo mimi” alijibu Lolita huku akiketi.

“Ngoja niwajulishe, huyu ni Lolita rafiki yangu,” alimjulisha Lolita kwa Rajabu, “Na huyu ni rafiki yangu vile vile ndiye Meneja wa hapa,” alimjulisha Rajabu kwa Lolita.

“Nafurahi kukuona,” Rajabu alimwambia Lolita.

“Na mimi pia nafurahi kukuona” alijibu Lolita.

Kisha Rajabu aliwaagizia vinywaji, “Sijui bibie utapendelea kunywa nini?”.

“Nafikiri itanifaa safari”.

“Na wewe Willy?”.

“Na mimi hiyo hiyo itanifaa kwa kuanzia.”

Vinywaji viliagizwa na Rajab akaondoka.

“Willy,” Lolita aliita kwa mshangao, Willy akajua kwanini?.

“Mara nyingi huwa nafika hapa kiasi cha kwamba huyu meneja amenizoea.”

“Ndiyo sababu ulikuwa hutaki kuja huku au sivyo?”

“Nilitaka libadilisha mazingira kidogo.”

“Mahala pazuri sana miye huwa napasikia tu sijawahi kufika, rekodi za bendi hii huwa nasisikia tu ndani ya radio, ama kweli anapiga sana.”

“Ni mahala pazuri sana.”

Vibywaji vilifika na kuanza kunywa huku wakiwa mara kwa mara wakiondoka kwenda kulisakata rumba.

Kiasi cha saa saba hivi usiku, wakati Willy na Lolita wakilisakata rumba uwanjani Willy alimuona Rajabu akielekea mezani kwao ambayo ilikuwa tupu. Alitazama kule na huku akionyesha dalili kuwa alikuwa akiwafuata.

“Nadhani Rajabu anatufuata,” Willy alimwambia Lolita.

“Umemwona wapi?” aliuliza Lolita huku akiendelea kucheza.

“Yuko pale mezani kwetu.”

“Ina maana wewe unacheza na huku ukiangalia mezani petu!”

“Inabidi nifanye hivyo Lolly mpenzi, maana hakuna mtu anayelinda meza yetu, anaweza kutokea mhuni au mlevi akanywa pombe yetu au akamwaga. Vile vile anaweza akatokea mtu anayechukia wewe au mimi akatuwekea sumu ndani ya pombe yetu,”

“Usiseme hivyo Willy, mimi sina mtu anayenichukia kiasi hicho. Lo ondoa wazo kama hilo.”

“Huwezi kujua, dunia ya siku hizi imejaa fitina tupu. Hebu twende tukamwone huenda anatuhitaji naona kama ana wasiwasi hivi!”

Kwa shingo upande Lolita alikubali kuondoka maana muziki waliokuwa wakiucheza ulikuwa muziki taratibu uliokuwa ukiliwaza mioyo ya wachezaji na wasikilizaji wote hawa waliokuwa katika mapenzi.

“Kuna simu yako ofisini kwangu”, Rajabu alimwambia Willy kwa shauku walipomkaribia.

“Asante” Willy alijibu kisha akamgeukia Lolita ambaye alikuwa akimwangalia kwa mshangao akamwambia, “Mpenzi, ningoje nikasikilize simu mara moja.”

“Nani anakupigia simu saa saba hizi za usiku?” Aliuliza Lolita.

“Nitamjuaje kabla sijaisikia simu yenyewe?” Alijibu Willy.

“Amejuaje kama uko hapa? Je kama tungeebda Mlimani Park?”.

“Nitajuaje kuwa amejua niko hapa kabla sijasema naye Loly mpenzi?”

“Haya baba nenda”, alijibu Lolita kwa sauti ya kutoridhika.

“Wasichana watu wa ajabu sana, kwa mawazo yake anafikiri simu hii inatoka kwa msichana mwingine”, alilalama Willy huku wakielekea ofisini kwa Rajabu.

Msichana akikupenda sana basi ujuwe amejawa na wivu juu yako, lakini hata hivyo Willy kama msichana hakuonei wivu ujuwe hakupendi. Hii inaonyesha waziwazi kuwa msichana huyu anakupenda sana”, alisema Rajabu huku wakiingia ndani ya ofisi.

Bila kumjibu Rajabu, Willy aliiendea simu na kuinua.

“Helo, nani mwenzangu?” aliuliza.

“Unastarehe tu mwenzetu, leo una chuma kipywa nini?” alijibiwa.

“Aah Maselina uko wapi?”

“Nipo nyumbani kwangu, nimejaribu Mlimani Park sikupata ikabidi nijaribu hapo, vipi muziki hapo.”

“Muziki safi tu, natumai hukunipigia saa hizi kuniuliza muziki hapa ukoje.” alijibu Willy kwa sauti nzito.

“Usiwe mkali baba, kwa taarifa yako kama ulikuwa na mipango ya starehe na hicho chuma ulichonacho basi sahau. Nimepata simu muda mfupi uliopita toka kwa Chifu, kwa hiyo njoo hapa kwangu haraka iwezekanavyo nina salamu zako maalumu,” alijibu kwa sauti ya utani.

Lakini kwa sababu Willy alikuwa akimwelewa sana Maselina, uso wake ulionyesha kuwa ulikuwa umezingatia vizuri sana ujumbe huu.

“Asante sana, nakuja,” halafu akamgeukia Rajabu, Sisi sasa tutaondoka”

“Vipi kuna matatizo nyumbani mbona haraka hivi baada ya kupata hiyo simu?”

“Hapana, hakuna matatizo yoyote ila kumefika wageni nyumbani, nilikuwa nimeacha ujumbe kuwa wakifika wakati wowote nielezwe.”

“Aisii, basi karibu tena wiki ijayo, mlete huyu mrembo tena maana hajastarehe vizuri leo.”

“Bila shaka nitamleta”.

“Oke Willy niagie na mrembo huyo.”

“Asante, nitakuagia. Kwa heri.”

“Kwa heri asante”, waliagana kwa kupeana mikono.

Alipokuwa akirudi kwenye meza yake, mawazo yake tayari yalikuwa kazini yakifikiri salamu zake kutoka kwa Chifu zitakuwa salamu za namna gani.

Alipofika mezani pake alimkuta Lolita anazozana na kijana mmoja aliyekuwa anataka kwenda kucheza naye kwa nguvu.

“Vipi ndugu mbona unakuja kufanya fujo hapa?” alimuuliza huyo kijana.

“Siyo fujo ila tu na mimi nataka kupata fursa ya kucheza na mrembo huyu itakuwaje tukuachie wewe ufaidi vyote peke yako?” Yule kijana alijibu kwa dharau. Willy alimwangalia akagundua kuwa tayari alikuwa ameishalewa vibaya sana.

“Twende zetu Loly, achana naye huyu kisha lewa.”

“Afadhali umekuja mapema alitaka kunivuta kwa nguvu”, alijibu Lolita huku akisimama.

“Haya kaka nenda kafaide peke yako. Lakini nakupa onyo usije na mrembo kiasi hiki siku nyingine lazima nitakufanyia fujo,” alisema yule kijana.

“Sawa mshindi ni wewe,” alijibu Willy kwa dharau huku wakiondoka akiwa amemkumbatia Lolita kiunoni.

Macho ya watu wengi yaliwaangaza huku wakidiliki kusema.

“Lo, kweli vijana hao wanapendeza kwa uwili wao”, kusema kweli vijana hao walikuwa wanapendeza sana. Kuchaguana walikuwa wamechaguana. Willy alikuwa mwenye sura ya kupendeza sana. Mavazi yalikuwa yakimkaa kama vile alizaliwa nayo kwa hivyo yalimfanya azidi kupendeza kiasi ambacho kila mtu aliyemuona alikiri kuwa alikuwa kijana nadhifu sana. Kwa jinsi hii haikuwa vigumu kwa Willy kuwa na uhusiano mzuri na wasichana wengi. Kwa upande wa mapato Willy alijulikana kuwa kijana mwenye kipato cha juu. Watu wengi hawakuelewa hasa alikuwa akifanya kazi gani, ila tu walijuwa alikuwa anashughulikia biasahara akiwa kama wakala wa makampuni ya nchi za nje katika Tanzania. Kwa hivi kusafirisafiri nchi za nje ambapo huyu kijana alikuwa akifanya mara kwa mara kuliweza kueleweka vilevile. Lakini ukweli wenyewe ni kwamba

kijana nadhifu huyu hakuwa mfanyabiashara ila alikuwa mpelelezi maarufu katika Afrika jina lake kamili akiitwa Willy Gamba, ila watu wengi walijua jina lake la kwanza, kwa hiyo kila mtu alimwita kwa jina la Willy.

Msichana aliyekuwa amefuatana naye usiku huu alikuwa msichana rafiki kati ya rafiki zake wasichana wachache aliokuwa nao mjini Dar es Salaam. Msichana huyu alikuwa akifanya kazi na shirika la Reli Tanzania kama mwandishi muhtasi.

Kati ya wasichana wazuri mjini Dar es Salaam huyu msichana alikuwa mmoja wao, kwani alikuwa mrembo hasa. Alikuwa na umbo zuri kiasi cha kwamba kila apitapo watu humwangalia. Toka chini hadi juu alitosheleza kuitwa mrembo kwa kila hali. Kwa hiyo vijana hawa walipoonana hawakuwa na budi kupendana, kwani kwa uwili wao walipendeza sana kwani walionekana kama mapacha.

“Simu ilikuwa inatoka wapi?” aliuliza Lolita.

“Ilikuwa ni simu ya kikazi.”

“Mteja wangu mmoja wa Lusaka amefika kuniona. Alipofika amepiga simu kwa mwandishi muhtasi wangu ambaye alianza kunitafuta mpaka amenipata. Kwa hivi inanibidi nikamuone sasa,” Willy alidanganya.

“Kwanini usingoje kesho, yanini kumfuata usiku huu,” Lolita aliendelea kudadisi,

“Unajua tena shughuli za kikazi, wateja wangu ni wafanyabiashara kama unionavyo mimi, kwa hiyo anaweza kuwa anasafiri kesho asubuhi huenda ndiyo maana ananihitaji haraka hivi,” alizidi kudanganya.

“Lo, mwandishi wako lazima awe na kazi sana, kuamshwa usiku hivi na kuanza kukutafuta! Je kama na yeye angekuwa ameenda kustarehe huyo mteja wako angekupataje?” Lolita aliuliza.

“Kama mimi niko nje lazima mwandishi wangu yuko nyumbani na kama yeye yuko nje mimi niko nyumbani, hii ni sheria yetu ya kazi maana kazi yetu tunaweza kuhitajiwa na wateja wetu saa yoyote ofisini au nyumbani.”

Walielezana yote haya huku wakielekea mjini wakirudi kutoka Kimara, “Sasa Loly mimi nitakupeleka mpaka nyumabani kwangu, halafu mimi nitakwenda nikaonane na huyu mgeni, mara moja nitakukuta.”

“Lakini usikawie, eh Willy mpenzi.”

“Usiwe na wasiwasi, nitarudi mara tu nimalizapo mazungumzo.” Kwa sababu saa hizi za usiku magari huwa hakuna, iliwachukuwa muda mchache kufika nyumabani kwa Willy, sehemu ya Upanga. Walipofika nyumbani, Willy alifungua nyumba wakaingia ndani.

“Mpenzi nenda kapumzike mimi nitarudi sasa hivi.”

“Willy mpenzi, usikawie.” Alilalamika Lolita huku Willy akimvuta na kumpa busu motomoto walikaa hivi kwa dakika mbili hivi ndipo akamwachia.

“Kalale Loly, nakuja sasa hivi,” Willy alisema na kuondoka aliingia ndani ya gari lake akawasha moto kuelekea sehemu ya Mikumi ambako ndiko Maselina alikuwa akiishi. Wakati akielekea kwa Maselina, Willy alimfikiria sana Maselina.

Alimfikiria kuwa msichana shupavu sana katika kazi yake. Maselina alikuwa mwandishi wa siri wa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Tanzania ambaye kiofisi alijulikana kama Chifu. Alikuwa na umri upatao miaka ishirini na sita (26) na alikuwa ameisha fanyakazi katika idara hii kwa muda wa miaka sita. Kwa ajili ya ushupavu wa kazi yake baada ya kuwa na idara hiyo kwa muda wa miaka mitatu aliweza kuchaguliwa kuwa mwandishi wa siri wa Chifu. Bado alikuwa hajaolewa na ilikuwa vigumu kujuwa ni kwa sababu gani kwani kama ni kwa uzuri alikuwa mzuri wa kutosha na kama ni kwa tabia alikuwa na tabia nzuri sana. Wafanyakazi wenziwe walifikiri kuwa huenda kazi aliyokuwa akiifanya ilimfanya asiweze kuolewa kwani kazi kama ile kwa mwanamke aliyeolewa ingekuwa ngumu kuitekeleza, Hata Willy alikubaliana na mawazo haya. Kila Maselina alipokuwa akiulizwa na marafiki zake juu ya suala hili la kuolewa alitabasamu tu na kusema,

“Muda wangu wa kuolewa bado haujafikia”, Willy na Maselina walikuwa wakielewana sana kikazi na kuelewana huku kulijenga urafiki wa aina yake kati yao. Watu wengi walifikiri kuwa walikuwa katika mapenzi lakini ukweli ni kuwa hata siku moja wazo hilo haliingia mawazoni mwao ingawaje siku zingine walikuwa wakienda kwenye starehe pamoja. Ili kuuzeza urafiki kati ya Willy na Maselina nitaeleweka vizuri nikisema urafiki huu ulikuwa kama wa mtu na dada yake.

Ilikuwa saa nane za usiku wakati Willy aliposimamisha gari mbele ya nyumba ya Maselina. Taa ilikuwa ikiwaka sebuleni iliyoonyesha kuwa Maselina alikuwa macho akimsubiri Willy, “Karibu Willy, inakuchukua mwaka kutoka Kimara kufika hapa au ilibidi ukakifiche hicho chuma chako kabla ya kuja hapa!”.

“Hauko mbali sana na ukweli,” alijibu Willy huku akiingia ndani na Maselina alirudishia mlango.

Maselina alikwenda kufungua barafu akatoa chupa ya Konyagi na vpande vya barafu na ndimu akatenga bilauli mbili na kuweka Konyagi kwa ajili ya Willy na akatayarisha nyingine kwa ajili yake mwenyewe.

“Nimepata simu kutoka kwa Chifu, masaa machache yaliyopita,” alieleza Maselina huku akiketi kitako, “Anakutaka ufike Lusaka kabla ya kesho mchana. Ameeleza kuwa kuna jambo muhimu sana kiasi cha kwamba unaweza ukahitajika kusafiri bila kurudi hapa Dar es Salaam. Kwa hivi ameamru kuwa ufanye safari yako kamili kamili kabisa. Hii Willy ina maana kuwa kuna safari nyingine kabambe inakungoja maana kufuatana na maelezo ya Chifu inabidi uende ukiwa na vyombo vyako vyote. Kuna ndege ya jeshi la Zambia ambayo ilifika hapa kuchukua mizigo yao, tayari mipango imeishafanywa uondoke nayo. Rubani wa ndege hiyo anazo habari kuwa atakuwa na abiria ambaye anahitajiwa kuhudhuria mkutano wa bodi ya wakurugenzi ya Tazara ambao unaendelea huko mjini Lusaka. Kwa hivyo utasafiri kama mfanyakazi wa Tazara hadi Lusaka ambapo utaonana na Chifu kwa maagizo zaidi. Ndege itaondoka saa nne asubuhi kwa hiyo nenda ukajitayarisha. Jina lako alilopewa rubani huyo ni Marko Mabawa, Meneja wa Shirika la Reli la Tazara. Nimempigia Wilson simu anakutayarishia hati ya kusafiria kwenda Lusaka kwa jina hilo ambayo ataleta moja kwa moja kwako asubuhi hii ya leo. Mambo mengine yamebaki juu yako kutekeleza. Je una swali kutokana maelezo hayo?” (Hapa Maselina alipumzika huku akimwanguka Willy kwa matumaini).

“La hasha”, Willy alijibu, “Nafikiri nimekuelewa kwa ufasaha kabisa. Lililobaki ni dukuduku moyoni mwangu kuna nini huko Lusaka, maana hata jinsi Chifu alivyoitwa na kuondoka ilikuwa kiajabu ajabu. Hata hivyo nitapiga moyo konde nikayajuwe nitakapofika. Hii ina maana nimeitwa peke yangu?”.

“Bila shaka, maana sikupata maelekezo ya mtu mwingine ila wewe tu”, Maselina alijibu.

“Asante Maselina, mimi naondoka nikajitayarisha, kama kukwa na jambo lolote zaidi unaweza kunipata nyumbani kwangu kabla ya hiyo saa nne”.

“Vizuri Willy, mimi ninakuomba safari njema uende salama Mungu awe nawe upate kurudi salama. Kama mara hii ni safari nyingine ya hatari ninakuomba ukajiangalie vizuri usije kupata madhala ya aina yoyote. Uwe ukikumbuka kuwa kila siku mimi nitakuwa pamoja nawe katika sala zangu, ukiwa na imani hiyo

naamini utarudi salama maana Mungu anasema aombaye atapewa na vilevile husema anamsaidia anayejisaidia. Kwa hiyo kwa sababu tunaombea usalama wako ni matumaini yetu kuwa Mungu atakupa usalama kwa sababu wewe kila wakati unajisaidia vilevile Mungu atakusaidia.

“Asante kwa kunipa maneno ya kunipa moyo, ndiyo sababu Maselina sintaweza kukusahau hata kwa siku moja maisha mwangu kwa kufuatana na maneno ambayo huwa ukinipa kila ninapokuwa nikikaribiwa na safari kabambe”, Willy alimaliza kinywaji chake akaagana na Maselina ambaye alimsindikiza hadi kwenye gari lake.

“Kwa heri Willy.”

“Kwa heri Maselina,” waliagana huku Willy akiondosha gari lake na kumpeperushia Maselina busu. Maselina alibaki pale nje ameshikwa na butwa na huku akisikia uchungu moyoni mwake kwa vile Willy alikuwa yumo mbioni kwenda katika safari zake za hatari.

Willy naye alishikwa na wasiwasi kuwa safari hii kwenda Lusaka ingezaa safari nyingine ya hatari. Lakini kwa vile Willy hatari ndiyo ilikuwa shughuli yake kidogo alikuwa akisikia roho ya furaha kujua kuwa alikuwa anakwenda kwenye safari nyingine ambayo ingeweza kuzaa hatari ila tu kilichokuwa kikimtia wasiwasi ni hatari za namna gani atakazo pambana nazo, maana safari hii ilikuwa ya kiajabu ajabu kufuatana na vile Chifu alivyo kuwa ameondoka na sasa alikuwa akimwita yeye Willy afike Lusaka upesi iwezekanavyo.

Willy aliwasili nyumbani kwake na kumkuta Lolita anagalagala tu kitandani bado hajalala.

“Mbona hulali Loly mpenzi?”

“Nitapataje usingizi bila ya wewe kuwa karibu nani? Nilikuwa ninakungoja kwa shauku sana.

Njoo basi unibembeleze nipate usingizi.” Willy alikata shauri apate usingizi ingawaje wa muda mfupi kwa hivi alichojoa nguo zake tayari kwa kulala.

“Mgeni wako umempata”, aliuliza Lolita huku akuwa amemkumbatia Willy.

“Nimeonana naye, na tumezungumza vya kutosha. Na katika mazungumzo yetu itanibidi asubuhi hii niende safari Lusaka.” Lolita alishituka kidogo na kuanza kulalamika.

“Aah Willy usiende kesho, hata hatujafaidi “week-end” hii wewe unapanga safari! Ngoja utaenda jumatatu”.

“Haitawezekana Loly, hata mimi ningependa nipumzike nawe “week-end” hii lakini inabidi niwe Lusaka kabla ya saa kumi mchana maana inabidi nionane na mteja wangu mmoja ambaye itambidi aondoke Lusaka Mjini Kuelekea Ulaya, kwa hiyo inanibidi nimuwahi kabla hajaondoka.

Usiwe na wasiwasi mimi nitarudi mara tu baada ya kuonana naye.”

“Haya baba mimi siwezi kukulazimisha. Sogea basi unikumbatie vizuri.” Willy alizima taa, akajisogeza na kumkumbatia Lolita vizuri.

Ilikuwa yapata saa kumi na mbili asubuhi Willy alipoamka na kuanza kujitayarisha. Lolita naye aliamka huku pombe bado zikiwa kichwani na usingizi ukiwa bado unamuelemea, lakini ilimbidi aamke kusudi aweze kumtengenezea Willy kifungua kinywa.

“Lala tu Loly mpenzi, mimi nitashughulika mwenyewe,”

Willy alimueleza alipomuona macho yake yakiwa mazito yamejaa usingizi.

“Hata ngoja nikutengenezee Chemsha kinywa, kama ni kulala nitalala wakati utakapoondoka.

“Hiari yako mama”

“Asante” alijibu Lolita huku akielekea jikoni. Willy alichukua mkoba wake maalumu wa kwa safari za namna hii na kuanza kuupakia. Alifungua sehemu ya uficho ya mkoba huu ambayo ikifungwa hakuna mtu anaweza kutambua kama kuna nafasi ya kutia vitu katika sehemu hiyo.

Alimchungulia Lolita na kumuona yupo jikoni akijishughulisha na kutengeneza chai. Aliendelea kufunguwa kabati lake, kisha akafunguwa saraka iliyokuwa ndani ya kabati na kutoa bastola tatu, fulana mbili zisizopenyezeka kwa risasi za bunduki, mabunda ya risasi na vitu vingine vingi vya kuweza kumsaidia wakati wa hatari kisha akaiweka ndani ya sehemu ya ufuko wa mkoba wake na kufunga. Baada ya kupakia vitu hivi aliingia kuweka vitu ambavyo mfanya biashara yeyote anategemea kuwa navyo safarini. Wakati akiwa katika pilikapilika hizi simu ililia na akaenda kuisikiliza.

“Hallo nyumbani kwa Gamba hapa,”

“Nani mwenzangu?”

“Wewe unataka kuzungumza na nani?”

“Naomba kuzungumza na ndugu Marko Mabawa”

“Subiri tafadhali,” Willy alijibu huku kwa sauti nzito.

“Mimi ni rubani Josiah Banda wa Jeshi la anga la Zambia, Nadhani una habari zangu!”

“Aaa ndugu Banda habari za asubuhi?”

“Ni nzuri tu, je wewe,”

“Mimi salama. Habari zako nimepata na mimi niko katika pilika za kujitayarisha, nitakuwa uwanja wa ndege mnamo saa tatu hivi,” alimweleza.

“Fanya mapema kidogo maanna tulikuwa tuondoke saa nne, lakini tumeamriwa sasa tuondoke saa tatu,”

“Sawa basi, “Willy alijibu, mimi nitakuwa hapo uwanjani kati ya saa mbili na saa mbili na nusu.”

“Haya vizuri asante, tutaonana wakati huo.”

“Asante kwaheri’ alijibu Willy na kukata simu. Baada ya simu hii aliendelea na kutayarisha vitu vyake vya safari. Alipokuwa tayari, Lolita naye alikuwa ameandaa meza tayari kwa chemsha kinywa. Wote walikaa na kuanza kustafutahi.

“Nitaenda na gari mpaka uwanja wa ndege na nitamuachia kijana mmoja wa ofisini kwangu ambaye atakuletea. Unaweza kutumia gari mpaka hapo nitakaporudi,” Willy alimweleza Lolita huku wakiendelea kula.

“Kama ni hivyo ngoja basi mimi nikusindikize hadi uwanja wa ndege na mimi nitarudi na gari,”

“Hapana, wewe pumzika tu maana hadi sasa bado hujalala.”

“Wewe Mbona ndiye kabisa hujalala.” Lolita alisema huku akimwangalia kwa macho ya kurembua.

“Mimi nimeisha zoea, usinitilie wasiwasi.”

“Kama utakavyopenda Willy”

“Vile vile ningefurahi kama ungekuwa unakuja kuangalia nyumba mara moja moja hadi nitakaporudi.”

“Ina maana utakaa sana.”

“Hapana, lakini huwezi kujua mambo ya safari hii naweka kama tahadhari tu.”

Kidogo walisikia gari linasimama nje. Willy alienda kufunguwa mlango akakuta ni Wilson.

“Karibu ndani,” Willy alimkaribisha.

“Asante nimekuletea Pasi yako, mimi nakwenda,” alijibu Wilson huku akiwa na wasiwasi kama kawaida yake kila aonanapo na Willy.

“Usiende, maana utanisindikiza hadi uwanja wa ndege. Gari lako acha hapa, utalichukuwa utakaporudisha gari langu.” Waliingia ndani lakini Wilson alikataa kukaribia mezani huku akimkodolea macho Lolita ambaye alikuwa amevaa vazi la usiku.

Baada ya kustafutahi Willy na Lolita waliingia chumba cha kulala kwa mazungumzo mafupi.

“Oke Loly mpenzi, mimi ninakwenda tutaonana nitakaporudi.”

Bila kumjibu Lolita alimng'ang'ania mabegani kwa kuanza kumpa busu kali sana lililochukuwa kama dakika tatu.

“Haya kwaheri Willy,” Lolita aliaga taratibu huku mwili wake ukitetemeka.

“Asante, usiwe na wasiwasi mimi nitarudi upesi itakavyowezezana.” Walitoka nje ya chumba.

“Twende zetu Wilson” Willy alisema huku amebeba mkoba wake ambao ulionekana mdogo sana, lakini huku ulikuwa umebeba mambo makubwa. Lolita aliwasindikiza mpaka kwenye gari, na walipoondoka alibaki machozi yakimtoka.

Willy alifika uwanja wa ndege kiasi cha saa mbili na dakika ishirini na kusimamisha gari lake kwenye lango la sehemu ya ndege za Jeshi la Tanzania.

“Wilson asante sana na sasa unaweza kurudi.”

“Asante, safiri salama.”

Kwenye lango alikuta mwanajeshi aliyekuwa kwenye zamu.

“Mimi ni Marko Mabawa ni abiria wa ndege ya Jeshi la Zambia,” alijitambulisha.

“Ahaa wanakusubiri nenda kwenye ndege ile pale,” askari alisema huku akionyesha kwa kidole ilipokuwa ndege ya Jeshi la Zambia. Alipofika alikuta Rubani Banda anamsubiri na baada ya kumaliza taratibu zote za safari za hapo kiwanjani waliingia ndani ya ndege tayari kwa kuruka kuelekea Lusaka, Zambia.

SURA YA TATU

KIKOSI CHA KISASI

Kwa mara nyingine tena chumba hiki cha mkutano ambamo jana yake walikutana wanakamati wa kamati ndogo ya usalama ya kamati ya Ukombozi ya Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika, kilikuwa kimekawa tena na watu wale wale jioni hii. Kila mmoja alipokwisha keti, Mwenyekiti alianza kusema, “Ndugu wanakamati nashukuru kuwaona wote mmehudhuria tena katika kikao chetu hiki cha pili cha mkutano huu wa maana sana katika Afrika. Nimatumaini yangu kuwa Wakurugenzi wa upelelezi wameweza kupata muda wa kukutana na kuzungumza kikamilifu juu ya utekelezaji wa suala hili. Vile vile ni matumaini yangu kuwa Ndugu Willy Gamba ameweza kupashwa habari na kuwasili mjini hapa ingawaje simuoni hapa,” alimaliza Mwenyekiti wa kamati ya ukombozi.

Bila kusita Mkurugenzi wa Upelelezi wa Zambia alisimama na kuanza kueleza.

“Ndugu wanakamati, nachukua fursa hii kwa niaba ya Wakurugenzi wenzangu, ili nipate kuwaelezeni ingawaje kwa muhtasari tu mambo tuliyoafikiana juu ya jambo hili. kwanza tumekubaliana kuwa ifunguliwe ofisi ya muda itakayo shughulikia operesheni hii na iwe hapa Mjini Lusaka chini ya uongozi wa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Tanzania akisaidiwa na Mkurugenzi wa Upelelezi wa Zambia. Huenda wengi wenu mnajiuliza kwa nini kama kiongozi wa ofisi ya operesheni hii ni kutoka Tanzania, Ofisi yenyewe isiwe mjini Dar es salaam. Kwa sababu makao makuu ya kamati ya ukombozi yako mjini Dar es salaam, tumeonelea ili kupoteza lengo ofisi hii ni ya muda isikae mjini hapo. Mkurugenzi wa Upelelezi wa Tanzania amechaguliwa kuongoza ofisi hii ya muda kwa sababu kiongozi wa 'kikosi cha kisasi' ambaye ndugu wanakamati mmemchagua anafanya kazi chini yake kwa hiyo itakuwa rahisi kwao kuelewana vizuri kuliko ikibidi mpelelezi huyu awe chini ya kiongozi ambaye hakumzoea. Kama nilivyokwisha tamka hapo awali sisi tumeendelea kuunga mkono uamuzi kuwa Ndugu Willy Gamba ndiye apewe rasmi jukumu hili kubwa. Kwa taarifa yenu ndugu Gamba ameisha wasili hapa mjini na huenda muda si mrefu atafika kuhudhuria kikao hiki kama ilivyokuwa akitakiwa. Juu ya kikosi chenyewe kitakavyokuwa tumeamua kuwa kikosi hiki kiwe na watu wanne. Yaani Gamba akisaidiwa na wapelelezi wengine wa hali ya juu watatu. Wapelelezi hawa wengine watatu majina yao yameisha pendekezwa na mara tu taratibu fulani fulani zitakapo malizika wataelezwa jinsi ya kuungana na

mwenzao huko mjini Kinshasa na ofisi hii ya muda itakavyokuwa ikishughulikia suala hili kuanzia sasa. Kwa kifupi, ndugu wanakamati, utekelezaji wa suala hili litakuwa jukumu la ofisi hii ya muda ikishirikiana na 'Kikosi cha Kisasi. Kwa niaba ya Wakurugenzi wenzangu ninadiriki kusema kuwa kama kuna watu watakaoweza kulifanya jambo hili lifaulu basi watu hawa waliokwisha pendekezwa ndio pekee wanaweza kulifanya lifaulu. Kwa hiyo ninalowaomba ndugu wanakamati, ni kukaza roho, tumuombe Mungu, yeye atawasaidia hawa vijana wetu hadi kufaulu, asante, alimaliza.

“Imenipa matumaini makubwa,” alisema Mwenyekiti, “Kuona kuwa kwa muda mfupi huu mmeweza kupanga jinsi ya kulikabili suala hili. Kwa vile nyinyi ndio wataalamu sisi hatuna budi kuchukuwa ushauri wenu na kuacha yote mikononi mwa ofisi hiyo ya muda ya kushughulikia suala hili. Nasi tunatumaini Mungu kuwa atakuwa pamoja nasi hadi tupatapo ushindi. Mimi nitaendelea kukaa hapa kusudi niweze kuwa karibu na mambo yanavyokwenda. Wanakamati wengine mnaweza kurudi kwenu, jinsi mambo yatakavyokuwa yakiendelea hii ofisi ya muda itawajulisheni. Kitu kikubwa ni kutoa shukrani zangu nyingi kwa jinsi mlivyoweza kufika na kutoa uamuzi kwa suala lililo gumu kuliko yaliyowahi kutokea katika bara letu hili la Afrika. nawaombeni mzidi kukaa na moyo wa namna hii. Kwa hivi ni...”

Alipokuwa amefikikia hapo, ghafla mlango wa chumba ulifunguliwa na Willy Gamba akaingia ndani. Wajumbe wote macho yao yalimwangaza kijana huyu nadhifu aliyeingia na kuanza kumchunguza toka chini hadi juu. Mkutano ni kama ulikuwa umepigwa bumbuazi, wakati vile vile Gamba alikuwa amepigwa na bumbuazi kutokana na jinsi alivyokuwa akiangaliwa.

“Asante,” walijibu kwa pamoja.

“Karibu,” Mwenyekiti alimkaribisha kwa kumuonyesha kiti kilichokuwa wazi karibu naye. Gamba alienda akakaa huku bado macho yake yako kwake. Wajumbe wengi ambao walikuwa bodo hawajamuona hata mara moja, walishangaa kuona kuwa kijana nadhifu na mwenye sura nzuri hivi ndiye alikuwa Willy Gamba ambaye sifa zake za ujasiri zilifana na kutapakaa Afrika nzima.

“Ndugu wajumbe huyu ndiye Willy Gamba tuliyekuwa tukimzungumzia. Na ndugu Gamba hawa ni wajumbe wa kamati ndogo ya usalama ya kamati ya Ukombozi ya Nchi huru za Kiafrika,” Willy alitingisha kichwa huku akiwaangalia wajumbe kwa makini mmoja baada ya mwingine, “Sidhani kama unajua kwa nini umeitwa hapa.”

“Sijui maana sijaambiwa kwa nini, mimi habari nilizozipata ni kuwa nifike hapa Lusaka. Na nilipofika hapa nimeamriwa nifike jengo hili na chumba hiki ambamo nitamkuta mkuu wangu wa kazi. Kwa mshangao mkubwa najikuta uso kwa uso na kamati ya usalama, sijui na mimi nimepandishwa cheo kiasi cha kuwa mwanakamati wa kamati mojawapo ya OAU.”

“La hasha, kwa taarifa yako ndugu Gamba umeitwa hapa na kikao hiki kwa jambo maalumu”, alimweleza Mwenyekiti kwa uso mzito, “Jambo uliloitiwa hapa ni kuwa, bara zima la Afrika limekuhitaji ukalisaidie kupigana vita dhidi ya wapinga mapinduzi wa Afrika. Nafikiri umepata habari za tukio la kifo cha Rais wa Shirikisho la vyama vya wapigania uhuru Kusini mwa Afrika Ndugu Edward Mongo kilichotokea siku mbili mjini Kinshasa Zaire”.

“Nimepata habari, nimesikia kwenye redio na nimesoma magazetini”.

“Kwa kifupi mkutano huu umekuita ili ukapeleleze kifo cha ndugu huyu. Jambo hili ni kubwa sana maana kifo hiki ni mojawapo ya vifo vingi ambavyo vimewahi kuwatokea ndugu zetu wapigania uhuru. Kwa hivi jukumu ulilopewa na Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika ni kuongoza kikosi kitakachopeleleza na kuwasaka hawa maadui wa Afrika wanaoua vijana wanamapinduzi wa Afrika eti kwa sababu wanapigania haki za nchi yao. Kwa hivi utaongoza kikosi kitakachoitwa “KIKOSI CHA KISASI” ambacho habari zake zaidi utapata kutoka kwenye ofisi ya muda inayoshughulikia suala hili. Nasema tena jukumu hili ni kubwa na tunakuomba ukalitekeleze kwa kadri ya uwezo wako, maana kushinda kwako ndiyo kushinda kwa Afrika. Mimi sina maelezo zaidi, maana maelezo haya utayapata kutoka kwa Mkurugenzi wako ambaye ndiye vile vile atakayeongoza ofisi hii. Una swali?”. Mwenyekiti alimuuliza Willy huku akimkazia macho.

“Ndugu Mwenyekiti mimi nikiwa mwana wa Afrika sina budi kuitika mwito niitwapo. Sina la kuuliza bali ningependa kusema tu kwamba jukumu mlilonipa nitalitekeleza kwa kadri ya uwezo wangu. Kwa vile umesema habari zenyewe juu ya jambo hili, maswali zaidi nitayauliza huko. Kwa hiyo hapa nasema tena msiwe na wasiwasi mimi nitajitahidi kadri ya uwezo wangu” alimazizia.

“Asante sana, tunapokuwa na vijana kama nyinyi, nasi hatuna budi kujivunia na kusonga mbele mapambano dhidi ya wapinga mapinduzi. Ndugu wanakamati sina budi kuwaageni tena. Mambo yote tunayaacha mikononi mwa ofisi ya muda, na nina imani kuwa mambo yatakwenenda vizuri. Tufunge mkutano tukitegemea mafanikio mazuri, kama tulivyoanza na mafanikio mazuri,” alimaliza Mwenyekiti na Wajumbe waliondoka ndani ya chumba cha mkutano, walipofika chini kwenye

maegesho ya magari. Mkurugenzi wa Usalama wa Zambia na wa Tanzania waliingia ndani ya gari moja halafu wakamweleza Gamba awafuate.”Tangulieni”, huku akiendesha gari lake la kukodi alilokuwa ameliegesha hatua chache. Aliingia ndani ya gari na kuanza kuwafuata japokuwa kwa mbali. Ndani ya mawazo yake Willy alijua mara hii alikuwa anakwenda kwenye tume kubwa kuliko zote alizowahi kwenda. Alifikiria upinzani ambao angeupata na kubashiri kuwa utakuwa mkubwa kutokana na habari walizokuwa nazo tayari juu ya hawa wauaji waliokuwa wakiwaua wapigania uhuru sehemu mbali mbali katika Afrika. Hata hivyo alipiga moyo konde na kungojea kusikia zaidi kutoka kwa Chifu kabla hajasumbua sana mawazo yake juu ya suala hili. Huku mawazo yote yakipita kichwani mwake aliendelea kuwafuata Chifu na mwenzake ambao walikuwa wakiingia barabara iliyokuwa ikichepuka na kuingia sehemu ya Lilanga. Kwa mawazo yake alifikiri kuwa huenda walikuwa wakielekea nyumbani kwa mwenziwe na Chifu kwa ajili ya chakula cha jioni. Punde si punde akaliona gari la akina Chifu likitoa ishara ya kuingia kwenye nyumba moja naye akafanya vile vile. Baada ya kungoja magari yaliyokuwa kwenye barabara kuu kupita walipiga kona na magari yote yalielekea kwenye nyumba hii iliyokuwa hatua chache tu kutoka barabarani. Nyumba hii ilikuwa imezungukwa na ua na ilikuwa na mlango mkubwa uliokuwa umefungwa na lango kubwa. Gari ya akina Chifu ilipiga honi na lango likafunguliwa na askari ambaye baada ya kulifungulia alikuja mpaka kwenye gari na kuinama akazungumza na mwenziwe na Chifu ambaye ndiye alikuwa akiendesha. Baada ya kuzungumza kidogo aliwaruhusu wakapita na Willy naye aliruhusiwa kupita bila kusimamishwa. Baada ya kulipita lango hiligari la Willy liliangaza nyumba moja nzuri iliyokuwa ikiwaka taa. Chifu na mwenzake wakaegesha gari lao karibu tu na mlango wa mbele ya nyumba hii na Willy naye akafanya vile vile. Chifu na mwenziwe alitoka na kusimama nje ya gari lao huku wakimsubiri Willy. Willy alipokuwa ameungana nao walimkaribisha ndani.

Kwa kuangalia mazingira ya nyumba yenyewe mara moja Willy alitambua kuwa haikuwa nyumba iliyokuwa ikikaliwa na watu bali ilikuwa nyumba iliyokuwa ikitumiwa kwa shughuli fulani fulani. “Karibu ndani ndugu Gamba,”

“Asante”, alijibu Willy.

Walipoingia ndani Willy ndipo alitambua hasa kuwa hii haikuwa nyumba ya kuishi kama inavyotegemewa kwa sehemu ya Lilandabali ilikuwa ni ofisi. Baada tu ya kuingia, walifika sehemu ya mapokezi ambako walikuta kuna wasichana wawili mmoja akiwa yule aliyewafungulia na mwingine alikuwa amekaa kwenye kiti

huku kulia kwake kukiwa na mashine ya teleksi na kushoto kwake kulikuwa na “Swichi-bodi” ya simu. Hawa wasichana wote walikuwa wakishughulika sana maana yule aliyekuwa akifungua mlango baada kuwafungulia tu alienda kwenye mashine ya kupiga taipu. Huyu mwingine alikuwa akihangaika, huku akijibu simu na huku akijibu au akipokea habari zilizokuwa zikitokea kwenye teleksi.

Willy aliwaangalia wasichana hawa kwa mara moja huku akiendelea kuwafuata Chifu na mwenzake ambaye walipita sehemu hii ya mapokezi kana kwamba hapakuwa na Kitu. Wale wasichana nao waliwahi kumwangalia Willy ingawaje kwa wasiwasi na kuendelea na kazi zao kanakwamba hakuna aliyekuwa ameingia ndani humo. Hii nidhamu ya kazi wasichana hawa imemuelewesha Willy kuwa hii ilikuwa ofisi maalumu. Mwenziwe na Chifu alitoa funguo mfukoni mwake na kufunguwa cha kwanza walichofika na kuingia ndani. Kilikuwa chumba kikubwa cha kutosha kiasi cha kuweza kuwa na meza ya mkutano.

“Karibu”, aliwakaribisha tena kwa kuwaonyesha viti vya kukaa.

“Hizi ndizo zitakuwa ofisi za ofisi ya muda itakayoshughulikia shughuli za “Kikosi cha Kisasi”, aliwaeleza.

Ziko mahala pazuri sana, maana panaonekana kama nyumbani kwa mtu tu” aliongeza Chifu.

“Kwa kweli ni sehemu nzuri na huwa inatumiwa kama ofisi yangu ya siri, na ni maofisa wa hali ya juu sana katika ofisi yangu wanaojua ofisi yangu hii iko wapi. Na tokea sasa ofisi hii itafungwa kwa shuguli zake za kawaida na itatumiwa tu na shughuli hii mpya. Hao wasichana mliowaona hapo mapokezi ni waandishi wangu wa siri na nimeonelea vizuri kuwaweka kama waandishi wetu kwa shughuli hii mpya.” Mkurugenzi wa Zambia alisema.

“Chifu, Maselina angefaa kuwa hapa, unaonaje ?” Aliuliza Willy kimatani.

“Anafaa huko huko aliko”, alijibu chifu naye kimatani.

“Ndugu Chifu, kama Gamba anavyokuita, hii ndiyo ofisi yetu karibu tuanze kazi”, alisema mwenyeji wao huku akiinua mkoba wake na kuanza kutoa makaratasi na kuyasoma taratibu. Willy yeye alichukuwa paketi yake ya sigara aina ya Benson & Hedges (B & H) na kutoa sigara na kuanza kuvuta taratibu huku akiwaangalia hawa mabosi wake waliokuwa wakisoma hayo makaratasi yao huku wakikunja uso utafikiri mwanamke anayejisikia uchungu wa kujifungua. Ilichukuwa zaidi ya nusu saa kumaliza kuyapitia makaratasi yao kabla hawajaanza kumhutubia Willy. Chifu

mara tu baada ya kusoma makaratasi haya uso wake ulibadilika kama kawaida yake anapokuwa karibu kuzungumzia kitu ambacho hakimpendezi.

“Willy sidhani kama kuna haja ya kukueleza jinsi suala hili lilivyo la muhimu, maana wewe mwenyewe umesikia umuhimu wake kutoka kwa kinywa cha Mwenyekiti mwenyewe. Kwa hivi sisi katika maelezo yetu tutakazia juu ya namna suala lenyewe inabidi lishughulikiwe”, alieleza Chifu huku mwenziwe naye akiwa ameishafunga jalada huku akimsikiliza kwa makini. Willy naye alikaa kimya huku akimsikiliza Chifu kwa makini sana alipokuwa akiendelea na maelezo yake, “Tatizo linalo tukabili ni kuhusiana na mauaji wanayofanyiwa wapigania uhuru. Kwa vile naelewa unajua kwa kirefu juu ya mauaji yaliyotokea hapo awali na bidii zilizofanywa na idara za upelelezi za kila Nchi iliyousika na mauaji haya, maelezo yangu yatasimama juu ya nini unatakiwa ufanye kwa sasa hivi. Kitu ambacho unatakiwa wewe pamoja na wenzio mtakaounda hiki “Kikosi cha Kisasi ni kukisaka kikundi kinachohusika na mauaji haya na kukifutilia mbali. Kikundi hiki ambacho tunaamini kumeundwa na Serikali za wapinga mapinduzi wa Afrika ni lazima kisakwe na kufutiliwa mbali kabla madhara yake hayajawa makubwa sana kiasi cha kuwakatisha tamaa wapigania Uhuru wa Kusini mwa Afrika. Haya mauaji yaliyofanyika juzi mjini Kinshasa, imeamuliwa upelelezi wake ufanywe moja kwa moja chini ya Kamati ya Ukombozi ya OAU badala ya kuiachia serikali ya Zaire kufanya upelelezi huu. Hii haina maana kuwa hii itaikataza Zaire isifanye upelelezi wake, na wala haina maana kuwa serikali ya Zaire inajua uamzi wa Kamati ya Ukombozi ya kufanya upelelezi chini yake yenyewe. Kwa hivi wewe tokea sasa utafanyakazi chini ya Kamati ya Ukombozi mpaka hapo tutakapojua mwisho wa jambo hili.

Kwa vile mauaji haya yametokea huko Kinshasa itakubidi uondoke ukaanzie huko huko Kinshasa upelelezi wako. Mauaji haya bado yako moto kwa hivi tunaamini kuwa ukifika na kuanza upelelezi kwa wakati huu tunatumaini unaweza kupata mwanzo mzuri. Kwa vile nimekueleza kuwa serikali ya Zaire haina habari juu ya uamuzi huu wa Kamati ya Ukombozi kwa wakati huu itabidi upelelezi wenu ufanyike kwa siri mpaka hapo itakapobidi serikali ya Zaire ipate habari. Dhamira yetu ni kutaka uwe Kinshasa kabla ya mazishi ya marehemu ili uweze kuyahudhuria. Hii itakupa nafasi ya kuwahi harakati zote zinazofanyika na vikundi mbali mbali juu ya tukio hili.

“Huko Kinshasa utamkuta kijana mmoja aitwaye Robert Sikawa, ambaye ni mpelelezi wa idara ya upelelezi ya Zambia lakini anafanya kazi katika ofisi ya

OAU iliyopo hapo mjini Kinshasa kama katibu mwenezi. Kijana huyu alipelekwa kwenye ofisi hii toka mwaka jana baada tu ya mauaji ya Meja Komba Matenga yaliyotokea huko Kinshasa. Tokea wakati huo mpaka sasa amekuwa huko na anaweza kuonyesha kuwa anafanya kazi yake. Kwa hivi itakubidi ifanye kazi bega kwa bena naye na vile vile ameamriwa akueleze habari zote anazozijua mpaka sasa. Ni imani yetu kuwa kutokana na habari utakazozipata kutoka kwa Sikawa zitakupa mwanga mkubwa jinsi gani ulishughulikie jambo hili. Vile vile utapata msaada kutoka kwa wapelelezi wengine wawili mashuhuri sana katika Afrika. Mmoja ni Kapteni Petite Osei kutoka Nigeria na mwingine ni Michael Degaro kutoka Msumbiji. Wapelelezi wote hawa wawili wameishapata habari na wameshauriwa wafikapo Kinshasa wafanye mipango ya kukuona kwani kazi yote watakiyofanya itakuwa chini yako. Kwa hivi wewe Willy pamoja na hawa vijana wengine watatu ndiyo mtaunda “Kkosi cha Kisasi”. Wewe ndiye utakuwa kiongozi wa kikosi hiki na hawa vijana na vijana wengine wameamriwa kufanya kazi chini amri yako. Wewe ndiye utakuwa wa kwanza kufika Kinshasa hawa wengine wawili watafuata, nawe utapata habari zao za kuingia Kinshasa kwa kupitia kwa Sikawa ambaye upashanaji wote wa habari utapitia kwake ila tu kwa habari ambazo utazona muhimu na ungehitaji kuziwasilisha mwenyewe moja kwa moja kwetu. Katika upashanaji wetu wa habari juu juu ya suala hili utajulikana kama “KK”. Utapewa nambari za simu na za teleksi zilizomo ndani ya ofisi hii kwa hiyo wakati wowote utakapoona inabidi kutupasha habari unaweza kuzituma.

Kwa vile shughuli mtakazozifanya huko ni za kisiri basi itabidi nanyi mwingine nchini na mjini hapo kwa siri. Wewe itaingia mjini hapo kama mfanyabiashara kama ilivyo kawaida yako. Kwa mara hii utakuwa Mkurugenzi wa Wakala wa makampuni ya nchi za nje katika Zaire ambaye yuko mjini Kinshasa kwa mapumziko ya kibiashara. Na hasa kusudi la kuwa kwako mapumzikoni kibiashara mjini Kinshasa ni kutafuta wakala kwa makampuni yaliyo mjini hapo ili yaweze kufanya biashara na makampuni ya hapa Zambia. Sina haja ya kukueleza zaidi maana wewe mwenyewe unajua vizuri kuwa na kazi hiyo. Jina utakalotumia ni Willy Chitalu, kabila Mnyanja wa Zambia. Wenzako nao wataingia Kinshasa kama wafanyabiashara. Wote wawili wataingia kwa pamoja kama wafanyabiashara kutoka Nigeria ambao vile vile wamefika mjini Kinshasa katika shughuli za kukuza biashara yao nchi za nje. Wao nao watakuwa wakitumia majina ya bandia. Kapteni Petite Osei atakuwa akitumia jina la Petit Ozu, Michael Degero atakuwa akitumia jina la Mike Kofi”, Chifu alipofika hapa alitoa picha mbili ndani ya bahasha na kumpa Willy. “Hiyo picha niliyokupa mwanzo ndiyo ya Petit Ozu na

ya pili ya Mike Kofi, nafikiri utawakumbuka ukiwaona uso kwa uso”, Willy alikuwa mtu mwenye akili ya kunasa sura za watu ya hali ya juu sana. Kwa hivi aliziangalia sura hizi kwenye picha kwa makini sana na baada ya kuziangalia sana akazirudisha kwa Chifu.

“Asante, nitawakumbuka”, nilimwambia.

“Unaweza kuziweka kwa ukumbusho wako”, Chifu alimwambia.

“Hapana nitawakumbuka, si vizuri kusafiri na picha za watu ambao inabidi usiwe umewafahamu tangu awali”.

“Vizuri kama unaona si lazima. Nafikiri ulipata ujumbe wangu kutoka kwa Maselina kuwa uchukue zana zako zote tayari kwa safari”.

“Ndiyo nilipata na nimechukua kila kitu ninachohitaji kwa safari kama hii”.

“Nafikiri maelezo niliyokupa yanatosha, mambo mengine yote tunayaacha mikononi mwako na wenzako. Wewe utaondoka hapa kesho asubuhi na ndege ya Shirika la Ndege la Zaire” kisha akafungua tena mkoba akatoa pasipoti na tikiti ya ndege “Hii hapa ni tikiti yako ya kusafiria hai Zaire na hii ni pasipoti utakayotumia kwa jina la Willy Chitalu”. Alifungua tena mkona na kutoa hundi za kusafiria na noti za dola ya Kimarekani. “Hizi pesa za matumizi na ukihitaji pesa zaidi wakati wowote Sikawa ameelekezwa akupatie. Nafikiri mimi kwa upande wangu nimemaliza, kwa hivi ninamwachia mwenzangu kama ana zaidi ya kukueleza”, alimaliza Chifu.

“Mimi sina mengi ya kueleza nadhani yote Chifu amekueleza kwa ufasaha. Sisi hata kama tukikuambia nini, haifai kitu, ngoma utaiona wewe mwenyewe, kwa hivi sasa tunabaki tukikutegemea wewe huku tukipiga mioyo yetu konde na kumuomba Mwenyezi Mungu aweze kuwasaidia hadi kufaulu hadi kufaulu katika suala hili. Kitu mnahitajiwa kuwa nacho ni ujasiri na kupigana hadi mwisho, maana tutakuwa tumeanguka sana mkishindwa vita hivi dhidi ya wauaji katili hawa. Vijana ambao utashughulika nao ni vijana jasiri na ni matumaini yangu kuwa chini ya uongozi wako shupavu ujasiri wao utaziidi. Sasa inakaribia saa nne za usiku, nafikiri tukuache ukapumzike kwani siku zitakazofuata zitakuwa hazina mapumziko ya kutosha. Mungu akusaidie.

“Asante sana wazee wangu” Willy alisema. Mimi nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu. Tuombeeni tu Mungu aweze aweze kutusaidia kwani sisi tunachokifanya ni haki yetu kwa hivi katuna budi kupata baraka za Mwenyezi Mungu katika

mapambano yetu. Asanteni sana”, alisema huku akinyanyuka kitini. “Haya Willy nadhani nitakupigia simu hapo hotelini kwako kabla hujaondoka kesho asubuhi”. Alijibu Chifu.

“Kwani amefikia hoteli gani? Maana nasikia alikataa nafasi aliyowekewa huko Lusaka Hoteli”, alieleza mwenzake na Chifu.

“Yuko Ridgeway Hoteli”, alijibu Chifu.

“Siyo kuwa nilikataa kukaa Lusaka Hoteli, bali tu kwa sababu ya kawaida. Mara nyingi mimi nikiwa hapa Hoteli yangu ya Ridgeway. Oke Chifu nitangojea simu yako na kwaheri kesho asubuhi”, alisema Willy huku akiagana nao kwa kushikana mikono.

Willy alifungua mlango wa chumba na kutoka kisha akarudisha mlango na kuwaacha mabosi wake waendeleo na mambo yao. Willy alijitokeza kwenye mapokezi ya hii ofisi ya waandishi wa siri wa Mkurugenzi wa upelelezi wa Zambia. Willy alipotokeza kwenye ofisi hii alikuta bado wale wasichana wapo. Yule msichana aliyekuwa anashughulika na simu pamoja na teleksi alikuwa bado anashughulika huku yule msichana mwingine aliyekuwa akipiga mashine alikuwa amekaa juu ya meza huku ameshika mkoba wake akionyesha kuwa amemaliza kazi. Walipomuona Willy anatokeza yule msichana aliyekuwa amekaa kwenye mezaa aliteremka haraka haraka na kujiweka sawa.

“Nafikiri tunaweza kusalimiana sasa, habari zenu?” Willy aliwasalimu.

“Habari zetu ni nzuri”, walimjibu kwa pamoja huku yule msichana wa simu akionyesha dalili kuwa alikuwa bado anazongwa na kazi.

“Poleni sana mpaka sasa bado mko kazini? Kusema kweli wasichana kama nyinyi saa hizi mnafaa muwe mko mahali mkistarehe, moyo kama huu ni wa kizalendo na mnastahili pongezi zangu.”

Wale wasichana walitabasamu tu bila kumjibu kitu. Kisha yule msichana mpiga mashine akamwambia mwenzake, “Mwambie mzee, mimi nimemaliza kazi naomba anifanyie mpango wa usafiri kurudi nyumbani,” Wakati yule msichana mwingine akizungumza na bosi wao, Willy ambaye sasa alikuwa karibu akiwaangalia vizuri wale wasichana, alimtolea yule msichana aliyekuwa akiomba usafiri tabasamu la haiba kisha akamwambia, “Hamna haja ya kuomba usafiri, kama hautajali sana mimi nitakupa msaada mpaka mahali popote unapotaka kwenda.”

“Asante sana, sisi tunao usafiri wetu, kwa hiyo hamna haja ya kukusumbua”, yule msichana alijibu.

“Hapana siyo kwamba kukupa msaada utakuwa unanisumbua, kusema kweli moyo wangu utafurahi sana kukupa msaada huo. Na kama kweli utanikatalia utakuwa umenisikitisha sana,”

“Yule msichana akiwa anasita kujibu huku yule mwenzake akiwa anamtolea jicho la pembeni naye akingojea mwenziwe atajibu nini, bosi wao alifungua mlango na kutokea hapo ofisini kwao. Mara moja wote wakawa wamejiweka vizuri, wakati bosi wao anamwangalia Willy kwa mshangao.

“Wewe bado unafanya nini hapa?” alimuuliza Willy.

“Mzee, unajua sisi vijana lazima tufahamiane, isiye siku moja tukagongana mitaani na hawa dada zangu tukafanyiana ubaya na hali sisi ni ndugu.” Jibu hili la Willy lilionekana kumtoshela bosi kwa hivi akaanza kumweleza yule msichana aliyekuwa akiomba usafiri, “Unaweza kwenda ila kesho asubuhi sana utakuja kuchukuliwa kuna kazi, kwa hivi kapumzike mapema upate kuamka mapema. Joyce piga simu kwa dereva alete gari,” alimwamru yule msichana mwingine.

“Hamna haja ya kumwita dereva mzee, kama amemaliza kazi na kwa vile mimi ninaondoka sasa hivi sioni kwanini tusiondoke pamoja,” Willy alishauri.

Bosi alimwangalia yule msichana halafu Willy akatingisha mabega yake kuonyesha kuwa yeye naye alikuwa haoni sababu kama Willy anakwenda huko kwanini wasiondoke pamoja.

“Haya kama unaona hatakusumbua unaweza kwenda.”

“Bila taabu mzee”. alijibu Willy huku anamshika yule msichana mkono na kumwongoza nje. Bosi na yule msichana mwingine wakabaki wanaangaliana kwa shauku.

Willy na yule msichana waliingia ndani ya gari na kuelekea mjini.

“Sijui mwenzangu unaitwa nani?” aliuliza Willy.

“Mie naitwa Amanda”.

“Jina zuri sana, unakaa sehemu gani?”.

“Nakaa hapa karibu, sehemu ya Kamwala karibu na sokoni.”

“Oho, nafikiri hutajali tukipita mara moja hapo Ridgeway ukapate kinywaji kidogo kabla hujaenda kupumzika.”

“Hapana, nafikiri umemsikia mzee alivyosema, itabidi nikalale mapema.

“Mimi najua ndiyo sababu nikasema kidogo,” Willy alimwalia tena na kutoa tabasamu la kukata na shoka.

“Uh... sijui kwa nini inakuwa vigumu kukukatalia kitu, haya twende ndugu...”

Ndugu Willy, ndilo jina langu”.

“Nafurahi kuwa na wewe, kusema kweli nimesoma habari zako jana, na ninasisimkwa kila nikifikiri niko na wewe,” Amanda alieleza huku akimwalia kidogo na kuangalia pembeni. Muda huu Willy ndipo alipokuwa anaanza kutambuwa kuwa msichana huyu aliyekuwa nae alikuwa msichana mzuri sana lakini uzuri wake ulikuwa hauwezi kujulikana kwa mara moja.

“Hata mie nafurahi kuwa nawe,” Willy alijibu huku akiwa anapiga kona kuingia Ridgeway Hotel. Aliegesha gari lake vizuri na kutoka nje.

“Mimi sijawahi kuingia hapa hotelini,” alisema Amanda.

“Wacha kwa nini?” Aliuliza Willy kwa mshangao.

“Basi tu, kwanza sina mtu wa kuweza kunileta hapa, maana tangu nianze kazi mwaka mmoja sasa kazi yangu imenitinga kiasi kuwa ni vigumu kupata mtu wa kuweza kuvumilia kiasi kile.” Willy aliweza kuelewa maana hata Maselina aliwahi kuwa na tatizo kama hilo. Kidogo alisikia huruma maana msichana huyu alikuwa bado mbichi kiasi cha miaka ishirini na moja au mbili hivi.

“Kama mimi ningekuwa hapa siku zote amini nakwambia ningepata muda tu.” alimjibu huku wakikaa kwenye meza moja kando ya bwawa lililotengenezwa hapo Ridgeway Hotel. Mtumishi alikuja akaagizwa vinywaji. Vinywaji vilipokuja walikunywa huku wakielezana mambo mbalimbali katika maisha yao ambayo yaliwafanya kustukia ni saa sita na kuhitaji waondoke.

“Asante sana Willy, umenifanya kuwa msichana wa furaha sana leo kwani kwa mara ya kwanza maishani nimepata mtu ambaye nimeweza kuzungumza naye na kunielewa. Tafadhali ukirudi toka Kinshasa rudi unione. Mungu atakusaidia najua utarudi salama kwa hiyo tafadhali rudi hapa unione eh Willy.

“Mungu akipenda nikiwa salama nitakuja usiwe na shaka”, Alijibu Willy wakiingia ndani ya gari. Amanda alimvuta na kuanza kumpiga busu. “Tafadhali urudi.” Alibwebweta.

“WP”

“Mabibi na mabwana, kwa niaba ya rubani wetu Godi Kazadi pamoja na wafanyakazi wenzake, ningependa kuwajulisheni kuwa mnamo dakika kumi na tano zijazo tutatua kwenye uwanja wa ndege wa Ndjili wa mjini Kinshasa. Ni matumaini yetu kuwa mmefurahia safari yenu ambayo mmesafiri na shirika la ndege la Zaire ndani ya ndege ya aina ya Boeing 737 ambayo imekuwa ikiruka kisi cha futi 30,000 juu ya usawa wa bahari. Kwa wageni ningependa kuwajulisha kuwa Kinshasa ndio mji mkuu wa Zaire ambao umejengwa pembeni mwa mto wa Zaire magharibi ya nchi. Mji wenyewe ni mtulivu kwa biashara na starehe na ninadiriki kusema kuwa ndio mji wenye anasa zaidi katika Afrika ya kati. Kwa hivi ni matumaini yetu kuwa mtafurahia kuwapo kwenu Kinshasa na tunawakaribisheni tena kusafiri na shirika la ndege la Zaire Mpatapo safari tena. Asanteni sana,” ilisikika sauti nyororo na tamu ya msichana ikinena.

Abiria wote walichangamka kule kusikia walikuwa karibu kutua mjini Kinshasa. Hata waliokuwa wamelala walianka.

SURA YA NNE

WILLY ambaye kwa muda mwingi alikuwa akisinziasinzia alikuwa sasa hivi yu macho. Alikuwa akisinziasinzia maana usiku ule alikuwa hakupata usingizi sawasawa. Alianza kufikiria usiku uliokuwa umepita. Usiku ule baada ya kuondoka na Amanda Ridgeway Hoteli, alimpeleka mpaka nyumbani kwake Kamwala. Alipofika nyumbani kwa Amanda. Amanda alimng'ang'ania aingie ndani. Amanda alikuwa akikaa peke yake kwenye nyumba ya chumba kimoja cha kulala na sebule. Kusema kweli kilitosha sana kwa msichana kama yeye na vyombo vilivyokuwa ndani vilionyesha waziwazi kuwa Amanda alikuwa na kipato cha juu. Haya yote Willy aliyaweka rohoni alipoingia ndani ya chumba hicho. Amanda alileta vinywaji wakaanza kunywa upya kabisa huku hali ya kimapenzi ikizidi kukomaa kati yao dakika hata dakika kiasi kwamba walijistukia ni saa tisa za usiku. Kwa hivi Amanda alimuomba Willy ajipumzishe pale kwa masaa yaliyokuwa yamebaki.

Kwa vile Willy hakutaka kumvunja moyo mtoto huyu alikubaliana naye na kwenda chumbani tayari kwa kulala. Sina haja ya kukueleza mengi kwani wewe mwenyewe unajua mambo wayafanyayo wawili wapendanao na hasa ikiwa penzi bado changa kama hili la Willy na Amanda. Kusema kweli watu hawa walistukia wale ndege wa asubuhi wanatoa salam zao kabla hata hawajafumba macho yao kusinzia. Hivi ilimbidi Willy aondoke awahi hotelini tayari kwa safari. Willy alikumbuka jinsi Amanda alivyomuaga huku machozi yakimtoka na huku akirudia neno lile anarudia usiku kucha “Willy mpenzi, sijui kwa nini nimekupenda kiasi chote hiki na huku kesho unaondoka tena! Tafadhali sana mpenzi ukienda urudi kuniona.” Baada ya kuondoka nyumbani kwa Amanda alirudi hadi hotelini kwake ambapo alianza kujitayarisha kwa safari.

Ilipofika saa kumi na mbili na nusu alipata simu toka kwa Chifu. Chifu alizidi tu kumhimiza umuhimu wa kazi aliyokuwa akienda kuifanya akimalizia kwa sentesi hii “Willy ni imani yangu kuwa kwa maadili na hamasa upiganaji wa kimapinduzi mtaweza kabisa kufauli katika jambo hili. Kwa hiyo nendeni mkaitende hii kazi kwa moyo safi na wa kimapinduzi, na Mungu atawasaidia”, Willy aliyafikiria yote haya kwa moyo wa uchungu sana kwani aliweza kuufikiria uzito wa mambo yaliyokuwa yakimngojea kuyakabiri huko Kinshasa.

“Funga mkanda wako”, alishituliwa Willy na msichana mmoja mfanyakazi.

“Tunatua sasa”

“Oho asante bibie, nilikuwa mbali”, Willy alijibu huku akijiweka sawa kwa kutua.

Ndege ilipokuwa imetua watu walianza kuteremka hapo kwenye uwanja wa ndege wa Ndjili wa mjini Kinshasa. Willy hakuwa mgeni sana mjini Kinshasa kwani alikuwa amewahi kufika mara mbili ingawaje kwa muda mfupi, hivi alikuwa akijua vipi mambo yalivyokuwa hapo uwanja wa ndege.

Akiwa amebeba mkoba wake Willy aliteremka pamoja na abiria wenzake kuelekea uhamiaji na ofisi ushuru wa forodha.

Willy aliweza kupita ukaguzi wa ofisi hizi bila shida na kutokea nje tayari kwa safari ya kuelekea mjini Kinshasa. Huku akiwa anaangaza huku na kule kuna kama kulikuwa na mtu ambaye alikuwa anaonyesha kumtegemea kuingia mjini Kinshasa. Alipoona hakuna mtu wa namna hii ila abiria waliowasili pamoja na ndugu zao waliokuja kuwapokea na taksi dereva walikuwa tayari kujipatia abiria wa kupeleka mjini. Willy alienda moja kwa moja mpaka kwenye ofisi za kampuni ya 'Soviete de Transport de Kinshasa' ijulikanayo kwa kifupi kama STK ambayo inashughulikia magari ya kukodisha. Alipofika kaunta ya ofisi hii aliwakuta wasichana waliokuwa wakishughulika.

“Habari yako dada?” Alimsalimia msichana aliyemkaribisha.

“Nzuri karibu, tukusaidie nini?” Yule msichana alimuuliza kwa sauti nyororo.

“Nahitaji gari”.

“Oho, hamna taabu tunayo magari mazuri aina ya Mercedes Benz”, alimweleza kisha akamwita msichana mmoja aliyekuwa amesimama hapo nje ya ofisi, “Marie, mpeleke abiria huyu mjini”, Hii kampuni ya STK madereva wake wa teksi asilimia sitini na tano ni wanawake.

“Hapana, mimi nataka gari ya kuendesha mwenyewe (Self drive) Willy alieleza.

“Vile vile hamna taabu”, yule msichana alimjibu kisha akaendelea, “Unayo leseni ya udereva?”.

“Ndiyo”, alijibu Willy huku akitoa leseni yake ya kimataifa ya udereva na kumpa yule msichana. Yule msichana aliangalia leseni kisha akamwangalia Willy halafu akasema. “Bosi, masharti ni kwamba itakubidi utoe amana ya Zaire mia mbili, na malipo mengine utayafanya siku utakaporudisha gari, kwani unategemea kukaa nayo muda gani?”.

“Huenda kiasi cha wiki moja au mbili”.

“Vizuri, kwa sasa lipa pesa hizo na jaza fomu hii”, akampa fomu. “Hebu nipe pasipoti”, Willy alimpa pasipoti yake huku akiendelea kujaza fomu ya kukodi gari. Alipomaliza akamuuliza, naweza kulipa katika dola”.

“Unaweza, nitakupa risti”.

Walipomaliza taratibu zote yule msicha alichukua ufunguo wa gari na kumpeleka Willy kwenye gari moja kati ya yale yaliyokuwa yameegeshwa karibu na ofisi ile.

“Nimekuchagulia gari nzuri sanana mpya aina ya Mercedes Benz, ina 'redio-cassette' ndani yake, kwa hiyo naamini itakufaa sana, hasa kwa mfanyabiashara kama wewe. Na ukipata matatizo yoyote tafadhali nijulishe, kadi yangu ya kazi hii hapa”, alimpa hiyo kadi Willy akaiangalia, ilikuwa na jina la msichana huyu ambaye jina lake aliitwa Ntumba Akanda. Vile vile kulikuwa na namba za simu yake ya nyumbani pamoja na ya kazini.

“Asante sana Ntumba, nikipata shida yoyote nitakujulisha”,

“Hata kama utakosa mahala pa kulala karibuni nyumbani”, alitania huku akicheka.

“Lo, afadhali nikose nafasi, ili nikaribishwe kwako,” alijibu Willy naye kimatani.

“Bila wasiwasi, haya kwaheri”.

“Asante sana bibie tutaonana”, wakaagana.

“Kutoka uwanja wa ndege wa Ndjjili hadi mjini Kinshasa ni umbali wa kilomita 30. Hivi, Willy aliwasha gari moto kuondoka kuelekea mjini. Kwa hivo alikata gari lake kulia na kuingia ndani ya barabara ya Patrice Emery Lumumba barabara kubwa itokayo uwanja wa ndege akielekea mjini.

Wakati huo Willy akielekea mjini kutoka uwanja wa ndege katika nyumba ya Mzungu mmoja iliyoko mtaa wa Gitronir sehemu ya kuishi ya Limete kulikuwa na watu wanne wakiwa na fikra ya jambo hilo hilo ambalo alikuwa akilifikiria Willy lakini kwa hali tofauti.

Kati ya watu hawa wawili walikuwa Wazungu, mmoja Muasia na mmoja Mwafrika. Watu hawa ambao saa sita hizi za mchana walikuwa wamekusanyika kwa kikao cha dharura, walikuwa ni viongozi wa kikosi cha siri kilichokuwa kikijulikana kama “WP” kirefu cha 'White Power' yaani 'Nguvu ya Mweupe' ambacho kilikuwa ni kikosi kilichoundwa na Shirika la ujasusi la Afrika Kusini

liitwalo 'Boss' kwa madhumuni ya kuwapiga vita wanamapinduzi na wapenda maendeleo wa Afrika. Kikundi hiki kilikuwa kimeundwa kwa ujuzi wa kijasusi wa hali ya juu kiasi kwamba mbali na 'Boss' hakuna shirika lingine la ujasusi pamoja na Idara zote za upelelezi na polisi duniani ambazo zilijua kuwepo kwa kikundi hiki. Kikundi hiki kilifanya shughuli zake makao yake makuu yakiwa mjini Kinshasa na kikiongozwa na Pierre Simonard ambaye ndiye alikuwa mwenye nyumba hii ambamo mchana huu alikuwa akikutana na wasaidizi wake hawa watatu.

Pierre Simonard alikuwa mtu mwenye umri wa miaka 52, mjini Kinshasa alijulikana kama Mbelgiji na alifahamika kwa watu wengi sana maana alikuwa na gereji ya magari ambayo ilitokea kupendwa sana na watu wa hali ya juu kutokana na utengenezaji wake mzuri wa magari. Gereji yake hii ambayo ilikuwa barabara ya tisa (9) sehemu ya Limete ilikuwa ikiitwa Garage Du Peuple!. Kutokana na hali hii ilikuwa vigumu kumfikiria Pierre kwa shughuli zinginezo mbaya. Jina lake la kweli aliitwa Peter Simon na alikuwa ofisa wa juu katika 'Boss'. Kabla ya kutumwa Kinshasa kuongoza 'WP' alikuwa kiongozi wa idara ya mateso na mauaji ya 'Boss'. Hii inaonyesha waziwazi Pierre alikuwa jasusi katili wa hali ya juu, na kuchaguliwa kwake kuja kuongoza kikundi hiki kulitokana na uongozi wake wa kikatili katika idara hii.

Pierre aliingia mjini Kinshasa mnamo mwaka kama mfanyabiashara wa Kibelgiji. Kusema kwelie Pierre hakuweza kutambulika kuwa si Mbelgiji kwa sababu hati zake zote za kusafirika zilionyesha kuwa yeye ni Mbelgiji kwa kila hali. Hati zake zilionyesha kuwa yeye alikuwa ni mhandisi wa magari na hivi aliomba leseni ya funguo gereji alipewa bila matatizo. Kwani jila lake lilipopelekwa Brussels kwa uchunguzi na idara ya uhamiaji ya Zaire majibu yaliyorudi yalionyesha kweli kuwa kulikuwa na Pierre Simonard ambaye alikuwa mhandisi na mzaliwa wa Ubelgiji. Hivyo mwishoni mwa mwaka 1968 Pierre alianzisha 'Garage Du Peuple' huku akiendelea na harakati zake za kuunda 'WP' huku akisaidiwa na wateja wake. Baada ya kuwa amejiweka katika hali ya usalama mwaka 1969 ndipo 'WP' hasa iliundwa.

Mwanzoni mwa mwaka huu wa 1969 Jean Vergeance aliingia nchini Zaire naye akitokea Brussels Ubelgiji. Jean naye kama Pierre alikuwa jasusi wa hali ya juu katika 'Boss'. Baada ya Pierre kutoa taarifa kwa wateja wake kuwa mambo yalikuwa yakienda sawasawa na hakukuwa na wasiwasi, ndipo 'Boss' walipomtuma Jean Vergeance ambaye hasa jina lake ni John George mwenye umri

wa miaka 36 kwenda Kinshasa. Jean alipoingia Kinshasa aliingia kama mtaalam na kuajiriwa na kampuni ya Fiat kama mtaalamu. Naye baada ya miezi sita alikwisha jijenga kwa wakubwa aliacha kazi hii na kuanzisha gereji yake binafsi ijulikanayo kwa jina ya 'Garage Auto Diesel' au kwa kifupi GAD ambayo iko sehemu ya Gombe barabara ya T.S.F, wakati wote huo walikuwa wakionana na Piere kwa siri, na hakuna mtu hata mmoja aliyekuwa akijua kama watu wawili hawa wanafahamiana ila tu kwa vile wote wawili walikuwa na gereji. Na huku kuwa na shughuli hii ndiyo ilikuwa mbinu ya Pierre katika mfumo wa kuunda 'WP'.

Katikati ya mwaka huu 1968, Mpakistan mmoja aitwaye Papadimitriou kwa kifupi akijulikana kama Papa aliomba leseni ya kufungua gereji sehemu za Lingwala. Mpakisitan huyu ambaye alikuwa ameingia Zaire kutoka Zambia kama mfanyabiashara wa duka kubwa sana la madawa. Lakini baada ya kukaa na kuanza kujulikana, naye katikati ya mwaka 1969 aliomba leseni ya gereji na bila matatizo akafanikiwa. Mpakistan huyu vilevile alikuwa ni jasusi wa shirika hili la ujasusi 'Boss', Yeye kweli alikuwa Mpakisitan aliyekulia mjini Johannesburg ambako alikuwa akifanya shughuli za biashara. Na wakati wakikaa Johanneburg ndipo 'Boss' ilipomchagua na kumfanya mmoja wa majasusi wake katika nchi za nje. Na baada ya mafunzo ya hali ya juu katika ujasusi Papa alijulikana ndani ya 'Boss' kama 'Executioner' yaani muuaji kwa kutokana na uwezo wake wa kuweza kumwinda mtu hata kama analindwa kiasi gani, na kumuua. Hivi 'Boss' alionelea vizuri kumtumia Papa katika 'WP' na mnamo mwisho wa 1968 wakamfanyia mpango wa kumwamru aende Kinshasa Zaire ambako angasubiri maelezo. Naye katika ya 1969 alipata amri aripoti kwa Pierre kwa siri na afuate maagizo yake. Na kwa kutokana na maagizo ya Pierre, Papa ilimbidi kuuza shughuli zake za duka la madawa na kuanzisha gereji iliyoitwa 'Garage Papadimitriou' ambayo iki barabara ya Kabambare sehemu za Lingwala.

Mwisho wa mwaka 1969 kijana mmoja ambaye kwa wakati huo alikuwa akiitwa Muteba Andre ambaye kwa sasa anaitwa Muteba Kalonzo aliingia mjini Kinshasa akitokea jimbo la Shaba. Kijana huyo mwenye umri wa miaka 32 aliingia Kinshasa na pesa nyingi kutoka jimbo la Shaba, na kuomba leseni ya kuendesha biashara ya magari ya kukodisha, Akiwa mzalendo haikuwa taabu kwake kupata leseni hii, hivyo baada ya kupata leseni hiyo alinunua magari ishirini ya aina ya Fiat 124 na kuyafanya tekisi. Kwa sababu vijana wengi mjini Kinshasa wana uwezo wa kufanya hivi, jambo hili halikumshangaza mtu yeyote hasa akiongezea kuwa kijana huyu alikuwa akitokea jimbo la Shaba. Mwanzoni mwa mwaka 1970 Muteba aliomba leseni ya kufungua gereji kwa sababu aliyoitwa ya kwamba kwa vile ana

magari mengi yake binafsi ingekuwa vizuri kuwa na gereji yake ambayo ingeweza kuhudumia magari yake na vile vile magari ya watu wengine. Sababu hii ilitosheleza sana kwa hiyo alipewa leseni ya gereji na kufungua gereji moja iitwayo 'Garage Baninga' katika sehemu ya Kintambo barabara ya Bangala. Ukweli ni kwamba Muteba naye alikuwa ameajiriwa na 'Boss' kama muuaji wao. Uhusiano wake na makaburu ulianza wakati bado akiwa na umri wa miaka 18, wakati kijana huyo alipokuwa akipigana na majeshi ya kukodishwa ya Tshombe huko Katanga. Muteba alionekana kijana jasiri sana katika mapigano haya, kwa hiyo wakati askari wa kukodishwa walipokuwa wakiondoka Katanga walimuomba afuatane nao. Na kwa sababu wakati huo Muteba alikuwa bado mdogo na mwenye uchu wa kuona ulimwengu ulivyo alikubali na kuondoka nao. Kwa bahati nziri au mbaya askari aliyetokea kumpenda sana alikuwa kaburu, hivyo alisafiri naye kuelekea Afrika Kusini. Na wakati akiwa na askari huyo ndipo 'Boss' alimkundua na kumuona kuwa yu kijana mwenye akili nyingi za kuzaliwa na wangeweza kumtumia kwa mambo yao maovu kama wangeweza kumpatia ujuzi zaidi katika mambo ya ujasusi. Hivi Muteba alikuwa amefanya maovu mengi katika Afrika kwa niaba ya makaburu. Kwa hiyo wakati mipango ya kuunda 'WP' inaendelea, ilionekana jambo muhimu kumshirikisha. Hivyo Muteba ambaye alikuwa Tanzania kwa wakati huo aliamriwa kwenda Kinshasa na kuripoti kwa siri kwa pierre ili aweze kupata maelekezo zaidi.

Hivi ndivyo viongozi wa 'WP' walivyoingia mjini Kinshasa mmoja mmoja na hatmaye kukamilika na kuunda kikosi cha 'WP' ambacho tokea wakati huo kimeweza kufanya madhara ambayo hayatasahaurika kwa wanamapinduzi wa Afrika na kwa watu wenye fikra za kimaendeleo kote Ulimwenguni.

Wakati huu Pierre, Jean, Papa na Muteba wakiwa wamekaa kwenye mkutano wa dharura ndani ya nyumba ya Pierre, 'WP' ilikuwa imekomaa sana na ilikuwa na matawi katika nchi zote za kimapinduzi.

Kikosi hiki kilikuwa na watu wengi sana na chenye uwezo wa kufanya madhara yasiyo kifani. Kama nilivyokwisha kusema Kinshasa ndipo palikuwa makao makuu, na magereji haya manne ndiyo yalikuwa makambi na viwanja vya mafunzo kwa wapinga mapinduzi hawa ambao tayari walikuwa wameweza kuwaua wapigania uhuru wenye sifa za juu sana.

“Jamani karibuni,” Pierre aliwakaribisha wageni wake, huku akiwawekea kinywaji cha 'Whiski' ndani ya bilauli zao.

“Asante,” walimjibu kwa pamoja. Alipokwisha kuwapa kinywaji alijiwekea na yeye halafu akaa chini tayari kwa mazungumzo.

“Nimewaiteni hapa ghafla kwa sababu nimepata habari ambazo nisingeweza kukaa nazo hata kwa muda wa saa moja. Nadhani mmeshangaa sana mimi kuwaiteni wakati majuzi tu ndipo tumeweza kufanya tukio la maana kiasi kwamba Ulimwengu wote unapiga kelele, huku tukiwa tumewapa pigo kubwa makafiri hawa ambao itawachukua muda kupona pigo hili. Naelewa waziwazi kuwa ni amri yetu kuwa kuwa baada ya tukio kama hili tusionane mpaka hapo mambo yanakapokuwa yamepoa lakini kwa sababu ya umuhimu wa mambo niliyoyapata imenibidi nichukue jukumu hili la kuitisha mkutano huu. Nafikiri tumeelewana.”

“Tumeelewa”. walijibu tena kwa pamoja huku wakiwa na shauku la kusikia jambo hili muhimu.

“Nimepata habari kutoka 'Boss' muda wa saa moja iliyopita. Habari hii imeeleza kuwa, 'Boss' imepata habari kutokana na Shirika la Ujasusi la Marekani 'CIA' kuwa juzi Mawaziri wa Ulinzi na Wakurugenzi wao wa Upelelezi wa nchi saba zilizo wanakamati wa kamati ndogo ya usalama ya Kamati Kuu ya Ukombozi ya Nchi Huru za Kiafrika, wameingia Lusaka kisiri. Jambo hili si la kawaida maana kwa mara ya kwanza wanakamati hawa wameandamana na wakurugenzi wao wa upelelezi na safari yao ilikuwa ya kisiri. Hivi ni bayana kuwa wamewasili Lusaka kuzungumzia tukio hili la majuzi. Hivyo 'Boss' imetujulisha jambo hili kusudi tuwe katika hali ya tahadhali. Bado hawajajua ni uamzi gani umefikiwa bali tu wamepata habari kuwa walifanya vikao viwili, lakini bado hawajaona kitu chochote kinachoweza kuonyesha ni uamzi gani wamefikia. Hivyo 'Boss' pamoja na 'CIA' ziko macho kuangalia hatua gani itafuata. Kwa hivi si...” kengere ya simu ilimkata kauli, “Samahani,” aliinuka na kwenda kuzungumza kwenye simu. “Hello Pierre hapa,”

“Aha Patron,” sauti ilijibu. Mara sura ya Pierre ilibadilika na kuwa nzito.

“Nakupata endelea,” alijibu.

“Nimepata habari, spea zimeondoka Lusaka,” alielezwa kutoka upande mwingine wa simu.

“Zote?”.

“Ziendazo Tanzania nusu zimeondoka nusu zimebaki.”

“Ina maana zimekoswa usafiri”.

“Haijajulikana bado, lakini tutapata habari karibuni. Ni hivyo tu. zilizobaki ni zile chache”.

“Habari zingine hizo”, aliwaeleza wenzake, “Hawa wanakamati wote wameishaondoka Lusaka kuelekea makwao isipokuwa mkurugenzi wa upelelezi wa Tanzania ndiye amebaki. Tutapata habari zaidi kwanini amebaki baadae,”

“Hakuna mpelelezi yeyote aliyeingia Lusaka kutoka nchi huru za Kiafrika?” aliuliza Papa.

“Jambo hili nimeulizia lakini mpaka leo asubuhi hakuna hata mmoja kwa wale wanaojulikana aliyeonekana kuingia Zambia,” alijibu Pierre.

“Ni lazima ijulikane upesi kwanini mkurugenzi wa upelelezi wa Tanzania amebaki. Kwa kutokana na rekodi zilizopo 'Boss' pamoja na utafiti wangu niliufanya wakati nikiwa Tanzania, Mkurugenzi huyu ni mshauri sana katika kazi yake, si mtu wa kumrahisisha”, alieleza Muteba.

“Sawa kabisa”, Pierre alisema, “Nitatuma habari wapate kushughulikia jambo hili kikamilifu. Vile vile inatubidi na sisi tuwe macho, kwa hivi lazima kwa wakati huu tuchukue jukumu lote la usalama wa 'WP' sisi wenyewe. Mpaka hapo tutakapoona vingine kuhusu amri zote juu ya tukio hili tunazitoa wenyewe na habari zozote lazima zitufikie sisi wenyewe moja kwa moja, kama mmoja wenu akipata habari zozote kuhusu tukio hili hata likiwa dogo kiasi gani lazima aniletee ripoti, maana 'Boss' inafikiria huenda 'OAU' ikaamua kulipiza kisasi jambo hili, kwa sasa hivi nchi huru za Kiafrika zemeanza kufikia maendeleo makubwa katika mambo mbalimbali hivi hatuwezi kuwapuuza,” aliwaeleza Pierre.

“Kuna jambo moja ilitubidi tuwe tumelifanya, kuwa na mtu wa kuchunga uwanja wa ndege, kuona kama kuna mtu yeyote ambaye kuingia kwake Kinshasa kunatia wasiwasi,” Jean alitoa oni.

“Sawa kabisa Jean, nilikuwa naelekea huko. Itabidi Jean usimamie kikundi chako ambacho kitaangalia usalama kwa ujumla, itabidi sehemu zote muhimu kama uwanja wa ndege na mahoteli yashughulikiwe kikamilifu. Vilevile itabidi utume mtu kwenye mazishi ambayo yameahilishwa mpaka kesho asubuhi ambapo huenda akapata fununu yoyote.”

“Hamna taabu, mambo yote juu ya usalama nitayashughulikia pale patakapohitaji msaada nitawajulisheni,” alijibu Jean kwa sauti ya uthabiti.

“Itabidi tusionanenane isipokuwa tu kwa lazima sana kama hivi. Kama kuna maelezo yoyote tunaweza kuwatumia vijana wetu kama kawaida”, alisema Pierre.

“Ok Patron, sisi tutajiweka katika hali ya tahadhali, lakini sidhani kuna kitu chochote, 'WP' imejificha kiasi ambacho hakuna idara ya upelelezi Afrika inaweza kugundua. Sidhani vilevile kuwa wanaweza kuwekea mashaka Kinshasa, saana wakaiomba Serikali ya Zaire kufanya upelelezi wa kinaganaga jambo ambalo Zaire haiwezi kufika popote Zaidi ya hapo sidhani kuna haja ya kuhangaika sana. Lakini hata hivyo hatutaacha njia yoyote wazi ikiwa 'OAU' itaamua kufanya matata,” alizungumza Papa.

“Kiusalama ni vizuri kuzuia kuliko kuponya”, alijibu Jean ambaye alikuwa amesomea sana mambo ya usalama katika shule za kijasusi za 'Boss'.

“Nakubaliana kabisa nanyi nyote, hivi hatuna budi kuwa na usalama wa hali ya juu. Inawezekana kifo hiki cha Mongo kimewapiga vibaya sana. Lakini hata wakiamua kufanya utafiti 'OAU' wenyewe sidhani watafika popote. Sidhani 'OAU' kiupelelezi inao uwezo wa kuingilia 'Boss' kabla 'Boss' haijaweza kuwasaga wapelelezi wake wote”, alijigamba Pierre.

“Ni kama Papa kupigana ngumi na Mohammed Ali”, alitania Muteba huku wote wakiangua kicheko.

“Oke jamani, kawawekeni watu wenu katika tahadhali, tuingojea nini kitatokea. Mambo mengine yanaendelea kama kawaida. Mimi nitajaribu kukusanya habari nyingi iwezenavyo, nyinyi tumieni majina yenu mazuri kupata habari, maana huenda kwa mara ya kwanza tukapata upinzani toka 'OAU' kutokana na tukio hili la juzi,” aliendelea kuasa Pierre.

“Patron, mbona unakuwa kama mtu mwenye wasiwasi. Usiwe na wasiwasi sisi tuko macho hakuna kitu kinachoweza kuingia 'WP' ambapo sasa ndipo iko imara kama chuma cha pua,” Papa alimhakikishia Pierre. Pierre aliagana na wageni hawa maarufu ambao waliingia ndani ya magari yao na kwenda zao, bila kujua kuwa Willy Gamba mpelelezi mashuhuri katika Afrika alikuwa ameingia mjini Kinshasa saa hizo hizo tayari kutafuta chanzo cha tukio hili.

Willy bila ya kujua kuwa alikuwa ameingia ndani ya mji ambao ndiyo Makao Makuu ya kikundi kiitwacho 'WP' kikundi maalumu cha 'Boss' ambacho kazi yake ilikuwa kuendesha hujuma dhidi ya harakati za Ukombozi wa Kusini mwa Afrika na vile vile kupiga vita harakati zozote zinazofanywa na wanamapinduzi wa Afrika ili kuendeleza fikra za kimaendeleo katika Afrika huru, aliendelea na safari kwenye

barabara hii ya Patrice Emery Lumumba akitokea uwanja wa ndege kuelekea mjini. Akiwa kwenye barabara hii Willy mawazo yake yalimfikiria marehemu Patrice Emery Lumumba, alikuwa amesoma habari za Lumumba na alikuwa mmoja wa wapenzi wake. Hivi moyo wake ulisisimkwa kufikiria kuwa alikuwa akiendesha kwenye barabara hii ambayo ilikuwa imeitwa kama kumbukumbu ya shujaa huyu wa Afrika.

Ghafla akiwa amesafiri kama kilomita kumi na tano hivi akiendesha njia panda ya 'Echangeur de Limete' mawazo yake yaliindea gari moja iliyokuwa nyuma yake ikiwa imehakikisha kuwa inabaki nyuma ya gari lake na huku katikati yao kukiwa na magari mawili au matatu. Willy alikuwa amejenga silika ya namna hii kiasi cha kwamba alikuwa akiweza tu kuhisi kitu bila sababu maalumu. Kwa sababu alikuwa akiamini sana silika yake, mara mawazo yake yalilitilia mashaka gari hili kuwa huenda linamfuata, alikata shauri kuthibitisha. Hivyo aliendelea na safari yake huku akiliangalia gari hilo ndani ya kioo cha kuendesha gari. Kila alipopunguza mwendo na mengine kumpita, gari hili lilihakikisha kuwa nalo linapunguza mwendo kubaki pale pale. Na kila alipokuwa anaongeza mwendo nalo linaongeza mwendo. Hivi alihakikisha kuwa gari hili lilikuwa linamfuata.

Alipofika kwenye kona ambapo barabara ya P.E Lumumba na barabara ya Bongolo zinapokutana alikata shauri kuingia barabara ya Bongolo ili aweze kulikwepa hili gari aliloamini kuwa lilikuwa linamfuata. Alipoingia barabara ya Bongolo gari hili nalo aliliona baada ya muda mfupi lilikuwa nyuma ya gari lingine likizidi kumfuata. Kisha alikata na kuingia barabara ya L'universete, tena baada ya muda mfupi aliliona gari hilo likiwa nyuma ya gari lingine likiwa bado linamfuata. Jambo hili lilimshangaza sana Willy maana yeyote aliyekuwa akimfuata alikuwa mjuzi sana katika kazi yake. Kitu kilichomshangaza sana ni kuwa alikuwa ameingia Kinshasa hata saa haijamalizika, na wala mjini alikuwa hajafika na tayari alikuwa ameanza kufuatwa.

Hili jambo lilikoroga mawazo yake kiasi kikubwa sana. Kwa mawazo yake alikuwa akitegemea kuwa ingemchukua muda kabla hajaweza kutambulika, lakini hii ilionyesha kuwa tayari usalama wake ulikuwa hatarini tokea dakika hii, aliamua kuweka mawazo yake pamoja na viungo vyake katika tahadhari. Alisogeza mkoba wake na kufungua zipu, akatoa bastola iliyokuwa juu. Kwani baada tu ya kuagana na Ntumba aliendesha gari mbali kidogo na uwanja wa ndege kisha akasimama na kufungua mkoba kwenye sehemu yake ya siri na kutoa bastola moja. Maana katika kazi ya akina Willy ilikuwa vigumu kukaa tu bila kuwa na silaha karibu hasa

ugenini kama hapo ambapo alikuwa ameingia tayari kwa mapambano yoyote yale ambayo yangeweza kutokea.

Huku akiwa anaendesha, mkono wake mwingine ulishughulika na kutoa bastola hii ambayo alikuwa ameiweka juu tu. Alipokwisha kufanya hivi aliichomeka bastola yake ndani ya suluali mbele kwenye kitovu na kuendelea na safari yake huku akifikiria amfanyie nini mtu huyu. Vile vile alionelea ni jambo la busara kama naye angeweza kumfahamu mtu huyu ni nani na kwa sababu gani alikuwa akimfuata.

Aliendelea na safari yake akaingia mtaa wa Sendwe kutoka mtaa wa L'universete, alipoangalia bado gari hilo ingawa kwa mbali bado lilikuwa bado likimfuata. Kutoka mtaa wa Sendwe aliingia mtaa wa Funa. Alipoingia mtaa wa Funa vile vile alipunguza mwendo na alipolina hilo gari sasa lilikuwa peke yake linafuata, alikata na kuingia kwenye Stesheni ya Petrol iliyoko mbele ya 'Funa Klabu' halafu akakata shauri kwenda moja kwa moja na kugesha gari lake katikati ya magari yaliyokuwa yameegeshwa na watu ambao walikuwa wamekuja kuogelea mchana huu katika bwawa la 'Funa Klabu'.

Baada ya kugesha gari lake, haraka aliteremka huku akiwa ameinama alikimbia kati ya haya magari na kuinuka umbali kidogo toka kwenye gari lake. Alipokuwa akiinuka ndipo lile gari lililokuwa likimfuata lilikuwa linaegeshwa karibu tu na gari lake na ndani ya gari hili mlikuwa na kijana wa umri kama miaka 30 hivi. Alivaa suti ya Abakozi, miwani ya jua na alionekana kijana muungwana kabisa. Alitazama huku na kule kwa mshangao halafu akaliendea gari la Willy na kuliangalia kwa mbali. Kisha akaelekea kwenye bwawa. Willy alipopata nafasi hii, alikimbia mbio tena huku akiwa ameinama katikati ya magari na bila kuonana na watu mpaka karibu na lile gari lililokuwa likimfuata. Gari lenyewe alipochungua ndani yake aliona hamna kitu.

Alipoangalia kule kwenye bwawa alimuona yule kijana anarudi huku akionekana mwenye kuwa na mshangao na wasiwasi. Willy alikata shauri kujificha pembeni ya gari la pili kutoka kwenye gari la huyu kijana, bila kumuona huku akiangalia nambali za gari la Willy kijana huyu alifungua mlango wa gari lake na kuingia ndani ya gari lake tayari kwa kuondoka.

Willy alimnyemelea polepole kwa kutambaa chini na wakati alipokuwa anawasha gari moto, na Willy naye akawa yuko sawa na mlango wa dereva. Huku akiwa na bastola mkono alifungua mlango wa dereva kwa ghafla kuhamaki yule kijana alijikuta akiwa anaangalia ndani ya mtutu wa bastola.

“Hapo hapo rafiki yangu usijitingishe hii itakuonyesha kuwa si adabu nzuri kufuatafuata watu,” Willy alimwambia kijeuri.

SURA YA TANO

MWANZO WA MAPAMBANO

Yule kijana alipoangalia usoni mwa Willy mara moja alijua huyu mtu hakuwa na mzaha. Hivi akiwa mikono yake ikiwa imeshika kwenye usukani wa gari na mwili wake mzima akiwa amekauka kama mti uliopigwa radi alimjibu Willy,

“Tafadhali niache, mimi ni Robert Sikawa.”

“Nitajuaje kama wewe ni Robert Sikawa?” Aliuliza Willy hali uso wake ukiwa bado mzito.

“Maana wewe ni Willy Gamba, kiongozi wa 'Kikosi cha Kisasi' kwa kifupi KK, ambacho makao yake makuu yako Lusaka...”

“Oke, siku nyingine ujiangalie unaweza kupatwa na matatizo bure. Vile vile unapofuata mtu, inabidi ufanye vizuri kuliko ulivyofanya hasa unapofuata mtu mwenye ujuzi katika mchezo wetu huu,” Willy alimweleza Robert huku akiwa ameisharudisha bastola yake na tayari uso wake ukiwa unaonyesha urafiki, na vile vile akiwa amempa nafasi Robert kutoka ndani ya gari na kusimama wote nje ya gari la Robert.

“Ama kweli ndiyo sababu umechaguliwa kuongoza 'KK’“, alieleza Sikawa.

“Mimi nilishangaa nilipoambiwa inabidi nichukue amri toka kwako tangu wakati utakapofika, maana mimi mwenyewe najiamini sana. Hivi sikuona kwanini tena aje mtu nichukue amri kutoka kwake badala yake yeye kuchukua amri kwangu. Hivi nilikuwa uwanja wa ndege kukupokea na vile vile kukujaribu una ujuzi kiasi gani. Jaribio langu dogo hili linanidhihirishia kuwa kweli wewe ni mjuzi katika mchezo wetu huu, maana mimi ninapomfuata mtu huwa ni vigumu sana kunigundua. Kule kwetu Lusaka katika idara yetu huwa wananiita 'Nyoka wa kijani' sababu hii hii. Hivyo boshi wangu ninakukaribisha mjini Kinshasa,” alieleza Robert.

“Ulijuaje kama ninakuja?”.

“Chifu wako alinitumia habari jana pamoja na picha yako ambayo ingeweza kunifanya nikutambue”.

“Picha, bado unayo?”

“Ndiyo”.

“Tafadhali itatue sasa hivi. Si vizuri kiusalama mpelelezi kutembea na picha ya mpelelezi mwenziwe, kitu anachobidi kufanya ni kuhakikisha kuwa anaangalia picha mara moja na kuiweka sura yake ndani ya kichwa chake kisha anaitatua hiyo picha hapo hapo”, Willy alimshauri.

“Vizuri”, alijibu Robert huku akitoa picha ya Willy ndani ya mfuko wa koti lake na kuwasha kibiriti na kuichoma hiyo picha pale pale.

“Utafikia hoteli gani?”, aliuliza Robert.

“Nafikiri Memling Hoteli itanifaa”.

“Yaa, hoteli hiyo ni tulivu itakufaa. Sijui tuonane muda gani ili niweze kukupa habari nilizonazo kikamilifu?”

“Tuonane jioni saa mbili hivi na kuendelea, maana sasa hivi itabidi nipumzike kidogo”.

“Sawa basi tuonane Vatican Klabu huko Matonge saa hizo.

“Sijui unaifahamu?”.

“Hamna taabu, naifahamu.” Alijibu Willy.

“Oke basi tuonane huko saa hizi”.

“Oke Robert, asante sana, tutaonana”, alijibu Willy huku akiondoka na kuelekea kwenye gari lake. Robert alibaki amesimama pale penye gari lake akimwangalia Willy kwa shauku.

Willy alipanda gari lake akalitia moto na kuondoka kuelekea Memling Hoteli. Alipofika Memling Hoteli alikuta kuna nafasi.

“Karibu,” alikaribishwa na mfanyakazi mmoja msichana aliyemkuta hapo kwenye mapokezi ya hoteli hii.

“Naweza kupata chumba?”, aliuliza Willy.

“Bila shaka, unakaribishwa kwa dhati. Una mzigo?”.

“Nina mkoba mmoja uko ndani ya gari”.

Yule msichana alimwita mchukuzi ili akachukue ule mzigo.

“Acha tu nitakwenda kuuchukua mwenyewe”, Willy alieleza huku akienda kwenye gari.

“Tunavyo vyumba wazi kwenye ghorofa ya pili, tatu na tano, sijui ungependelea ghorofa ipi?”, yule msichana alimuuliza Willy, aliporudi na mkoba wake.

“Wewe unafikiri ghorofa ipi ni nzuri?”.

“Hii inategemea na uchaguzi wa kila mtu binafsi”.

“Uchaguzi wako ndiyo utakuwa wangu”, Willy alimwambia yule msichana huku akimtolea bongwe la tabasamu.

“Chumba nambari 240 kwenye ghorofa ya pili kitakufaa,” yule msichana alimjibu Willy naye akitoa tabasamu.

“Asante sana, hicho hicho chumba kitanifaa.” Willy alijaza fomu kama ilivyo desturi, kisha akapelekwa na askari wa hoteli mpaka chumbani kwake. Chumba alichokuwa amepewa kilikuwa kwenye sehemu nzuri sana na chumba chenyewe kilikuwa kimepangwa na kuwekwa vyombo vizuri saana. Askari alipokuwa amekwishaondoka, Willy alianza kukipekua kile chumba, na kukikuta salama. Alipokwisha kufanya hivyo alifungua mkoba wake na kuanza kupanga vitu vyake. Alipomaliza alienda akaoga kisha akateremka chini kwenda kupata chakula cha mchana. Alipomaliza kula alipita pale kwa yule msichana wa mapokezi.

“Haya kisura bado unaendelea na kazi!”

“Ndiyo, heri nyinyi wenye bahati ya kutembea nchi mbali mbali na kustarehe. Sijui lini mimi nitapata nafasi kama hii!”, alijibu yule msichana kwa masikitiko.

“Siku ipo itafika usiwe na shaka, ya Mungu mengi sana. Fanya kazi yako kwa bidii, tumia mapato yako kwa mpango, huku ukiweka akiba kwa ajili ya safari kama hii, ukifanya hivi nina imani siku moja ndoto zako za kutembea nchi mbali mbali zitakuja kweli,” alimshauri Willy.

“Ndivyo wewe ulivyofanya?” Yule msichana alimuuliza.

“Lazima, hamna dawa nyingine,” alijibu Willy huku akitoa pesa ili kubadilisha kutoka kwenye dola ili apate Zaire. Msichana yule alipombadilishia pesa zake, Willy alitoa Zaire kumi akampatia yule msichana.

“Za nini?” Yule msichana alimuuliza.

“Asante yako kwa kunipokea vizuri. Wewe unaitwa nani?”

“Naitwa Mwadi,” yule msichana alisema huku akionekana kuwa na mshangao.

“Jina zuri 'Mwadi', haya asnate Mwadi tutaonana jioni”.

“Jioni nitakuwa nimeishamaliza kazi, namaliza saa tisa mchana, hivi nitakuwa nyumbani.”

“Basi tutaonana kesho,”

“Haya asante,” alijibu Mwadi, huku akimwangalia Willy kwa macho malegevu. Willy alipoondoka alimwacha yule msichana moyo wake unapiga haraka haraka. Maishani mwake alikuwa ameishaona wavulana wengi sana, hasa ukitilia maanani kazi yake hii, lakini alikuwa hajaonana na mvulana mwenye kuisisimua kama huyu. Pale pale alijawa na moyo wa kimapenzi juu ya Willy.

Willy naye alienda chumbani kwake na kupumzika.

Baada ya kuondoka nyumbani kwa Pierre, Jean aliendesha gari lake moja kwa moja mpaka kwake 'G.A.D'. Alikuta kazi ya kutengeneza magari inaendelea kama kawaida. Alikaguakagua kazi kisha akawaita faraghani wafanyakazi wake wawili ambao walikuwa wakisimamia kazi. Mmoja aliitwa Kabeya Mwabila na mwingine Charles Besaleti, mwenye asili ya Kibeligiji. “Jamani kuna kazi muhimu”, aliwaeleza. “Tunatakiwa tuchunge kiwanja cha ndege na mahoteli yote kuhakikisha kuwa hakuna mgeni ambaye anaingia mjini hapa bila sisi kuwa na maelekezo yake. Mnaweza kuweka watu wengi mnavyoweza na kutumia kiasi chochote ili mradi jambo hili lishughulikiwe kikamilifu. Kufanyika lifanyike kwa siri kama kawaida kiasi cha kwamba Polisi au CND* haiwezi kututuhumu. Tumeelewana?”. alimaliza Jean.

“Tumeelewa, hilo hamna taabu, litafanyika kwa makini kabisa maana kila hoteli tunaye mtu kwenye orodha yetu ya mshahara ambaye kazi yake ni hiyo kila tuhitajipo maelezo,” alijibu Charles.

“Sitaki kusikia makosa, Kazi hii ifanyike kikamilifu kabisa, watu mnao, pesa zipo, ninachohitaji ni utekelezaji.” Jean aliwatilia mkazo.

“Usitie shaka, kazi itakwenda kama siku zote,” Kabeya alimhakikishia na wote wawili wakatoka ndani ya ofisi ya Pierre tayati kufanya kazi.

CND Idara ya Upelelezi ya Zaire.

“Wewe shughulikia mahoteli na mimi nitashughulikia njia zote za kuingia Kinshasa, hasa uwanja wa ndege na kwenye kivuko cha kwenda Brazaville.” Charles alimshauri mwenziwe.

“Vizuri, mahoteli yote nitayashughulikia mimi na pale patakapokuwa lazima nitapashughulikia mwenyewe”.

“Oke, basi tulishughulikie mara moja”.

Kila mmoja aliondoka na kupita kwa vijana waliokuwa wanashughulikia magari, wakiitwa mmoja mmoja hapa na pale tayari kwenda kwenye shughuli hii maalumu ambayo kimsingi ndiyo ilikuwa kazi waliyoajiriwa. Haya mambo ya kutengeneza magari ilikuwa geresha tu, ili kuivuruga serikali isijue maovu yao.

Ilikuwa yapata saa tisa kasoro robo wakati Kabeya ambaye alikuwa ofisini mwake huku akipiga simu mahotelini kwa wadukuzi wake alipofika Memling Hoteli kwenye orodha yake.

“Hapo ni Memling Hoteli?” aliuliza.

“Ndiyo”.

“Mwadi yupo?” Mwandi ndiye alikuwa kwenye orodha ya mshahara ya 'WP' hapa Memling Hoteli kutokana na habari alizokuwa akizitoa kuhusu wageni. Kwa vile alikuwa akilipwa vizuri kwa kutoa habari ambazo alifikiria hazina madhara, alikuwa anaona kama ni bahati kwa upande wake alipoambiwa na Kabeya kufanya hivyo kwa malipo hayo.

“Ndiyo, yupo subiri”, alijibiwa. Baada ya muda kidogo aliweza kuunganishwa na Mwadi.

“Halo Mwadi hapa”.

“Ohoo Mwadi, Kabeya hapa habari yako?” Moyo wa Mwadi ulistuka kidogo kumsikia ni Kabeya, ingawaje alikuwa anajua habari alizokuwa anazitoa kwa Kabeya hazikuwa mbaya, lakini wakati mwingine alikuwa akiingiwa na wasiwasi hasa kwa vile sura ya Kabeya ilikuwa ikionyesha uovu mwingi sana. Kwa hivi alipopata simu mchana huu kutoka kwa Kabeya moyo wake ulishtuka sana, bila kuwa na sababu kamili.

“Mzuri, habari yako na wewe?”.

“Mzuri tu”.

“Unasemaje, maana mimi namaliza kazi nataka kwenda kupumzika”.

“Nina kazi kidogo tu Mwadi, ile ya kila siku. Naomba unipe majina na maelezo ya wageni walioingia hotelini kwako toka jana hadi leo na vile vile endelea kunipa kwa siku hizi zitakazofuata. Malipo yako yatakuwa mara tatu ya kawaida. Tafadhali maelezo hayo yanahitaji kabla ya saa kumi leo. Yatakuja kuchukuliwa mahali pa kawaida. Sawa Mwadi?” Mwadi ambaye mara moja mawazo yake yalikwenda kwa kijana yule ambaye alikuwa amewasili mchana ule alisita kidogo kisha akasema.

“Sawa Kabeya nitashughulikia”.

“Asante”, alijibu Kabeya na kukata simu.

Mwadi alibaki huku akiwa na wasiwasi, na alikuwa hajui kwa nini roho yake ilikuwa haipendi kufikiria juu ya kutoa maelezo ya huyu kijana Willy Chitalu kwa Kabeya.

“Sijui ni kwa sababu nimempenda?” alijiuliza. Mawazo mengine yalimjia yakiwa yanamshauri kuwa maelezo haya yalikuwa yakitakiwa kwa ubaya ndiyo sababu walikuwa wako tayari kumlipa mara tatu ya kawaida. Hata hivyo moyo wake nao ulikuwa na wasiwasi na Willy maana kijana huyu alimsisimua sana. Mwishoni aliamua kuwa afadhali atengeneze orodha na kumpelekea Kabeya bila ya kina la Willy, kusudi kama maelezo haya yatakuwa kwa ubaya, ubaya huu usije ukamduru kijana huyu ambaye moyo wake ulikuwa umempenda bila kijana mwenyewe kujua. “Afadhali mimi nipate matatizo kuliko yule kijana,” alijisemea.

Ilikuwa saa tatu wakati Willy alipofika Vatican Klabu. Alikuta magari yamejaa kiasi cha yeye kukosa maegesho. Hivi aliondoka na kwenda kugesha gari lake kwenye mtaa wa Kasavubu.

Vatican Klabu ni klabu nzuri sana. Watu wenye heshima zao hufika hapa ili kustarehe. Hamna fujo na kila mtu ambaye anafika hapa inabidi kujiheshimu. Hivi watu wa madaraka Serikalini, makampuni, watu tajiri na mabalozi mara nyingi ndiyo hufika hapa ili kustarehe. Kwa sababu Robert alikuwa akipewa heshima za Kibalozi, mara kwa mara alikuwa akifika kustarehe katika klabu hii ambayo ndiyo ya hali yake. Ingawaje Kinshasa ni mji unaojulikana Ulimwengu mzima kwa kuwa na bendi nyingi zenye ujuzi wa hali ya juu katika mambo ya muziki, lakini Vatican Klabu ni Klabu kubwa ambayo haina bendi bali kuna 'disco'.

Baada ya kuegesha gari lake, Willy alienda moja kwa moja mpaka kwenye lango la ua wa Klabu hii ambapo alifunguliwa na kukaribishwa na askari aliyekuwa pale. Alipita na kwenda mpaka kwenye mlango wa klabu ambao ulifunguliwa na mtu mwingine na kukaribishwa ndani. Ndani ya Vatican Klabu mna nafasi kubwa sana. Wakati unapoingia ndani ya klabu karibu na mlango kuna vyumba vitatu vitatu kila upande. Mbele ya vyumba hivi kuna uwanja wa kuchezea dansi huku ukiwa umezungukwa na sehemu nyingi za kukaa na mbele yake ndipo kuna kaunta ya klabu hii. Hivi Willy alipoingia alikuta watu wameisha jaa alipita akaangalia chumba hadi chumba bila kumuona robert, alipotokea kwenye uwanja wa muziki ambao kwa wakati huo ulikuwa hauna mtu ndipo alipomuona Robert kushooto kwake akiwa amekaa na kijana mwingine. Kwa vile alikuwa hana haja ya kuonana na mtu mwingine ila Robert alikata shauri kwenda kulia kwake ambapo alipata meza iliyokuwa haina kitu na kukaa. Robert alikuwa amemuona alijitafadhalisha kwa kijana aliyekuwa amekaa naye na kuhamia mezani kwa Willy.

“Habari za saa hizi?” Robert alimpa Willy hali.

“Safi tu, naona umeisha wahi kabisa kabisa,” alimtania Willy.

“Ee bwana, chelewa chelewa mbaya,” alijibu Robert kimatani vile vile.

“Robert alimwita mfanyakazi na kumwagiza vinywaji. Yeye alikuwa amehama na kinywaji chake.

“Utakunywa nini Willy?”.

“Anipe Dimple kubwa na Tonic soda.”

“Umesikia, kalete haraka, mimi niongezee Martel”, Robert alimsisitiza mfanyakazi.

“Kabla sijaanza mambo mengi, nimepata habari kutoka Lusaka kwa Chifu, ameniambia nikueleze kuwa Petit Ozu na Mike Kofi watawasili hapa kesho mchana na ndege ya shirika la ndege la Nigeria, ambayo itatua mjini hapa saa nane kamili. Hivi ndizo habari nilizopata.”

“Asante sana, nitawashughulikia watakapofika.” alijibu Willy huku akipokea kinywaji, “Sasa tuendelee unipe hata kama ni kwa muhtasari tu mambo yalivyo hapa.” Robert alisafisha koo kwa kohozi ili apate kueleza vizuri.

“Mimi nimefika hapa mjini Kinshasa toka mwisho wa mwaka jana. Nilijaribu sana kuchunguza kifo cha Meja Komba lakini bila mafanikio. Nimeweza kuwa na

uhusiano na afisa mmoja wa C.N.D ambayo ndiyo idara ya upelelezi ya hapa, ili niweze kupata habari zingine kutokana na upelelezi waliokuwa wameufanya, lakini na wao vile vile hawakuweza kufika popote. Jambo hili liliweza kunifanya nihisi mambo mawili, aidha Komba alikuwa ameuawa kwa mpango ambao Serikali iliujua kikamilifu au alikuwa ameuawa na kikundi cha kijasusi ambacho ni chenye ujuzi wa hali ya juu. Hili jambo la kwanza nililitilia wasiwasi maana baada ya kufanya upelelezi sana ilionekana uliokuwa umefanywa na Serikali ya Zaire ulikuwa umefanywa kwa dhati na kiukweli.

Hivi nilibaki na jambo la pili ambalo nimekuwa nalifanyia upelelezi bila kufika popote hadi hapa majuzi ndugu Mongo alipouawa. Suala hili la kuwepo kwa kikundi cha ujasusi kinachoendesha uovu limeweza kuthibitika kwangu kutokana na mauaji haya ya juzi. Tatizo lililopo hapa Kinshasa ndugu Willy ni kwamba, nchi hii ina watu wa nje wengi na inafanya biashara na nchi nyingi sana hata Afrika ya Kusini na Rhodesia. Hivi ni rahisi sana kwa majasusi wa kutoka nchi hizo kuweza kuingia nchini hapa na kufanya uovu kama huo. Kwa mfano katika upelelezi wangu nimekuta kuwa kila mwaka Zaire inapata bidhaa toka Afrika Kusini zenye zaidi ya thamani ya R40m. Vitu hivi hutumwa kupitia Rhodesia na Zambia kwa Reli na kwa bahari mpaka Matadi.

Lakini vile vile bidhaa nyingine inaingia Zaire kwa njia ya barabara kwa kupitia Rhodesia na Zambia. Kwa mfano hivi karibuni kumekuwa na mkataba kati ya Zaire na Rhodesia ambapo malori makubwa kiasi cha mia mbili yanaingia Zaire kutoka Rhodesia kila mwezi. Mia moja na ishirini ya malori hayo hubeba makaa ya mawe na yaliyobaki hubeba mahindi. Kutokana na mipango kama hii ni rahisi sana kwa majasusi ya Afrika Kusini na Rhodesia kuingia mjini hapa wakiwa aidha kama madereva wa magari haya au makarani. Vile vile utakuta kuwa kampuni za Afrika Kusini za biashara ziko na wakala wao hapa mjini Kinshasa. Kwa mfano Zaire ina mpango wa kupeleka bidhaa yake Japan kwa kupitia Afrika Kusini, na mkataba wa tani 125,000 za shaba ziendazo huko Japan kwa mwaka ulitiwa saini ya kusafirisha tani hizo kupitia kampuni moja iitwayo Grindrod Cots Stevedoring iliyoko mjini East London, Afrika Kusini.

Kampuni hii ina wakala wake mjini hapa. Kutokana na ukweli wa mambo haya ulivyo ni wazi kuwa, ni rahisi sana kuwa na ukanda wa kijasusi wa Afrika Kusini ukifanyakazi yake hapa unapona ya kuwa watu wanaouawa ni wale wenye uhusiano na wapigania uhuru wa Kusini mwa Afrika. Kutokana na hali hii mimi

ningeshauri tuanze upelelezi mkali kwa watu wa makapuni haya yenye asili ya Afrika Kusini”, alimalizia Robert.

Willy ambaye alikuwa amesikiliza maneno yote haya kwa makini alimuuliza, “Marehemu Mongo alikuwa amefikia hoteli gani?”

“Intercontinental hoteli”, Robert alijibu.

“Uliwahi kukagua vyombo vyake uliposikia ameuawa?”.

“Ndiyo, nilifika pale nikiwa pamoja na ofsa huyu wa C.N.D. Kusema kweli tulikuta chumba kile kimepekuliwa sana ingawaje kwa ustadi ambao mtu wa kawaida hawezi kugundua. Hatujui mtu aliyekuwa amekipekua alitaka nini au alichukua nini sababu hatukuona kitu cha maana kilichochukuliwa. Vitu vyake vingi hata zile karatasi za maelezo ya mkutano wa Libreville tulizikuta. C.N.D wamejaribu kupata alama za vidole bila mafanikio. Hii ina maana kuwa walitumia mifuko ya mikono 'gloves', Baadaye siku ile nilifanya upelelezi wangu kwa watu kadhaa na pale Intercontinental ambao walikuwepo tokea Ndugu Mongo anawasili pale kama waliwahi kuona kitu chochote cha kutilia mashaka lakini hawakunipa jambo lolote la maana.

“Alikuwa akilala chumba namba ngapi?”, Willy aliuliza.

“Nambari 501”.

“Hili gari marehemu alikuwa amepewa na nani?”.

“Lilikuwa la Wizara ya Mambo ya Nchi za nje”.

“Alikuwa akiendesha mwenyewe?”.

“Wakati alipopatwa na ajali alikuwa mwenyewe”.

“Jaribu kupeleleza ni wakati gani alipewa hilo gari. Na kabla ya kupewa hilo gari lilikuwa wapi. Ni mahala gani alipokuwa ameliegesha, na kama kuna mtu maalumu aliyelishughulikia gari hilo kabla marehemu hajapewa. Kwani alikuwa na muda gani Kinshasa tangu kufika kwake hadi kuuawa?”.

“Yeye aliwasili hapa saa nne za usiku, kesho yake saa tano ndipo alipopatwa na ajali hii,” Willy alifikiri sana kisha akasema.

“Vizuri Robert, nitaenda kuyafikiria maelezo yote uliyonipa usiku huu na uamzi wangu nitakueleza kesho nini tufanye. Umekuwa ukifanyakazi na maelezo yako ni ya kufaa sana. Mazishi yatakuwa kesho saa ngapi?”.

“Saa nne asubuhi, na atazikwa kitaifa”, Robert alijibu.

“Mimi nitahudhuria mazishi”.

“Na mimi nitakuwepo”, alijibu Robert.

“Kwa hiyo tuta...”, Willy alikatwa kauli na jamaa mmoja aliyefika kwenye meza yao akiwa ameandamana na msichana mmoja.

“Halo Robert, habari za leo?”

“Oho Kalenga, habari zenu, karibu bibie”, Robert aliwakaribisha hawa watu.

“Asante asante,” alijibu Kalenga huku akikaa.

“Willy onana na Bwana na Bibi Kalenga Mbizi. Bwana Kalenga ni Meneja Maslahi katika kampuni ya Fiat, yeye ndiye aliyenifanyia mpango wa kununua gari yangu ya Fiat 132 GLS. Na huyu ni ndugu willy Chitalu kutoka Lusaka, yeye ni mfanyabiashara. Ni wakala wa makampuni ya nchi za nje katika Zambia”, Robert aliwafahamisha.

“Vizuri kuonana”.

“Vizuri kuonana”, walijibishana.

Pombe ziliagizwa na muziki ulianza kuwa moto moto, hivi kundi hili likageuka kutoka mazungumzo waliyokuwa nayo na kuwa kundi la starehe, maana saa hizi watu wa kila aina wliojuana na Robert walipoingia walienda kukaa kwenye meza hiyo hiyo.

SURA YA SITA

ASUBUHI yake Willy alipoamka alikuwa mchovu sana, maana usiku ule alikunywa pombe za kutosha, kwani walikaa Vatican mpaka saa saba za usiku huku wakinywa na kucheza dansi. Alipoangalia saa yake alikuta ni saa moja unusu, basi aliamka na kuelekea maliwatoni. Baada ya kukoga, alinyoa ndevu, kisha akavaa vizuri kabisa na kuonekana mtu wa amani, tayari kamili kwa shughuli za siku hiyo. Kisha aliteremka chini ili kuwahi chemsha kinywa. Alipokuwa anapita pale mapokezi alimwona Mwadi tayari yuko kazini, hivi aliamua kumsabahi.

“Hallo Mwadi, Sango nini?”, alimsabahi kwa kilingala kiutani. Mwadi ambaye alikuwa akishughulika na kujaza rejesta ya wageni aliinua kichwa na kumwona Willy, alipomuona tu mwili wake ukasisimka.

“Ohoo Willy malamu”, alimjibu huku akiwa amemjengea tabasamu kubwa. Willy alirudisha tabasamu hilo na kuendelea zake kwenda kwenye chumba cha chakua.

Baada ya kustafutahi, Willy alirudi chumbani mwake, akajitayarisha tayari kwa kwenda kwenye mazishi.

Ilikuwa saa tatu kamili alipotoka hotelini kwake kuelekea mazishini. Alipopita pale mapokezi alimkuta Mwadi akiwa na shughuli nyingi hivi alienda akapanda gari lake na kuondoka. Robert alikuwa amemwambia kuwa mazishi yatafanyika kwenye makaburi yaliyoko mtaa wa 30 Juin. Alipofika kwenye makaburi haya alikuta watu wamejazana kibao. Alirudi nyuma na kuegesha gari lake kwenye maegesho ya jengo liitwalo INSS. Alipomaliza kufunga milango alirudi na kuja kungojea maiti pamoja na wananchi wengine.

Kusema kweli mazishi haya yalikuwa yametayarishwa kitaifa. Kulikuwa na gwaride la askari wa jeshi la Zaire, wakiwa tayari kutoa heshima zao za mwisho kwa marehemu huyu ambaye alikuwa mwanamapinduzi imara wa Afrika. Ilipokaribia saa nne, watu wenye vyeo vikubwa wakiwa mawaziri, mabalozi na viongozi wengine wa serikali waliwasili. Saa nne kamili ndipo maiti ya marehemu ilipofika. na pale pale bendi ya jeshi ikaanza kupiga wimbo wa kimapinduzi ambao uliwafanya maelfu ya wananchi waliofika kutoa heshima zao za mwisho kwa marehemu wakitokwa na machozi. Mkuu wa majeshi ndiye aliongoza mazishi haya ambayo hayatasahaurika katika historia ya mjini Kinshasa.

Uchungu huu uliwapata hawa wananchi wa kawaida mpaka wale watu wa vyeo vya juu waliohudhuria mazishi haya, ndiyo uchungu ule ule uliompata Willy. Kwani mtoto mmoja aliyekuwa amesimama karibu na Willy alimuuliza, “Mzee kama mtu huyu alikuwa anapendwa na watu wote hivi kwanini wamemuua”, Willy alimwangalia mtoto huyu asiyezidi umri wa miaka nane akajibu, “Mtu hakosi adui, unaweza kupendwa na watu maelfu lakini ukachukiwa na mtu mmoja tu”.

“Kama ndio hivyo kwanini watu wengi hawa wasimpate mtu huyo na kumuua? Maana mama ameniambia asubuhi eti mtu aliyemuua hawamjui!”

“Tutamtafuta tukimpata tutamuua vile vile”, alijibu Willy huku akizidi kupandwa na uchungu.”

“Kweli, ukimpata ukamuua nitafurahi.” Yule kijana alijibu. Mtoto huyu alimzidishia mawazo Willy hivi akaamua kutoka pale na wazo moja.

Ampate huyu muuaji wa Mongo, amue ili watoto wa Afrika waweze kufurahi na kuzidisha mapambano dhidi ya wapinga maendeleo. Kwa sababu watu walikuwa wengi sana aliona kuwa asingeweza kuona jambo lolote la maana hivi akaamua kurudi hotelini kwake ili akajitayarisha kwenda kuwapokea akina Ozu.

Alipofika hotelini alimkuta Mwadi akiwa peke yake.

“Hallo Willy, ulitoka saa ngapi? Maana sikukuona wakati ukitoka”.

“Wakati ninatoka ulikuwa na shughuli nyingi usingeweza kuniona”, alijibu Willy huku kwa mara ya kwanza tangu amuone Mwadi alianza kutambua kuwa msichana huyu alikuwa na kitu fulani ambacho kilikuwa kinagusa moyo wake. Si kwamba Mwadi alikuwa msichana mzuri sana la hasha, alikuwa msichana mzuri kiasi cha kawaida tu, lakini kitu hiki alichokuwa nacho kilichokuwa kikigusa moyo wa Willy, kilimfanya Willy amue kuwa karibu na msichana huyu ili aweze kukijua ni kitu gani hiki.

“Ulishawahi kufika Kinshasa au hii ni mara yako ya kwanza?”, Mwadi aliuliza.

“Nilishawahi kufika ingawaje sikukaa sana”. Alijibu Willy. “Ahaa...” Mwadi alionekana anataka kusema kitu, halafu akasita.

“Leo unatoka saa ngapi?”. Aliuliza Willy. Huku macho yake yakitoa mwanga wa kuonyesha furaha ya kuulizwa swali hili Mwadi alijibu, “Kama jana tu, nitaondoka saa tisa na kuingia tena kesho asubuhi saa moja”.

“Una muda mwingi sana wa kupumzika”, alisema Willy halafu akatania, “Sijui nani anakusaidia kuusukuma muda wote huo?”.

“Aka, sina mtu maalumu anayenisaidia kuusukuma muda wangu. Hata wewe unaweza kusaidia kuusukuma ukitaka!” Alijibu Mwadi kwa sauti ya utani. Willy aliona hapa hapa ndiyo ulikuwa muda wa kuanzisha urafiki na huyu msichana.

“Na kweli kabisa, maana sina msichana wa kusaidia kuusukuma muda wangu hasa ukitilia maanani kuwa mimi niko mapumzikoni ingawaje na kazi”.

“Karibu basi nyumbani jioni, nitakupikia 'Maboke'. Umeisha kula maboke ya hapa Kinshasa?”. Aliuliza Mwadi.

“Kwanza sijui maboke ni nini”, alijibu Willy.

Mwadi aliangua kicheko kisha akasema, “Hii inaonyesha kuwa kweli bado hujafahamu Kinshasa. Maboke ni chakula kinachopendwa na watu wote hapa mjini, ni samaki na nyama ambayo hupikwa ndani ya majani ya ndizi. Vipi utakuja?”.

“Nitakuja”, alijibu Willy, “Sijui unakaa wapi?”

“Ninakaa huko Bandalugwa mtaa wa Kimbondo nyumba nambari 79, utapajua?”.

“Usiwe na shaka nitakuja, nisubiri saa moja hivi jioni”.

“Haya asante, tutaonana saa hizo”, alijibu Mwadi kwa moyo wa kuridhika sana, maana alikuwa ameweza kirahisi sana kumpata kijana huyu ambaye alikuwa akimsisimua sana.

Ilikuwa saa saba kamili, Willy alipoingia ndani ya baa ya uwanja wa ndege wa Ndjili wa mjini Kinshasa, tayari kuwapokea akina Ozu. Ndani ya baa mlijaa watu wengi waliokuwa wakisubiri wageni wao. Willy aliamua kwenda kwenye kaunta ambapo aliagiza kinywaji. Ilipotimia saa saba unusu Robert naye aliingia ndani ya baa hii na alipomuona Willy alimfuata moja kwa moja.

“Vipi umeshafika huku?” Robert alimuuliza Willy.

“Bila shaka nimefika ndiyo sababu niko huku”. Alijibu Willy kimatani.

“Salama lakini?”.

“Salama tu”.

“Vipi ulifika kwenye mazishi?”.

“Ndiyo nilifika, lakini watu walikuwa wengi mno sikukaa sana”.

“Lo, kweli marehemu kazikwa kishujaa kweli kweli. maelfu ya wananchi wamehudhuria mazishi. Watu wamesema yalikuwa mazishi ya kihistoria.”

“Hata mimi sijawahi kuona mazishi kama haya”, alijibu Willy.

“Juu ya mambo yale uliyoniagiza jana. Marehemu alipewa gari lile asubuhi ya siku ile aliyowawa saa mbili hivi. Hili gari lilikuwa limetoka matengenezo siku hiyo hiyo.”

“Gereji gani?”. Aliuliza Willy kwa sauti nzito.

“Gereji moja iitwayo Papadimitriou, ambayo ni kati ya nyingi maarufu zinazotengeneza magari aina ya Peugeot hapa mjini Kinshasa”.

“Una maana gari alilokuwa anatumia marehemu ilikuwa aina ya Peugeot?”.

“Ndiyo ilikuwa Peugeot 504. Na inasemekana kuwa marehemu hakuwa ameliweka mahali popote kwa muda mrefu kiasi cha mtu kuweza kulifanyia mbinu za namna hiyo. Lakini ukifikiria teknolojia ilivyo kwa sasa hivi inaweza kumchukua mtu muda mfupi sana kutega bomu kwenye injini ya gari.”

“Hii gereji ni ya nani?”.

“Gereji hii ni ya Mpakistani mmoja tajiri sana aitwaye Papadimitrian. Ni mtu anayeheshimika sana hapa mjini, na ana mahusiano mazuri na Serikali, sababu magari mengi ya serikali yanatengenezwa kwake.”

“Ni mzaliwa wa wapi?”.

“Ni mzaliwa wa Pakistani, lakini ameingia hapa kwa kutokea Zambia ambako alikuwa akifanya biashara”, Hata mimi nakumbuka kuwa alikuwa na duka kubwa sana la nguo mtaa wa Cairo mjini Lusaka. Yeye aliingia hapa mwaka 1968 na kabla ya kuwa na gereji hii alikuwa na duka kubwa la madawa huko Gombe mtaa wa Posta. Kwa ujumla ni mtu mwenye sifa nzuri na hana rekodi yoyote mbaya”.

“Sikuwa na maana kuwa anaweza kuwa na ubaya, ila tu nilitaka kuwa na uhakika na gereji hii ni ya namna gani.”

“Ni sawa kabisa kumtilia mashaka maana jambo hili lilipotokea hata mimi ilinibidi niwe na uhakika na gereji hii kabla sijaendelea popote.” Mara walikatwa kauli na tangazo.

“Tafadhali sikilizeni, tunawatangazia kuwasili kwa ndege ZC 883 ya Shirika la Ndege la Nigeria itokayo Logos na kupitia na kisha kuelekea Libreville na kisha kuelekea Brazaville. Abiria wote wanaoondoka na ndege hiyo wanaombwa kuelekea kwenye chumba cha kuondokea. Asanteni.

“Hao wanaingia, je wewe unawafahamu?” aliuliza Robert.

“Ndiyo, kwa picha. Wewe je?”.

“Mimi siwafahamu ila nilifikiri kuwa utakuwa unawafahamu ndiyo sababu nimekuwahi.” Waliondoka na kuelekea sehemu ya kuagiza 'waving bay', watu walikuwa wamejazana sehemu hii. Willy na Robert walijipenyeza na kuiangalia ndege hii ya aina ya DC 8 ikishuka taratibu.

Wakati ndege hii ya Shirika la Ndege la Nigeria ikiteremka, huko Limete kwenye gereji iitwayo 'Garage du Peuple' aliingia kijana mmoja wa kizungu ambaye alionekana kuwa na wasiwasi sana.

“Bwana Pierre yupo?”, aliuliza.

“Ndiyo yupo. Nenda moja kwa moja ndani”. Alimjibu kijana mmoja aliyekuwa mlangoni. Alipofika ndani ya maofisi ya gereji hii, alimwendea msichana mmoja aliyekuwa anapiga mashine na kumweleza.

“Nataka kumwona Bwana Pierre.”

“Nenda chumba cha tatu toka hiki upande huu huu.” Alijibiwa. Alipoingia hiki chumba alikuta kuna wasichana wawili ambao alihisi ni waandishi mahsusi wa Pierre.

“Bwana Pierre yupo.” Aliuliza bila hata kuwasabahi.

“Yupo. Unamhitaji kwa jambo gani?”. Aliulizwa na msichana mmojawapo.

“Mwambie nimetumwa na wakala.”

“Yule msichana aliinua simu na alipokwisha kuzungumza na Pierre alimwambia apite ndani.

“Karibu, lete habari,” Pierre aliuliza upesi upesi kijana yule alipoingia. Bila kujibu kitu kijana yule alitoa karatasi ya teleksi na kumpa Pierre. Pierre alipoisoma sura yake ilibadilika akasema,

“Haya asante kwa heri”. Kwa maneno haya ya mkato yule kijana aliondoka. Pierre aliinua simu na kuanza kupiga yeye mwenyewe moja kwa moja.

“Jean”.

“Ndiyo”.

“Pierre hapa”.

“Ehe”.

“Nimepata habari, kutoka Wakala. Wamesema habari kutoka kwa wateja wetu wanasema kuna spea zinawasili hapa toka Nigeria kwa ndege ya shirika la ndege la Nigeria ambayo inaingia sasa hivi tunavyozungumza. Ni spea za aina mbili. Moja ni ndefu kama futi 5inchi 10, nyeusi, imefunikwa kwa suti nyeusi. Nyingine nayo ni ndefu futi 5 inchi 6, maji ya kunde, imefunikwa kwa suti nyeusi vile vile. Spea hizi ni za hatari sana lazima zikaangaliwe zinapelekwa duka gani ili iwe rahisi kuzinunua. Kwa sababu ni za hatari, lazima watu wenye ujuzi wa juu ndio wapelekwe kuzitambua. Umenielewa?”

“Hakuna taabu, tayari nina watu wenye ujuzi wa hali ya juu katika spea huko uwanja wa ndege nitawapasha habari mara moja”.

“Wapashe habari mara moja, maana saa zenyewe ni hizi”.

“Oke, nitapiga baada ya kuwapasha habari,” alijibu Jean na kukata simu.

Wakati mlango wa ndege unafunguliwa ili abiria wapate kutoka ndani ya ndege, Mtu mmoja ambaye ni mfanyakazi wa Idara ya Uhamiaji ya Zaire alikuwa akipokea simu. Mtu huyu alikuwa kwenye orodha ya mishahara ya 'WP' kwa ajili ya kutoa habari na vile vile kuwa kiungo kati ya ofisi ya 'WP' na wafanyakazi wa 'WP' ambao wanaweza kuwa kiwanjani. Mtu huyu alikuwa akipata maagizo moja kwa moja kutoka kwa Charles wa G.A.D. gereji. Hivi simu hii aliyokuwa ameipokea ilikuwa imetoka kwa Charles ikiwa na maagizo kwa wafanyakazi wawili wa 'WP' ambao walikuwa wamepelekwa hapo uwanja wa ndege ili kuchunguza watu wote waliokuwa wakiingia Zaire kwa njia ya ndege. Baada ya kupata simu hii aliinuka na kupanda ngazi haraka haraka kwenda kwenye sehemu ya kuagia ambapo alijua ndipo Mulumba mmoja wa wafanyakazi wa 'WP' waliokuwa hapo uwanjania alikuwa. Watu walikuwa wengi sana, lakini kwa bahati Mulumba alikuwa amesimama kando kwenye sehemu ambayo mtu alimwona moja kwa moja.

“Mulumba, nina maagizo yako”, huyu mtu alimwambia alipofika.

“Nitakuja ofisini kwako,” Mulumba alijibu.

“Ni ya haraka sana inatoka kwa Charles.” Alimweleza huku akimvuta kando.

“Ehe anasemaje?”.Mulumba aliuliza kwa makini.

“Kati ya watu wanaoteremka ndani ya ndege hii, mna wapelelezi wawili mashuhuri wa Afrika. Mmoja ni mweusi kiasi cha futi 5 inchi kumi kwa urefu amevaa suti nyeusi na mwenzie ni maji ya kunde kiasi cha futi 5 inchi 6 nae amevaa suti nyeusi. Wanatoka Lagos Nigeria. Anasema ni watu ambao hamuwezi kuwakosa, lazima mtawatambua. Vile vile ameonya kuwa ni watu hatari sana hivi msiwafanyie jambo lolote ila tu muwafuatie mjuwe wamefikia wapi na mripoti moja kwa moja kwake. Vile vile lazima mlinde mahali watakapofikia mpaka hapo watu wengine watakapokuja kuchukua nafasi zenu. Amesema kuwa msiwaache wakawapotea hata kidogo hiyo ni amri.”

“Oke, hao abiria wanaanza kutoka, nenda kwenye chumba cha kufikia ukamweleze Kasongo yuko huko”, Mulumba alieleza.

“Oke, bahati njema”, Mulumba alijiweka sawa kwenye nafasi ambayo angeweza kuona vizuri kila abiria anayeteremka bila kujua kwamba hatua tu kwenye jukwa hilo hilo walikuwa wamesimama wapelelezi mashuhuri wa Afrika waliokuwa wamefika kungojea watu wale wale ambao yeye naye alikuwa akiwangojea.

Willy na Robert walikuwa wakiwaangalia abiria waliokuwa wanateremka kwa makini sana vile vile bila kujua kuwa hatua chache tu kutoka sehemu waliyosimama kulikuwa na mtu wa 'WP' kikundi ambacho ndicho alikuwa hasa ametumwa kuja kukitafuta.

“Huyo ni Kofi”, Willy alimweleza Robert wakati kijana mmoja aliyevalia suti nyeusi na huku akitembea kifahari alipokuwa akiteremka kutoka katika ndege.

“Ahaa,” aliitikia Robert huku akimwangalia Kofi kwa makini ambaye alikuwa akielekea chumba cha kufikia pamoja na abiria wenzake. Ozu ndiye alikuwa mtu wa mwisho kuteremka ndani ya ndege, na mara alipojitokeza tu Willy alimtambua na hata Robert ambaye alikuwa bado hajawahi kumwona alihisi ya kuwa huyo ndiye alikuwa Ozu kutokana na miondoko yake ilivyokuwa.

Mulumba naye alipomwona Ozu naye alihisi mara moja kuwa ni mmojawapo wa watu aliokuwa ameelezwa, ingawaje Kofi aliteremka bila yeye kumtambua. Hivi

baada ya kumhisi huyu mtu Mulumba aliteremka upesi upesi ili akambonyeze Kasongo kuwa amemtambua mtu huyu.

“Huyo ndiye Ozu”, Willy alimweleza Robert.

“Hata mimi nilihisi ndiye yeye, miondoke na umbo lake la kimwanariadha limemfanya aonekane waziwazi”.

“Teremka chini tukawasubiri,” alishauri Willy wakaanza kuteremka.

“Mpango utakuwa ka ule uliofanya. Sisi tutabana mahali ambapo mtu yeyote hatatuona na kuwaacha watangulie kuondoka, halafu sisi tutawafuata. Mimi nitatangulia wewe utanifuata nyuma. Kama kutatokea kitu chochote cha kutaka cha kutaka wewe usihusike nitatoa mkono wangu nje na kuuonyesha juu. Nikifanya hivyo nipite moja kwa moja ukanisubiri hotelini. Na kama kuna kitu nataka tusaaidiane nitatoa mkono wangu nje na kuuegesha kwenye dirisha, nikifanya hivyo jiweke katika hali ya tahadhari,” alishauri tena Willy.

“Kwani unadhani kitu chochote kinaweza kutokea?”. Aliuliza Robert.

“Huwezi kujua maana inabidi ujuwe kuwa Ozu na mwenzake ni wapelelezi mashuhuri”.

Ozu ambaye aliteremka mwisho alifanya hivyo kwa sababu maalumu. Alikuwa amevaa miwani, na miwani hii haikuwa ya kawaida ingawaje ilionekana kama miwani ya jua ya kawaida. Miwani hii ilikuwa na kioo maalumu kinachovuta vitu vilivyo mbali na kuvileta karibu. Hivi Ozu alipotokea kwenye mlango wa kutokea wa ndege aliweka miwani hii na kuangalia moja kwa moja kwenye jukwa ambapo watu wanasubiri wageni hukaa. Na mara moja aliweza kutambua kitu ambacho alikuwa akihisi. Baada ya kutambua kitu hiki alitoa hiyo miwani na kuendelea kuteremka ngazi za ndeeg.

Mulumba ambaye aliingia ndani ya chumba cha kufikia wasafiri, alionekana mtu mwenye wasiwasi sana na mara Kasongo alipomwona katika hali hii alijua lazima kuna kitu hivi alimsogelea.

“Vipi?”, Kasongo aliuliza.

“Nimemtambua mmoja wao lakini mwingine bado, kwa sababu wako safari moja itakuwa rahisi kuwatambua. Maana itabidi wawe pamoja”, alijibu Mulumba.

“Kwa hiyo tuwe macho na huyu mtu uliyemtambua, tusimuachie hata kwa dakika moja”.

“Huyo anaingia”, Mulumba alimtambulisha Kasongo.

Kasongo alimwangalia kwa chati kijana huyu ambaye alipita sehemu za uhamiaji bila wasiwasi wowote. Walijaribu kuchunguza katika abiria wote kama wangeweza kumtambua huyu wa pili ambaye alikuwa ameelezwa, lakini bila mafanikio, kwani kulikuwa na abiria wengi waliokuwa na maelezo sawa na yale yaliyotolewa juu ya mtu huyu wa pili, hivi ilikuwa vigumu sana kumtambua.

“Itabidi tumg'ang'anie huyu ndiye atatuonyesha huyu wa pili”, alishauri Kasongo.

“Sawa, twende nje tukamsubiri kule”, Mulumba alikubaliana/

“Hapana siye tukae hapa hapa kwenye makochi kwa vile tutaona kila kitu nje itakuwa rahisi kumwona na atakapochukua gari ndipo sisi tutamfuata bila mtu kushuku”, alishauri Kasongo.

Mulumba alikubaliana na jambo hili wakaketi kwenye makochi kama watu wengine waliokuwa wakisubiri wageni.

Willy na Robert walipoteremka chini walienda moja kwa moja mpaka kwenye chumba cha kupokelea wageni ambao husafiri ndani ya Zaire tu. Walichagua sehemu hii maana ilikuwa sehemu nzuri ambayo mtu anaweza kuangalia mambo yote yanayoendelea kwenye sehemu ya nje ya uwanja wa ndege, na vile vile kuangalia kitu kinachofanyika ndani ya chumba cha kupokelea wageni watokao nchi za nje. Maana sehemu zote hizi ni vioo vitupu. Hivi Willy na Robert walipoingia walichanganyikana na kundi la watu ambao walikuwa wamefika kuwapokea ndugu zao lakini macho yao yakiwa katika tahadhari ya kuangalia mambo yote ambayo yangeweza kutokea hapo nje.

Bila kujua nini kinatendeka. Kofi alikuwa katika kundi la kwanza lililomaliza kukaguliwa. Akiwa katikati ya kundi hili la wenzake aliweza kuingia kwenye chumba cha kupokelewa na kisha kutoka nje bila ya Mulumba na mwenzake kumtambua ingawaje alipita mbele yao. Kofi na Ozu walikuwa wamepanga kuwa wafikapo Kinshasa kila mtu achukue njia yake ila tu waonane baadae wakishafika mjini. Kwa sababu hawakuwa wageni sana mjini Kinshasa jambo hili lilionekana safi kabisa kiusalama.

Wakati Kofi anatoka nje, Willy na Robert alimwona, “Huyo Kofi anatoka”, Robert alimweleza Willy ambaye alikuwa akiangalia mambo mengine. Walimwangalia Kofi ambaye alikuwa pamoja na abiria wengine, akienda na kuingia ndani ya tekisi

iliyokuwa karibu na kuondoka huku wakipita mbele ya Willy na Robert kuelekea mjini. Willy alichukua namba ya tekisi na kuiweka kichwani.

“Ngoja mimi nimfuate Kofi, halafu wewe utamfuata Ozu akitoka maana naona wamekata shauri kila mmoja wao kuchukua njia,” Robert alishauri.

“Hapana tusiwe na haraka tumsubiri Ozu mpaka naye atoke”, Willy alieleza.

Ozu ambaye kama nilivyokwisha eleza hapo nyuma alikuwa amevuta sura za watu waliokuwa jukwaani wakati anateremka katika ndege kwa miwani yake, na katika sura zilizokuwa hapo sura tatu kati ya hizo alizitilia mashaka kwani macho ya sura hizi yalionekana yakimwangalia yeye moja kwa moja. Naye mara moja sura hizi akaziweka kichwani mwake, hivi alipomaliza kukaguliwa na kuingia kwenye chumba cha kupokea wageni, alizungusha macho yake kwa chati kwa watu wote waliokuwa humo. Macho yake yalipomwangalia Mulumba yalimtambua moja kwa moja lakini wale wengine hakuweza kuwatambua. Hivi akijifanya kama hakuna kitu aliendelea na abiria wenzake na kutoka nje. Baada ya Ozu kutoka nje. Mulumba na Kasogo walisimama na kwenda hadi karibu na mlango na kumwangalia Ozu ambaye alikuwa akizungumza na dereva wa tekisi. Kisha alipanda ndani ya tekisi na kuondoka kuelekea mjini.

Willy na Robert nao walikuwa wakimwangalia Ozu kwa uangalifu kabisa. Baada ya gari la Ozu kuzunguka na kupita mbele yao tayari kwa kuelekea mjini walikata shauri kutoka nje ili wapate kumfuata. Walipokuwa wakifungua mlango ili watoke, waliona watu wawili nao wanafungua mlango wa chumba cha kupokelea wageni watokao nchi za nje na kutembea haraka haraka nusu wakikimbia kuelekea kwenye maegesho ya magari.

“Hebu ngoja,” Willy alimsukuma kidogo Robert na kurudi ndani, “Unawaona wale watu?”

“Ndiyo,”

“Hebu tuone wanataka kufanya nini”.

Watu hawa walikuwa ni Mulumba na Kasongo ambao waliingia ndani ya gari lao na kuondoka kwa kasi sana kumfuata Ozu.

“Sasa Robert itabidi tuondoke ndani ya gari moja, maana inaonekana watu wawili wanamfuata Ozu kutokana na jinsi walivyoondoka. Unasemaje?”.

“Sawa, twende zetu tusije tukawapoteza. Lo, kweli subira huvuta heri.”

Willy na Robert waliingia ndani ya gari la Willy alilokodi na kuondoka zao kuwafuata hawa watu waliotangulia.

Mulumba na Kasongo walikwenda kasi kwenye hii barabara ya P.E. Lumumba ili wapate kuisogelea teksi iliyokuwa imembeba Ozu. Ingawaje magari yalikuwa mengi wakati kama huu wa mchana lakini walifanya kila ujuzi kuyapita magari mengine na kulisogelea gari la Ozu. Walipokuwa wameacha gari moja kati ya gari lao na gari la Ozu, walituliza mwendo wao na kufuata wakiwa nyuma ya gari hili jingine.

SURA YA SABA

OZU ambaye wakati wanaondoka uwanja wa ndege alipata fursa kumwona tena huyu kijana aliyekuwa amemwona kwenye jukwa akiwa amesimama kwenye mlango wa kutokea ndani ya chumba cha kupokelea wageni watokao nchi za nje, alihisi kuwa lazima alikuwa anafuatwa hivi mara kwa mara aliangalia nyuma kuona kama kulikuwa na mtu aliyekuwa anafuata.

Willy na Robert nao walitumia kila ujuzi wao mwenye msululu huu wa magari mpaka wakawa wameacha magari mawili kati yao na gari la akina Mulumba na kutuliza mwendo wao.

“Hawa watu ni watu gani?” Aliuliza Robert.

“Tutajua tu, usiwe na haraka”, alijibu Willy bila wasiwasi.

Walipokaribia njia panda ya barabara ya P.E. Lumumba na barabara ya 'Poids Lourds', Ozu ili kusudi aweze kuhakikisha kama kweli anafuatwa alimwambia dereva tekisi.

“Tuingie barabara ya 'Poids Lourds'.

“Likambo te!” Alijibu tekisi dereva katika Kilingala, maana yake 'hamna taabu', na kuonyesha taa za gari kuwa anachepuka kuingia barabara nyingine. Mulumba na Kasongo kuona hivi nao wakaonyesha taa kuwa na wao walikuwa wanachepuka kuingia barabara hiyo.

“Kwanini anaingia barabara hii?”, Kasongo aliuliza.

“Kaa macho, huyu mtu ujue ni mpelelezi maarufu kama tulivyoielezwa kwa hivi ni mtu hatari anaweza kuwa ametuhisi, hivi anatafuta njia ya kujihami. Hivyo weka bastola yako tayari, maana hii barabara haina watu wengi ni ya upweke sana, anaweza kuanzisha kitu chochote”, alieleza Mulumba huku akiwa na wasiwasi kidogo.

Willy na Robert walipoona gari la Ozu na la hawa watu wengine yakichepuka na kuingia Poids Lourds hawakuwa na budi ila nao kuingia barabara hii.

“Kwanini Ozu anaingia barabara ya upweke namna hii na huku anafuatwa?”. Aliuliza Robert.

“Inawezekana amehisi kitu na anataka kuhakikisha,” alijibu Willy huku akiwa tayari ameingia ndani ya barabara hii ya Poids Lourds.

“Lakini barabara hii ni ndefu sana na ya upweke sana kiasi kwamba jambo lolote likikutokea kupata msaada ni vigumu.”

“Ngoja tuone nia yake ya kufanya hivi ni nini”.

Ozu alipoona magari mawili yanamfuata nyuma huku yakiwa yameweka umbali ambao hayakuwa yanauzidi kati yao, aliridhika kuwa alikuwa anafuatwa na vile vile alihakikisha kuwa wale watu wawili aliokuwa amewaona kwenye jukwaa lakini hakuwa amewaona ndani ya chumba cha kupogkelea wageni, nao walikuwa wanamfuata ndicho kisa cha kuwepo magari mawili yakifuatana. Alifikiri afanye nini, lakini moyo wake ulimkataza asifanye chochote maana upinzani ungekuwa mkali sana kwake. Hivi akaamua kuendelea hivi hivi mpaka mjini ambako huenda angeweza kupata nafasi ya kuwakwepa watu hawa. Kwa hiyo alimwambia dereva, “Hebu ongeza mwendo kwa kadri ya uwezo wako”.

“Barabara hii ina mashimo mengi sana lakini nitajitahidi”, alijibu dereva huku akiongeza mwendo.

Mulumba na Kasongo walipoona gari iliyombeba Ozu inaongeza mwendo, nao wakaongeza mwendo. Akili yao ilikuwa imejawa na kumfuata Ozu kiasi cha kwamba hawakutilia maanani gari lililokuwa linawafuata nyuma.

“Inaonekana Ozu ametambua kuwa anafuatwa angalia jinsi gari lake ambavyo limeongeza mwendo”, Robert alisema.

“Naona hata mimi. Ili kusudi tuhakikishe kuwa watu hawa wanamfuata Ozu ni lazima sisi tuwasimamishe. Maana inaonekana haja yao ni kumfuata tu wala si kumsimamisha na kumfanyia chochote. Kwa vile pia tumetambua kweli kuwa wanamfuata litakuwa jambo la maana kuwakamata watu hawa tujuwe ni akina nani na kwanini wanafanya hivi. Hasa ninapofikiria ya kwamba Ozu na Kofi wameingia hapa mjini kisiri, hili jambo la watu kuwafuata linatia wasiwasi,” Willy alieleza wasiwasi wake.

“Sawa, mimi niko tayari kwa kitendo chochote utakachoamua”.

“Vizuri, una silaha?”.

“Sina”, alijibu Robert.

“Kwanini unatembea bila silaha nawe unajua uko kazini?”

“Mimi ninatumia silaha inapokuwa lazima sana. Kawaida yangu katika kashikashi ya kawaida judo, kareti na Kung-Fu ambayo nina ujuzi wa hali ya juu sana, wewe mwenyewe utachoka ukiniona niko kazini,” Robert alieleza kwa sauti ya kujiamini sana.

Willy ambaye alimwamini moja kwa moja alimweleza, “Kwa sababu hujui watu hawa ni watu wa namna gani lazima uwe tayari kwa yote. Mimi nitalitia gari mwendo wa kasi kiasi cha kuwapita hawa jamaa. Nikishawapita tu nitapiga breki mbele yao kiasi cha kwamba watatugonga nyuma. Hapo ruka mara moja na kumteka jamaa wa upande wako, nami nitamteka wa upande wangu. Kwa sababu tutawashtua nafikiri kazi itakuwa rahisi sana”, Willy alitoa bastola ndani ya koti na kumpa Robert, “Chukua hii”.

“Asante, kwa upande wangu hamna taabu, sijui wewe dereva”.

“Kwangu ndiyo hamna kabisa,” alijibu Willy huku akiongeza mwendo.

Walipopita gereji ya Fiat tu. Willy aliweka mwendo wa kasi sana kwa gari hili la aina ya Mercedes Benz na gari likapaa. Sehemu hii waliyokuwa wamefikia ilikuwa sehemu ya upweke sana, na Willy aliiona ndiyo sehemu safi ya kufungia kazi.

Mulumba ambaye ndiye alikuwa akiendesha gari lao aina ya Fiat 124 aliona kwenye kioo chake cha kuendeshea, gari lililokuwa nyuma yao linakuja kasi sana. Mara moja akaingiwa na wasiwasi na kumwambia Kasongo aweke silaha tayari.

Gari hilo sidhani lina usalama,” alimalizia na huku gari la akina Willy linaanza kuwapita. Willy aliwapita kwa mwendo huo huo, alipopita mbele yao tu, akaliingiza gari sawasawa na gari la akina Mulumba, huku akiwa kana kwamba ameona shimo. Alifunga breki ghafla na kuliacha gari lijililie. Mulumba alishindwa kulikwepa gari hili na akaligonga kwa nyuma kama vile Willy alivyotaka. Willy na Robert waliruka toka ndani ya gari lao, na huku wakati ule ule, Mulumba na Kasongo nao waliruka toka ndani ya gari lao, Kasongo ndiye alikuwa wa kwanza kufyatua, lakini risasi yake ikamkosa Robert ambaye alikuwa amekwisha jirusha toka alipoangukia na kuangukia karibu na Kasongo, na kufumba na kufumbua akaipiga teke bastola ya Kasongo na kuangukia upande. Robert kuona hivi alirudisha bastola yake ndani ya koti ili amkabiri Kasongo mikono mitupu.

Naye Willy aliporuka alijiviringisha na alipoinuka tu akakuta Mulumba naye anajiweka tayari kufyatua risasi, lakini Willy alikuwa mwepesi zaidi akawahi kufyatua risasi ya kichwa na kumuua pale pale. Alipoona hivi aliruka mara moja

kwenye upande ule ambako Robert na Kasongo walikuwa wanazipiga na kumkuta Kasongo amepigwa ile mbaya mpaka hajiwezi kabisa.

“Basi, basi, inatosha, mwingize ndani ya gari yetu, twende naye, huyu ndiye atatupa habari”.

Wakati Robert anamwingiza Kasongo ndanu ya gari. Willy aliangalia lile gari kwenye karatasi za bima akakuta ni gari la kukodi la S.T.K. Kisha akajaribu kunyoosha gari lake kwa nyuma ambako lilikuwa limebonyea kiasi cha kugusa kwenye tairi. Alipolinyoosha kiasi cha gari kuweza kwenda, alipanda ndani ya gari akalipiga moto na kuondoka. Tayari Robert na mtu wake walikwisha starehe nyuma ya gari. Mambo yote haya hayakuchukua zaidi ya dakika mbili. Willy alifikiria wapi wampeleke mtu huyu kumhoji, mara akapata wazo. Aliendelea moja kwa moja mpaka akaingia barabara ya 30 Juin kisha akaingia barabara ya Kasavubu halafu akaingia barabara ya Sendwe halafu barabara ya Universete. Alipoingia ndani ya barabara hii akaenda moja kwa moja mpaka Chuo Kikuu. Alipofika hapa Robert ambaye alikuwa anashangaa wanakwenda wapi aliuliza, “Wapi tunakwenda?”.

“Sehemu ambayo huyu ndugu yetu anaweza kutueleza vizuri mambo tunayotaka kuyajua”, Willy alijibu Robert naye alihisi sehemu gani Willy alikuwa amefikiria.

Walipofika kwenye msitu ulio karibu na Chuo Kikuu na shule ya sekondari ya wasichana ya Kimwenza, Willy alienda taratibu na kuyaacha magari yampite. Yalipokuwa yamempita magari yote alisimama na kutoka. “Bado amezirai?”, Willy aliuliza.

“Anaanza kupata fahamu”.

“Tumbebe, hapa ndipo mahali petu ambapo tunaweza kuzungumza na huyu mtu”, walimbeba na kuingia naye ndani ya msitu huu. Kwa vile Kasongo alikuwa bado hajapata fahamu vizuri, Willy alichukua galonoya maji iliyokuwa ndani ya gari na walipopata mahali pazuri ndani ya msitu huu walimweka chini Kasongo na kuanza kumwagia maji. Kasongo alipopata fahamu vizuri Willy alitoa bastola yake na kuilenga kichwani mwa Kasongo na kuanza kumhoji.

“Wewe ni nani?”, Willy aliuliza.

“Kwani nyie ni nani?”, Naye Kasongo aliuliza.

“Tafadhali kijana kama unataka usishi tafadhali sana jibu maswali yetu tutakuacha uende nyumbani, la hutaki leo ndiyo mwisho wako.

“Msipoteze muda wenu. Mimi sintawaeleza lolote, kama ni kuniua basi niueni mwende zenu.”

“Lakini tuna njia nyingi za kuweza kukushawishi ujibu maswali yetu, lakini sisi tusingependa kuzitumia njia hizi kama utatujibu moja kwa moja”.

“Nimesema nimesema, kama kuniua mniue neno hata moja hamtapata kutoka kwangu”, alijibu Kasongo kwa ujasiri mwingi sana.

“Wewe unamkawiza”, Robert alimwambia Willy.

“Majitu kama haya hayafai kubembelezwama maana yamezoea taabu”, Robert alimfungua Kasongo suruali, halafu akamteremsha suruali pamoja na chupi, kisha akawasha kiberiti chake cha gesi na kuanza kumchoma kwenye sehemu zake za siri. Kasongo alianza kupiga kelele maana alipata uchungu mwingi sana.

“Niache, niache, aaa mnaniua”, alilia Kasongo.

“Jibu wewe ni nani na nani amekutuma?”.

“Sijui... aaa... sijui”, aliendelea kupiga makelele, Robert alisogeza moto, Kasongo aliachama na kuzungusha zungusha ulimi wake halafu kitu kama peremende ndogo sana kikatokea mdomoni mwake na kukazana kukimeza. Willy alipokiona tu alimrukia kusudi asikimeze lakini kwa bahati mbaya hakuwahi. Kwani Willy alikitambua kitu hiki kuwa ni kidonge cha sumu ambacho hutumiwa hasa na majasusi ya hali ya juu sana wanaposhikwa ili wajiue wasiweze kutoa siri.

“Ni kazi bure tumefanya Robert, atakufa sasa hivi, amemeza kidonge cha sumu. Inaonekana hawa ni majambazi ambao wanalifanyia kazi kundi la hali ya juu sana, maana kundi la kawaida haliwezi kutumia njia hizi”, alisema Willy kwa huzuni sana.

“Mimi kwanza nilikuwa na wasiwasi nikijua tumepambana na vijana wa CND, lakini hii imehakikisha kuwa kuna kundi la kijasusi mjini hapa na leo tumelitonisha kidogo, sasa tusebiri tuone nini kitafanyika”, Robert alieleza. Willy alikagua mifuko yote ya Kasongo, kitu cha kutatanisha alichokipata kilikuwa kikaratasi kidogo kigumu kilichoandikwa, “Muone Kabeya Charles”, Willy alikiangalia sana kikaratasi hiki kisha akampa Robert ambaye naye alikiangalia sana.

“Kitatue, lakini majina hayo yaweke kichwani, huenda yakawa na maana sana”, alishauri Willy.

“Lazima ni ya maana sana, lakini tukiweke kwanza,” alijibu Robert.

Waliondoka sehemu hii na kurudi mjini huku wakiwa na mawazo mengi sana juu ya tukio hili la kushangaza. Kwani huenda walikuwa kwa bahati mbaya wameligusa kundi linalohusika na mauaji ya wapigania uhuru, hivi ndivyo waifikiri wakati wakirudi mjini.

SURA YA NANE

WASIWASI

Ozu ambaye alikuwa amefikia Hoteli Regina, alimaliza kuoga. Aliangalia saa yake akakuta inakaribia saa kumi na moja za jioni akaona ajitayarisha kusudi awahi ahadi yake na Kofi huko Restaurant Namouna ambako waliagana wakutane mnamo saa kumi na moja na nusu, ili wapate kuelezana mambo yalivyokuwa. Alivaa vizuri akapanga vitu vyake vizuri, kisha akafungua mlango, akachukua kijikaratasi akakibana na mlango, akaufunga akaondoka kwenda zake. Funguo za chumba chake hakuzirudisha mapokezi isipokuwa aliondoka nazo moja kwa moja.

Restaurant Namouna iko ghorofa ya nne ndani ya jengo maarufu liitwalo Galleries Presidentielles. Na kutoka Hoteli Regina mpaka jumba hili ni karibu sana, kiasi cha mwendo wa dakika tano kwa miguu. Hivi Ozu aliondoka kwa miguu akaelekea kwenye mkahawa huu. Alipofika alimkuta Kofi tayari ameiwasili huku akiwa anakunywa kahawa na Sangweji.

“Katibu”, Kofi alimkaribisha.

“Asante”, alijibu Ozu huku anakaa. Kofi alimwagizia Ozu kahawa vile vile.

“Ehe, umekata shauri kwenda hoteli gani?” Ozu alimwuliza Kofi.

“Nimefikia Hoteli Intercontinental”.

“Mimi niko Hoteli Regina”, walielezana.

“Mimi safari yangu kutoka uwanja wa ndege ilikuwa safi kabisa. Maana nilipotoka hapo nje nilichukua taksi na hatukupata tatizo lolote mpaka tulipofika Intercontinental. Baada ya kuchukua chumba nimejitayarisha na kuja hapa, sijui wewe mwenzangu ilikuwaje”, aliuliza Kofi.

Ozu alimeza mate, akamwangalia Kofi kwa macho makali kisha akamwambia.

“Mimi rafiki yangu mambo hayakuwa mazuri kama yako. Wakati nateremka tu ndani ya ndege, ndipo hapo mambo yalianza. Kulikuwa na watu wanatusubiri. Inavyoonekana wewe hawakuweza kukutambua, hivi umepita bila taabu. Lakini mimi walinitambua na ndiyo sababu walinifuata. Ajabu ni kwamba kulikuwa na makundi mawili. Na walinifuata katika magari mawili tofauti. Nilipotaka kuhakikisha kama kweli nafuatwa nilimwamru taksi dereva achepukie kwenye

barabara ya Poids Lourds, na kweli nilikuwa nafuatwa na makundi yote mawili. Sasa sikiliza kitu cha kushangaza. Nilipoona kuwa siwezi kuwakabiri watu hawa peke yangu nilimweleza dereva aongeze mwendo. Magari haya ya nyuma nayo yaliongeza mwendo. Tulipovuka Fiat tu, pale kwenye msitu, niliona lile gari la nyuma aina ya Benz linakuja kasi. Mimi nikajua sasa nitafungiwa kazi, kwa hiyo nikamwamru dereva azidishe mwendo kwa kadri ya uwezo wake. lakini Kofi, ajabu ni kwamba niliona kitendo cha ajabu. Lile gari la nyuma lilipolipita lile la mbele tu likafunga breki, ikabidi itokee ajali maana lile ambalo lilipitwa ilibidi lijigonge kwenye lile la nyuma na hapo hapo watu waliokuwa ndani ya magari haya waliruka nje na kuanza kushambuliana. Mimi kuona hivi nilizidi kumwamrisha dereva akaze mwendo na kuja moja kwa moja mpaka Hoteli Regina. Yaliyotokea hapo nyuma siyaelewi”. Ozu alinyamaza kiasi cha kupitisha mate kisha akaendelea.

“Kitu kinachonishangaza sana ni kwamba watu hawa ni akina nani? Na kwanini wameshambuliana? Wamejuaje kuwa sisi tunafika? Nafikiri tukishajibu maswali haya basi tutakuwa tumeshapata jawabu la tukio hili”, alimalizia Ozu.

“Ahaa, afadhali wewe maana umeona vituko. Mimi nafikiri makundi mawili ni makundi tofauti katika misingi ya shughuli zao. Tuliarifiwa kuwa tukifika hapa tumwarifu Robert ambaye atamwarifu Willy kuwa tumefika. Inawezekana Willy na Robert walishaletewa habari kuwa tutafika, hivi walifika kutupokea na wakati wanafanya hivi ndipo waligundua kuwa kuna kundi jingine lililokuwa linatusubiri. Kati ya wale watu uliowaona jukwaani lazima Willy na Robert au mmojawapo walikuwemo, lakini kwa sababu hatuwajui kwa sura ndiyo sababu hukuweza kuwatambua. Mimi nahisi kuwa Willy na Robert ndio walikuwa ndani ya Benz na walifanya mashambulizi ya kukunusuru wewe. Lakini tusichoshe vichwa vyetu maana itabidi tuonane na Robert jioni hii”, alishauri Kofi.

“Mawazo yako ni sawa kabisa. Hata mimi nilikuwa nashauri katika misingi hiyo hiyo. Swali moja limebaki bila kujibiwa. Hili kundi jingine limejuaje kuwa sisi tunawasili hapa mjini na hali kuingia kwetu ni siri ya hali ya juu “, aliuliza Ozu.

“Kama Willy na Robert wamenusurika katika mashambulizi haya wataweza kutujibu swali hili,” Ozu aliangalia saa yake akaona ni kiasi cha saa kumi na mbili unusu.

“Sijui tumpigie simu Robert au tumfuate nyumbani kwake?”, Ozu aliuliza.

“Nafikiri tumpigie simu kama yupo, na kama yupo tumfuate”, Ozu alitoa kijikaratasi ambacho kilikuwa kimeandikwa simu na sehemu ambayo Robert alikuwa akikaa kama walivyopewa na ofisi ya 'KK' ya Lusaka. Walikuwa wameelezwa kuwa Robert alikuwa akikaa sehemu iitwayo Macampagne mtaa wa Marais nyumba nambari ya kiwanja 2994. Ozu alikwenda kaunta akaomba kama anaweza kupiga simu. Kijana aliyekuwa kaunta alimruhusu apige kwa Robert, “Hallo,” Ozu aliuliza simu ilipoinuliwa kule kwingine.

“Hallo, nani mwenzangu”, sauti nzito ilijibu.

“Hapo ni nyumbani kwa Robert Sikawa?” Ozu aliuliza.

“Ndiyo”, sauti ilijibu.

“Mwenyewe yupo?”.

“Ndiye anazungumza”.

“K.K”, Ozu alisema.

“Kikosi cha Kisasi,” Robert alijibu. Hii ndiyo namna walivyokuwa wanajitambulisha.

“Habari yako Robert? Ozu hapa”.

“Nzuri, salama lakini”.

“Salama kabisa, sisi tuko hapa Restaurant Namouna, pamoja na Kofi, tuonane wapi?”

“Nafikiri ingekuwa vizuri kama tungeonana hapa maana Willy naye yuko hapa kwa wakati huu. Mimi nakaa...”

“Usiwe na wasiwasi tunapajua mtusubiri tunakuja sasa hivi”, Ozu alimkata kauli.

“Oke, tunawasubiri, fanyeni haraka maana Willy ana miadi yake,”

“Sasa hivi,” alijibu Ozu na kukata simu.

Wakati Ozu na Kofi wanaelekea nyumbani kwa Robert, katika ofisi za gereji G.A.D. kulikuwa na kikao cha dharura cha 'WP', viongozi wote wanne wa 'WP' walikuwepo katika kikao hiki. Pierre alikaa huku anavuta mtemba wake katika hali ya majonzi kabisa. Wenzake walikaa kimya wakisubiri atasema nini. Maana alikuwa amepata habari za kifo cha Mulumba lakini mpaka dakika hii walikuwa

hawajapata habari zozote za Kasongo. Jinsi mambo yote yalivyotokea, walikuwa wamehisi na hiki ndicho kitu kilikuwa kinawapa wasiwasi mkubwa sana.

“Jamani hapa ndio tumefikia muda wenyewe. Huu ndiyo utakuwa muda wetu mgumu tangu ianzishwe 'WP', maana kwa mara ya kwanza 'WP' imeingiliwa kiasi cha vijana wao mmoja kuuawa na mwingine kutekwa nyara. Jambo hili naamini wote tulilitegemea na ndiyo sababu tumeunda kundi kubwa lenye nguvu la kuweza kuvunja nguvu zozote za upinzani. Hivi tupo hapa sasa hivi kulishughulikia suala hili kikamilifu. Toeni wasiwasi,” alisema Pierre katika hali ya kuwatia wenzake moyo, maana alijua mambo yameharibika.

“Sisi, Patron hatuna wasiwasi, tuko tayari kabisa kupambana na hawa watu kikamilifu,” alijibu Jean huku wengine wakitingisha vichwa kuonyesha kuwa wanamuunga mkono.

“Nafikiri sasa tuanze mipango ya kushughulika na jambo hili. Kitu cha kwanza ninachotaka kujua, Mulumba na Kasongo walikuwa watu wenye ujuzi kiasi gani?” aliuliza Pierre.

“Mulumba na Kasongo ni kati ya vijana wetu ambao walikuwa na ujuzi wa juu katika kumfuata mtu na wasiweze kutambuliwa. Ndiyo walikuwa wamefanya kazi hii kwenye matukio yote tuliyofanya sehemu mbali mbali katika Afrika na wakawa wameimudu vizuri sana. Kwa mfano, waliweza kumfuata Nelson Chikwanda yule tuliyemuua Lagos Nigeria kwa muda wa wiki moja bila kugunduliwa na wakaweza kutueleza nyendo zake zote kiasi ya kuwa ilikuwa rahisi kwa Masamba kumpiga risasi na wote wakaondoka bila kugunduliwa. Vile vile kwa upande wa kutumia silaha walikuwa na ujuzi wa hali ya juu sana. Wote wawili waliweza kutumia silaha kila aina, ukiongezea kuwa Mulumba alikuwa na ujuzi wa hali ya juu katika kareti. Kwa ujumla Patroni, vijana hawa walijua kazi yao vizuri sana na ndiyo sababu waliwekwa mahali pa maana kama uwanja wa ndege,” alieleza Jean.

“Hii ina maana kuwa watu hawa wawili walioingia si wa kuchezea”, alizingatia Muteba.

“Ndiyo si wa kuchezea. Kutokana na habari kamili nilizozipata toka 'Boss' kwa kupitia wakala jioni hii kabla sijapata habari za mambo haya yalivyotokea, ni kwamba huyu mmoja aitwaye Petit Osei ni mpelelezi maarufu sana. CIA imekuwa inamwangalia kwa muda mrefu sana na inamtambua vizuri sana, na ndiyo sababu walipomnasa kwenye kanda zao za kipelelezi akija hapa baada ya tukio hili kubwa sana kutokea ilibidi kupasha mashirika mbali mbali wanayoshirikiana nayo, habari

za safari ya mtu huyu. huyu wa pili hajulikani kabisa, ila alionekana akitembea na Osei mjini Lagos na CIA ikajuwa lazima walikuwa na safari moja. Na kweli wamesafiri pamoja na wote wana pass za Nigeria ambazo bila shaka ni za bandia. Vile vile wanatumia majina ya bandia, Osei anajiita Petit Ozu na mwenzie Mike Kofi. Kusema kweli CIA na Boss imeshaturahisishia kazi lililopo ni kuwasaka tujuwe wamefikia hoteli gani na kisha tuwafyagilie mbali, ndipo watambue 'WP' maana yake nini,” alieleza Pierre kwa sauti ya uchungu.

“Kama ni watu wa ujuzi kiasi cha kwamba CIA inawatambua na wako kwenye orodha yao basi ni wajuzi kweli. Kwa hiyo mambo waliyowafanyia Mulumba na Kasongo ni kipimo chao. Hii ina maana kuwa lazima tokea sasa jambo hili liwe chini ya uangalizi wetu moja kwa moja maana sasa tunashughulika na watu wenye ujuzi kama sisi,” alishauri Papa.

“Maelezo yako sawa kabisa, inatulazimu kufanya hivyo. Bila shaka itakuwa rahisi kwetu kuwapata upesi na kuwafutulia mbali maana sisi tunao watu na vifaa vya kutosha. Hii ni faida tunavyowazidi wao,” Pierre alisema.

“Kasongo watakuwa wamempeleka wapi?” Aliuliza Muteba.

“Hili ndilo jambo ambalo linanikera. Kitu ninachoogopa wasije wakamlazimisha Kasongo akalopoka maneno ambayo yanaweza kuwafanya wakavumbua siri yetu hii ambayo tumeweza kuificha kiasi cha kwamba Serikali ya hapa haijatugundua. Hivi inatubidi usiku huu tutumie kila tulichonacho kutambua Kasongo yuko wapi,” Pierre alinena. “Kuropoka Kasongo hawezi kuropoka, maana wamepewa amri ya kawaida ya 'WP' kuwa, mtu akishikwa na ukahisi kuwa unateswa kiasi ambacho huwezi kuvumilia urnameza kidonge cha sumu na kujiua. Kama sisi wote tunavyojua, kama Kasongo amelazimishwa kusema lazima ameishajiua, maana afadhali ajiue kuliko kurudi 'WP' huku akiwa ametoa maelezo juu ya 'WP'. Anajuwa vizuri kuliko kufanya hivyo, maana haya maelezo niliwapa tangu nilipowachukua chini yangu. Kwa hiyo mimi nina imani asilimia mia moja kuwa Kasongo ameisha kufa hivyo hakuna haja ya kupoteza muda kumtafuta. Jambo la maana sasa la kufanya ni kuwatafuta hawa watu wawili tuweze kujua wapi walipo ili tukawafutilie mbali kabla hawajaleta madhara,” alijigamba Jean.

“Kama una uhakika huo vizuri. Sasa lililopo ni kutaka kujwa hawa watu wamefikia hoteli gani,” Pierre alisema.

“Hilo lisikupe taabu, Kabeya anazo njia za kuweza kutupatia hoteli pamoja na vyumba wanavyolala. Hebu nikawaone ofisi ya pili maana nilimwambia yeye na

Charles wasitoke ofisini mpaka hapo nitakapowaeleza,” alijibu Jean huku akiondoka kwenda kuwaona Kabeya na Charles. Wakati Jean ametoka mazungumzo kati ya hawa wengine yaliendelea.

“Jean atakapokuwa ametupatia hoteli walizomo, Muteba na kundi lako mtamshughulikia Kofi, wakati wewe Papa utamshughulikia Ozu. Nataka kufikia kesho saa kama hizi tuwe na mpango kamili wa kuwaua hawa watu au wawe wameishauawa tayari,” alitoa amri Pierre.

“Hamna taabu Patroni, kazi rahisi sana, tukishaweza kuwaweka machoni kazi yao imekwisha,” Papa aliwahakikishia.

Jean alirudi akiwa na uso wa furaha furaha, na kuwaeleza, “Vijana wangu wanafanya kazi nzuri sana. Kila mtu ambaye ni mgeni anayeingia hapa mjini na kuchukua chumba ndani ya hoteli yoyote kubwa na zile za hali ya katikati, majina yao yanapelekwa moja kwa moja kwa Kabeya. Kwa hiyo wageni wote walioingia Kinshasa anayo, Hata majina ya Kofi na Ozu ameisha yapokea lakini alikuwa bado hajaweza kujuwa ni kwa ajili gani wameingia hapa mjini. Kwa kifupi Petit Ozu yuko Hoteli Regina chumba nambari 108 na Mike Kofi yuko Hoteli Intercontinental chumba nambari 401,”

“Lo, kazi nzuri Jean, kazi nzuri kabisa, namna hii bila shaka kazi yetu itakwenda sawa. Sasa kazi imebaki kwenu yaani kwako Papa na Muteba, Jean atawasaidia katika kuwapa habari na katika kuwawinda hawa watu wawili. Tusipumzike mpaka tutakapokuwa tumeweza kunasa nyendo zao na kuwa tayari wakati wowote kuwashambulia,” alisisitiza Piere.

“Usiwe na wasiwasi Patron, sisi sasa tunakwenda kushughulikia jambo hili kikamilifu. Vijana wote wako katika tahadhali, na usiku huu huu tutakujulisha mambo yalivyo,” alieleza Muteba huku wote wakisimama tayari kuondoka kwenda kuanza kazi hii muhimu.

“Sawa, mimi nitakuwa nyumbani nikisubiri kutoka kwenu wakati wote,” Pierre alisema huku anaingia ndani ya gari lake na wenzake nao wakiwa tayari kwenda kwenye uwanja wa mapambano.

Wakati kikao cha dharura cha 'WP' huko kwenye ofisi za gereji ya G.A.D. kikiendelea. Kikao kingine cha 'KK' kilikuwa nacho kinaendelea nyumbani kwa Robert Sikawa huko Macampagne. Kofi na Ozu baada ya kumpigia Robert simu waliteremka chini na kuchukua teksi iliyowapeleka moja kwa moja mpaka nyumbani kwa Robert. Waliwakuta wenzao wakiwasubiri kwa hamu na kweli

walipoonana walikumbatiana kwa furaha kubwa. Kusema kweli kama ungewaona vijana hawa ungeamini kuwa ni watoto wa mzee mmoja maana walifanana.

Kweli ni ajabu sana Ozu na Kofi walimfurahia sana Willy kumuona maana sifa zake nyingi walikuwa wamezisikia. Kwa mawazo yao walifikiri ni mtu wa kutisha sana, lakini kwa mshangao wao walimkuta ni kijana wa rika yao na sura ya kupendeza ajabu kiasi kuwa mtu kwa mtu yeyote angempenda. Kweli alikuwa rijali. Willy na Robert nao waliwafurahia wenziwe na katika muda wa dakika chache vijana hawa walitaniana na kuchekeshana kana kwamba walishafahamiana miaka kumi iliyopita.

Baada ya mazungumzo haya ya kukaribishana, waliingia katika mazungumzo ya kikazi, Willy alieleza kwa kirefu sana mambo yote kuhusu nia na utekelezaji wa kazi waliyopewa. Baada ya maelezo haya aliwaeleza maendeleo waliyokuwa wameyafanya katika shughuli, na kuwafikisha mpaka kwenye tukio la akina Ozu, Mulumba na Kasongo.

“Kwa kifupi ndivyo hivyo mambo yalivyokuwa mpaka sasa hivi. Swali linabaki pale pale hawa watu ni akina nani, na wanawakilisha kundi gani?”. Alimalizia Willy.

“Vizuri sana umetuweka katika hali nzuri ya kujua mambo yalivyo. Kweli suala linabaki ni hilo hilo,” Ozu alisema.

“Hiki kijikaratasi huenda kina maana. Kabeya ni nani na Charles ni nani? Ndilo suala jingine”, Willy alijaribu kutafuta mawazo.

“Unajua katika Zaire siku hizi majina ya kizungu hayatumiwi, basi hii inaonyesha kuwa aliyeandika kikaratasi hiki ambaye ni Charles si Mzaire”, Robert alieleza.

Willy alikitoa kile kikaratasi ndani ya mfuko wake wa shati na kuanza kukiangalia tena. “Ahaa angalieni mwandiko huu ni wa Kizungu si wa Kiafrika, unajua miandiko ya Kizungu na Kiafrika inatofautiana! Wote walicheka kutokana na jinsi Willy alivyokuwa akieleza.

“Ni kweli, huu ni mwandiko wa Kizungu”, walikubaliana wote.

“Hii ina maana hawa watu walikuwa na uhusiano na mzungu. Kwa hiyo itabidi tujaribu kumtafuta Kabeya na huyu Charles, naamini tukiwapata watatueleza zaidi”, alizungumza Willy kimatani.

“Tutawapataja na huku kuna Kabeya chungu mzima Kinshasa na akina Charles chungu nzima vile vile”, alisema Robert.

“Ndiyo sababu sisi tunaitwa wapelelezi,” Willy alimkumbusha, “Sasa itabidi tupeleleze hata ikiwa ni lazima kuwakusanya watu wote wa majina haya itatubidi tufanye hivyo. Maana maelezo yoyote tuliyonayo sasa ya kuweza kutusaidia ni hayo tu na lazima tuyatumie”, alimalizia Willy.

“Majina haya yanaweza kuwa ya bandia na yakawa hayana maana yoyote”, Ozu alisema.

“Si kitu, sisi tutajaribu tu, kitu ambacho najua ni kweli kwamba watu hawa wapo hata kama majina haya ni majina ya bandia watu hawa wapo na wana uhusiano mkubwa na watu wale tuliopambana nao mchana. Mimi nina miadi yangu saa moja ambayo sasa imeshafika tayari kwa hiyo itabidi niondoke. Kitu muhimu cha kufanya sasa, inabidi sisi wote sasa tuwe macho hasa wewe Ozu maana wewe tayari wamekwisha kutambua na ni imani yangu kuwa wako mbioni kukusaka. Hivyo wewe ndiwe utakuwa chambo na wewe ndiwe utaweza kutufanya tuwajue watu hawa. Hivi lazima tuwe katika tahadhari kubwa maana kitu chochote kinaweza kutokea wakati wowote. Huu ni wakati wa wasiwasi sana hivi itabidi tuwe na moyo wa utulivu kabisa. Kesho asubuhi nitajaribu kuwaona watu wa STK, ili nipate kujua ni nani aliyekuwa amekodi lile gari walilokuwemo wale majambazi. Mmefikia hoteli gani?” Alimazia Willy kwa kuuliza.

“Mimi niko hoteli Regina chumba nambari 108 na Kofi amefikia Hoteli Intercontinental,” alijibu Ozu.

“Chumba nambari 401,” aliongezea Kofi.

“Vizuri, kama nilivyokwisha sema kaeni macho. Kama kitatokea kitu chochote habari ziletwe hapa kwa Robert. Mimi nimefikia Hoteli Memling, chumba nambari 240, ikiwa nitahitajika. Ninayo imani kubwa saba baada ya kuwaona, Kuwa Mungu akipenda tutashinda vita hivi. Robert peleka habari Lusaka kueleza kuwa wote tumekwishawasili mjini hapa na shughuli zimeanza. Vile vile gari nililokodi tulifanyia ajali, liweke ndani mpaka kwanza tuone uchunguzi wa tukio hili utafikia wapi, mimi nitaendelea na gari hili ulilokodi wewe. Asanteni mimi naondoka,” Willy alimalizia kunena huku akisimama tayari kwa kuondoka.

“Vipi una miadi na mtoto nini?”, Ozu alitania

“Kitu kama hicho”, alijibu Willy huku akimwemwesa.

“Una bahati basi mara hii tayari. Haya starehe njema,” Ozu alimwombea.

“Asante.” Waliagana Willy akaondoka kuwahi miadi yake na Mwadi ambayo alikuwa tayari amechelewa. Aliingia ndani ya gari alilokuwa amekodi Robert, baada ya kufanya ajali na lile gari jingine, na akaondoka kwenda zake. Robert na wageni wake walibaki na wote kwa pamoja wakakata shauri kutengeneza chakula cha jioni hapo nyumbani kwa Robert wao wenyewe. Kwani Robert hakuwa hata na mfanyakazi hivi ndivyo alivyokuwa akiishi. Mtu aliyekuwa akifika hapa nyumbani kwake mara kwa mara na kumsaidia kusafisha nyumba na mara nyingine kumsaidia kupika alikuwa rafiki yake msichana aitwaye Ebebe, ambaye walipendana sana.

Ilikuwa yapata saa mbili kamili Willy alipoingia mtaa wa Kimbondo katika sehemu ya Bandalungwa. Aliendesha pole pole huku akiangalia namba za nyumba kila mara, na kusimama ili kuona vizuri. Mwishowe aliona nyumba nambari 79. Aliposimamisha gari tu mbele ya nyumba hii. Mlango ulifunguliwa na Mwadi akatokeza kuja kumpekea.

“Karibu Willy, nilikuwa na wasiwasi mkubwa kuwa huenda umeponda miadi yetu”.

“Lo, hiyo isingewezekana Mwadi, nilikuwa bado nakuja ila tu nilicheleweshwa na watu fulani waliofika tuweze kuzungumza mambo ya biashara. Unajua tena mambo ya biashara!” Willy alieleza huku wanaingia ndani.

“Karibu keti,” Mwadi alimkaribisha Willy. Willy aliketi kwenye kochi.

Nyumba ya Mwadi ilikuwa ndogo yenye sebule na chumba kimoja cha kulala, ikiwa pamoja na jiko, bafu na choo. Sebule ilikuwa na vyombo vizuri vya gharama ya juu ambavyo vilifanya chumba kuonekana maridadi kabisa, hasa ukiongezea kwamba hiki chumba ni cha msichana na wewe mwenyewe unajua jinsi wasichana wanaojipenda wanavyofanya.

“Hapa ndipo ninapoishi”.

“Mahali pazuri sana Mwadi”.

“Asante,” alijibu Mwadi, “Utakunywa nini bia au Whiski?”

“Nipe bia”, alijibu Willy.

“Skol au Primus?”.

“Nipe Primus”.

Mwadi alifungua barafu na kutoa bia mbili za Primus, kisha akazifungua na alichukua bilauri na kumimina.

“Karibu”, alisema huku akimkabidhi Willy kinywaji. Willy aliinua bilauri yake na Mwadi akainua ya kwake, kisha Willy akasema. “Triniens.”

“A la sante ya Willy,” alijibu Mwadi wakagonganisha bilauri zao wakaanza kunywa. Muziki taratibu ulitokea kwenye santuri, Willy aliamka akaenda kuchagua sahani za santuri ambazo zilikuwa nyingi sana, hii ilionyesha kuwa Mwadi alikuwa mpenzi wa muziki maana nikitaka kusema ukweli alikuwa na maktaba nzima ya muziki. Sahani zilipangwa kwenye kabati kubwa, na kila fungu la sahani lilikuwa na karatasi ambayo iliandikwa majina ya kila wimbo. Willy alitafuta kati ya rekodi alizozipenda, akapata rekodi moja ya Orchestra Shamashama iitwayo 'SHAMASHAMA' akaiweka kwenye santuri na kuicheza.

Wakati Willy anashughulika na muziki Mwadi alishughulika jikoni kutayarisha chakula. Willy alipokuwa ameweka sahani na santuri za kutosha kwenye santuri alimfuata Mwadi jikoni huku amebeba bia yake. “Nimekuja unionyeshe jinsi ya kupika mabokey”, Willy alisema.

“Bahati mbaya nimeishapika 'mabokey' yameiva, ingekuwa vizuri kama ungewahi kabla sijapika. Hata hivyo kama bado upo tutapika wote siku moja”.

“Haya, kati ya siku hizi za karibuni tutakuja tupike mabokey wote”, walikubaliana.

Mazungumzo matamu kati yao yaliendelea mpaka wakati wa chakula, Willy alikula 'mabokey' chakula ambacho alikuta kitamu sana na kilikuwa kimepikwa vizuri sana. Kusema kweli alikula sana.

“Kweli Mwadi mpenzi, kwa muda mrefu sijala chakula kitamu namna hii, chakula hiki sintakisahau maishani. Asante sana,” alisema Willy alipomaliza kula.

“Bila ya asante Willy”, alijibu Mwadi kwa moyo wa furaha.

Ilipofika saa tatu na nusu, walikata shauri waende kwenye dansi.

“Unaonaje tukienda kwenye muziki,” alishauri Mwadi.

“Hata mimi nilikuwa na mawazo hayo hayo,” Alijibu Willy. “Chagua mahala pa kwenda maana wewe ndiye mwenyeji hapa”.

“Wewe unapendelea bendi gani?.” Aliuliza Mwadi.

“Nimekuachia uchague wewe, bendi unayopenda ndiyo hiyo itakuwa chaguo langu”, Willy alijibu.

“Mimi napendelea Orchestra Veve ya Verckys.”

“Vizuri twende huko huko. Leo wanapiga wapi?”

“Wapo Parafifi Bar”, alijubu Mwadi.

“Haya kajitayarishe twende”.

Mwadi aliingia chumbani na kuanza kujitayarisha. Willy alibaki sebuleni akisikiliza muziki huku akiendelea kunywa bia. Mwadi alipomaliza kuvaa alijitokeza sebuleni. Alikuwa amevalia vitenge toka juu mpaka chini katika staili ya Kizaire. Kusema kweli alionekana wakupendeza sana. Willy alithibitisha ya kwamba alikuwa amepata msichana mzuri wa kutosha.

“Ama kweli nina bibi”, Willy alisema Mwadi alipojitokeza.

“Mimi ndiye nimepata bwana wa sheria yake basi,” alijibu Mwadi kimatani.

Baada ya kutaniana hivi waliamua kuondoka. Kwa sababu Willy alikuwa amepita hotelini kwake jioni ile na kubadili nguo hakukuwa na sababu kwake kubadili tena, maana alionekana nadhifu wa kutosha. Hivi waliondoka moja kwa moja kuelekea Parafifi Bar. 'Parafifi Bar' ni bar mojawapo maarufu sana mjini Kinshasa ambapo vijana wengi hupenda kwenda na kustareheshwa na muziki wa bendi mbali mbali ambazo huwa zinafika hapa kuwaburudisha. Bar yenye iko kwenye kona ya mtaa wa Assossa na mtaa wa Victoire.

SURA YA TISA

WILLY na Mwadi walipofika kwenye bar hii ilikuwa kiasi cha saa nne na nusu na tayari magari yalikuwa yamejaa sana kuonyesha kuwa watu wengi walikuwa wamewahi. Walihangaishwa kidogo na mahali pa kuegesha gari maana sehemu yote ya karibu na bar ilikuwa imejaa, kwa bahati mtu alikuwa akitoka, wakapata mahali pa kuegesha. Walifunga gari lao na kuelekea kwenye mlango wa kuingilia ambapo walikata tiketi za kuingilia kwa wote wawili. Willy alilipa Zaire tatu.

Watu kama walivyokuwa wamehisi, walikuwa wamejaa tayari. Muziki ulikuwa unaendelea na watu kadhaa walikuwa uwanjani wakilisakata rumba. Walitafuta mahala pa kukaa na kwa sababu Mwadi alikuwa anafahamika sana pale walifanyiwa msaada na kupata mahala pa kukaa.

“Tumepata nafasi nzuri, maana ni karibu na watu wanapochezea. Hii itatupa nafasi ya kuona mitindo ya dansi ya hapa mjini Kinshasa,” alieleza Mwadi.

“Na hasa, maana huu ndio mji wenyewe kwa muziki. Tena inafurahisha sana kuwaona hawa wapiga muziki macho kwa macho maana sisi tumezoea kuwasikia mwenye redio na santuri tu,” alijibu Willy kisha waliagiza vinywaji.

“Mimi niagizie Whisky ndiyo itaniletea nishai upesi. Maana mimi bila nishai nakuwa mzito katika kucheza dansi,” Mwadi alieleza.

“Hamna taabu, hata mimi Whisky ndiyo itanifaa kwa wakati huu,” Willy alijibu. Hivi waliagiza whisky na walipoiletewa wakanywa huku wakiendelea na mazungumzo ya hapa na pale. Ilipofika saa sita ndipo muziki ulipopamba moto. Watu walikuwa wengi sana sasa, na wengi wao wakiwa wawili wawili walikuwa uwanjani wakilisakata rumba, kila mmoja akijaribu kuonyesha ujuzi wake. Akiwa Willy waliendelea kuzungumza huku Willy macho yake yakiwa uwanjani ambapo alifurahishwa sana na mitindo ya dansi iliyokuwa ikitokitolewa na wachezaji. Vijana wa Orchestra Veve nao ilipofika wakati huu, wakaanza kupiga zile nyimbo tamu tamu. Ulipoanza kupigwa ule wimbo uitwao 'Natamboli motu' Mwadi alisimama na kumwambia Willy, “Tukacheze wimbo safi sana huu. Unajua maana yake?” alimuuliza Willy huku wakiingia uwanjani.

“Hapana,” alijibu Willy.

“Unasema kichwa changu hakifanyi kazi, na mimi Willy kichwa changu, nacho hakifanyi kazi sasa hivi kwa ajili yako,” alisema Mwadi huku wanaanza kucheza. Willy alizubaa tu kwa maneno ya huyu msichana ambaye alionekana alikuwa amejawa na mapenzi makali juu yake, hivi hakujibu neno.

Mwadi naye kama wasichana wengi Kinshasa alikuwa anajua namna ya kulisakata rumba sawasawa, kiasi kwamba wakati mwingine Willy alikuwa akijisahau na kusimama huku akifurahia jinsi Mwadi alivyokuwa akikatika maungo hasa kiuno. Wasichana wote waliokuwa uwanjani utafikiri walikuwa wakishindana, maana kila mmoja alicheza na kujinyonga kwa mtindo wake.

Baada ya wimbo huo vijana wa Veve walipiga wimbo mwingine uitwao 'Zonga Andowe' yaani kwa kiswahili 'Rudi Andowe'. Bila kwenda kupumzika Mwadi na Willy waliendelea na kucheza nyimbo hizi tamu. Hivi ndivyo walivyostarehe usiku huu ambao wote wawili walijuana katika ulimwengu wao wa kipekee.

Wakati walipokuwa wamerudi mezani pao wanaburudika na vinywaji hali ya kimapenzi ilikuwa imepamda sana rohoni mwao , “Mwadi sikujua ungeweza kuwa msichana wa kusisimua hivi. Sasa hivi najiona kama niko juu ya dunia”, alidiriki kusema Willy.

“Mimi je? Mimi ndiye siwezi hata kueleza, maana naona hata haya kukueleza jinsi moyo wangu ulivyokufa juu yako, ee Willy wangu mtoto wa Kizambia”, alisema Mwadi kwa sauti ambayo ungefikiri anataka kulia. Wakiendelea na mazungumzo yao ya kimapenzi mara Willy aliona watu wanaangalia sehemu uliko mlango wa kuingilia. Maana 'Parafifi Bar' ina mlango mmoja tu na huku ikiwa imezungukwa na sehemu zote na nyumba na nyumba ya ghorofa. Willy alipogeza kichwa chake kuona watu wanaangalia nini, moyo wake uliruka mapigo. Maana aliona msichana mzuri ajabu akielekea sehemu waliyokuwa wamekaa na huku macho yote ya wanaume kwa wanawake waliokuwepa hapo, yakimwangalia na kuthibitisha kuwa kweli huyu alikuwa ni mrembo hasa.

Msichana huyu alikuwa mrefu wa kutosha, na rangi yake, rangi ya shaba. Alikuwa na nywele nyingi nyeusi sana na nzito na jinsi alivyokuwa amezichana zilitoa sura ya ki- Afro. Uso wake ulikuwa na umbo la moyo. Alikuwa na macho makubwa yaliyozungukwa na nyusi nyeusi nzito na kope nzito. Pua yake ilikuwa ndogo na ya kuchongoka kiasi cha kupendeza. Midomo yake ilikuwa ile ambayo kila mtu alitamani kuibusu, maana ilijaa ujana. Mashavu yake yalijaa kiasi cha kufanya sura ya uso mzima wa msichana huyu kuonekana ya kupendeza sana. Kifua chake kilijaa matiti ambayo yalikuwa yamejaa kabisa kiasi cha kwamba hata

ungeyaminyu ungesikia ugumu wake. Na bila shaka yalikuwa na joto la kutosha. Tumbo lake lilinyooka jembemba utafikiri hali chakula. Miguu yake ilikuwa mirefu kiasi kinachohitajina na ilikuwa imeshiba kiasi kwamba ukiangalia hutapenda kutoa macho yale kwa jinsi ilivyoumbika vizuri, nyuma alikuwa amejengeka kwa namna ya peke yake, kiasi kwamba siwezi kukuelezea mpaka umuone wewe mwenyewe mrembo huyu. Kwani matako yake pamoja na sehemu za mgongo kuteremka chini, alikuwa ameumbwa kwa mahesabu ya peke yake. Alikuwa na shingo la urefu uliotakiwa kupendeza umbo lake zima. Alikuwa amevaa 'maxy ya kijani kibichi ambayo ilizidisha rangi yake ya shaba kung'aa. Msichana huyu ndiye alikuwa na haki ya kiitwa kisura.

Willy aliendelea kumwangalia msichana huyu akisogea. Alikuwa akitembea taratibu kwa hatua zilizokuwa zinatupwa kwa mahesabu. Msichana huyu aliangalia huku na kule lakini kwa chati sana kiasi kwamba mpaka uwe mtu mjuzi kama Willy ndipo ungeweza kutambua. Hii ilimtambulisha Willy kuwa msichana huyu alikuwa akijua kuwa yeye ni mrembo sana hivi kila jambo alilolifanya alilifanya kwa sheria yake. Miondoko yake ilikuwa vile vile ya peke yake, ili kukamilisha urembo wa msichana huyu ambaye nimeshindwa maneno ya kuelezea urembo wake, afadhali siku moja ukipata nafasi fika Kinshasa umtafute mrembo huyu ili ujue uzuri ni nini. Alipozidi kusogea mahali walipo Willy alihisi kuwa huenda alikuwa anamtafuta mtu. Mwadi alingusa Willy kwenye mkono na kumshitua kutoa mawazo huko yalikuwa.

“Msichana mzuri sana au siyo Willy?” Aliongea Mwadi huku akumwangalia Willy machoni. Willy hakutambua kwa nini Mwadi aliuliza swali hili, lakini ili aweze kueleza ukweli wake alijibu.

“Ndiyo ni msichana mzuri sana”.

“Ni rafiki yangu.” Mwadi alijibu kwa mkato. Willy alishangaa kusikia msichana huyu tena ni rafiki wa Mwadi. “Kweli maajabu hayataisha ulimwenguni,” alijisemea rohoni. Kabla mshangao wake haujaisha msichana huyu akawa amefika kwenye meza yao. Alikuwa akitabasamu, tabasamu lililofanya nywele za Willy kusimama na jasho kumtoka mwili mzima.

“Eee Mwadi, mbote,” yule msichana alisamu katika Kilingala.

“Mbote,” alijibu Mwadi huku naye akitabasamu.

“Sango nini?”

“Malamu,” alijibu Mwadi kisha akamkaribisha, “Approchez”.

“Merci,” alijibu yule msichana. Kisha yule msichana akamgeukia Willy macho yao yakaonana. Macho ya huyu msichana yalikuwa malegevu lakini yenye nguvu fulani ambazo zilimwingia hata Willy.

“Mbote”, Willy alisalimiwa.

Willy alitabasamu, na baada ya kusita kidogo alijibu “Mbote,” Mara moja yule msichana alihisi kuwa huyu kijana aliyekuwa na Mwadi si mwenyeji wa Kinshasa na wala Zaire. Moyoni mwake msichana huyu alivutiwa sana na kijana huyu aliyekuwa na Mwadi akakata shauri kuvuta kiti, akakaa.

“Nafikiri inabidi niwafahamishe,” Mwadi alisema.

“Litakuwa jambo la maana”, alijibu Willy.

Mwadi alimwalia yule msichana akamwambia, “Huyu ni Willy Chitalu ni raia wa Zambia. Yeye ni mfanyabiashara na yuko hapa katika mapumziko ya kikazi kwa muda mfupi.” Kisha alimgeukia Willy na kumfahamisha, “Huyu msichana ni rafiki yangu anaitwa Tete. Yeye anafanya kazi na kampuni iitwayo Agence Sozidome.” Baada ya kufahamishwa walishikana mikono na kusalimiana. “Habari za siku nyingi,” Mikono ya msichana huyu ilikuwa laini sana, kiasi cha kuufanya mwili mzima wa Willy usisimke.

“Mimi nilipomuona tu huyu rafiki yako nilijua si kinois,” Tete alimweleza Mwadi.

“Unajua kinois ni nani?” Mwadi alimuuliza Willy huku akicheka.

“Kinois ni mtu yeyote ambaye maskani yake ni hapa hapa mjini Kinshasa bila kujali anatoka wapi”, Mwadi alieleza.

“Kwa hiyo hata mimi nikihamia hapa nitaitwa kinois.”

“Bila wasiwasi”, alijibu Mwadi.

Willy alimwagizia Tete kinywaji, huku wakiendelea na mazungumzo ambayo yalinoga zaidi kwa kuongezeka kwa Tete.

“Kampuni unayofanya kazi inashughulika na mambo ya wakala au siyo?” Aliuliza Willy maana neno Agence ina maana wakala.

“Ndiyo kampuni yetu ni wakala ya makampuni mengi sana ya nje ambayo yanapenda kufanya biashara na Zaire,” alijibu Tete.

“Ahaa, kumbe tuko kwenye kazi sawa maana hata mimi kampuni yangu inashughulika na shughuli za Wakala, inaitwa 'Zambia Overseas Agency'. Hata safari yangu hii kama Mwadi alivyokueleza ni ya mapumziko na kikazi. Huenda itakuwa vizuri nikifika ofisini kwenu ambako naweza kuonana na wakubwa wako wa kazi ambao wanaweza kunieleza vizuri juu ya makampuni ambayo naweza kufanya nayo biashara”, Tete alifurahi sana kuona kuwa ameweza kukutana na mfanya biashara ambaye angeweza kuletea kampuni yake biashara. Maana ofisini kwao walikuwa wameelezwa kuwa kila walipo wao ni wawakilishi wa makampuni yao.

“Itakuwa vizuri. Kampuni yetu ni kampuni kubwa na inajulikana sana. Hata imeweza kuwa Wakala wa makampuni ya Afrika Kusini katika Zaire. Kwa mfano miezi miwili iliyopita tuliweka saina mkataba kwa niaba ya Serikali ya Zaire, mkataba ambao ulikuwa kati ya Serikali na kampuni moja ya Afrika Kusini iitwayo Grindrod Cots Stevedoring ya mjini East London wa kusafirisha tani 125,000 za shaba ziendazo Japan kwa kupitia kwao. Hii itakuonyesha jinsi kampuni yetu ilivyo maarufu. Mimi naamini kuweza kuwa na uelewano mzuri zaidi kati yetu na makampuni ya Zambia kuliko nchi nyingine yoyote”, Tete alisisitiza.

Kwa kusikia maneno haya moyo wa Willy ulipiga haraka haraka maana maelezo haya yalikubaliana sana na maelezo aliyopewa na Robert juu ya uhusiano wa Zaire na Afrika Kusini kibiashara. Vile vile alikumbuka wasiwasi wa Robert kuwa makampuni yanayoshughulikia maslahi ya wafanyabiashara wa Afrika Kusini, yanaweza kutumiwa kijasusi na nchi hiyo ambayo iko mstari wa mbele katika kupinga maendeleo ya nchi huru za Kiafrika na zile ambazo bado zinapigania uhuru. Bila kuonyesha dukuduku lake Willy alisema, “Ni jambo la bahati sana kuonana mimi na wewe, na inabidi nimshukuru Mwadi kunifahamisha kwako. Hii kampuni yenu ni ya Kizaire au ni ya watu kutoka nje?” Aliuliza Willy.

“Hii kampuni inaongozwa na Wabelgiji. Lakini wamekuwa hapa kwa muda mrefu sana, na wameweza kufanya biashara na nchi karibu zote za Afrika.

“Vizuri basi, nitafika ofisini kwenu kesho. Ofisini zenu ziko wapi?”

Tete alifungua kimfuko chake kidogo akatoa kadi ya biashara akampa Willy, “Hiyo itakupa maelezo yote.” Tete alisema. Willy aliangalia kadi hiyo akajibu, “Asante sana.”

“Mimi nitaondoka Mwadi, maana nilikuwa napita tu. Muteba alikuwa amenipigia simu tuonane 'Vis-a-vis bar ambako O.K Jazz wanapiga leo, lakini nimemsubiri sana hakuja. Nilitoka nikaenda nyumbani kwake hayuko vile vile nilifikiri yuko hapa lakini pia hayupo. Nikimuona atanikoma.” Tete alimweleza Mwadi.

“Lazima atakuwa amepata matatizo. Ninavyomjua Muteba alivyokufa juu yako, hawezi kuwa hakufika hivi hivi tu,” Mwadi alijibu huku akitabasamu.

“Wacha maneno yako,” alijibu Tete huku akisimama. Willy na Mwadi nao walisimama na kumuaga mrembo huyu.

“Haya tutaonana kesho,” Willy alisema.

“Vizuri, mimi nitakuwepo. Maana ukifika tu mapokezi utanikuta mimi pale,” alijibu Tete.

Aliondoka taratibu, huku mamia ya watu waliokuwepo hapa wakifurahia miondoko ya mrembo huyu wa aina ya peke yake. Willy alijiona mtu mwenye bahati sana kufahamiana na mrembo huyu kwani hata watu walibaki wakiwaangalia Tete alipokuwa ameondoka.

Willy na Mwadi waliendelea kunywa na kucheza kwa muda mfupi, na kwa vile Mwadi alianza kulewa aliomba waondoke. Walipotaka kuondoka vijana wa Veve wakiongozwa na mwanamuziki mashuhuri Verckys walipiga wimbo mmoja uitwao 'Toweli Nini' yaani 'Mnagombea nini.' “Muziki mtamu sana huo, tukacheze ndiyo uwe wa mwisho”, alishauri Mwadi.

Baada ya wimbo huu waliondoka na kelekea Bandalugwa nyumbani kwa Mwadi, na ilikuwa saa tisa walipofika nyumbani. Wakiwa wana nishai ya kutosha, waliingia ndani na tayari kwa kupumzika.

“Willy mimi ninakupenda sana,” alisema Mwadi huku akijitoa kabisa kwa Willy.

“Na mimi vile vile,” alisema Willy akimvuta na kuanza kumbusu, busu motomoto. Hali hii ya kimapenzi iliwajaa, wakaanza kufanya mapenzi ambayo yaliwafanya wote kutosheka kabisa. Wakiwa wanapumzika, Mwadi akiwa anambabata Willy kifuani alisema. “Willy mimi mapenzi yangu kwako yalianza toka siku ile uliyoingia tu pale hotelini. Nilipokuona tu mwili wangu wote ulisiimkwa sana nikajua nimepata mwanaume ambaye mwili wangu umempenda, na niliamini kuwa wewe tu ungeweza kunitosheleza kimapenzi.

“Kweli,” alijibu Willy huku akisikia usingizi.

“Kweli kabisa, hata kuna mtu mmoja huwa ananilipa mimi kwa kumpatia majina ya wageni wanaoingia hapo hotelini, hata jana aliniomba majina ya watu walioingia hapo hotelini kwetu, lakini bila sababu moyo wangu haukupenda nimpe jina lako, sijui kwa nini nilifanya hivi, huenda ni kwa sababu nilikuwa nimekupenda sana kuanzia wakati huo”. Kusikia maneno haya Willy aliyekuwa anasinziasinzia, mara moja usingizi wote ulimtoka na akili yake ikawa katika hali ya tahadhari.

“Mtu gani huyo”, aliuliza Willy kana kwamba hana haja ya kujua.

“Mtu mmoja anaitwa Kabeya,”

Kwa kutaja jina hili Willy alistuka.

“Majina hayo huwa anayahitaji kwa nini?” Willy aliuliza.

“Sijui mimi huwa anayahitaji kwa ajili gani. Huwa nikisha mpa ananilipa basi yanakwisha. Sasa jana aliniambia nimpe majina ya watu walioingia jana na niendeleo kumpa majina hayo mpaka atakaponiambia yeye mwenyewe, akasema atanilipa mara tatu ya kawaida.

“Huyu mtu anafanya kazi wapi?”

“Aliwahi kuniambia siku moja kuwa anafanya kazi gereji moja iitwayo G.A.D. iliyoko barabara ya T.S.F. sehemu za Gombe.”

“Na unasema jina langu hukumpa?”.

“Ndiyo, kwani nilifanya vibaya?”.

“Hapana, ulifanya vizuri sana”, Willy alifikiria habari hizi alizokuwa amezipata, akaonaa mtu mwenye bahati sana, na kufikiria kuwa Mungu ndiye alikuwa amepanga yeye apendane na msichana huyu ili aweze kupata habari hizi alizozipata. Kwani huyu Kabeya ndiye kile kikaratasi alichokikuta mfukoni mwa yule mtu aliyejiua kilikuwa kikimtaja. Hivyo alijua sasa amepata mahali pa kuanzia kesho yake. Alipanga kesho yake aende kwenye gereji hii ya G.A.D. ajue nini kiko pale.

Mawazo haya yakiwa yanapita kichwani mwake alimvuta Mwadi na kumkumbatia.

Usiku huu ambao Willy alikuwa na pilika za starehe, wenzake nao walikuwa na mengi. Baada ya kupika chakula na kula, vijana hawa waliendelea na vinywaji

huku wakiangalia 'Televishen' ambako kulikuwa na kipindi cha muziki wa bendi ya Lipua Lipua ambao walifanya na maonyesho.

Waliendelea hivyo mpaka ilipotimia saa sita za usiku.

“Nafikiri sasa twende ili tukapate kupumzika, maana huenda kesho itakuwa siku ya pilika nyingi”, Kofi alishauri.

“Hata mimi naona hivyo”, Ozu alijibu.

“Si lazima mwende, mnaweza kulala hapa, ili tupate muda zaidi wa kuongea. Nyumba hii ina vyumba chungu nzima, wote wanne tunaweza kuishi hapa”, Robert alishauri kutaka kwa vile alivyopendezwa na ugeni wa vijana hawa.

“Haitakuwa vizuri kiusalama”, aliasa Ozu.

“Siku moja tutakapokuwa tumemaliza shughuli hii, ni lazima mje tukae wote hapa kwa mapumziko.”

“Tuombe Mungu tuvuke salama,” alijibu Kofi.

Walimaliza vinywaji vyao na kuondoka. Waliingia ndani ya gari la Robert ili Robert aweze kuwapeleka mahotelini kwao. Walipofika kwenye kona ya 30 Juin na 8 Armee ambapo ndipo Hoteli Tip Top imejengwa. Ozu alimshauri Robert watelemke hotelini hapo wapate bia moja moja ya kulalia.

“Mimi nimeisha tosheka”, alijibu Robert, “Huenda niwasindikize nyinyi”.

“Kama ni hivyo wewe tuache hapa sisi tutajua namna ya kwenda,” alijibu Kofi.

“Ndiyo, wewe tuache hapa, kwa Kofi hapa ni karibu anaweza kwenza kwa miguu mpaka Intercontinental bila taabu na mimi nitachukua tekisi mpaka hotelini kwangu,” Ozu alikubaliana.

“Haya vizuri, tutaonana kesho,” Robert alijibu na kuagana nao hawa wenzake. Ozu na Kofi waliteremka na kungia Hoteli Tip Top na kwenda moja kwa moja mpaka kwenye kaunta ya baa na kuagiza Primus mbili baridi. Walikunywa huku wakizungumzia hali halisi kama walivyokuwa wakiiona kwa wakati huu.

“Mimi najisikia mchovu sana, ngoja nikalale,” Kofi alieleza.

“Sawa hata mimi najisikia uchovu. Mimi nitachukua hapa tekisi inirudishe hoteli kwangu,” alijibu Ozu.

Waliongozana nje ya hoteli wakaagana.

“Njoo hotelini kwangu asubuhi baada ya chemsha kinywa. Utakuta tayari nimeisha zungumza na Willy au Robert,” Ozu alieleza.

“Nitegemee kiasi cha saa mbili hivi. Jihadhari lakini,” Kofi alimuaga.

“Na wewe jihadhari vile vile”, alijibu Ozu akimwangalia Kofi anaelekea Intercontinental kwenye barabara hii ya Armee. Ozu alibaki akingojea tekisi yoyote ambayo ingepita au kufika pale aisimamishe.

“Vipi, mbona umesimama hapa?,” askari anayechunga magari hapo nje ya Tip Top alimjia Ozu na kuuliza.

“Mimi nangojea tekisi nataka kwenda Regna Hoteli”, Ozu alijibu.

“Lo, saa hizi tekisi hapa ni shida sana, afadhali uende Intercontinental ambapo kuna tekisi masaa ishirini na nne”, askari alimshauri, Ozu aliona mawazo haya yanafaa.

“Asante kwa kunishauri, nitafuata tekisi Intercontinental”, akifuata barabara hii ya 8 Armee. Alimuona Kofi kwa mbele, lakini alikuwa ameshaenda mbali kiasi cha kwamba hata angetembea haraka namna gani asingemkuta. Hivi alikata kshauri kutomharakia.

Kofi ambaye alitembea kwa hatua ndefu, alitembea kwa tahadhari kubwa maana mawazo yake yalikuwa yakifikiria sana kazi hii waliyokuwa wamefikia mjini hapa kushughulikia. Akiwa anatembea pembeni mwa barabara na chini ya vivuli vya nyumba alivuka mtaa wa Asemblee na kuendelea na 8 Armree kwenye upande wa shule ya Athene'e de la Gombe, ambapo magari mengi yalikuwa yameegeeshwa. Gari moja kati ya magari haya yaliyokuwa yameegeeshwa liliwasha taa ambazo zilimmulika Kofi usoni na kuzimishwa tena. Kitendo hiki kilimfanya Kofi asimame kuona kama gari lile lilitaka kuondoka. Kwa tahadhari yake alikata shauri avuke barabara kwa upande wa pili tayari kwa kuingia kwenye maegesho ya magari ya Intercontinental, ambayo vile vile kuna mlango wa kuingilia hotelini. Kabla hajavuka alisimama nyuma na akaona kwa mbali mtu anakuja. Alipoangalia vizuri aliona miondoke ile ni ya Ozu, akakata shauri asimame amngojee ajue kwa nini anamfuata, vile vile alikuwa na wasiwasi na lile gari lililowashwa taa, hivi aliweka mkono wake kwenye bastola yale aliyokuwa ameiweka ndani ya mfuko wa ndani ya koti.

Kwa silika, bila kujua kwa nini . Kofi aligeuka nyuma kama umeme huku akiwa ametoa bastola yake lakini mkono ulipigwa kareti na bastola yake ikaanguka chini. Kuangalia akajikuta anaangalia ndani ya midomo ya bastola mbili.

“Usifanye lolote la sivyo utauawa mara moja,” alielezwa. Gari lile lililowashwa taa lilipiga moto likajitokeza kwenye maegesho na kupiga breki mbele ya Kofi na milango ikafunguliwa. “Ingia ndani,” Alielezwa Kofi akisukumwa ndani. Aliingia na wale watu waliokuwa wamemvizia nao wakaingia ndani na gari likaondoka. Tukio hili lilichukua chini ya dakika moja.

Ozu ambaye aliona tukio hili lakini kwa mbali kidogo alikimbia huku akijificha ndani ya vivuli vya michongoma iliyokuwa imezunguka nyumba zilizo sehemu hii, Lakini hakuweza kuwahi tukio lenyewe lilifanywa kwa ujuzi wa hali ya juu kiasi kwamba lilichukua muda kidogo sana. Alipoona Kofi ameingizwa ndani ya gari na gari linaondoka alirudisha bastola yake kwenye mfuko wa 'Jaketi' alilokuwa amevaa, akatoa funguo malaya za gari la Kijapan. Yaani funguo hizi zinaweza kufungua gari lolote lililotengenezwa na kampuni ya magari yoyote ya Japan. Aliharakisha kutafuta gari la Kijapan katika gari zilizokuwa zimeegeshwa barabarani. Gari ya kwanza kuiona ilikuwa Mazda Delux 1800. Alifungua akaingia ndani na kuwasha gari, na kuondoka kama mshale akalifuata gari lililokuwa limemteka nyara Kofi.

SURA YA KUMI

“GARAGE PAPADIMITRIOU”

Gari hili lilipotoka barabara ya 8 Armee liliingia mtaa wa 30 Juin, Ozu alilifuata kwa mbali akiwa anafuata taa za nyuma na lile gari, kiasi ambacho kisingeweza kuwagutua watu waliokuwa ndani ya gari hilo.

Kofi ambaye sasa mawazo yake yalikuwa yameishatengamaa, aliwaangalia watu waliokuwa wamemvamia. Ndani ya gari hili mlikuwa na watu wanne, yeye wa tano. Dereva alikaa mbele na mtu mmoja, na nyuma walikaa watu watatu pamoja na yeye, yeye akiwa katikati. Watu hawa wawili walishikilia bastola tayari tayari kabisa kwa msukosuko wowote. Hakuna neno lolote lilizungumzwa ndani ya gari hii. Kutoka mtaa wa 30 Juin mtaa wa Victimes de la Rubelion. Ozu alisimama, maana kulikuwa hamna magari yaliyoingia Juin mtaa wa Victimes de la Rubelion isipokuwa gari lililomteka nyara Kofi. Kusudi asiye akawagutua, alingojea waende mbali kidogo ndipo yeye akatokeza kwenye mtaa huu wa Juin mtaa wa Victimes de la Rubelion. Gari la mbele lilienda kisha likaonyesha taa ya kuwa lilikuwa linaingia mtaa wa Kabambare. Ozu aliongeza mwendo nae akaingia Kabambare kwa mwendo mdogo sana. Kwa mshangao wake aliona gari lile likipita kwenye lango moja, na kuingia ndani. Ozu alipofika sehemu ile alikuta lango limefungwa na walinzi wasiozidi watatu wakiwa mlango hapo. Alipoangalia jengo lenyewe liliandikwa 'GARAGE PAPADIMITRIOU', aliangalia mambo yote haya huku akiendesha kwa mwendo kasi kabisa, alipokuwa amefika sehemu hii, ili asiweke mashaka yoyote kwa wavamizi wa Kofi ambao alihisi wangukuwa kundi kubwa.

Jengo hili la Garage Papadimitriou lilikuwa karibu na njia panda ya Kabambare inapokutana na mtaa wa Assossa. Kulikuwa na nyumba nyingine tatu kutoka kwenye gereji hii hadi Assossa. Hivi Ozu alipitiliza na kuingia mtaa wa Assossa ambako aliegesha gari na kutoka ndani na kurudi tayari kutaka kujua nini kinaendelea huko 'Garage Papa'.

Gari lililokuwa limemteka nyara Kofi, pamoja na abiria wake lilipoingia mtaa wa gereji hii, liliendeshwa moja kwa moja mpaka ndani kabisa ambako kulikuwa na nyumba ambayo ndani mlikuwa na ofisi ya gereji hii. Kofi aliweza kuwaona walinzi watatu waliokuwa kuwenye lango. Ndani ya ngome ya jengo hili ambayo ilikuwa imejengwa kwa matofali ya saruji na yenye urefu usiopungua mita tisa, mlikuwa na uwanja mkubwa sana. Ndani ya uwanja huu mlijaa magari mengi

ambayo yalikuwa yamekuja kutengenezwa. Wakati wanayapita magari haya kuelekea kwenye ofisi. Kofi aliweza kuona vivili vya watu waliokuwa wamesimama kando kando mwa njia hii iliyokuwa inaelekea ofisini. Hivi alihisi kuwa kulikuwa na ulinzi kabambe ndani ya ngome ya gereji hii. Kusema kweli kwa mara ya kwanza moyo wake ulipata wasiwasi.

Gari liliposimama milango ilifunguliwa na watu wengine wawili ambao walijitokeza ndani ya magari mabovu yaliyokuwa yameegeshwa ndani humo huku wakiwa na bastola zao mikononi tayari kwa kuzitumia.

“Teremka, na tafadhali usijaribu ujanja wowote, kwani kwa kufanya hivyo utakuwa unaomba kifo chako mapema zaidi,” Kofi alielezwa na mmoja wa wavamizi wake.

“Sawa bwana mkubwa, mimi niko chini ya ulinzi wako hivyo usiwe na wasiwasi na mimi hata kidogo,” alijibu Kofi kwa sauti ya kejeri. Waliandamana chini ya ulinzi mkali sana na kuingia ndani ya ofisi.

Pale mapokezi walimkuta mtu mwingine naye akiwa na bastola mkononi ambaye aliwaeleza, “Nendeni ndani ya chumba cha mkutano bwana mkubwa anawangojea huko”. Walienda moja kwa moja mpaka kwenye chumba kilichokuwa kimeandikwa 'CHUMBA CHA MKUTANO', yule mtu aliyekuwa mbele aligonga mara tatu, kisha mlango ukafunguliwa na mtu mwingine kwa ndani ambaye vile vile alikuwa na bastola mkononi.

“Ingieni,” mtu huyu aliwaamru. Kundi zima liliingia ndani ya chumba hiki cha mkutano ambako walimkuta mtu mmoja mwenye asili ya Kiasia amekaa huku akiwa anazungumza na walinzi wake watatu.

“Haya huyu aliye mbele yako ni Mike Kofi ambaye tumemleta kwa mazungumzo nawe kama ulivyoagiza,” alisema mmojawapo wa watu waliokuwa wamemteka nyara Kofi, ambaye alionekana kuwa kiongozi wao.

“Asante sana, karibu bwana Kofi. Samahani sana kwa kuletwa namna ulivyoletwa, lakini natumaini hakukuwa na njia nzuri zaidi ambayo ingeweza kukushawishi uje kuzungumza ila njia iliyotumika peke yake. Karibu keti kwenye kiti,” Papa alieleza. Kofi ambaye alikuwa amesimamishwa upande mwingine wa meza, alivuta kiti na kukaa bila kusema kitu. Wale walinzi wake kila mmoja wao alichukua nafasi kwenye ukuta, wakiwa wamezunguka meza kila mmoja wao bastola mkononi. Baada ya kukaa, na mwili wake ukiwa katika tahadhari ya hali ya juu kabisa Kofi aliinua macho yake ambayo yalionana ana kwa ana na macho ya

yule waliyekuwa wanamuita Papa. Macho yao yalipoonana wote walitambuana kwa kutokana na ujasiri katika macho yao kuwa wote walikuwa watu katika mchezo mmoja. Kofi alishangazwa sana kupambana na mtu mwenye asili ya Kiasia jambo ambalo hakulitegemea kabisa. Akiwa anasubiri nini atafanyiwa alijiweka tayari kuyakabiri mambo yote yatakayomtokea kiume. Wazo ya kwamba Ozu aliona mambo yaliyompata ilimtia moyo, lakini vile vile alikata tamaa kupata msaada kutoka kwake kwa sababu ulinzi aliokuwa ameuona hapa nje, kwa mtu mmoja kuingia ilikuwa kazi bure.

“Bwana Kofi nina maswali machache ya kukuuliza. Ningependa kukueleza kuwa, sitapenda kutumia njia yoyote ya kukushawishi ila napenda ujibu mwaswali yangu kwa hiari yako. Lakini kama utapenda nitumie kishawishi basi utakuwa umenilazimisha nami sitakuwa na budi kufanya hivyo”, alisema Papa taratibu.

“Bwana Papa, ninaomba niulize na mimi swali moja kabla hujaanza kuniuliza,” aliomba Kofi.

“Ehe, uliza”, Papa alimjibu.

“Wewe ni nani na kwanini niko hapa?” Aliuliza Kofi.

“Baada ya muda mfupi utajua kwanini uko hapa, na vile vile utanitambua mimi ni nani,” alijibu Papa kwa jeuri.

Kofi alielewa kwa ufasaha maana ya maneno haya na haikuwa mara ya kwanza kuyasikia hivyo alijibu, “Sawa.”

“Bwana Kofi wewe pamoja na mwenzako Petit Osei kwa jina la bandia Petit Ozu, mmefika hapa mjini kwa shughuli gani?” Aliuliza Papa huku akimwangalia Kofi kwa macho makali sana. Kofi kusikia jambo hili la kutambuliwa kiundani kabisa yeye pamoja na Ozu kulimshitua sana ingawaje sura yake haikuonyesha. Alijua kuwa mara hii walikuwa wamepambana na kundi hatari kabisa, lenye upelelezi wa hali ya juu. Mara moja alihisi lazima watu hawa watakuwa ni majasusi wa Shirika mojawapo la kijasusi ambalo ni maarufu sana.

“Bwana Papa, kama utanisamehe ningependa uniulize vitu vinavyonihusu mimi mwenyewe, kwa sababu mimi nimeingia hapa peke yangu na wala mtu unayemzungumzia simjui. Nikijibu swali lako mimi nimefika hapa kwa shughuli za kibiashara,” alijibu Kofi kwa sauti ya kutokujali kabisa.

“Kitu ninachotaka ni kunieleza ukweli, kama usiponieleza ukweli utanifanya nitumie vishawishi na nikivitumia utasikitika kwanini hukutaka kushirikiana nasi.

Bila kupoteza muda nieleze kwa ufasaha nyinyi mmefika hapa kufanya nini. Maana mimi najua shughuli zenu na kuniongopea kutazidisha hasira yangu bure”, alisema Papa kwa hasira.

“Kwanza nataka kujua namjibu nani? Nyinyi mmenileta hapa kwa kikuku. Sasa sielewi nyinyi mnawakilisha serikali au nani. Maana kama mna mashaka na kuingia kwangu hapa mnipeleke polisi na vile vile mnipe nafasi ya kumwarifu balozi wangu”. Alijibu Kofi huku akinunua muda.

“Huyu hawezi kueleza chochote bila kishawishi Papa,” alishauri yule mtu aliongoza msafara kumteka nyara Kofi.

“Kwa usalama wako jibu swali langu. Na kwa taarifa hapa ulipo huna haki ya kuuliza jambo lolote, ni aidha ujibu kwa hiari yako au utajibu kwa lazima,” Papa alimweleza kama onyo la mwisho.

“Sawa kwanini nisiwe na haki yoyote katika nchi huru ya Kiafrika wakati sikufanya lolote. Tatizo ni dogo sana nieleze na mimi nikueleze,” Kofi alijibu kwa dharau kubwa. Jambo hili lilimchukiza Papa, na akaona siasi ingempotezea muda mwingi na njia rahisi ilikuwa kupata maelezo aliyoyataka kutoka kwa mtu huyu kwa njia ya nguvu. Aliwaangalia wale wavamizi wa Kofi akawatingishia kichwa. Kofi aliona ishara hii akajua nini kitafuata hivi akaweka mwili wake tayari.

Wale watu walimwendea Kofi wakamvuta toka kwenye kiti. Kofi alisimama wakamshika huku watu wawili na huku wawili na mmoja akasimama mbele yake na kukunja ngumi tayari kwa kumtwanga masumbwi. Mmoja wa walinzi wa Papa alijaribu akiwa ameweka bastola yake tayari kabisa kwa tukio lolote. Kofi aliangalia yote haya na kujiweka tayari kwa kipigo. Alijua kama angejaribu chochote hapa asingeweza maana hawa watu walikuwa wengi na walikuwa na silaha. Kufanya lolote kungekuwa na maana ya kuuawa mara moja, hivyo alionelea aendelee kupoteza muda akitafuta nafasi nzuri kama itatokea jambo ambalo hakulitegemea.

Yule jamaa alianza kumtwanga masumbwi babu kubwa tumboni. Kofi alistahamili kwa muda mrefu mauivu haya haya makali aliyoyapata lakini mwishowe hakuweza kustahamili tena akasema.

“Ngoja ngoja nitawaeleza mnachotaka!”

Papa ambaye alikuwa akiangalia kwa makini kipigo hiki cha kuridhisha aliamru wamuachie ili aweze kuwaeleza.

“Nime... nime... ku... kuja... kufanya... biashara”, alijibu Kofi kwa kutetemeka.

“Aa, aa, aa, bado ananitania ongeza mara mbili zaidi”, aliamru Papa na kipigo kikaanza tena.

Ozu ambaye alikuwa ameacha gari mtaa wa Assossa, alirudi kuja kutafuta namna ya kuingia ndani ya gereji hii ajue nini kinafanyika. Alitoa bastola yake tayari tayari. Bastola ilikuwa sailensa. Alipita kwenye vivuli vya nyumba zilizokuwa karibu ya gereji kwa kuvizia. Alipofika kwenye nyumba iliyokuwa inapakana na gereji alisimama na kujibanza sawa sawa na ua wa michongoma iliyokuwa imezunguka nyumba hii. Alipochungulia aliona mlinzi mmoja anazunguka zunguka upande ule aliokuwa yeye yaani kwa nje ya ukuta uliokuwa umezunguka gereji. Hii ilionyesha kuwa zaidi ya kuwa na walinzi ndani ya gereji hii kulikuwa na walinzi wengine nje.

Hivi Ozu alikata shauri amvizie huyo mlinzi kwanza. Karibu na alipokuwa amejibanza aliona mti mkavu. Alijivuta taratibu halafu akautupa na ukuaanguka katikati ya ukuta na ua wa gereji na ua wa nyumba ambako yeye alikuwa amejibanza. Yule mtu kusikia kishindo hiki aligeuka na kuja kuangalia ni kitu gani kilikuwa kimeanguka. Alikuwa bastola mkononi na akitembea kwa uangalifu sana. Ozu alijibanza akiwa ameinama na kufichwa na kivuli cha michongoma. Yule mtu alipofika karibu aliwasha tochi, akamulika ule mti halafu akamulika upande ule aliokuwepo Ozu lakini alimulika kwa juu hivi hakumuona Ozu ambaye alikuwa tayari kabisa kwa mapambano. Alipogeuka kumulika sehemu nyingine na wakati huo akiwa hatua moja toka pale Ozu alipokuwa amejibanza. Ozu alimrukia na kumpiga kareti ya shingo na bila hata kupiga kelele mtu huyo alizirai pale pale. Ozu alimgonga zaidi ili kuhakikisha kuwa asingeweza kuamka masaa yasiyopungua kumi. Alimvuta akamlaza kwenye kivuli cha michongoma akachukua bastola yake na tochi akajiweka tayari kwa pambano jingine.

Akiwa anautawala upande huu wa ukuta, alikwenda mpaka kwenye pembe ya kuelekea nyuma nyuma ya ukuta huu wa ua wa gereji. Alipofika hapa alichungulia akamwona mlinzi mwingine aliyekuwa anazunguka zunguka huku nyuma. Ozu alimpigia mlinzi mluzi wa kumwita. Na huyo mlinzi alifikiria kuwa huyo ni mwenzake akaja mbio mbio. Alipokaribia kabisa na kabla hata hajamwangalia Ozu vizuri, Ozu alimuonyesha kidole atazame kule alikokuwa akionyesha. Mtu huyu alipopotea kuangalia kule tu. Ozu alimpiga kareti ya shingo nae akazirai pale pale. Baada ya kumhakikisha kuwa hangeweza kuamka mpaka asubuhi. Ozu alimvutia

kwenye shimo la taka lililokuwa karibu, yeye akasonga mbele. Alizunguka kwa nyuma mpaka akafika kwenye pembe ya nyuma na ile ya upande mwingine.

Huku nako alikuta kuna mlinzi, akamfanyia 'ssss'. Yule mlinzi nae akadhani ni mwenzake alikuja upande ule aliokuwa Ozu mbio mbio. Ozu akajibanza kwenye ukuta akajiweka tayari. Vile vile kwa sababu kwenye kona hii kulikuwa na mwanga kidogo alijibanza kusudi mtu huyu asiye akamtambua kabla hajafika karibu. Alipokuwa amekaribia alisimama akafungua mdomo wake kutaka kusema kitu lakini kabla hajasema akashtuka, nafikiri alimtambua mtu huyu hakuwa mlinzi mwenzake. Ozu hakupoteza muda, mtu huyu aliposhtuka tu alimpiga risasi na yule mtu akafa pale pale.

Aliangalia huku na kule kama kulikuwa na walinzi zaidi lakini hakuona mtu. Hivi alijua kutakuwa kumbaki wale walinzi watatu wa mbele ambao alikata shauri asiwagutue ila tu lililobaki kuingia ndani ya ngome ya gereji hii kwa kupanda ukuta wa sehemu hii ya nyuma. Kama nilivyokwisha kukueleza ukuta wa ngome hii ulikuwa kiasi cha mita tisa hivi. Ozu alitafuta mti mgumu kiasi cha kuweza kubeba uzito wake, ili umsaidie katika kupanda ukuta. Kwa ufundi na ujasiri mwingi aliweza kupanda na kushika juu kabisa ya ukuta. Alipokwisha kufanya hivi alisukuma ule mti ukaanguka chini. Alipochungulia ndani ya ngome hii akajikuta anaangalia nyuma ya nyumba na kati ya hii nyumba na ukuta wa ngome kulikuwa na nafasi kubwa ambayo ilikuwa tupu. Sehemu hii haikuwa na mlinzi. Alipokuwa anahakikisha kuwa hakukuwa na hatari yoyote, Alivuta mwili wake wote akalalia tumbo juu kabisa ya ukuta kisha akajining'iniza kwa ndani, halafu akajiachia na kuangukia ndani.

Alianguka kwa kishindo, hivyo upesi sana alikimbia mpaka kwenye ukuta wa nyumba akajibanza na kusikiliza kama angesikia lolote. Ghafla alisikia nyayo zinakuja tokea upande wa kulia wa nyumba. Hivyo alikimbia bila kishindo akaenda kujibanza kwenye pembe hii ambayo nyayo zilikuwa zikisikika zinatoka. Mtu akiwa na bastola na tochi mkononi akajitokeza. Mtu huyu bila kumwona Ozu alimulika mbele yake huku akitembea taratibu na kumpita Ozu. Alipompita tuu Ozu alimrukia akamtia kabali kiasi cha kukata roho, alimlaza taratibu chini, halafu akakaa kimya tena kusikiliza kama kulikuwa na kitu kingine. Aliposikia kimya kwa nje alijiweka tayari kwa mapambano zaidi.

Katikati ya nyumba hii mlikuwa na dirisha moja kubwa. Dirisha hili lilikuwa la vioo na mapazia makubwa ambayo yalifunika dirisha hili kwa ndani. Ndani ya chumba ambacho dirisha hili lilikuwa mlikuwa mnawaka taa, hivi Ozu alihisi,

huenda mngekuwa na watu. Alienda mpaja nyuma ya dirisha hili akasikiliza. Alisikia watu wanazungumza. Alipilichunguza dirisha hili lilikuwa limefungwa kwa ndani. Kuona hivi, alivua peke yake ya almasi ambayo alikuwa amepewa na mchumba wake siku waliyochumbiana, akaishika vizuri halafu akaitumia kukata kioo cha dirisha hili. Alikata kipande cha kutosha na kwa uangalifu kisije kikaanguka, alikitoa na kukiweka chini taratibu.

Kisha pole pole alivuta sehemu ndogo ya pazia ambayo ilimwezesha kuona ndani. Ndani aliona watu wawili ambao walikuwa wamekaa kwenye meza wameelekeza migongo yao kwake. Alipoona hivi alivuta pazia zaidi aweze kuona hasa chumba hiki kilikuwa na nini zaidi, akakuta kilikuwa chumba cha simu. Watu hawa walikuwa ni maopereta wa simu na 'radio-call'. Alimsikiliza mmoja wao akizungumza na 'radio-call' na alipomaliza kuzungumza akamwambia mwenzake,

“Nenda kamwambie Papa kuwa mpaka sasa hivi Ozu hajafika hotelini kwake na wala hawajui yuko wapi”, Yule mwenzie alisimama na kuondoka. Ozu alisisimkwa aliposikia maneno haya. Aliinua bastola yake ghafla akavuta pazia kwa nguvu yule mtu kugeuka ili kuangalia nini kinatokea Ozu alimpiga risasi katikati ya paji la uso akafa pale pale. Kwa sababu bastola yake ilikuwa na sailensa tukio hili halikuwa na sauti yoyote. Haraka haraka Ozu alipitisha mkono ndani ya sehemu ya kioo aliyoikata akafungua dirisha lote, akapanda na kutumbukia ndani ya ofisi hii ya simu. Kisha alirudisha dirisha halafu akavuta pazia na kuweka sehemu ile katika kawaida yake.

Alipokwisha kufanya hivi aliangalia ofisi hii, mlikuwa na taa mbili moja ilining'inia katikati ya dari na nyingine ilikuwa kwenye ukuta karibu na meza ya kupokelea simu. Ozu alitafuta swichi ya taa hizi akakuta zote ziko karibu na mlango wa kutokea nje. Alienda akajaribu swichi hizi kuona ni ipi inawasha taa ipi. Alipokwisha gundua, alizimisha taa ile ya karibu na meza, kisha akatoa pakiti yake ya sigara mfukoni akaifungua halafu akatoa karatasi la ndani linalong'aa kama fedha. Halafu akatoa balubu ya taa hiyo ya mezani akaizungushia karatasi hili la sigara, ambalo alikuwa amelikunja kiasi kwamba ile sehemu ing'aayo ndiyo ilizunguka sehemu yote ya chini ya balubu kisha akairudisha ndani ya soketi yake.

Mambo yote haya aliyafanywa haraka haraka, huku akimsubiri yule mtu aliyekuwa ametumwa. Ile maiti ya yule mtu aliyempiga risasi alimwinamisha vizuri kwenye meza halafu akaenda kwenye mlango kumsubiri yule mtu mwingine. Haukupita muda mrefu akasikia mtu anakuja akajiweka tayari. Mtu huyo alifungua mlango wa nguvu, na kuingia moja kwa moja. Alipogutuka kuona damu zilizokuwa

zimetapakaa mle ndani Ozu alimwekea bastola sikioni akamwambia. “Usijitingishe tafadhali”.

Ozu alirudisha mlango. “Papa ni nani?”. Ozu aliuliza.

“Ndiye mwenye gereji hii”, alijibu yule mtu huku akiwa anatetemeka vibaya sana.

“Yule mtu aliyetekwa amewekwa wapi?”

“Yuko chumba cha mkutano wanamhoji”.

Ozu kusikia hivi moyo wake uliingiwa na matumaini kuwa Kofi alikuwa bado yuko hai.

“Sasa utafanya kama nitakavyokuambia la sivyo hayo yaliyomkuta mwenzio, na wewe yatakupata”, Ozu alimtisha.

Kwa vile mtu huyu hakuzoea mambo kama haya alikubali amfanyie lolote mtu huyu asiye na yeye akauawa, naye alikuwa akiogopa sana kifo.

“Usiniue mimi nitakufanyia lolote unalotaka.

“Ndani ya chumba cha mkutano mna watu wangapi?”

“Yumo Papa, walinzi wanne na yule mtu waliyemleta.

“Na wewe kazi yako ni nini?”

“Mimi ni karani tu. sijui mambo yoyote ya kupigana, tafadhali usiniue,” yule kijana alizidi kuomba, na aliyokuwa akisema ilikuwa ni kweli.

“Walinzi wengine wako wapi?”.

“Wako nje, ila mmoja yuko mapokezi”.

“Anaweza kumuona mtu akiwa anatokea huku, usinidanganye.”

“Hawezi maana yeye analinda mtu asiingie ndani bila ruhusa.”

“Sasa wewe na mimi tutatembelea chumba cha mkutano, na tutaingia kwa kufuata sheria za hapa na wewe unazijua. Kumbuka ukijaribu ujanja wowote nitakuua, lakini ukifuata masharti yangu hutapata taabu yoyote.”

“Sawa,” alijibu yule mtu akiwa bado yuko katika hofu kubwa. Ozu alifungua mlango, alimtanguliza yule mtu kisha akarudisha mlango. Akiwa anashikiria bastola yake mgongoni mwa huyu mtu waliongozana ukumbini kana kwamba hakukuwa na kitu kibaya kati yao. Walipopita vyumba viwili na kufika cha cha

tatu, yule mtu akanong'ona, “Chumba chenyewe ni hiki.” Ozu alikiangalia kilikuwa kimeandikwa.

“Chumba cha mkutano”.

“Najua mna namna yenu ya kugonga ili kujitambulisha, usije ukagonga vingine unasikia?” Ozu alimweleza.

“Ndiyo”, alijibu.

“Haya gonga sasa”, Ozu alimwamrisha.

Ndani ya chumba Kofi alikuwa anaendelea kunyukwa.

“Nimekwambia sasa hivi, ongeza mapigo mara mbili,” Papa aliamrisha. Yule mtu aliyekuwa anampiga Kofi, alibadilishana na mwenziwe ili apumzike maana alikuwa naye amechoka. Yule aliyebadilishana naye, alikuwa ni mpigaji stadi zaidi.

“Sema Ozu unafikiri yuko wapi sasa?” Papa alimuuliza Kofi.

“Simjui Kofi na wala sielewi unasema nini!” alijibu Kofi ambaye sasa alikuwa ameanza kupata maumivu na akiwa anatafuta njia ya kuweza kuanzisha sarakasi ya kujiponyesha. Alipoendelea kupigwa alijifanya amesikia uchungu sana na karibu azirai akasema tena.

“Ime... tosha... imeto... sha nitawaeleza chochote mnachotaka.

“Mwacheni, mwacheni ajibu maswali yangu,” Papa aliamru na wakamwachia.

“Unamjua Ozu?,” Papa alimuuliza Kofi.

“Ndi... ndi... ndiyo,” alijibu Kofi huku anatingisha kichwa chake kutuliza akili yake.

“Ni nani”.

“Ni... ni... mwenzangu,” Kofi alijibu huku anaweka viungo vyake katika hali ya ukakamavu na katika tahadhari ili akipata nafasi kidogo ya kuanzisha rabusha akili zake na mwili uwe tayari.

“Sasa naona tutaelewana, unafikiri sasa hivi yuko wapi?”.

“Atakuwa hotelini kwake!”

“Hotelini kwake nimepata habari hajafika, unafikiri atakuwa mahali gani pengine saa hizi?” Kusikia hivi mwili wa Kofi ulisisimkwa zaidi kuona ya kwamba kumbe Ozu naye alikuwa akingojewa kama yeye. Lakini kwa vile mpaka saa hizi alikuwa bado hajafika alifikiri lazima aliona kutekwa kwake nyara na inawezekana atakuwa amempasha habari Robert na huenda Ozu na Robert walikuwa wakifanya mbinu za kumtafuta.

“Itakuwa vigumu kujua maana tuliachana Hoteli Tip Top na akachukua tekisi ya kwenda hotelini kwake.

“Una... u... Papa alikatwa kauli na mtu aliyegonga mlango. Mlango uligongwa mara tatu, kitu ambacho Kofi alitambua kuwa ndiyo ilikuwa ishara yao kuonyesha kuwa aliyetaka kuingia alikuwa mmoja wao.

“Kafungue”, Papa alimwamrisha mlinzi wake mmoja. Kofi alijiweka vizuri maana kila wakati mlango ulipokuwa ukifunguliwa, ndipo alipokuwa akitafuta mwanya wa kuanzisha sarakasi ya kuweza kujiokoa. Hivi alijiweka tayari kama angeweza kupata mwanya safari hii kuufikia mlango kabla haujafungwa, maana walikuwa kama hatua nne kutoka waliposimama mpaka kwenye mlango. Yule mlinzi alikwenda akafungua mlango. Kufungua mlango tu Ozu ambaye tayari alikuwa ameshikilia bastola mbili mkononi, alimsukuma yule mtu aliyegonga mlango kwa nguvu sana kiasi kwamba aligongana na yule mlinzi aliyekuja kufungua wote wawili wakaanguka ndani. Ozu alijirusha ndani ya chumba na wakati ule ule akapiga risasi mfululizo na kuweka chumba kizima katika hadhaa, halafu akapiga taa risasi chumba kikawa giza. Kofi ambaye alikuwa tayari tayari alipoona yule mlinzi anagongana na yule mtu aliyegonga mlango, aliwatia mateke wale walinzi waliokuwa karibu naye kisha akarukia pale watu wale walipokuwa wamerukia na kuidaka bastola ya yule mlinzi na kujiviringisha kukwepa risasi zozote ambazo zingekuwa zinamfuata.

“Wapige risasi”, sauti ya wasiwasi ya Papa ilisikika. Papa ambaye alikuwa hategemei kabisa kuingiliwa kiasi hiki kwa kufuatana na ulinzi uliokuwa nje, aliingiwa na hofu. Wale walinzi wa Papa nao hawakutegemea kabisa shambulio kama hili, hivi hofu iliwafanya wachelewe hata kutumia silaha zao vizuri na walipoanza kuzitumia walipiga risasi ovyo bila kujua wanapiga wapi na kwa nini. Ozu alipopiga taa na kuwa giza alikuwa ameisha muona Kofi alikorukia na Kofi naye alikuwa ameshatambua kuwa ni Ozu, hivi shambulio likawa limekamiliika. Taa kuzimika katika chumba hiki kuliwafanya wababaike zaidi. Ozu

aliwashambulia kwa risasi wale walinzi waliokuwa wamemshikilia Kofi. Wakati Kofi yeye alishambulia kule alikokuwa Papa na walinzi wake.

Ozu aliwaua walinzi hawa watano na Kofi aliwawahi wale walioanguka pale chini na huku akiendelea kumvizia Papa na walinzi wake wasije huku mlangoni, kwani alichokuwa wanatafuta ni nafasi ya kutoka chumbani humu na hatimaye kutoka ndani ya ngome hii. Papa akitumia ujuzi wake na akiwa ni jasusi maarufu, alijaribu kila njia kuweza kuwazuia watu hawa wasije wakaondoka, kwa kupiga risasi huku na kule katika giza ili kuongeza nazaa ndani ya chumba na wakati ule ule aweze kupata msaada kutoka nje. Jambo hili ndilo vile vile lilikuwa likiwaogopesha Kofi na Ozu, kwa hivi walipopata mwanya tu iliwabidi watoke. Kofi ndiye alijiviringisha kwanza na kurukia sebuleni, huku Ozu akimzuia Papa na walinzi wake kwa risasi nyingi wasije wakapata nafasi ya kumjeruhi Kofi. Kofi naye alipofika sebuleni alikuta kuna walinzi wawili wanakuja mbio sebuleni huku, basi akawawahi mara moja na kuwaua. Akiwa sasa analinda sebule Ozu naye alipata nafasi ya kuruka toka mle mchumbani mpaka sebuleni huku risasi za Papa na walinzi wake wawili waliobaki zikimkosakosa.

Walinzi waliokuwa nje walikimbia kuingia ndani ili kusaidia katika mapambano yaliyokuwa yakiendelea ndani. Kwa sababu kulikuwa hakuna mtu wa kuwaongoza watu hawa, kila mtu alifanya alivyoamua, kiasi kwamba wote walikuwa wanakimbilia ndani walikosikia mlilo wa basitola na kujua ya kwamba kulikuwa na mapambano ndani ya chumba.

“Twede huku,” Ozu alimwambia Kofi, alipokuwa tayari amesimama. Walikimbia kwenye chumba kile cha simu huku wakipiga risasi kuzuia Papa na walinzi wake wasitoke mlangoni pa kile chumba na vile vile kuwazuia wale walinzi waliokuwa wanatoka nje. Walipofika kwenye chumba hiki Ozu alimwambia Kofi, “Endelea kuwazuia,” Ozu alifungua mlango akaingia ndani, Kofi akabaki amejibanza kwenye mlango huku anajibizana risasi na kundi la Papa. Ozu alienda akafungua dirisha, halafu akamwambia Kofi. “Ruka dirishani halafu panda ukuta,” Kofi alikimbia akaruka nje kupitia dirishani. Ozu alienda akawasha taa ile ya karibu na mezani ambayo alikuwa ameifungia karatasi ya kung'aa ya sigara. Alipowasha tu, taa zote za umeme za gereji zililipuka na gereji yote ikawa giza.

“Watatoka nje wazuieni kwa nje, nyuma ya nyumba kwenye dirisha la nje la ofisi ya simu”, aliamrisha Papa kwa kelele kubwa. Lakini walikuwa wamechelewam Ozu na Kofi walikwea ukuta kama nyani na kujitupa nje kabisa ya ngome ya 'Garage Papadimitriou'.

Papa akiwa anajigonga ovyo gizani aliingia ndani ya chumba cha simu na kutambua kuwa watu hawa walikuwa wamemzidi maarifa na walikuwa wamekwenda zao.

“Mama yangu mzazi watu hawa wameniadhiri sana lakini wataniona na watajua kwa nini 'BOSS' inaniita 'EXCUTIONER' alitamba Papa.

Ozu na Kofi walikimbia mpaka pale Ozu alipokuwa ameliacha gari alilokuwa ameliiba wakalikuta bado liko pale pale na hakukuwa na mtu wa kulitilia mashaka. Waliingia ndani ya gari wakalitua moto na kuondoka.

“Umefunga kazi takatifu Ozu, bila wewe sasa hivi mimi ngingekuwa maiti!” Kofi alimshukuru Ozu.

“Usiseme, bila wewe mimi vile vile nisingetoka ndani humo. Sikutegemea ungekuwa mwepesi katika vitendo kama ulivyokuwa,” Walicheka pamoja kwa furaha na kupeana mikono ya kuonyesha wako bega kwa bega.

“Tusirudi mahotelini kwetu, wewe wanakusubiri hotelini kwako mpaka sasa hivi,” Kofi alieleza.

“Ala, sasa tutaenda wapi?” Ozu aliuliza.

“Kuna hoteli moja sio hoteli hasa ila ni kijihoteli kinaitwa Hoteli Mazeza; kiko kwenye kona ya mtaa wa Kasavubu na Victoire. Twende pale kijana anayefanyakazi pale ninamfahamu sana maana nilipokuwa mjini hapa mara ya mwisho miezi mitatu iliyopita nilimfanyia msaada fulani ambao aliahidi kuulipa wakati wowote atakaponiona. Tukifika pale mahali atatupatia mahali pa kupumzika mpake kesho. Kazi iliyofanyika leo inatosha,” Kofi alishauri.

“Sawa, naona shughuli hii inaanza kuwa tamu. Gari hili nimeliiba hivi twende tukaliache katikati ya magari mengine pale Vatican Klabu, maana sasa hivi klabu hiyo bado watu wanaendelea na starehe. Kutoka pale tutatembea kwa miguu mpaka kwenye hoteli ya rafiki yako,” Ozu alishauri.

“Sawa na tufanye hivyo,” Kofi alikubali.

SURA YA KUMI NA MOJA

MAUAJI YA KISHENZI

Ilikuwa yapata saa kumi na mbili asubuhi, Willy alipoegesha gari lake katika maegesho ya Hoteli Memring.

“Tutaonana baadaye”, Mwadi alimwambia Willy huku wakiteremka toka kwenye gari.

“Asante sana, nitatoka asubuhi hii kwenda ofisini kwa akina Tete kwa mazungumzo ya kibiashara nikirudi toka huko ndipo nitakueleza kama nitakuwa na shughuli au vipi. Kama sitakuwa na shughuli mchana nitakuja nyumbani, lakini yote hayo nitakueleza tutakapoonana mchana,” Willy alieleza.

“Vizuri, mimi nitasubiri unieleze mchana,” Mwadi alijibu kisha akainama akampiga busu motomoto Willy.

“Asante,” Willy alishukuru, Mwadi aliondoka kwenye maegesho na kuelekea hotelini kuanza kazi yake. Willy alingojea mpaka Mwadi alipokuwa ameingia ndani ya hoteli maana hakutana watu wote wajue kuwa alikuwa amekuja na Mwadi. Ndipo akateremka na kufunga milango ya gari na kuelekea zake hotelini. Kwa sababu alikuwa ameondoka na funguo za chumba chake, alipanda moja kwa moja mpaka chumbani kwake, Kwa sababu hawakuwa wamepata usingizi wa kutosha aliamua ajilaze kidogo hadi saa mbili hivi ambapo angeweza kwenda kwenye ofisi za 'Agence Sozidime'. Kutokana na mafikira ya Robert kuhusu Kampuni ambayo ni wakala wa Kampuni ya Afrika Kusini, Willy alikuwa ameamua kuwa lazima akaonane na watu wa kampuni hii aweze kuwapima yeye mwenyewe. Kufahamiana na Tete usiku uliokuwa umepita Willy alichukulia kama bahati kubwa kwa upande wake. “Siku zote mimi husema bila bahati huwezi kufanikiwa katika shughuli za upelelezi,” Willy alijisemea moyoni na kujilaza tayari kuvuta usingizi kwa muda mfupi.

Willy aliamshwa na kengele ya simu iliyokuwa ikilia. Aliamka na kuangalia saa yake akaona ilikuwa imetimia saa moja unusu. Aliiendea simu, akaiinua, “Hallo,” aliita.

“Hapa mapokezi kuna simu yako kutoka nje,”

“Asante,” alijibu huku akingojea opereta amuunganishe na nje.

“Halo,” simu iliita.

“Haloo, nani mwenzangu,” Willy aliuliza.

“Robert hapa, habari za asubuhi?”

“Safi yahhe, salama wewe?”

“Mimi salama, lakini naamini wewe salama zaidi”, Robert alisema kwa sauti ya utani.

“Hujakosa bado, mimi salama zaidi”, Willy alijibu.

“Wote tuko hapa tafadhali fika upesi iwezekanavyo kuna habari muhimu sana,” Robert alimwambia. Kutokana na usemi huu Willy alitambua kuna mambo muhimu.

“Nakuja sasa hivi”, alijibu Willy na kukata simu.

Willy aliondoka na kwenda maliwatoni kujimwagia maji. Alipokuwa amemaliza kuoga, alitafuta suti yake moja iliyokuwa inampendeza sana akaiweka tayari kwa kuivaa, maana alitaka aonekane nadhifu iwezekanavyo tayari kwa mazungumzo ya kibiashara na meneja wa 'Agence Sozidime'. Ghafla alikumbuka kitu akainua simu na kuzungumza na mapokezi. Nipe STK ofisi zao zilizoko kiwanja cha ndege,” alimweleza opereta.

“Subiri,” opereta alijibu. Aliweka simu chini akaendelea kuvaa. Baada ya muda kidogo simu ililia. “Halo”, Willy aliita.

“Zungumza na STK,” opereta alijibu.

“Halo naomba zungumza na Ntumba,” alijibiwa.

“Halo Willy hapa, sijui bado unanikumbuka?”

“Aah Mzambia we, uko wapi toka juzi? Umemezwa kabisa na mji huu, mwanaume wewe!” Ntumba alilalamika.

“Nipo tu nilikuwa bado najiweka sawa,” alijibu Willy.

“Wacha uongo wako mimi najua kuna maguberi chungu mzima hapa Kinshasa ndiyo yatakuwa yamekuweka sawa.”

“Ya nini nitafute maguberi na watoto wabichi kama wewe wapo mjini hapa?”.

“Utajua wewe, nasikia maguberi yana fedha hivi yanawahonga vijana kama wewe.” Wote wawili walicheka kisha Ntumba akaendelea.

“Ulikuwa unasemaje mwanaume wewe?”

“Nakuomba unieleze kitu fulani lakini kiwe siri yako, unasemaje?”

“Uliza tu toka juzi nimekwambia hata ukitaka kukaa nyumbani kwangu itakuwa siri yangu,” Ntumba alijibu kwa kejeli.

“Jana mchana kuna gari lenu lilipatwa na ajali barabara ya Poids Lourds, unaweza kuniambia nani alikuwa amelikodi?”

Ntumba alikuwa amezoea kuulizwa maswali ya ajabu ajabu kama haya mara kwa mara. Kwa vile alikuwa ameisha mwahidi kijana huyu alijibu. “Gari hili lilikuwa limekodiwa na kijana mmoja wa Kizungu aitwaye Charles, aliacha anwani yake na tulikuwa na nambari ya leseni yake ya kuendeshea. Kitu cha ajabu ni kwamba anwani aliyotuachia na leseni vyote ni vitu vya bandia hivi tunahisi hata jina lake ni la uongo. Je una zaidi?”

Willy alipata zaidi kuliko alivyotegemea hivi alijibu.

“Sina zaidi, asante sana.”

“Umefikia hoteli gani?” Ntumba aliuliza.

“Hoteli Memling”.

“Mbona husemi karibu? Basi mimi nakukaribisha nyumbani kwangu.”

“Asante sana. Mimi nina simu ya nyumbani kwako nitakupigia simu”.

“Lini?” Aliuliza Ntumba.

“Kesho, maana leo nitakwenda Brazzaville na kurudi kesho asubuhi.” Willy aliongopa.

“Haya, asubuhi nitasubiri simu yako, mimi natoka kazini saa kumi mchana”.

“Vizuri, tegemea simu yangu kesho jioni. Kwa heri.”

“Asante kwa heri,” Walikata simu. Willy alimaliza kuvaa, akajiangalia kwenye kioo kuna kama alikuwa amejiweka katika sura ya mfanyabiashara aliyeendelea. Kusema kweli alionekana mfanyabishara wa hali ya juu kabisa kutokana na alivyoonekana. Alichukua bastola yake akaiweka ndani ya koti lake na kuteremka chini.

Ilikuwa saa mbili na nusu Willy alipofika nyumbani kwa Robert. Aliwakuta wote watatu wako mezani wanapata kifungua kinywa. “Karibu karibu”, Robert alimkaribisha.

“Vipi unaenda kuoa au una miadi kwa mara ya kwanza na msichana?” Kofi aliuliza huku wote wakicheka.

“Kwa nini?” Aliuliza Willy.

“Umevalia vizuri sana”, alidakia Ozu.

“Ninaenda kwenye miadi ya kikazi,” alijibu Willy huku akivuta kiti kwenye meza ili na yeye aweze kupata chochote kwani hakuwa amechukua kule hotelini. Walisalimiana huku wakiendelea na chakula. Willy alipowaangalia vizuri alitambua kuwa Ozu na Kofi walikuwa hawakupata usingizi wa kutosha na vile vile nguo zao zilikuwa zile zile za jana yake na zimechafuka, kitu kilichomuonyesha kuwa walikuwa bado hawajafika mahotelini kwao tokea jana yake.

“Ehe, leteni habari,” Willy alisema.

“Nafikiri Ozu ataeleza vizuri zaidi,” alisema Kofi baada ya kutazamana na Ozu nani aeleze.

“Oke mimi nitaeleza,” alijibu Ozu. Ozu alimweleza Willy mambo yote tokea walipokuwa wameachana mpaka muda ule wa asubuhi. Kisha alimalizia .

“Asubuhi tulipoamka tulionelea tuonane kwanza ili tuweze kuelezana tukio hili kabla hatujaendelea na mambo mengine. Kwa hivyo tulikata shauri tuje hapa ambapo tungeweza kukutana kwa urahisi”. Willy aliyekuwa anasikiliza maelezo haya kwa makini alivuta pumzi ndefu na kusema. “Kazi mliyoifanya inastahili pongezi. Sasa nina imani kazi hii itafanikiwa.”

“Unaona mambo yanavyokuja yenyewe Willy. Ni jana tu ulipouliza maswali mengi juu ya Papadimitriou, na sasa amejifunua mwenyewe,” Robert alisema.

“Mimi nilipatwa na mashaka jinsi gari ya marehemu ilivyoweza kuwa imetegwa bomu. Sasa imedhihirisha waziwazi kuwa Papadimitriou alijua gari hilo litatumiwa na nani, kwa hivi wakalitega gari moja kwa moja kabla halijatoka gereji. Hii inaonyesha kuwa kuna mtu katika Wizara ya mambo ya nchi za nje ambaye anashirikiana na watu hawa, hivi Robert jaribu tena kutumia uhusiano wako ulio nao na CND uweze kujua ni nani hasa alishughulika na kupanga hili gari kuwa

linatumiwa na marehemu. Tukishampata mtu huyu tutakuwa tumeunganisha mambo haya.”

“Hata mimi nilikuwa na mawazo hayo hayo,” alijibu Robert. Kisha Willy naye aliwaeleza maelezo yote aliyokuwa amepata kutoka kwa Mwadi juu ya Kabeya vile vile aliwaelezea kukutana kwake na Tete na juu ya 'Agence Sozidime'.

“Kutokana na maelezo Robert aliyokuwa ameeleza juu ya Wakala wa Makampuni ya Afrika Kusini, mimi nimeonelea nizitembelee hizi ofisi za Sozidime huenda nikabahatisha mambo fulani fulani,” Willy alimalizia.

“Lo naona Mungu amekuwa upande wetu usiku wa jana maana sasa naweza kuona mwanga wa mambo haya yalivyo. Kitu kimoja kinachoonekana waziwazi ni haya magereji. Inaonekana majambazi haya yanatumia magereji kama makambi yao kutunzia na kuimarisha ujambazi wao. Mimi nitaenda kupeleleza nani mwenye hii G.A.D. gereji halafu ndipo tutaangalia habari za gereji hii zaidi,” Robert alishauri.

“Mimi sidhani hawa watu ni majambazi wa kawaida. Nina imani hiki ni kikundi maalumu ambacho kimewekwa hapa kwa nia fulani ya kisiasa na ndiyo sababu wamemuua Ndugu Mongo pamoja na wanamapinduzi wengine waliokwisha uawa hapa mjini. Hivi hatuna budi kuliangalia kuliangalia suala hili katika mfumo wa namna hiyo,” alisema Kofi.

“Sawa kabisa, na hayo ndiyo mawazo ya kamati ya Ukombozi ya OAU. Je huyu Papadimitriou wewe ulimkadiria vipi?” Willy alimuuliza Kofi.

“Macho yetu yalipogongana moja kwa moja tulitambuana kitu kimoja, wote tulikuwa watu ndani ya mchezo mmoja. Huyu mtu ni hakika kabisa ni jasusina jasusi wa hali ya juu. Kitu hiki kinaonekana waziwazi katika macho yake... nadhani mnaweza kutambuana,” Kofi alieleza huku wenzake wakitingisha vichwa kuonyesha kuwa wameelewa.

“Robert itabidi upeleke maelezo yote haya Lusaka. Halafu uwaambie wajaribu kutafuta habari za huyu Papadimitriou kama anaweza kuwa jasusi wa kundi gani na watuletee habari haraka sana. Nafikri itakuwa rahisi hasa kwa vile mtu huyu amewahi kukaa Lusaka.” Willy alimshauri Robert.

“Sawa nitafanya hivyo,” Robert alijibu.

“Sisi tutarudi mahotelini kwetu tukapumzike kidogo na kubadilisha mavazi,” Ozu alisema.

“Jiangalieni sana maana inavyoonekana watu hawa wana mbinu nyingi sana. Huyu Kabeya ana uhusiano na Mahoteli karibu yote makubwa kama nilivyokwisha kuwaeleza, hivyo msipuuze kitu chochote dakika yoyote,” Willy aliwashauri.

“Tuonane tena hapa wote mchana kiasi cha saa saba ili tuelezane maendeleo ya asubuhi hii, maana kama Robert kama Robert ataweza kupata hizo habari nafikiri litakuwa jambo la maana sana. Sasa mimi naondoka lakini tutaonane wakati huo,” Willy alisema huku akisimama. Aliangalia saa yake ilikuwa tayari saa tatu.

“Oke, saa saba tutaonana.” Walijibu wenzake, yeye Willy akaondoka.

Wakati Willy anaondoka nyumbani kwa Robert saa tatu hivi mkutani mkali ulikuwa ukiendelea nyumbani wa Pierre huko Limete. Mkutano huu ulikuwa umeanza saa moja ya asubuhi lakini ulikuwa bado unaendelea. Mazungumzo hasa katika mkutano huu yalikuwa yanahusika na tukio lililokuwa limetokea usiku ule huko 'Garage Papadimitriou'. Pierre ambaye alikuwa ametoa maneno makali sana kwa kushindwa kwao katika tukio hili, alikuwa saa hizi amesimama na huku anatembea toka pembe mpaka pembe ya chumba kitu ambacho kilionyesha kuwa alikuwa na mafikira mengi sana.

“Hili tukio ndilo liwe la mwisho kwetu kushindwa. Ni aibu kubwa kuona ya kwamba kundi tulilolijenga muda mrefu liweze kuingiliwa na kutingishwa na watu wawili. Hapana watu hawa lazima watafutwe na wauawe mara moja, maana sijui BOSS italipokea vipi tukio hili wakati mjini hapa imeweza kuweka watu wake mashuhuri na wenye vyeo vya juu kabisa wapatao watano, na eti ipate habari kuwa wapelelezi wawili na wakiwa na wakiwa Waafrika wameweza kuingia ofisi mojawapo ya 'WP' na kuua watu wake chungu nzima. Hapana jamani lazima jambo hili sasa limegeuka linahitaji tulishughulikie sisi wenyewe, huenda hawa vijana wetu hawana ujuzi wa kutosha,” alieleza Pierre kwa uchungu.

“Sawa Patroni jambo lililotokea jana limekuwa ni fundisho kubwa sana. Kosa ni langu kwa sababu niliwadharau watu hawa, nilifikiri wasingeweza kuwa na ujuzi kiasi cha kuweza kutuingilia namna ile. Lilikuwa kosa kubwa mno watu hawa ni hatari sana na wana ujuzi kama sisi au zaidi,” alikiri Papa.

Muteba na Jean waliokuwa wamesikiliza maelezo ya Papa kwa makini sana, waliendelea kunyamaza kwani mambo mengi yalikuwa yakipita mawazoni mwao. Walijua ya kwamba wakati umefika sasa ambao wao wenyewe ndio watatumika na wala hawatamtuma mtu. Walitambua kuwa muda wa mapumziko umekwisha

kwani kwa muda mrefu sana wamekaa kibwana mkubwa na kuishi kifahari lakini sasa wakati wa kulipa umefika.

“Mbona mmeduwaa namna hii?” Pierre aliwashtua.

“Mimi niko tayari kabisa kupambana na watu hawa na wala wasikupe taabu,” aliropoka Muteba.

“Na mimi vile vile niko tayari ni siku nyingi sijapata muda wa kashikashi kama huu naamini naamini nitaufurahia sana. Nitawaonyesha watu hawa kuwa sisi sio vipimo vyao,” alijitapa Jean.

“Kama tulivyopata bahari, watu hawa hawakurejea tena mahotelini kwao jana usiku. Lakini nina imani mchana huu watu hawa lazima watarudi kubadilisha nguo zao. Hivi itabidi tuwe na watu wa kuangalia mahoteli haya, na wawe na ujuzi wa kuweza kumfuata mtu bila ya yeye kutambua. Ni dhahiri kuwa watu hawa wanatembea kwa tahadhari kubwa, na wanalindana kutokana na tulivyojifunza na tukio la jana, hivi itabidi kati yetu tuongoze watu watakaofanya kazi hii na kama mtu akipata nafasi nzuri anaweza kufanya mashambulizi.” Pierre alieleza. Muteba na Jean walijitolea kuwa wangeongoza watu hawa.

“Nashukuru,” alijibu Pierre. “Lakini kumbukeni watu hawa ni hatari, mkipata nafasi nzuri msiwape nafasi waueni pale pale mimi sijali tena litakalotokea. Hasara waliyokwisha tupa ni kubwa mno kiasi kwamba sijali tena. Mimi nitakuwa gerejini kwangu, ripoti zote mtaniletea huko. Na kama mimi nitawahitaji nitawaeleza.

Wote walisimama wakaondoka kimya kwenda kwenye uwanja wa mapambano. Walipokuwa wameishaondoka Pierre alienda kupiga simu. “Hallo Sozidime hapa,” sauti ya msichana alijibu.

“Hapa ni Garege du Peuple, Mkurugenzi yupo?” Aliuliza Pierre.

“Ndiyo yupo”.

“Nipe nizungumze naye,” Pierre aliomba.

Ofisi za 'Agence Sozidime' zilikuwa ziko sehemu ya Gombe mtaa wa Aviateurs karibu na jumba la sinema liitwalo Cine Rac. Habari zote hizi zilikuwa kwenye kadi ambayo Tete alikuwa amempa Willy, hivyo haikuwa vigumu kwa Willy kuipata ofisi hii. Wailly aliipata ofisi hii karibu na 'Cine Rac' kama ilivyokuwa imeelezwa kwenye kadi. Ofisi yenyewe ilikuwa ndani ya nyumba moja ndogo ambayo ungefikiri ni nyumba ya mtu binafsi ya kuishi. Ilikuwa imezungukwa na

michongoma mirefu ambayo ilikuwa inaimeza nyumba, na mbele kulikuwa na lango kubwa. Mbele ya lango ndipo kulikuwa na ubao mkubwa uliokuwa umeandikwa kwa maandishi makubwa sana, 'AGENCE SOZIDIME'. Willy aliingia kwenye lango hili na kusimama. Mlinzi aliyekuwa pale mlangoni alimwonyesha ishara ya kupita moja kwa moja. Ndani alikuta nafasi kubwa ya maegesho akaegesha gari lake. Kulikuwa na magari mengine yapatayo karibu ishirini ambayo yalimfanya Willy kutambua kuwa kampuni hii ilikuwa na maofisa wengi. Vile vile alipoangalia mazingira ya nyumba na ofisi hii alihisi kuwa zamani lazima ilikuwa nyumba ya mtu binafsi. Alisukuma mlango wa mbele wa nyumba hii ambao ulikuwa umeandikwa kwa karatasi iliyoandikwa SUKUMA.

SURA YA KUMI NA MBILI

BAADA ya kuingia alijikuta yuko kwenye sebule kubwa iliyotandikwa zulia moja safi sana toka ukuta hadi ukuta. Chumba hiki kilizungukwa na makochi mazuri sana yakiandamana na meza ndogo ndogo. Hewa ya humu ndani ilikuwa baridi sana kitu kilichoonyesha kwamba mashine ya kuleta baridi 'air condition' ilikuwa inatumika. Nyumba nzima ilikuwa kimya isipokuwa mashine ya kupiga chapa iliyokuwa ikisikika tokea vyumba vya ndani. Willy alijikuta anaangaliana moja kwa moja na Tete ambaye uzuri wake uliongezea uzuri wa chumba kizima. “Karibu Willy,” Tete alimkaribisha Willy wakati alipomuona. Mwili mzima wa Willy ulisisimkwa kwa kusikia sauti nyororo ya msichana huyu, pamoja na macho ya msichana huyu yaliyokuwa yakimtazama kama kwamba yanamwambia 'usijaribu kunisahau'. Willy alisogea akataka kujibu, lakini sauti ikakwama, akatoa kohozi, na kwa sauti ya kubabaika alijibu, “Asante”. Kusema kweli msichana huyu alikuwa mzuri nadiriki kurudia kukueleza tena, mimi nina imani kama wewe ndiye ungekuwa mahali pa Willy ungepatwa na kizunguzungu na ungeweza kuanguka chini, maana nasikia kuna watu wamewahi kupatwa na mkasa huo. Lakini kwa vile ni Willy alikaza roho na kumsogelea msichana huyu. “Habari za toka jana,” Tete alimsalimu.

“Nzuri ulifika salama?”

“Nilifika ingawaje gari langu lilinifanyia uhuni kidogo.” Alijibu Tete huku akiendelea kumwangukia Willy kwa macho malegevu. Moyo wa Willy ulipiga haraka haraka akajibu, “Pole sana.”

Tete naye moyo wake ulikuwa unapiga haraka haraka, maana naye kwa sababu asizozijua alijukuta anaguswa vibaya sana moyoni kwake na kijana huyu ambaye asubuhi hii alikuwa akipendeza zaidi kuliko alivyokuwa amemuona usiku uliopita.

“Karibu kaa kwenye kiti, nimeisha kufanyia miadi na Meneja wa Biashara ambaye yuko tayari kuonana na wewe. Nilifanya miadi na Mkurugenzi lakini ana shughuli nyingi sana wiki hii hatakuwa na nafasi. Subiri nimuulize Meneja wa Biashara kama yuko tayari sasa hivi,” alieleza Tete. Willy alikaa kwenye kochi. Kwenye meza iliyokuwa mbele yake kulikuwa na magazeti mengi. Aliyaangalia akaona gazeti la 'Salongo' la siku ile akaanza kuliangalia huku akingojea Tete arudi. Alichunguza gazeti hili na kwenye pembe moja ndani ya gazeti alikuta kitu ambacho alikuwa akikihitaji kukiangalia. Kulikuwa kumeandikwa kwa kifupi sana

habari za ajali waliyoifanya na wale watu waliokuwa wanamfuata Ozu. Gazeti lilisema tu kwamba mtu mmoja alikutwa barabara ya Poids Lourds amepigwa risasi na gari aliyokuwa akiendesha ikiwa imepata ajali. Liliendelea kusema polisi walikuwa bado wanaendelea na uchunguzi wa tukio hili.

“Yuko tayari kukuona,” Tete alimweleza.

“Asante,” Willy aliweka gazeti chini akaanza kumfuata Tete ambaye alifungua mlango wakaingia ndani, wakamkuta msichana wa kizungu ndiye alikuwa mwandishi mahsusi wa Meneja wa Biashara.

“Oh asante sana, karibu Willy,” msichana huyo wa kizungu ambaye naye alikuwa mzuri sana alimkaribisha Willy.

“Asante,” alijibu Willy huku wakisalimiana.

“Wille. Lucie atakushughulikia, tutaonana ukitoka,” Tete alimwambia na kumminya jicho, kitu kilichomshinda Willy na kubabaika hata hakuweza kujibu. Baada ya Tete kuondoka Lucie alimsindikiza Willy ofisini kwa meneja wake.

“Bwana Max tafadhali onana na bwana Willy,” Lucie aliwafahamisha.

“Oh bwana Willy karibu, nimepata habari zako toka asubuhi,” alijibu Max

“Asante sana, nami nimefurahi kufika ili tuweze kuzungumza,” walielezana huku wakishikana mikono. Lucie alitoka akawaacha waendeleo na mazungumzo yao. Willy alivuta kiti akaa huku akimwangalia meneja huyu wa kizungu tayari kuanza mazungumzo naye.

“Nimepata habari kuwa unawakilisha kampuni moja ya wakala ya nchini Zambia,” Max alisema.

“Ndiyo mimi ni mwakilishi wa kampuni iitwayo 'Zambia Overseas Agency' na natumaini umewahi kuisikia,” Willy alifungua mkoba wake, akatoa kadi yake ya kibiashara kati ya kadi alizokuwa ametayarishiwa na Chifu kabla ya kuondoka mjini Lusaka. Max aliiangalia kisha naye akatoa akampa Willy.

“Ni jambo zuri kwa kufika kwako hapa kutuona kwa mazungumzo ya kibiashara, Kusema kweli kampuni yetu ni kubwa na ina uhusiano wa kibiashara na nchi nyingi sana. Ilikuwa bahati mbaya tu kuwa bado tulikuwa hatuna uhusiano wa kibishara na makampuni ya Zambia. Hivi tunakukaribisha sana,” mazungumzo haya alizungumza max.

“Asante sana, kusema kweli bwana Max kampuni yetu ndiyo wakala wa makampuni mengi nchini Zambia. Kwa sasa hivi Shirika la Mazao la Zambia ambalo ni kati ya makampuni tunayowakilisha linahitaji kuuza mahindi nchi za nje, hivi limetupa jukumu la kutafuta wanunuzi. kutojkana na habari za kibiashara Zaire inahitaji sana mahindi, Kwa hivi nimefika hapa kuwaona baada ya kupata habari kuwa kampuni yenu ndiyo inawakilisha makampuni mengi ya humu nchini na makampuni ya njeyanataka kufanya biashara nchini huku. Natumaini mtanitatulia shida yangu,” alisema Willy.

“Ahaa, nimekuelewa kwa ufasaha sana. Kusema kweli Zaire inahitaji sana mahindi, na kwa sasa hivi inaagiza mahindi kutoka Rhodesia. Tukiangalia na upande mwingine Zaire ikiwa ni nchi ya Kiafrika na mwanachama wa OAU na Umoja wa Mataifa si vizuri kisiasa kufanya biashara na serikali ya walowezi ya Rhodesia. Lakini kutokana na hali halisi ya kiuchumi ilivyo Zaire imebidi kufanya biashara na Rhodesia. Litakuwa jambo la maana sana bwana Willy kama Zambia itakuwa tayari itakuwa tayari kuisaidia Zaire kibiashara ili iweze kupunguza biashara na Rhodesia na hatmaye kuikomboa kabisa Zaire kutoka mikononi mwa walowezi kiuchumi,” Max alimweleza. Willy aliyekuwa anasilikiliza maelezo ya mzungu huyu ambaye alikuwa ameanzisha mazungumzo yanayoingiliana na siasa kali iliyokuwa inamgusa moyo, alimtilia mashaka sana mtu huyu kama kweli alikuwa anazungumza kutoka moyoni mwake au alitaka kumsikia yeye Willy amesimama wapi. Hivi alijibu.

“Jambo hili niachie nitalishughulikia, kwani umefikia wapi?” Max aliuliza.

“Niko Hoteli Memling,”

“Utakuwa hapa mjini kwa muda gani?”

“Leo ni Jumatano... nitakuwa hapa mpaka wiki ijayo”, alijibu Willy.

“Vizuri bwana Willy, mimi nitakupasha habari kati ya kesho au kesho kutwa, maendeleo nitakayokuwa nimeyafanya juu ya suala hili. Nitazungumza na Wizara ya Kilimo na Mashirika yanayohusika. Usiwe na shaka jambo hili limefika mahali penyewe,” Max alieleza huku akisimama, akaenda ukutani akawasha mashine ya kuleta baridi. Kitendo hiki kilimgutua kidogo Willy lakini akaona kweli hali ya joto ilikuwa imeanza kuingia.

“Lini umefika hapa mjini?” Max alimuuliza.

“Toka Jumatatu,” alijibu Willy kisha aliendelea na mazungumzo ya kibishara kwa muda kidogo halafu Willy akaamka tayari kwa kuondoka. “Nashukru sana bwana Max nafikiri sasa nitaondoka. Mimi nitakuwa nasubiri kusikia toka kwako,” Willy aliaga.

“Karibu tena siku nyingine”, Max alijibu naye akasimama kumsindikiza Willy. Max alimsindikiza na kuingia kwenye ofisi ya Lucie.

“Asante sana Lucie, mimi ninaondoka,” Willy aliaga.

“Asante karibu tena,” Lucie alijibu. Max alimsindikiza Willy mpaka mapokezi ndipo akamuaga.

“Oh Willy nitakupigia simu.”

“Asante nitaisubiri,” walipeana mikono Max akarudi ofisini kwake huku Willy akibaki anazungumza na Tete.

“Vipi mazungumzo yenu yameambua chochote cha maana?” Tete aliuliza.

“Oh yamekuwa mazuri kiasi ambacho sikutegemea” alijibu Willy.

“Nashukuru imetokea hivyo. Je leo mtakuwa wapi?” Tete aliuliza.

“Sijajua bado mpaka nimwulize Mwadi ambaye ndiye mwenyeji wangu. Je ulikuwa unasemaje?” Willy aliuliza.

“Basi nitampigia simu Mwadi”, Tete alijibu kwa mkato.

“Haya vizuri, nitajua toka kwake,” alijibu Willy. Kisha waliagana na kuahidiana kuwa huenda wangeonana jinsi ile baada ya kila mmoja wao kuzungumza na Mwadi. Willy aliingia ndani ya gari lake huku akiwa na mafikira mengi sana juu ya ofisi hii. Baada ya kufikiria mambo kadhaa yaliyomtia wasiwasi juu ya ofisi hii kuwa itambidi arudi na kuingia ndani ya ofisi hii wakati itakapokuwa imefungwa, hasa wakati wa usiku kwa siri ili aweze kutuliza wasiwasi wake. Alipoangalia saa yake aliona ni saa tano, akaamua kufika madukani kidogo.

Ilikuwa saa sita kamili Willy alipofika hotelini kwake na alimkuta Mwadi yuko kazini. “Habari za saa hizi?” Willy alimgutusha Mwadi aliyekuwa ameinama huku anaandika.

“Oh Willy mpenzi, habari zangu ni nzuri tu. Vipi shughuli zako?”

“Shughuli zangu zimeenda vizuri sana, nafikiri mambo yangu yatafanikiwa haraka zaidi kuliko nilivyotegemea”, alijibu Willy. “Ehe nipe mipango, ningetaka kuonana na Tete jioni ili aweze kunieleweshwa vitu fulani fulani, kwa hivyo nitakupitia jioni tukamwone halafu ndipo tutaendelea na mambo mengine baada ya hapo.”

“Tete amenipigia simu, akiuliza tuna mipango gani jioni. Mimi nimemjibu kuwa mpaka tuonane ndipo nitamjibu. Sasa mimi nitamwambia kuwa tutaenda kwake jioni atusubiri. Sawa?” Mwadi aliuliza.

“Sawa kabisa, kwani yeye anakaa wapi?” Willy aliuliza.

“Anaishi huko Ndolo, unakujua ndolo?”

“Ndiyo”.

“Basi ana nyumba moja nzuri sana huko, barabara ya Kibinda nyumba nambari 16, nyumba yake inatazamana na kiwanja cha ndege cha Ndolo”, alisema Mwadi kwa utulivu.

“Nyumba hiyo amepanga ama ni mali yake?”, Willy aliuliza.

“Ni mali yake. Watu wengi wanasema nyumba hii alinunuliwa na rafiki yake Muteba. Kama ulivyomwona msichana mwenyewe hata wewe kama angekwambia umnunulie nyumba naamini ungefanya hivyo”, Mwadi alimtania.

“Wacha mambo yako”, Willy alijibu huku anaangalia saa yake.

“Twende tukapate chakula cha mchana”.

“Nenda tu mimi niko kazini mpaka baadaye.” Mwadi alijibu.

“Nisubiri nyumbani nitakupitia kiasi cha saa kumi na mbili au saa moja jioni”.

“Usiwe na shaka mimi nitakuwepo nikikusubiri kwa hamu sana,” Mwadi alijibu.

“Willy alielekea kwenye chumba cha chakula, huku nyuma Mwadi akiwa anamwangalia hadi alipopotea. “Nitahakikisha kijana huyu anaondoka na mimi,” alijisemea Mwadi. Baada ya chakula Willy aliondoka na kuelekea nyumbani kwa Robert, ili kuwahi miadi yao waliyokuwa wameipanga hapo awali.

“Nilipoingia chumbani kwangu nilikuta chumba kimepekuliwa vibaya sana lakini kwa ujuzi wa hali ya juu kiasi kwamba mtu wa kawaida hawezi kujua

kimepekuliwa. Hii inazidi kuthibitisha kuwa watu hawa si wa kawaida ila nao ni watu wenye ujuzi,” alieleza Willy alipofika.

“Mimi nilikuwa ninayo mawazo kuwa, jioni ingebidi tukaangalie hii gereji iitwayo G.A.D. ili tuhakikishe kama kuna huhusiano kati yake ya Garage Papadimitriou?” Kofi alishauri.

“Hili lipo nilikuwa bado nakuja kulizungumzia. Mpango wa leo utakuwa kama ifuatavyo. Sasa hivi itabidi tupumzike mpaka jioni kwani usiku wa leo ndipo kazi itafanyika. Saa kumi na mbili jioni mimi nitaondoka kwenda kumwona Tete, maana nina miadi na Mwadi ili aweze kunipeleka huko.

“Shughuli zangu itabidi nizifanye katika muda wa masaa matatu ili kiasi cha saa tatu usiku niwe nimerudi hapa tayari kwa shughuli za usiku. Kama Kofi alivyosema itabidi tuitembelee Garage 'G.A.D'. Kwa hivyo sasa hivi tutapumzika kusudi tujiweke katika hali nzuri ya kuweza kukabili mambo yoyote yatakayotokea usiku”. Willy aliwaeleza.

“Jambo la maana kabisa sababu usiku wa jana hatukupumzika vizuri,” alijibu Ozu. Wote walikubaliana na maelezo ya Willy na kuondoka kuelekea kwenye vyumba vya kupumzika ndani ya hii nyumba ya Robert ambayo ilikuwa nyumba kubwa sana.

Wakati Willy na wenzake wakiendelea na mazungumzo. Pierre na wenzake nao walikuwa wamekusanyika ofisini kwake wakiwa na mazungumzo vile vile.

“Wale watu ni watu wenye ujuzi wa hali ya juu sana. Jinsi walivyotukwepa na kutufanya tusiwaone ni kwa namna ya ujuzi wa pekee Patron, mimi nimeridhika kabisa kuwa watu hawa kama alivyosema Papa wana ujuzi sawa sawa na sisi huenda hata na kuzidi. Hivi itabidi sasa tutumie mbinu zetu zote tukitaka kuwafutilia mbali,” alikiri Muteba. Jean naye alieleza maelezo kama haya haya naye vile vile akakiri kuwa watu waliokuwa wanapambana nao hawakuwa mchezo.

Pierre aliwasikiliza kwa utulivu sana kisha akasema;

“Kwa taarifa yenu kuna mtu mwingine ambaye anaweza kuwa mmoja wa watu hawa kwa vile sababu zilizomleta ni sawa sawa na za hawa watu wawili. Yeye naye alifika mjini hapa juzi Jumatatu akitokea Lusaka akiwa katika mapumziko ya kikazi. Mtu huyu anasema yeye ni mwakilishi wa kampuni moja ya wakala ya Zambia iitwayo 'Zambia Oversea Agency'. Mtu huyu leo alikwenda kwenye ofisi

za Sozidime akaonana na Max wakazungumza mambo ya kibiashara. Mtu huyu anasemekana alionana jana usiku na Tete huko Parafifi Bar, na kupeana miadi ya kufika ofisini kwao kwa mazungumzo ya kibiashara na wakuu wake, kitu ambacho ametimiza.

Muteba ambaye moyo wake ulikuwa ukipiga haraka haraka kwa kusikia jina la Tete linatajwa katika habari hii aliinua macho yake ambayo yalionana sawa sawa na Pierre, ikabidi Pierre amuulize, “Unasemaje Muteba?”

“Hizi habari umezipataje?” Muteba aliuliza.

“Kama unavyojua wakala wanafanya kazi zao kwa makini sana. Wao toka nimewapasha habari juu ya matukio ya jana mchana na usiku wako macho. Waliposikia kuwa kuna mtu wa namna hii anakuja kuwaona walitia mashaka. Na mashaka yao yalizidishwa baada ya kumwona mtu huyu, mtu huyu wanahisi lazima awe mpelelezi tu kutokana na alivyo. Hivyo walinasa mazungumzo yake kwenye utepe uliokuwa umefichwa ofisini mwa Max. Mazungumzo yote nimeyasikia kwani wamenieleza. Kwa kujibu suala lako Muteba hivi ndivyo nilipata habari hizi. Mtu huyu anajiita Willy Chitalu. Mkurugenzi amepeleka habari hizi BOSS waweze kuchunguza na kutujibu kama wanaweza kuwa na habari za mtu huyu akiwa kama ni mpelelezi. Wakati huo huo huenda itakuwa rahisi kwako Muteba kuweza kupata habari kamili za mtu huyu kutoka kwa rafiki yako Tete ambaye ndiye amemfahamisha mtu huyu huko Sozidime.”

Muteba alijawa na wasiwasi kwani kujiingiza kwa Tete katika suala hili ingeweza kuwa hatari kwake, kwa kutaka kumtetea alijibu, “Mimi nina imani Tete alifanya hivi kikazi bila kujua jambo lolote kwani yeye hajui shughuli za kisiri za Sozidime. Kwa hivi alimjulisha mtu huyu kikazi kabisa. Lakini hata hivyo nitazungumza niweze kujua alimfahamufahamuje mtu huyu kiasi cha kuwekeana miadi,”

“Hata mimi naamini kuwa Tete hakumjulisha kwa nia mbaya, bali chunguza tu na ikibidi jaribu kumshawishi akujulishe kwa mtu huyu. Kazi hii jaribu kuishughulikia leo hii maana kama kweli na huyu vile vile ni mmoja wao inabidi tuwe na uhakika tuweze kujua nguvu za upinzani wetu,” kisha alimgeukia Jean akamwambia, “Mtu huyu amefika toka Jumatatu, na amefikia Hoteli Memling, na mimi nilikueleza wageni wote toka juzi waorodheshwe hasa kama huyu ambaye anatoka Lusaka sijui kama yuko kwenye orodha yako?”

“Jina hilo bado halijanifikia, nashangaa kwa nini. hebu nipe simu.” Jean alipiga simu ofisini kwake akazungumza na Kabeya. Wengine waliendelea na

mazungumzo. Alipomaliza aliwaeleza. “Ni jambo la ajabu sana. Kabeya anasema amepata majina ya watu wote waliofika hoteli Memling kwa msichana mmoja aitwaye Mwadi ndiye anampa maelezo yote kwa muda mrefu sasa ila anashangaa kwa nini jina la mtu huyu lilisahuliwa. Amesema atachunguza kwa nini.”

“Mwadi ninamfahamu sana ni rafiki yake Tete, hivyo mueleze Kabeya asifanye lolote anisubiri tutalishughulikia jambo hili pamoja,” Muteba alishauri.

“Jambo zuri sana, kama utalishughulikia jambo hili, maana nahisi kuna kitu kati ya wasichana hawa na mtu huyu. Ufanye kila mbinu uweze kuonana naye”, Pierre alimweleza Muteba.

Mambo ya huyu Chitalu tuyaache mikononi mwa Muteba na Kabeya wayashughulikie,” Papa alikubaliana.

“Tatizo lililobaki ni kwamba hawa watu wawili Ozu na Kofi bado wanatusumbua, usiku wa leo lazima tuwe na ulinzi mkubwa huko 'Garage Papadimtriu' maana wanaweza kwenda huko na leo tena. Vile vile magereji mengine yawe katika ulinzi wa kutosha maana huwezi kujua watu hawa wanajia kiasi gani. Fikiria, kama huyu Willy ni mmoja wao vipi ameweza kuitilia mashaka Sozidime? Hivyo lazima tuwe tayari kila dakika kuwakabili watu hawa wakijitokeza. Halafu msako wa watu hawa lazima uongezwe, na mahali popote watakapoonekana tu wauawe pale pale msisubiri maana kama mnavyosema wenyewe watu hawa ni hatari. Msilogope polisi, nyinyi shughuliken, mambo ya polisi mniachie mimi,” Pierre aliwaeleza.

“Jambo la maana kabisa Patron, tokea sasa hivi ninaongoza msako huu, kwani hawa watu nina deni nao, lazima tuonane tena uso kwa uso ili ijulikane waziwazi, nani ni nani kati yetu,” alijigamba Papa. Baada ya mkutano huu, watu hawa waliondoka kwenda kushughulikia kazi kila mmoja aliyoipewa.

Ilikuwa saa kumi na mbili za jioni wakati Willy alipoondoka nyumbani kwa Robert, ili kuelekea Bandalungwa nyumbani kwa Mwadi. Wenzake aliwaacha bado wanapumzika. Kiasi cha saa kumi na mbili na robo ndipo Willy alikuwa anaegisha gari lake nje ya nyumba ya Mwadi. Alifungua mlango wa gari akaenda kubisha hodi mlangoni, lakini hakupata jibu lolote. Alishangaa sana kwa kutomkuta Mwadi nyumbani na hali alikuwa amemuahidi kuwa atakuwa anamsubiri.

Kisha aliamua kumsuburi kidogo, kwani aliona kulikuwa na umuhimu wa kumsubiri ili waende wote kwa Tete. Maana aliamini kuwa angeweza kupata maelezo mengi zaidi kutoka kwa Tete kwa kumtumia Mwadi. Alimsubiri hapo nje

kiasi cha robo saa zaidi mpaka akaanza kuingiwa na wasiwasi. Alienda akaujaribu mlango kama umefungwa, akakuta uko wazi kitu ambacho kilimwonyesha kuwa Mwadi hakuwa ameenda mbali. Alipoingia ndani tu, mara kengele ya tahadhari ikalia kichwani mwake maana aliona matone ya damu chini kwenye zuria. Alirudisha mlango haraka na kutoa bastola, huku akichunguza huko na huko. Alifungua mlango wa chumba cha kulala kwa ghafla na kuingia ndani. Loo tishio alilolikuta ndani mle ni lile ambalo hatawahi kulisahau.

“Mama yangu mzazi” Willy alilalamika kwa hasira. Mwadi alikuwa amekakwa na huku amelazwa kitandani na ametumbuliwa matumbo nje. Yalikuwa mauaji ya kishenzi ambayo Willy alikuwa hajawahi kuyaona. Haraka haraka Willy alichukua shuka akaifunika maiti ile, akaangalia huku na huku lakini hakukuwa na kitu chochote cha maana kwa uchunguzi akamuapia Mwadi kwa sauti, “Mungu mmoja, mpenzi wangu Mwadi, watu waliokufanya hivi, nitakulipizia kisasi kwa mkono wangu. Maana umekufa kwa ajili yangu. Nitakukumbuka daima,” Alipokwisha kusema maneno haya alitoka haraka haraka na kufunga mlango wa chumba na wa mbele akiwa amejawa na hasira na uchungu mwingi aliamua kwenda Ndolo.

Mawazo yake yalikuwa yamemtuma kuwa, mauaji ya Mwadi lazima yalikuwa yameletelezwa na uhusiano wa yeye, na vile vile alihisi kuwa lazima angekuwa anajua habari fulani fulani juu ya mauaji haya, maana Tete na Mwadi walikuwa wamepigiana simu mchana na ndiye mtu aliyejua Willy atakuja kwa Mwadi na vile vile kuwa Mwadi atakuwa nyumbani. Akiendesha kama mwendawazimu alielekea Ndolo nyumbani kwa Tete. Alipofika Ndolo alikumbuka kuwa Mwadi alikuwa amemwambia kuwa Tete alikuwa na nyumba yake iliyokuwa inatazana na uwanja wa mdogo wa ndege wa Ndolo.

Alienda mpaka sehemu hii akaikuta nyumba nambari 16 ambayo ilikuwa imezungukwa na seng'enge pamoja na michongoma. Kulikuwa na lango kubwa, lakini wakati huu lango hili lilikuwa wazi. Willy aliingiza gari lake moja kwa moja ndani ya ua. Alikuta kuna gari moja ndogo aina ya 'MG Sports' akahisi kuwa hii ilikuwa gari ya Tete kwa sababu alikuwa ameiona pale Sozidime. Huku akiwa katika tahadhari kubwa aliteremka ndani ya gari na wati huo huo Tete naye alikuwa amefungua mlango wa mbele ya nyumba.

“Ooh karibu Willy, mbona uko peke yako, Mwadi yuko wapi?”, Tete alimkaribisha Willy na kumuuliza.

Willy alijibu, “Asante.” Jibu hili lilimtatanisha Tete lakini hakusema kitu.

“Nani mwingine yuko hapa nyumbani kwako,” Willy aliuliza huku amepandwa hasira wakati wameingia ndani ya kurudisha mlango.

“Hamna mtu mwingine,” Tete alijibu kwa woga maana aliona sura ya Willy imebadilika kiasi kwamba alionekana kama mzee. Willy alimshika Tete, akaanza kumtwanga makofi.

“Niambie nani amemuua Mwadi la sivyo nitakuua na wewe,” Willy alimwambia kwa hasira. Tete ambaye alikuwa ameanza kupiga makelele kwa kupigwa makofi alinyamaza ghafla baada ya kusikia maswali haya ya Willy.

“Niache, unasema nini?” Tete aliuliza huku macho yote yamemtoka na uso wake ukapoteza rangi naye vile vile akaonekana kama mzee. Kuona hivi Willy alimuachia akamjibu.

“Mwadi ameuawa kishenzi kabisa naamini wewe unajua nani amemuua kwa sababu ni wewe na mimi tuliojua mienendo ya leo ya Mwadi.

Kusikia hivi Tete alianza kulia kwa uchungu mwingi.

“Sikiliza Tete, mimi sikuja hapa kukuangalia unalia, ninachotaka kujua nani amemuua Mwadi, au niulize hivi mtu gani amekuuliza habari za Mwadi leo?” Willy alimuuliza. Tete aliinua macho yake akamwangalia Willy kisha akasema kwa sauti ya uchungu.

“Mwadi alikuwa rafiki yangu sana, tumefahamiana muda mrefu toka tuko shule. Siamini kama amekufa”.

“Kama kweli alikuwa rafiki yako mimi nataka kulipizia kisasi. Sasa lazima unisaidie, kuna mtu amekuuliza habari za Mwadi leo?” Willy aliuliza baada ya kuona Tete analalamika.

Tete alianza kufikiria jinsi mpenzi wake Muteba na rafiki yake Kabeya walivyokuja saa kumi ile baada ya kutoka kazini na kumuulizia juu ya Willy na Mwadi na sasa alishangaa kusikia Mwadi ameuawa. Hakuamini kuwa Muteba angeweza kufanya jambo hili. Kufikiria hivi kulimfanya machozi mengi yazidi kutiririka kwani alijukuta katika hali ya kutatanisha sana. Alianza vile vile kumfikiria huyu kijana aliyesimama mbele yake alikuwa na nini kiasi awe kwamba uhusiano wake na Mwadi umefanya akina Kabeya wamuue Mwadi, hata yeye alianza kuogopa. Kutokana na maswali aliyokuwa ameulizwa na akina Kabeya naye alianza kuamini kuwa wangeweza kuwa ndio wamemuua Mwadi, kwani walisema walikuwa wanaenda kumwona. Alisikia uchungu na huzuni kubwa juu

ya Mwadi na akili yake ilivurugika aliposikia ya kwamba Muteba, mpenzi wake alikuwa anahusika na mauaji haya.

“Niambie Tete, muda unakimbia?” Willy aliuliza baada ya kuona kuwa Tete kweli kuna kitu alikuwa anakifahamu.

“Kwa nini usiende Polisi ukapige ripoti?” Tete aliuliza.

“Mimi sina haja ya Polisi, kama una haja ya Polisi nenda wewe, mimi ninataka unielekeze nani unafikiria?” Willy alijibu kwa mkato.

Tete aliamua amweleze, maana kwa sababu asizozijua alikuwa anamchukia sana Kabeya, Hata alikuwa amewahi kumweleza Muteba juu ya chuki yake kwa Kabeya, lakini Muteba hakutilia manani jambo hili. Alikuwa anahisi kuwa Kabeya alikuwa mtu mbaya katika matendo yake, hata aliwahi kumfikiria kuwa angeweza kuwa jambazi. Sasa wasiwasi wake ulikuwa umethihirika, ila kilichokuwa kinamsikitisha ni kwa nini Muteba ajiingize kwenye matendo maovu ya mtu huyu. Alimjua Muteba fika, hivi alishangazwa na kitendo hiki ambacho kilikuwa hakilingani naye, kwani alikuwa mtu tajiri na mwenye kuheshimika kama yeye Tete alivyomjua kwa binafsi hivi aliamua amweleze Willy kwani kumficha kungekuwa na maana kwamba alikuwa amefurahishwa na mauaji ya Mwadi. kitu ambacho kingemhangaisha moyoni mwake.

Aliinua kichwa chake akaangalia juu kwenye dari huku machozi yanaendelea kumtoka. Akiwa kama mtu ambaye yumo mwenye njozi alizungumza taratibu. “Nilifika hapa nyumbani kiasi cha saa kumi na robo hivi kutoka kazini. Kwa sababu Mwadi alikuwa ameeleza kuwa mtakuja nilifika hapa mapema ili kuwaandalia chakula cha jioni. Saa kumi na nusu hivi nikapata wageni. Wageni hawa walikuwa na rafiki yangu Muteba na rafiki yake Kabeya. Nilifurahi kumwona Muteba kwa sababu nilikuwa nimemtafuta kwenye simu bila kumpata. Niliwakaribisha halafu mimi nikaenda jikoni kuendelea na shughuli zangu. Kisha wote wawili wakaja jikoni ndipo Muteba akaanza kuniuliza juu ya uhusiano kati yako na Mwadi.

Kwanza nilishangaa wamejuaje hizi habari lakini nikafikiria kuwa huenda walikuwa wameonana na Mwadi na amewaeleza. Najua kuwa Kabeya alikuwa anamtaka hivyo kuwapo kwake nilikuelewa. Niliwaeleza yote ninayojua kati yako na Mwadi. Vile vile waliniuliza lini ulifika hapa mjini, nikawaeleza kuwa ulifika Jumatatu iliyopita. Walizungumza wao wenyewe mambo fulani kuhusu majina, na Kabeya akasema kuwa Mwadi lazima ndiye anajua kwa nini jina lako halikuwemo.

Sikuelewa maana yake na wala sikutilia maanani kiasi cha kuwauliza. Hivyo Kabeya aliaga akamwambia Muteba anaenda kumuona na Mwadi.

Muteba alibaki nyuma, kwani nilimweleza kuwa wewe na Mwadi mngefika hapa kututembelea na kuwa nilikuwa nimemtafuta kwenye simu muda mrefu bila kumpata, na kwa vile alikuwa amekuja nilimuomba abaki kusudi tuwasubiri wote. Akakubaliana na mimi akasema naye alikuwa anapenda kuonana na wewe lakini anaomba aende nyumbani kwanza akabadilishe mavazi ndipo arudi. Tokea hapo hajarudi tena. Hayo ndiyo ninayoyajua”, alimalizia Tete huku akiendelea kutazama juu.

“Huyu rafiki yako Muteba yeye anashughulika na nini?” aliuliza Willy kwa sauti ya huruma.

“Yeye ni mfanyabishara ana gereji yake inayoitwa Garage Banninga.” Kusikia hivi moyo wa Willy uligonga haraka haraka kwani ilionekana watu wote wenye magereji hapa mjini Kinshasa walikuwa wameunda kundi la ujambazi.

“Mmefahamiana toka lini?”

“Tuna mwaka na nusu sasa. Maana tulifahamiana baada ya mimi kurudi mjini hapa kutoka Brazzaville ambako nilikuwa nafanya kazi, kwani mjomba wangu yuko huko. Wakati natafuta kazi ndipo nilionana naye na ni yeye aliyenitafutia kazi huko Sozidime,” Tete alieleza. Willy alianza kuona mwanga mkubwa sana sasa. Kumbe Sozidime ilikuwa na uhusiano na haya magereji ya majambazi. Kitu hiki kilimpa dukuduku kubwa sana moyoni.

“Unajua huyu Kabeya anakaa wapi?” Willy aliuliza.

“Anakaa huko Yolo-Sud, barabara ya Ezo, nyumba nambari 32.” Tete alijibu.

“Tete tafadhali sana usimwambie mtu yeyote kuwa umenieleza mambo haya jaribu kurudia hali yako ya kawaida, na hata mpenzi wako Muteba usimweleze, maana maisha yako yanaweza kuwa hatarini ukieleza mambo uliyonieleza. Mimi nakwenda nitakuja kukuona tena. Kifo cha Mwadi nimeapa nitalipiza”, alisema Willy huku uchungu unampanda tena.

“Lakini hasa wewe ni nani, maana mawazo yangu yanaanza kukufikiria kwamba wewe si mfanyabiashara. Jinsi unavyofanya na jinsi ulivyo kama mcheza sinema.” Tete alimuuliza huku sasa akiwa anamwangalia Willy.

“Kiasi unachokijua kinakutosha, kunijua sana kunaweza kukawa hatari kwako”, alijibu Willy huku akisimama.

“Usiniache hapa Willy twende wote, nasikia woga tafadhali usiniache,” Tete alianza kulia tena. Kwa vile Willy alikuwa bado ana shughuli ya kufanya alimwambia:

“Wewe nenda ukalale kama una pombe kali, kama vile Whisky, kunywa halafu lala, mimi nitakuona baadaye,” alimwacha Tete analia Willy aliondoka akaingia ndani ya gari na kukata shauri kwenda nyumbani kwa Kabeya. Aliomba amkute Kabeya nyumbani maana alikuwa amepatwa na hasira juu ya mauaji ya Mwadi.

Alikuwa anajiona kuwa yeye ndiye chanzo cha kifo cha Mwadi, hivi mzigo wote wa kifo hiki aliamua kuubeba yeye mwenyewe binafsi. Wakati anaelekea nyumbani kwa Kabeya, mawazo yake yalikuwa yanafanya kazi sana. Habari alizokuwa amezipata kwa Tete zilianza kuleta picha yote ya mambo yalivyo. Ilikuwa inakaribia saa mbili wakati Willy alipowasili sehemu ya Yolo-Sud.

Alitafuta barabara ya Ezo mpaka akaipata. Kuangalia nambari za nyumba alikuta ameingilia kwa juu kwani alikuta yuko nyumba nambari 110 hivi alianza kuteremka polepole kwenye barabara hii mpaka akaiona nyumba nambari 32, akapitiliza mpaka mbele kidogo, akasimama na kuteremka na kuanza kurudi pole pole huku akiwa amejiweka tayari kabisa kwa mapambano ya aina yoyote.

SURA YA KUMI NA TATU

NYUMBA ya Kabeya ilikuwa imezungukwa na ua wa michongoma mifupi. Ilikuwa nyumba ndogo lakini nzuri. Willy alisikia furaha kwani aliona taa inawaka ndani ya nyumba hii kitu ambacho kilimaanisha kuwa kulikuwa na mtu ndani. Willy aliamua kuingilia nyumba hii kutokea nyuma. Hivi alizunguka nyumba hii kwa kupitia kati ya ua wa nyumba ya jirani na nyumba hii, na alitembea kana kwamba yeye ni mwenyeji wa sehemu hiyo ili wasiweze kumtilia mashaka. Alipofika nyuma ya nyumba hii aliruka ua na kutumbukia ndani ya ua wa nyumba hii. Alipotumbukia alianza kuizunguka nyumba hii kwa kunyatia na huku anasikiliza kama kulikuwa na mtu ndani.

Alisikia mtu anapiga mluzi ndani, akawa na uhakika kabisa kuwa Kabeya alikuwepo maana ni mara chache kumsikia mtu asiyekuwa mwenye nyumba kupiga mluzi saa kama hizi ndani ya nyumba. Alikagua madirisha ya vyumba vya upande wa kulia akakuta yote yamefungwa. Alirudi nyuma ya hii nyumba akatoa funguo zake malaya, akaufungua mlango wa kutokea uani kwa uangalifu na utaratibu sana bila kufanya lolote. Alipoingia ndani alijikuta yuko jikoni. Huku akiwa katika tahadhari, bastola mkononi alifuata kule mluzi ulikokuwa unatokea.

Alipofungua mlango wa jikoni alijikuta yuko sebuleni. Juu ya meza moja iliyokuwa na chupa ya primus, meza yenyewe ilikuwa karibu na makochi, hii chupa ilikuwa nusu na glasi iliyokuwa imejaa pombe. Hii ilimuonyesha Willy kuwa kulikuwa na mtu mmoja tu hapa ndani. Muziki ukiwa unatoka taratibu kwenye radio, mluzi uliendelea kusikika kutoka kwenye chumba kilichokuwa kushoto kwa Willy alipokuwa amesimama. Akisha viweka vitu vyote hivi maanani aliamua kuunguruma. Kabeya ambaye alikuwa na uhakika kuwa ni yeye.

Alinyata alikwenda mpaka kwenye ule mlango wa chumba na ghafla ule mlango wa chumba ulifunguka huku Willy akiwa ameiweka bastola yake mkononi ikiwa imemlenga mtu huyu aliyekuwa ndani ya chumba hiki akivaa nguo baada ya kukoga kama alivyoonekana.

Mtu huyu aliingiwa na hofu kubwa kwani ilionekana hakuwa kabisa anategemea kuwa jambo kama hili lingeweza kumtokea.

“Weka mikono juu,” Willy alimwambia huku anarudisha mlango. Mtu huyu ambaye alikuwa anafunga mkanda wa suruali, akiwa bado hajavaa viatu alifanya kama alivyoagizwa.

“Nasikia ulikuwa unanitifuta, nimekuja sasa. Mwadi amenieleza kuwa ulikuwa kwake kiasi cha saa kumi na moja unaniulizia. Niulize mimi mwenyewe sasa maana Mwadi alishindwa kukujibu,” Willy alimweleza kwa kebehi.

Kabeya alitetemeka kusikia maneno haya maana alikuwa ana uhakika kuwa alikuwa amemuua kabisa Mwadi kabla hajaondoka.

“Mimi sijui unavyozungumza,” Kabeya alijibu kwa hofu kwani sura ya Willy ilionyesha chuki kubwa sana,

“Sikiliza Kabeya, wewe ulikuwa unanitifuta mimi Willy, na ndiyo sababu umemuua Mwadi kwani Mwadi hakuweza kukueleza lolote juu yangu. Ukweli ni kwamba Mwadi alikuwa hajui lolote, lakini wewe hukutaka kumwamini mpaka umemuua, sasa mimi mwenyewe nimekuja niulize, la sivyo utaenda kuonana na Mwadi huko kwa Mungu mkashitakiane vizuri”

Kabeya alijui sasa ndiyo mwisho wa maisha yake, maana jinsi alivyokuwa ameingiliwa alikuwa hana hamu tena kabisa. Moyo wake wote wa ujasiri uliyeyuka kama kipande cha samli kwenye kikaango. Alianza kujuta kwa nini alimsikiliza Muteba ajiunge naye. Kila wakati alikuwa akijuta siku moja mwisho wake utakuwa mbaya, pesa kupenda pesa kulikuwa kumemponza, aligwaya Kabeya rohoni.

“Kama huwezi kuniuliza mimi, mimi nitakuuliza wewe. Hii GAD Garage ni mali ya nani?” Bila hata kufikiria Kabeya alijibu.

“Ni mali ya mzungu mmoja aitwaye Jean, ni raia wa Ubelgiji”.

“Umefanya naye kazi kwa muda gani?”

“Miaka mitatu na nusu sasa”.

“Je Muteba mna uhusiano gani?”

“Ni rafiki yangu, na tunatoka sehemu moja huko jimbo la Shaba. Ni marafiki wa siku nyingi. Muteba ndiye aliyenitafutia kazi na kunijulisha kwa Jean.”

“Nieleze yote unayoyajua juu ya njama zinazofanyika kati ya gereji Baninga, Papadimitriou, GAD na kampuni ya wakala ya Sozidime. Usinifiche kwani

kunificha unanunua tiketi ya kifo. Mimi ndiye jaji wako, naweza nikakuhukumu kufa au kukusamehe kutokana na ambavyo utakuwa tayari kushirikiana na mimi.”

Kabeya ambaye kwa kuogopa kufa alikuwa amesahau masharti yote ya 'WP' alianza kuropoka.

“Wote wanachama wa 'WP' moyo wa Willy ulishtuka akauliza. 'Wp' maana yake ni nini?” Kabla Kabeya hajajibu walisikia gari linafunga breki mbele ya nyumba hii. Kabeya akakumbuka kitu kilichokuwa kimemruka mawazoni ya kwamba Charles alikuwa aje kumpitia hapa ili waende kwenye shughuli ya kuwasaka akina Ozu na Kofi.

“Nani huyo?” Aliuliza Willy.

Kabeya akiwa amepata imani kidogo kuwa Charles akishirikiana naye angeweza kuokoka alijibu;

“Sijui ni nani”, Willy alijua amedanganywa. Charles akiwa pamoja na kijana mwingine waliingia moja kwa moja nyumbani kwa Kabeya kwani ni kitu ambacho walikizoea.

“Hey Kabeya uko wapi?” Charles aliuliza.

“Nakuja Charles,” alijibu kwa sauti ya wasiwasi Kabeya.

Willy alijua sasa mambo yameiva kwa Charles ndiye alikuwa amekodi gari lile lililokuwa linamfuata Ozu kutoka S.T.K. Mawazo ya Willy yalifanya kazi haraka sana kwa sababu alijua sasa hali ya hatari hata kwake ilikuwa imetangazwa. Ilibidi acheze vizuri mchezo huu la sivyoyangeweza kumletea matatizo. Alisikia Charles anazungumza na mtu mwingine akajua wako watu wawili, hapo sebuleni. Aliangalia saa yake akaona muda umekwenda. Alimuonyesha ishara Kabeya afungue mlango atoke nje, huku akiwa amemlenga bastola.

Kabeya alianza kupata moyo tena wa kijasiri akaamua hapa ndipo atajaribu kuokoa maisha yake. Willy alikuwa akimwangalia kila hatua yake. Kabeya alifungua mlango taratibu akatoka nje, Willy akiwa anamfuatia bastola mkononi. Ghafla kama umeme Kabeya alijitupa. Willy akafyatua risasi ikamkosa. Charles akatupa kimeza kidogo kilichopiga bastola na kutoka mikononi mwa Willy. Yule kijana mwingine alitoa bastola yake na kupiga risasi upande wa Willy, lakini aliruka kutoka pale kabla risasi haijafika, akamfikia Kabeya ambaye alikuwa anaanza kusimama na kumsukumia kwa nguvu sana kwa yule kijana mwenye bastola wakagongana huku bastola inafyatua risasi ovyo.

Charles ambaye alikuwa bado akili yake haijajua hasa nini kinatokea alimtwanga Willy teke la tumbo, lakini Willy akawahi kumshika na kumsukuma kwenye kochi ambalo alianguka nalo. Aliona bastola yake ilipokuwa kumbe na Kabeya ambaye alikuwa ameanguka juu ya yule kijana alikuwa na yeye ameiona. Hivi Willy alipoirukia na Kabeya naye alirukia wakafika wakati mmoja. Willy alimpiga kichwa Kabeya na kuruka pembeni kabla yule kijana mwenye bastola hajapiga risasi. Yule kijana alipopiga risasi zilimkosa Willy lakini zilimpata Kabeya ambaye alikuwa hajiwezi kutokana na dhoruba ya kichwa alichopata toka kwa Willy.

Risasi hizi zilimpiga Kabeya kichwani na kumjeruhi vibaya sana. Kitendo hili kilimshtua yule kijana, na kushtuka kwake kulimpa muda Willy kumrukia na kupiga teke bastola ile na ikaanguka sehemu nyingine ya chumba. Charles alikuwa amejikwa tayari lakini woga ulimwingia baada ya kuona kuwa Kabeya alikuwa amejeruhiwa vibaya sana kwa mikono yao wenyewe. Hata hivyo alijikaza akatupa konde moja safi sana, lililompata Willy na kumfanya aepesuke.

Yule kijana alichukua nafasi hii akampiga Willy ngwala na kumuangusha chini. Charles alimrukia hapo chini lakini Willy alimwahi na kumpiga farasi teke akaanguka upande ule mwingine na wakati huo huo Willy akawa amesimama na kukabiliana na yule kijana mwingine. Yule kijana alitupa ngumi ya kwanza Willy akaiona, akatupa ya pili akaiona, akatupa ya tatu Willy akaiona na pale pale akatupa shoto lake alilokuwa ameliweka kwa nguvu zote na kumtwanga huyo kijana ambaye alianguka chini na kushindwa kuinuka. Willy alimgeukia Charles ambaye alikuwa amesimama kutoka pale akamwambia.

“Mimi nachukia wazungu ambao wanaokuja kufanya udhalimu katika Afrika, leo utaniambia.” Akiwa amepandwa na mori na huku Charles naye akiwa amejawa na hasira walikabiliana kama mafahari ya ng'ombe. Charles alibadilisha akaanza kupiga kareti, kumbe hakujua kareti Willy ndiyo alikuwa mwenyewe. Walizipiga wakazipiga. Willy akaona huyu mtu anamchelewesha akambadilishia mitindo ya kareti kama mitatu halafu akamfungia kazi ya Kung-Fu. Alimpiga na dhoruba moja ya Kung-Fu ambayo Charles hakuweza kuizuia, ikamdhoofisha sana. Willy alimrukia akashika kichwa chake na mabega akapanda na kuvunja shingo lake na kumuua pale pale.

Wakati anazipiga na Charles alikuwa vile vile anaangalia kama yule kijana ameamka ama vipi. Mara hii alipogeuka baada kumuua, alikuta yule kijana anainua bastola huku akitetemeka karibu kufyatua risasi. Willy aliwahi tena kuruka kabla risasi hazijamiminika pale alipokuwa, na pale aliporukia palikuwa karibu na pale

Kabeya alipokuwa amelala na bastola yake ilikuwa karibu pale. Hivi alipotua pale tu alinyanyua bastola na kuwahi kumpiga yule kijana risasi na kumwua pale pale.

Willy alisimama bastola mkononi akamwendea Kabeya. Hali ya Kabeya ilikuwa mbaya sana kiasi cha kwamba angeweza kukata roho wakati wowote. Willy alimtingisha na kumuuliza, 'WP' ni chama gani," Kabeya aliinua macho na kumwangukia Willy huku sauti ikiwa inafifia alisema, "White po... po... power," halafu akakata roho. Willy aliondoka ndani ya nyumba hiyo huku akitembea haraka haraka aliingia ndani ya gari lake na kuelekea nyumbani kwa Robert.

Ilikuwa saa tatu na dakika kumi Willy alipowasili nyumbani kwa Robert. Alipoingia ndani alikuta wenzake wote wako tayari na wanamsubiri kwa hamu. Kule kuingia tu wenzake walijua jambo kubwa lilikuwa limetokea kwani sura yake ilikuwa imebadilika kabisa na kwenye bega shati lake lilikuwa na damu. Aliondoka akiwa amevaa suti lakini sasa alikuwa hakuvaa koti na wala tai hii yote ilidhihirisha kuwa huko alikokuwa mambo yalikuwa yamechafuka. Wote walikaa kimya huku wanamwangukia. Willy alienda akaketi kwenye kochi na Robert akamletea glasi ya whisky. Willy alianza kuwasilimulia kwa kinaganaga mambo yote yaliyokuwa yametokea toka alipoondoka mpaka wakati huo alipokuwa amerudi.

"Hii ina maana kuwa kuna chama au kikundi kinachoitwa White Power. Tukigundua kikundi hiki ni kikundi gani na kina madhumuni gani, na kwa nini kinaua ndugu zetu wapigania uhuru basi kazi yetu itakuwa imekamilika," Willy aliwaambia. Wenzake waliokuwa wanamsikiliza kwa makini, walionyesha sura ya masikitiko sana.

"Ingawa nilikuwa sijamwona Mwadi, nimehudhunishwa sana na tukio hili," alisema Kofi. Ozu na Robert nao walitingisha vichwa kuonyesha kuwa na wao walisikitishwa sana na mauaji haya ya kishenzi.

"Kama nilivyofikiria toka mwanzo baada ya kufanya upelelezi wangu kuwa kampuni yoyote iliyokuwa inawakilisha maslahi ya makaburu kiuchumi lazima itakuwa inashughulikia na maslahi mengine ya kisiasa kwa makaburu, sasa naanza kuona mwanga kabisa kwa haya magereji na hii kampuni ya wakala ya Sozidime ni ofisi za kijasusi za makaburu wanazozitumia huku wakidanganya watu kuwa zinashughulikia biashara. Kama Kofi alivyoieleza, nakubaliana naye kuwa watu wenye magereji haya na kampuni hiyo ni majasusi. Hii ndiyo sababu wameweza kufanya uhalifu mkubwa bila kujulikana kwa sababu wote hawa ni majasusi wa ujuzi wa hali ya juu kiasi cha kwamba idara ya polisi au ya upelelezi ya nchi ya

Kiafrika ni vigumu kuwagundua. Hivyo hii habari ya watu hawa kuwa na gereji ni geresha tu ya kuficha shughuli zao hasa,” alisema Robert kwa kirefu.

“Nafikiri ingekuwa rahisi kwetu kukikabili kikundi hiki cha 'WP' kama serikali ya Zaire ingekuwa inajua tuko hapa kwa sababu ya shughuli hiyo. Maana najua kuanzia sasa lazima tuwe macho maana tunaweza tukajikuta mikononi mwa polisi kabla hatujatekeleza shughuli yenyewe,” alisema Ozu.

“Maneno yako ni sawa, lakini tatizo tulilionalo ni kwamba msimamo wa serikali ya Zaire juu ya jambo kama hili haujulikani bado. Nafikiri hii ndiyo sababu tumetumwa hapa kisiri kwa sababu ofisi inayoshughulikia jambo hili nayo haijawa na uhakika na msimamo wa serikali ya Zaire. Lakini hata hivyo inabidi itabidi Robert amwambie Chifu juu ya matatizo tunayoweza kuyakabili kama serikali ya Zaire haitakuwa na habari yoyote kuhusu sisi. Uamzi atakatoa ndiyo huo tutaufuata, kwa sasa hivi sisi tuendeleo na shughuli hizi kisiri kama tulivyoagizwa,” alifafanua Willy.

“Sisi tuko tayari kwenda huko ‘GAD GARAGE’ kama tulivyokuwa tumepanga nafikiri kazi uliyoifanya kwa leo imetoshwa, wewe baki sisi twende,” Ozu alimshauri Willy.

“Hata kidogo, kazi tunayoenda kuifanya ni ngumu, hivi lazima twende wote ila Robert itambidi abaki”, Willy alieleza.

“Hapana, na mimi lazima niende, lazima na mimi nipewe nafasi ya kupambana na watu hawa.” Robert alilalamika.

“Si hivyo, shughuli hii ni kubwa hivi hatuwezi kwenda wote kwa pamoja, tutakuwa tunafanya mchezo. Kwanza wewe ni mtu ambaye huwezi kukisiwa kwa jambo lolote ovu na mtu yeyote hivyo lazima ubaki kama akiba yetu kwa wakati mbaya zaidi. Vile vile itabidi ubaki ili uweze kuzungumza na ofisi yetu ya Lusaka, kusudi uweze kuwaeleza yote yaliyotokea vile vile wakueleze kama wana habari zozote,” Willy alimweleza.

“Sawa kabisa, lazima Robert abaki,” Ozu alikubaliana na Willy.

“Na mimi nakubaliana na nyinyi kabisa, lazima Robert abaki kwa usalama wetu baadaye,” Kofi alimuunga mkono.

“Haya wengi wape”, alijibu Robert kwa masikitiko.

“Wewe ni balozi bwana tuachie sisi huu unyama”, Ozu alimtania.

“Nimeishiwa risasi, Robert nisaidie,” Willy aliomba.

Robert aliingia chumbani na kurudi na pakiti mbili za risasi. Willy alijaza bastola yake halafu akawauliza kama wenziwe walikuwa wanahitaji nao.

“Sisi tuko tayari kabisa”, Ozu alijibu. Kofi alionyesha bastola zake mbili alizokuwa ameisha zijaza risasi tayari. Willy aliwagawia wenzake risasi za akiba. Roberti alimletea Willy shati la kubadilisha. baada ya hapo wakaondoka kuelekea 'GARAGE GAD'

Saa hizi saa tatu za usiku, Pierre alikuwa nyumbani kwake akingojea kwa hamu kupata maelezo kamili, juu ya msako uliokuwa ukiendelea. Alikuwa ameishapata ripoti kutoka kwa Muteba, kuhusu maelezo waliyokuwa wameyapata toka kwa Tete juu ya Willy. Vile vile alimweleza kuwa Kabaya alipokwenda kumwona Mwadi alihisi kuwa Mwadi alikuwa anajua mengi juu ya Willy lakini hakutaka kueleza hivi Kabeya akamuua.

“Ni dhahiri kuwa huyu Willy ni mpelelezi, mmoja wa wale wengine, kwa hivi katika msako wetu na yeye yumo,” Muteba alikuwa amemweleza. Akiwa anangojea ripoti wa Pierre alikuwa na wasiwasi sana juu ya wapelelezi hawa. Mara simu ililia akainua haraka haraka.

“Hallo,” aliita.

“Patron, Muteba hapa, kumetokea mauaji mengine kwa upande wetu. Kabeya, Charles na Ngoma wameuawa. Bila shaka wameuawa na huyu Willy.” Kwa sauti ya utaratibu Pierre aliuliza.

“Unazungumzia wapi?”

“Nipo nyumbani kwa Kabeya”.

“Wape habari Jean na Papa kuwa wote njooni tuonane hapa,” Pierre aliamru na kukata simu.

SURA YA KUMI NA NNE

USIKU WA KAZI

Wakati wanaelekea gereji G.A.D. Willy aliwaeleza wenziwe mpango aliokuwa nao juu ya mashambulizi ya usiku huu. Baada ya mabishano kwenye mambo fulani fulani walikubaliana mpango huo. “Kwa hiyo jamani usiku huu utakuwa ni usiku wa kazi kubwa,” Willy alimalizia.

“Tumwombe Mungu.” Ozu alisema.

“Mungu atatusaidia, maana sisi tunachopigania ni haki za ndugu zetu huko Kusini mwa Afrika na wala hatumuonei mtu,” Kofi aliongezea.

Gereji G.A.D. ilikuwa sehemu za Gombe barabara ya T.S.F karibu na stesheni ya Televisheni lakini kwa upande mwingine. Willy alikuwa ameitafuta gereji hii wakati wa mchana na alikuwa ameiangalia kwa uangalifu sana. Basi akiwa anaendesha kwenye hi barabara ya 30 Juin alikata kona na kuingia barabara ya T.S.F. Akiwa anaendesha kwa mwendo wa kawaida alipita mbele ya gereji.

Ozu aliangalia saa yake ilikuwa ni saa nne kasoro. “Bado mapema sana, tungoje mpaka watakapofunga stesheni hapo saa tano,” Ozu alishauri.

“Hata mimi naona hivyo maana hata mitaa ya huku bado ina watu, waweza kutuletea kisanga,” Willy alisema, Kofi ambaye macho yake na mawazo yake yalikuwa kwenye hilo jengo la G.A.D. aliangalia ingawaje kwa upesi na kuona kuwa kulikuwa na walinzi upande ule wa mbele wa jengo hili.

“Kutakuwa na ulinzi mkali kwenye jengo hilo baada ya tukio la jana,” aliwaeleza wenziwe.

“Lazima tutegemee hivyo,” alijibu Ozu. Willy alienda mbele kidogo akageuza gari na kurudi huku wakipita kwa kasi sana mbele ya jengo hilo.

“Naona twende Cafe de la Paix tukapoteze muda pale, nadhani ni mahali penye usalama wa kutosha”, Willy alishauri.

“Pale ni pazuri sana, tunaweza tukauwa hii saa moja pale bila shida,” alijibu Kofi. Cafe de la Pix iko barabara ya 30 Juin. Willy aliendesha gari hadi pale, akaliegsha wakateremka.

“Tukae kwenye viti vye nje”, alisema Willy. Walikaa hapo nje na wakaagiza vinywaji. Kila mmoja wao aliagiza Whiski. Wakati wakiendelea na kinywaji chao Willy alimwita mfanyakazi mmoja aliyepita pale karibu.

“Samahani ndugu naomba kukuuliza”, Willy alimwambia.

“Bila samahani”, alijibu.

“Unaijua gereji Banninga?”

“Ndiyo”.

“Iko wapi?”

“Iko huko sehemu za Kintambo, barabara ya Bangala iko karibu na shule.”

“Asante sana nimeelewa”, Willy alijibu na yule mtu aliondoka.

Mahali penyewe nimepafahamu sasa nimeishafika pale. Mbele ya ile shule kuna kiwanja cha mpira na gereji hii inatazana na goli la mwisho kama ukiwa unatokea Kasavubu”, alieleza Kofi.

“Basi hamna taabu,” alijibu Ozu. Ilipotimia saa tano, waliondoka na kuingia ndani ya gari lao na kuelekea gereji G.A.D. Walipoingia barabara ya T.S.F. waliegesha gari lao karibu na majengo ya stesheni ya Televisheni na wote wakateremka. Wakati wafanyakazi wa stesheni ya Televisheni walikuwa wamemaliza zamu yao ya saa tano walikuwa wanaishiaishia kuondoka. Kwa hivi kuegesha gari lao wakati ule ilikuwa vigumu kutambulika.

“Mimi na Kofi tutatangulia kuingia ndani. Ozu atatufuata mara tu ukisikia mlilo wa bunduki”, Willy alieleza.

“Vizuri,” alijibu Ozu.

“G.A.D. Gaereji” ilikuwa imejengwa kwa mtindo sawa na 'Garage Papadimitriou' Willy na Kofi waliamua kuingilia gereji hii kwa kupitia nyuma. Waliingia kwenye uchochoro uliokuwa kati ya nyumba ya pili na ya tatu toka kwenye gereji na kuelekea nyuma ya nyumba hizi na nyumba ya barabara ya pili.

Walitembea kwa tahadhari kubwa, lakini walipofika nyuma ya ngome ya gereji hawakukuta ulinzi wowote.

“Nitatangulia mimi”, Kofi alimnong'oneza Willy. Kofi alipanda juu ya mabega ya Willy akashika juu kabisa ya ngome. Aliangaza chini akakuta yuko nyuma ya ofisi

kama vile alivyoona kule 'Gereji Papadimitriuos'. Hakukuwa na mlinzi yeyote kitu kilichomshangaza sana. kwani baada ya tukio la jana alitegemea kukuta ulinzi mkali kwenye magereji ya hawa watu. Alipanda juu akajitandaza juu ya ukuta wa ngome kisha akampa Willy mkono wake na kumvuta ili kumsaidia kupanda. Walipokuwa wamepanda wote ukuta waliteremka taratibu na kuangukia ndani ya ngome.

“Kama nyumba hii imejengwa kama ile ya Papadimitriuo, kuna dirisha kubwa kuzidi hili la nyuma kwa upande wa kushoto. Dirisha hili liko kwenye chumba cha mkutano, Tukiweza kupita humo tutakuwa tumeingia ndani ya chumba cha mkutano,” Kofi alimnong'oneza Willy.

“Tutajaribu kupitia huko”, Willy alijibu.

Walipoenda kwenye pembe ya upande wa kushoto Willy aliona kuna mlango upande ule, na wakati akichungulia mlango huo ulifunguliwa. Alimfanyia ishara Kofi na kumtahadharisha. Watu wapatao sita wakiwa na bunduki kubwa kubwa, walitokea kwenye mlango huu. Willy alishukuru bahati yao nzuri kwani alitambua kuwa walikuwa wamewawahi wakati watu hawa aidha akijitayarisha au wakihutubiwa. Ilionekana watu hawa hawakutegemea shambulio lolote kabla ya saa sita, watu wanne kati ya hawa sita walielekea upande wa mbele wa nyumba na wawili walielekea upande huu wa nyuma ambako Willy na Kofi walikuwa.

“Watu wawili wanakuja huku”, Willy alimnong'oneza Kofi. Walijibanza sawa na ukuta kusubiri. Watu hawa bila kujua kuna nini walikuja wanazungumza pole pole. Walipofika kwenye pembe hii ya kwenda nyuma wakasimama wakaweka silaha zao tayari. Kwa sababu hapakuwa na mwanga wa kutosha hawakuweza kuwaona upesi akina Willy kwa namna walivyokuwa wamejibanza kwenye ukuta. Willy alimwacha yule wa mbele akampita kidogo, yule wa pili aliyekuwa anafuata wenzake karibu karibu huku wanaangalia kwenye ngome alimgusa Willy maana alipita karibu sana na ukuta. Kugutuka tu Kofi na Willy waliwashambulia kabla akili zao hazijajua ni nini kinatokea. Kofi alimshambulia yule wa mbele na Willy yule wa nyuma. Watu hawa walipigwa na kuwaua kwa mikoni bila hata kupiga kelele. Pala karibu kulikuwa na gari bovu wakalifungua wakarundika maiti za watu hawa humo ndani zikafichika. Walipoangalia zile bunduki wakakuta ni 'machine gun' ambazo zilikuwa zimeishapakiwa risasi tayari kwa kutumika.

“Loo tumepata silaha, sheria yake”, alisema Kofi huku anaipima pima bunduki aliyochukua kutoka kwa yule mtu aliyemuua. Willy naye alichukua ile ya mtu mwingine.

“Nia yangu ni kutaka kuingia ndani, hivyo tutaingilia kwenye mlango huo waliotokea hawa watu”, Willy alimnong'oneza Kofi.

“Sawa”. Kofi alijibu. Wakiwa sasa wamebeba hizi 'machine gun' tayari tayari walielekea kwenye mlango. Walipofika kwenye ule mlango Wili aliweka sikio kwenye tundu la kuwekea ufunguo wa kufungulia, lakini hakisikia kitu. Alijaribu mlango akakuta umefungwa. Alitoa funguo zake malaya, akafungua kufuli taratibu bila kelele. Wakati huo Kofi alikuwa tayari tayari kwa lolote ambalo lingeweza kutokea. Walifungua mlango, na kuingia ndani na kufunga tena na funguo. Walijikuta wamo kwenye chumba kikubwa ambacho hakikukwa na kitu chochote ndani.

“Nafikiri wanachukulia mazoezi humu.” Kofi alisema.

“Nafikiri”, Willy alijibu kwa mkato. Walienda na kujaribu mlango mwingine wa kutokea ndani, wakakuta haukufungwa. Willy aliufungua taratibu akachungulia, hakukuwa na mtu ukumbini, akamfanyia Kofi ishara, wakajitokea ukumbini. Chumba kilikuwa kinatazamana na chumba walichokuwa wametoka kilikuwa kimewekwa kibao kilichoandikwa 'MKURUGENZI' Willy alimuonyesha Kofi ishara kuwa alikuwa anataka waingie mle.

Willy alijaribu ule mlango akakuta umefungwa, alitoa funguo zake malaya akajaribu tena zikafungua, wakaingia ndani na kujifungua. Kofi alitoa kurunzi ndogo mfukoni akaangaza kwenye meza kubwa iliyokuwemo, mbele ya meza kulikuwa na kibao kilichoandikwa “Jean Vergence” Hiki kibao kiliwafahamisha kuwa hii ofisi ilikuwa ni ya mwenye gereji. Willy alichukua kurunzi kutoka kwa Kofi akaanza kuangaza kwenye ukuta. Nyuma ya kiti kwenye meza hii kulikuwa na kabati la chuma. Willy alifikiria kuwa humo ndani ya hili kabati ndimo kungekuwa na makaratasi ya maana ambayo yangeweza kuwasaidia katika shughuli zao. Alisogelea kabati akaanza kulichunguza kama angeweza kulifungua. Kofi naye alisogea na kuliangalia. Willy alitoa fungu la funguo malaya zikiwemo funguo kadhaa malaya za kufungulia makabati kama haya. Funguo hizi alikuwa amezichukua kwani alitegemea matatizo kama haya.

Alijaribu ufunguo wa kwanza lakini haukufungua, alijaribu wa pili nao ulikataa, alipojaribu wa tatu ukafungua. Ndani ya kabati hili la chuma mlikuwa na sanduku dogo la fedha. Willy hakuwa anatafuta hicho hivyo alimulika mle ndani vizuri akaona mlikuwa na saraka ndani. Alivuta akakuta imefungwa alitoa funguo zake malaya tena akaanza kujaribu kufuli la saraka hii, kwa bahati alipojaribu tu mara

moja ikafunguka. Alipovuta akakuta mna bahasha moja kubwa akaitoa na kuifungua. Mara akasimama na bahasha yake mkononi.

“Hawa watu wamekwenda wapi?” walisikia mtu anauliza ukumbini.

“Hatujui maana sisi tulikuwa wanne tulioelekea mbele na wenyewe wakaelekea nyuma ya ofisi kama walivyotupanga, sasa hatuelewi imekuwaje...” sauti nyingine ilijibu. Walisikia mlango wa kile chumba walichoingilia unafunguliwa na sauti ikapotea.

“Wanawatafuta, watawaona sasa hivi.” Kofi alinong'ona.

“Tuondoke humu”, Willy alijibu.

Willy aliweka bahasha aliyokuwa ameichukua vizuri ndani ya shati, akafunga mkanda wake wa suruali sawa sawa, akafungua mlango akiwa 'machine gun' yake ameiweka begani na bastola mkononi tayari kukabiri hatari yoyote. Kofi naye alitoka nyuma ya Willy na kurudisha mlango. Ghafla mlango wa mbele wa nyumba ulifunguliwa na mlango wa kile chumba kikubwa nao ukafunguliwa. Kwa sababu taa ilikuwa inawaka ukumbini wale watu waliofungua mlango hii walionana ana kwa ana na Kofi na Willy. Wale watu walizubaa kidogo maana wao hawakutegemea kukutana na mtu yeyote ukumbini. Yule wa mbele alitaka kurudisha mlango lakini Willy aliwahi kumpiga risasi kabla yeye hajaweza kufanya hivyo. Alipoanguka chini bastola yake ilifyatuka na kufanya kelele nyingi. Bastola za akina Willy zilikuwa hazikufanya kelele kwani walikuwa wakitumia sailensa.

Baada ya mlio huu wa bastola, walisikia watu wanakimbia kwa nje. Kusikia hivi wakajua mambo yameiva. Waliweka bastola mifukoni, na kushikilia 'machine gun' vizuri. Kisha wakaruka ndani ya chumba kikubwa, wakasubiri kwani walisikia nyayo zikija, kwa upande wa mlango wa kutokea nje wa chumba hiki. Mara mlango ukafunguliwa kwa teke na risasi zikamiminika ndani ya chumba hiki, wao wakabana kabisa kwenye ukuta.

Yule mtu aliyekuwa anamimina risasi alipohakikisha kwamba hakuna mtu, aliingia ndani na hapo ndipo alishambuliwa na Kofi aliyemwauza kwa risasi. Walipokwisha kufanya hivi walitoka nje kwa kutokea mlango walioingilia pembeni mwa nyumba hii. Kofi aliekea nyuma na Willy akaelekea mbele ya nyumba hii. Wakaanza mashambulizi thabiti.

Ozu aliyekuwa amejificha kwenye uchochoro mmoja karibu na gereji hii, aliposikia mlio tu wa bunduki alijua kuwa kazi imeanza. Alikimbia mpaka kwenye lango la mbele, na kama alivyofikiria alikuta walinzi waliokuwa pale mlangoni wanakimbilia ndani kufuata mlio wa bunduki ulikotokea. Hivi hakupata upinzani wa aina yoyote pale langoni, kwa bahati alikuta lango limerudishwa tu bila kufungwa. Alisukuma lile lango na kuingia ndani, huku akiwa amejikinga mwenye magari mabovu akielekea kule kwenye ofisi ambako ndiko kulikuwa kunatokea milio ya bunduki.

Masamba ambaye ndiye alikuwa ameachiwa jukumu la kulinda gereji hii wakati Jean ameondoka alijikuta katika wakati mgumu sana. Alikuwa ameachiwa walinzi sita wakiwemo wapiganaji bunduki sita hodari sana. Yeye mwenyewe alikuwa muuaji hodari wa 'WP'. Na kazi hii alikuwa ameitekeleza vizuri kabisa kila alipokuwa ameamriwa kufanya. Akiwa katika ofisi yake, na huku akisikia mapigano yanaendelea huko nje, aliinua 'machine gun' yake na akachukua bastola mbili akaondoka tayari kwa kusaidia walinzi wake kwenye uwanja wa mapambano. Willy na Kofi walikuwa wamewazingira walinzi wa gereji hii. Ilikuwa rahisi kwao kuwazingira kwani walinzi hawa walikuwa wamekimbilia kule mlio wa bunduki ulikuwa bila kwunza kuangalia mambo yanakwendaje. Walitupiana risasi na Kofi kwa upande ule wa nyuma ya ofisi. Willy ambaye aliwaingilia kwa kutokea mbele hawakumuona, wao walifikiria wako kule risasi zilikokuwa zinatokea tu.

Willy alitambaa juu huku akiwa amezuiwa na magari haya mavovu. Kofi aliendelea kijibishana risasi na hawa watu ili kumpta nafasi Willy kuwashambulia kwa nyuma bila wao kutambua. Willy alipofika karibu kabisa nao, aliweza kuona jinsi walivyokuwa wamejipanga. Alitoa bastola yake na kuwapiga walinzi wawili risasi waliokuwa karibu naye. Kwa sababu bastola yake ilikuwa na sailensa wale walinzi wengine hawakutambua maana kulikuwa na giza.

Akasogea tena mpaka akawakaribia wengine wawili nao akawapiga risasi, mmoja wao haikumpata vizuri hivi akageunza na kuanza kupiga risasi upande ule wa Willy alikokuwa lakini Willy alimuwahi na kummaliza. Tukio hili ndilo liliwafahamisha walinzi waliokuwa wamebaki kuwa walikuwa wameishaingiliwa kwa nyuma. Kwa hofu walianza kupiga risasi hovyoo hii ikampa nafasi Kofi kutoka kwenye kona aliyokuwa amejibanza na kushambulia watu hawa kwa 'machine gun'. Wawili kati ya walinzi hawa waliuawa, na mmoja alitupa silaha yake akakimbilia mwenyewe magari kuelekea mlangoni.

Willy walikutana na Kofi na kujibanza kwenye gari moja.

“Naona tumewamaliza”, alidai Kofi.

“Sina uhakika”, alijibu Willy.

Ozu aiyekuwa anatafuta mlilo wa bunduki taratibu na kwa tahadhari kubwa alijigonga kwenye kitu. Alipoangalia amejigonga kwenye nini, akakuta ni mdomo wa tanki la petroli, linalopeleka petrol ndani ya gereji. Mara mawazo yake yakashituliwa kwani aliona mlango wa mbele unafunguliwa. Aliona mtu anachungulia kwa uangalifu sana halafu akatokeza akiwa ameshikilia bunduki yake tayari. Ozu aliona huyo si Kofi wala Willy, hivi akamwendea. Alichukua jiwe akalitupa nyuma ya huyu mtu. Mtu huyu aligeuka kama umeme huku akimimina risasi. Ozu alichukua nafasi hii akampiga risasi ambayo ilimpata huyu mtu kwenye bega, akatupa bunduki yake na kuruka wakati huo huo nyuma ya gari mojawapo, Masamba alijua huu ndiyo mwisho wa maisha yake. Hakujua mtu aliyekuwa amempiga risasi alikuwa amepiga kutokea sehemu gani. Alifikiria kukimbia lakini akaona hakuna njia ya kutoka sehemu hii, hivi aliamua apigane na watu hawa mpaka mwisho wake.

“Lazima Ozu ameingia unasikia mlilo huo,” Kofi alimnong'oneza Willy.

“Kumbe bado kuna walinzi, wewe zunguka ulikotokea, mimi nitarudi nilikotokea. Ukifika kwenye pembe ya nyuma na ya upande wa kushoto piga risasi, hii itanipa mimi nafasi ya kuwaingia watu hawa kumsaidia Ozu,” Willy alieleza. Ozu alijua amempiga yule mtu risasi, lakini haikuwa imemuingia sana kwa kutokana na yule mtu alivyoruka baada ya kupigwa risasi. Ilimdhihirishia Ozu kuwa mtu huyu alikuwa ni hodari, hivi alikata shauri amwendee kwa pupa. Mara alisikia risasi zinalia upande aliokuwa ameangukia huyu mtu. Hii ikampa nafasi Ozu na Willy kujua mtu huyu alikuwa wapi.

Ozu alipiga risasi mahali pale ambako Masamba alikuwa. Masamba alijiviringisha kutoka mahali pale lakini Willy akamuona na kumwachia risasi chungu nzima, na kumuua pale pale. Baada ya hapo kila mmoja wao alijibanza kukawa kimya. Ozu alipiga mluzi ambao ulikuwa ni wa kujijulisha. Willy alijibu halafu Ozu akabibu walisubiri tena kidogo kuhakikisha kuwa hakuna mtu mwingine ndipo wakapigiana mluzi wa kuondoka. Wakati wanakutanika mbele ya ofisi hii ndipo waliona yule mlinzi mmoja aliyekuwa ametupa bunduki yake na kukimbia akipitia kwenye lango na kukimbia nje.

“Huyo mmoja amewahi kutoroka”, Ozu aliwaonyesha.

“Tuondoke hapa, maana polisi au kundi la watu hawa linaweza kufika wakati wowote”, Willy alishauri.

“Pale mbele nimeona mahali ambapo tanki ya petrol lilipochimbuliwa, mnaonaje tukilipua gereji isionekane tena kabisa?” Alieleza Ozu.

“Wazo zuri sana, hakika tukilipua gereji hii tutakuwa tumbomoa kambi moja ya hawa wadhalimu na kubakiwa na makambi mawili ambayo vile vile itabidi tusalipue,” alijibu Willy. Ozu alichukua machine gun iliyokuwa imetupwa na Masamba, na haraka haraka wakakimbilia pale kwenye mdomo wa tanki. Mfuniko wa mdomo wa tanki ulikuwa umefungwa na kufuli. Ozu alipiga kufuli kwa risasi likasambaa na akafungua mfuniko wa tanki hili. Tanki lilikuwa limejaa petroli.

“Tangulieni,” Ozu aliwashauri. Willy na Kofi walikimbia kwenye uficho na kumwacha Ozu akishughulika. Ozu alichukua kitambaa chake, akakilowanisha ndani ya petroli akachukua kiberiti toka mfukoni kwake, akaenda mbele hatua chache halafu, akakiweka kile kitambaa moto, akakitupa pale kwenye mdomo wa tanki akaondoka mbio. Kufika mlangoni akakuta akina Willy wameshafika ndani ya gari, akarukia na wakaondoka kasi. Walipofika kwenye kona ya T.S.F. na 30 Juni walisimama kidogo kungojea kama mlipuko utatokea au vipi! Lakini waliona gari la polisi linakuja ikabidi waondoke.

“Tunaelekea 'Garage Baninga'... kabla hata Willy hajamaliza kusema, kulitokea mlipuko mkubwa ambao uliitingisha sehemu nzima ya Gombe.

Yule mlinzi aliyetoroka kutoka ndani ya ile gereji, alikimbia mpaka kwenye kibanda cha simu kilichokuwa karibu. Alipiga simu kwenye nambari ya simu waliyokuwa wamepewa kupiga kama jambo lolote litatokea.

“Hallo,” aliita.

“Hallo unasemaje?” Sauti ilijibu.

“G.A.D.” alijibu.

“WP”, alijibiwa.

“Aha, G.A.D imeshambuliwa tafadhali tumeni msaada upesi sana kama kikosi kizima kinatushambulia,” alieleza huku akitetemeka.

“Sawa,” alijibiwa na simu ikakatwa. Pierre na wenzake walikuwa wamemaliza mkutano wao uliokuwa umeitishwa usiku ule wakati simu wakati simu ilipolia. Pierre aliinua simu, “Hallo”, aliita.

“Patron?” aliulizwa.

“Ndito”, alijibu. 'G.A.D. inashambuliwa sasa hivi. Mapambano bado yanaendelea, nimetuma watu wengine kwenda kusaidia kutoka Papadimitriou,” alielezwa.

“Vizuri tunakuja,” alijibu na kukata simu. “G.A.D. inashambuliwa twendeni”, aliwaeleza wenzake kwa kifupi.

“Hapana Patron, wewe baki sisi tutaenda kule hatuwezi kwenda wote”, Jean alishauri.

“Ndiyo sisi tutakwenda wewe baki”, Papa alikubaliana na Jean

“Mkiwakuta watu hawa tafadhali wauweni kabisa, sina haja ya kuwahoji, wameishafanya ubaya mwingi kiasi cha kuonana nao. Mimi nitawapa muda wa kutangulia halafu nitampigia afisa mmoja wa polisi rafiki yangu kuwa wezi wanashambulia gereji 'G.A.D.’, alieleza Pierre. Kisha aliingia ndani ya stoo akatoa bunduki na mabomu ya mikono akawapa hawa wenzake na wakaondoka wakiwa tayari kwa mapambano huko G.A.D.

SURA YA KUMI NA TANO

NI WAKATI walipokuwa wanaingia barabara ya Bokasa waliposikia mlipuko mkubwa uliotingisha sehemu nzima ya Gombe. Waliongeza mwendo na walipofika kwenye kona ya barabara ya 30 Juin na T.S.F. ndipo walipotambua kilichokuwa kimetokea kwani, watu wote waliokuwa wanakaa sehemu hiyo walikuwa wanakimbia ovyo kwa hofu. Walipofika sehemu ya 'Gereji G.A.D' ilipokuwa imesimama hawakukuta kitu. Tokea majengo, magari na kila kitu kilichokuwemo ndani ya sehemu ile kiliteketezwa. Nyumba zilizokuwa jirani nazo ziliharibika ingawaje si sana, maana ngome ya gereji ilizisaidia kustahimili mlipuko huu, kwani ngome yote nayo ilianguka.

“Hakika hawa watu ni wanaharamu sana,” alisema Jean kwa chuki. Mara wakasikia milio ya magari ya polisi na zimamoto unaelekea sehemu hii.

Walinzi waliokuwa wametokea Gereji Papadimitriou walifika nao wamechelewa.

“Rudini sehemu zenu”, Papa alimwelezea kiongozi wa watu hawa. Papa, Muteba na Jean waliingia ndani ya gari lao na kuelekea gereji ya Papadimitriou katika uchunguzi mwingine.

Wakati Willy na wenzake wakielekea gereji Baninga. Kofi aliwaeleza namna gereji ile ilivyokaa maana aliwahi kufika kwenye gereji hii alipokuwa ameharibikiwa na gari, safari moja alipokuwa hapa mjini Kinshasa. “Gereji yenyewe imezungukwa kwa ua wa seng'enge na uwanja wake ni mkubwa kuliko G.A.D. Kuna stesheni ya petroli nje tu ya gereji, na stesheni hii ni mali ya gereji hii. Hivi nina imani kuwa tanki la petroli la stesheni hii litakuwa ndani ya ua wa gereji kwa usalama. Kuna majengo mawili makubwa mojawapo likiwa ni ofisi na moja linatengeneza kivuli cha magari. Kitu kingine cha kufikiria ni kwamba katika sehemu hii ya Kintambo kuna kambi ya jeshi ambayo iko karibu nusu maili kutoka kwenye gereji hii. Nafikiri maelezo haya yatawapa mwanga jinsi gani tutakavyoiingilia gereji hii”, alimaliza Kofi.

“Kama ni hivyo, mimi naona ya kwamba uzi uwe ule ule. Tukifika pale mashambulizi yetu yawe ya moja kwa moja. Ozu kazi yake itakuwa kutafuta mdomo wa tanki uko wapi wakati sisi tukipambana na walinzi watakaokuwepo. Ozu akishapata mdomo huu, atapiga risasi hewani kutupa ishara, halafu atafanya kama alivyofanya kule na kuondoka. Shambulizi hili itabidi tulifanye kwa muda

mfupi sana ili tusiwape nafasi wanajeshi kutuwahi. Kwani ikiwa watasikia mlio wa bunduki lazima watakuja. Nataka wafike wakati sisi tumeishaondoka,” alishauri Willy.

“Hamna taabu silaha tulizonazo zinatoshia kabisa kuzuia jeshi zima”, alisema Ozu ambaye alikuwa anafurahishwa sana na matukio ya usiku huu. Yeye kama wenzake alipenda sana kashikashi za namna hii. Walipofika barabara ya Bangala walisimamisha gari karibu na shule halafu walichukua silaha zao na kuanza kukiimbilia gereji Baninga. Kila mtu alichukua sehemu yake. Ozu ndiye alikuwa aingie kwa mbele. Kofi kwa nyuma na Willy kwa pembeni. Wote walipokuwa wameshika nafasi zao walingojea Kofi aanze mashambulizi kama walivyokuwa wamepanga.

Kofi aliruka ua wa seng'enge na kutumbukia ndani ya gereji na pale pale akaanza kusambaza risasi. Wale walinzi waliokuwa pale wengine walianza kusinzia. Mara waliposikia mlio wa bunduki walishika bunduki zao na kuanza kukimbia bila mpango. Willy aliruka seng'enge kwa upande wa pembeni na kuanza kushambulia vile vile. Ozu naye aliruka upande wa mbele na kuanza kushambulia vile vile. Walinzi wa hapa waliingiwa na kiwewe maana walisikia mashambulizi yanatoka kila sehemu.

Hii iliwafanya waende ovyo na hivi ikawa rahisi kwa Willy na wenzake kuwashambulia. Ozu aliangalia stesheni ya petroli ilipokuwa na akahisi sehemu gani tanki lingeweza kuwa. Huku akiwa anashambulia alienda sehemu ile na kuanza kutafuta. Willy na Kofi walikuwa wanashambulia vizuri sana na walikuwa wameua walinzi wengi. Walinzi waliobaki waliendelea kujihami kwa kupiga risasi mfululizo bila kukoma, ili kuzuia mashambulizi yaliyokuwa yanakuja. Kwa ajili ya kiwewe hawakujua kuwa kwa kufanya hivi wangeweza kumaliza risasi, mkasa ambao walijikuta wamo baada ya muda mfupi. Hivi walianza kukimbia ovyo.

Ozu aliona mdomo wa tanki akapiga risasi hewani. Kisha akaanza kulishambulia kufuli, na baada ya kulisambaza kwa risasi akafungua mdomo wa tanki. Willy na Kofi walisikia ishara hii waliruka na kutoka nje ya ua. Wakati Willy anaruka alimuona mlinzi mmoja naye anaruka ua karibu na yeye, Willy alimfuata na kumkamata. Mara Kofi naye alifika wakamvuta yule mtu na kukimbia naye. Tanki la petroli lilikuwa karibu na seng'enge, hivi Ozu alitafuta tambara akalipata, akalichovya ndani ya petroli, na halafu karuka ua wa seng'enge. Alipofika nje ya seng'enge aliwasha lile tambara moto, akalitupa kwenye mdomo wa tanki lilipokuwa limefunikwa na akaanza kukimbia kule walikoacha gari.

“Tayari”, aliwaeleza wenzake ambao walikuwa na mateka wao. Aliingia ndani ya gari wakaondoka. Kazi hii ilikuwa imefanywa kwa dakika nne. “Je huyu mnampeleka wapi?”, Ozu aliuliza.

“Atatusaidia kazi moja sasa hivi,” Willy alijibu.

“Mbele kidogo kwenye barabara ya Kasavubu baada ya kona ya Kasavubu na barabara ya Bangala kama unaelekea mjini walikuta kibanda cha simu. Willy alisimamisha gari na kumuamuru yule mtu ateremke. Willy, Ozu na yule mtu waliteremka na kumuacha Kofi akiwa ameliwasha gari tayari tayari kwa kuondoka wakati wowote. Walipofika kwenye kibanda cha simu Willy alimweleza mtu huyu,

“Kama unataka kuishi nipe nambari za simu ya gereji Papadimitriou. Nikipiga nikiwapata, nitakupa simu uzungumze nao. Waeleze maneno haya. Gereji Baninga imeshambuliwa lakini hawa watu walioshambulia tumepambana nao wakakimbilia hapa shuleni, sasa tumewazingira tunarushiana risasi tunaomba msaada, umeelewa?” Willy alimuuliza.

“Ndiyo”, yule mtu alijibu kwa woga. Mtu yule alitoa nambari za simu ya Papadimitriou bila kusita. Willy alipiga na ikapokelewa mara moja akampa yule mtu. Yule mtu alizungumza nao, na baada ya kujitambulisha aliwaeleza maneno aliyokuwa ameelezwa kusema na Willy, na baada ya kuzungumza tu Willy akakata simu. Halafu akamkata huyu mtu mkono na shingo akaanguka chini akiwa amezirai.

“Twenze zetu sasa gereji Papadimitriou,” aliwaeleza wenzake huku wakiingia ndani ya gari.

“Ahaa, nimekuelewa sasa kwanini umefanya hivyo. plani nzuri sana,” alisema Ozu. Mara wakasikia mlipuko mkubwa mno uliotetemesha sehemu yote hii ya Kintambo.

Jean, Muteba na Papa walikuwa wanaingia ofisini kwa Papa, ili wafanye mipango ya kuwazuia watu hawa, wakati Lemba mmoja wa wasaidizi wao wakubwa aliyekuwa amebaki baada ya Kabeya, Charles na Masambba, alipowajia.

“Tumepata simu kutoka Baninga kwa Mavungu. Anasema Baninga nayo imeshambuliwa lakini wameweza kupambana na watu hawa, na hivi sasa wamewazingira pale shuleni wanaomba msaada kwani mapigano makali yanaendelea”.

“Kazi nzuri, twende huko sisi wenyewe, Lemba acha watu wanne tu hapa wengine wote twende mchana hapo sasa ndio mahali pa kufa na kupona”, Papa aliamrisha. Wote wakiwa wamebeba silaha zao tayari, waliingia ndani ya magari matatu na kuelekea Kintambo. Bila kujua wakapishana na gari la akina Willy ambalo lilikuwa linaelekea gereji Papadimitriou. Plani ya Willy ilikuwa imefanya kazi.

Magari ya akina Papa yalipopishana na gari la akina Willy, nara moja akina Willy waliyatambua.

“Hao wanakwenda plani yangu imefanya kazi,” Willy aliwaeleza wenzake.

“Lo, tuna bahati sana usiku huu”, alinena Ozu.

“Hii gereji Papadimitriou iko vipi?” Aliuliza Willy.

“Imejengwa sawa sawa na gereji G.A.D. haina tofauti hata kidogo. Jinsi ulivyoona ndani ya G.A.D ndivyo ilivyo hivyo na Papadimitriou”, alieleza Kofi.

“Inabidi tutumie uzi ule ule wa kuyalipua makambi haya. Je kuna petroli stesheni mle ndani?” Aliuliza Willy tena.

“Kama nilivyokwambia petroli stesheni ya Papadimitriou iko ndani kama ile ya G.A.D. na imekaa vile vile. Nafikiri hata mahali tanki lilipochimbiwa litakuwa katika sehemu kama ya kule G.A.D.,” Kofi alisisitiza.

“Bila shaka”, alizidi kusiondwa Ozu.

“Kama ni hivyo operesheni yetu ni kama kawaida. Hapa napo lazima tufanye haraka kama tulivyofanya kule Baninga, maana watu hawa wakikuta wamedanganywa watarudi kama risasi,” alieleza Willy wakati anasimamisha gari lake kwenye kona ya barabara ya Assossa na Kabambare. Kila mtu akiwa amechukua silaha yake kamili kamili walikimbia huku wakiwa wanajificha ndani ya vivuli vya nyumba za jirani.

Wote waliamua kushambulia kutoka kwa nyuma, na kwa vile walikuwa wamepandwa na mori sasa walikuwa wakifurahia shughuli yote hii. Walipandishana ukutani haraka haraka na kutumbukia ndani. Walinzi wote wanne waliokuwa wamebaki hapa walikuwa wako mbele ya ofisi wakielezana walivyokuwa na bahati ya kuachwa kwenda kwenye mapambano na watu hawa watatu.

“Nasikia watu hawa wana ujuzi kweli, kuonana nao ni kutafuta kifo tu, ni watu wasiowezezana,” mmoja wao alieleza.

“Mimi leo ndiyo mwisho wangu kwa kazi hii, kesho natoroka moja kwa moja sitarudi,” wa pili alieleza. Wote wakacheka bila kujua kuwa wameingiliwa.

“Utaacha pesa zote hizi! mimi niko tayari nipambane na hao watu ili nipate hizi pesa ikiwa nitamaliza mkataba huu hai”, mwingine alisema.

Willy na wenzake waligawanyika. Willy alipita upane wa kulia na Kofi na Ozu wakapita upande wa kushoto na kunyatia wakielekea mbele. Walipofika karibu na mbele wote walisikia maneno waliyokuwa hawa walinzi wanazungumza.

Walipokuwa wamefika kabisa kwenye pembe ya kutokea mbele. Willy alijitokeza na kusambaza risasi na Kofi na Ozu wakafanya hivyo vile vile. Walinzi wote wanne waliuawa pale pale.

Bila kupoteza muda walitafuta mahali tanki lilipokuwa limechimbiwa wakapata bila taabu. Ozu alifanya shughuli yake kama kawaida baada ya kufungua mdomo wa tanki, akachovyo kitambaa alichopewa na Kofi ndani ya petroli wakaondoka hatua chache . Ozu akawasha kitambaa akakitupa pale kwenye mdomo wa tanki, na wote wakakimbia na kuondoka pale. Walienda moja kwa moja mpaka kwenye gari lao wakaingia wakawasha moto huku wakingojea mlipuko.

“Haya matanki ya petroli yameturahisishia kazi. Usiku wa leo sintakaa niusahau”, alisema Ozu. Mara wakasikia magari yanakuja.

“Hao wanarudi”, Willy aliwatahadharisha wenzake. na wakati huo huo mlipuko ukatokea uliotetemeshwa sehemu nzima ya Lingwala. “Kwa leo kazi hii imetosha twendeni tukapumzike”, Willy alishauri.

SURA YA KUMI NA SITA

MAPAMBANO BADO YANAENDELEA

Ilikuwa yapata saa nne za asubuhi Willy alipoamka. Kwani usiku ule walikuwa wameingia kitandani kiasi cha saa kumi ya asubuhi baada ya pilika pilika kubwa walizokuwa wamezifanya. Wote walikuwa wamerudi nyumbani kwa Robert, kwani waliogopa kurudi mahotelini kwao wakihiisi kuwa wangekuwa wanangojewa na magaidi hawa. Alipoamka alienda akaoga halafu akaelekea sebuleni kuangalia kulikuwa na nini. Aliwakuta Ozu na Kofi wameisha amka na walikuwa jikoni wanakaanga mayai.

“Loo, hata mimi njaa inaniuma afadhali nimewahi”, Willy alisema.

“Njoo ujisaidie,” Ozu alijibu.

Wote watatu walikaa jikoni wanakula mayai ya kukaanga bila chai wala kahawa.

“Robert yuko wapi?” Willy aliuliza.

“Aliacha ujumbe kuwa tusiondoke tumsubiri mpaka atakapokuwa amerudi,” Ozu alijibu.

“Mliwahi kuzungumza naye usiku tuliporudi?” Willy aliuliza.

“Ndiyo alikuja chumbani kwetu na tukamweleza kwa kifupi tu mambo yalivyokwenda. Tuliagana kuwa tungezungumza kwa kirefu asubuhi hii,” alijibu Ozu.

Wakiwa bado wanazungumza, walisikia gari linapiga breki mbele ya nyumba. Ozu alipochungulia alimwona ni Robert alikuwa amerudi. Wote walihama jikoni na kwenda kuketi sebuleni.

“Huu ndiyo utakuwa mwisho wa kujipikia, msichana wangu anarudi leo kutoka Brazzaville,” Robert alisema huku akiketi chini.

“Hakuna haja, sisi wenyewe ni wapishi hodari”, alijibu Kofi.

“Lo, msichana wangu ni mpishi stadi kweli chakula chake akipika ni kitamu kama yeye. Ozu alikusanya sahani zao walizotumia kwa kula mayai akazirudisha jikoni. Willy alienda chumbani kwake akaichukua ile bahasha aliyokuwa ameichukua

kule G.A.D. akarudi nayo sebuleni. Willy alimweleza kwa kirefu Robert juu ya shughuli waliyokuwa wameitekeleza usiku ule.

“Kwa ujumla makambi wa wadhalimu hawa tumeyateketeza, sasa lililobaki ni kuwakamata watu hawa wanaohusika ili kuvunja kabisa kikundi hiki kinachojiita 'White Power'. Sasa namna ya kuwakamata na kupata ushahidi kamili wa kuweza kuiridhisha Serikali ya Zaire kuwa kweli hawa ndio wamehusika na mauaji mengi yaliyotokea katika Bara la Afrika, ndilo tatizo kubwa lililobaki”, Willy alimalizia.

Kisha alifungua ile bahasha akaanza kutoa makaratasi yaliyokuwemo. Mlikuwa na makaratasi mengi yaliyokuwa yanazungumzia mambo ya biashara ya spea za magari. Kwanza Willy aliyapitia makaratasi haya haraka haraka huku akiyapitisha kwa wenzake.

Karibu na kuyamaliza makaratasi mengi yaliyokuwa ndani ya ile bahasha. Willy aliona barua moja iliyokuwa inatoka kwenye Kampuni moja iitwayo Baseh Overseas Speres Supplies (S. African) Ltd. Ilikuwa imeandikwa kwa Mkurugenzi wa Kampuni ya 'Sozidime Agence' ikimtaka amweleze mkurugenzi wa gereji iitwayo 'Garage du Peuple' kuwa ajitayarishe kupata spea kutoka kwa kampuni za watu wafuatao.

1. Leon Fadaka
2. Nelson Chikwanda
3. Komba Matengo
4. Omo Nene
5. Edger Mongo
6. John Lupala
7. Mateo Chiunia
8. Lumala Nchitole
9. Stephen Magwasa
10. David Makandala

Maelezo zaidi yatafuata baadaye. Willy aliweka chini makaratasi mengine akasema.

“Mwishowe tumepata kitu tulichokuwa tunatafuta hebu sikilizeni niwasomee barua hii,” Willy alieleza kisha akawasomea. Wenzake wote waliinuka na kumzunguka Willy ili kuiangalia ile karatasi kwa macho yao, karatasi hii ilikuwa nakala.

“Unaona sasa, ukichukua kifupi cha Kampuni hii, inakuja BOSS. Hii ina maana kikundi tunachoshughulika nacho ni kikundi cha Shirika la kijasusi la Afrika Kusini (BOSS). Robert alivyokuwa amebuni ni sawa kabisa”, Willy alieleza.

“Afadhali sasa tumekuwa na uhakika na ushahidi angalau kidogo kuwa Kampuni ya Sozidime Agence pamoja na magereji mengi ya hapa mjini Kinshasa ni ofisi za Boss zinazoendeleza udhalimu katika Afrika. Inaonekana magereji yanayohusika ni mengi, 'Garage du Peuple' mimi ninaifahamu ni gereji moja kubwa sana iliyoko kwenye sehemu za viwanda huko Limete. Kama tulifikiria kazi imekwisha inaonekana kuwa ndiyo imeanza”, Robert alieleza.

Hakika kazi ndiyo imeanza, majina yote yaliyokuwa yametajwa Willy alikuwa anawajua watu hawa, bila shaka hata wewe umeweza kugundua kuwa majina matano ya kwanza yalikuwa ya watu waliokuwa wameisha uawa. Wale watano waliobaki vile vile walikuwa ni maofisa wa juu sana waliokuwa wanaongoza harakati za ukombozi kusini mwa Afrika. Hivi Willy alianza kuwaelezea wenzake juu ya watu hawa.

“Tuna bahati kuwa tumeipata orodha ya maofisa wa wapigania uhuru ambao Afrika Kusini imeamua kuwaua, watano tayari wameishauawa na watano walikuwa mbioni kuuawa. Robert inakubidi umwarifu Chifu juu ya orodha hii bila kuchelewa. Na umuulize karatasi hii tuifanyeje.” Willy alimweleza Robert. Willy aliangalia hiyo karatasi tena, akakuta ilikuwa imeandikwa tarehe 15 Juni miaka mitatu iliyokuwa imepita waliyaangalia makaratasi mengine na wakawa wamekusanya maelezo kamili kuhusu kikundi hiki kiitwacho 'White Power' ambacho sasa walijua kwa dhati kuwa ni tawi la BOSS.

“Kama tulivyo kwishasema hawa watu wote tunaopambana nao ni majasusi wa Boss. Boss imeingia katika nchi huru ya Afrika na kuweka mizizi huku ikiwa imekaa raha mustarehe ni jambo la kusikitisha sana,” Kofi alisema kwa masikitiko makubwa.

“Hilo ndilo tatizo tulilonalo Afrika,” alijibu Ozu.

“Haya tuyaache yalivyo kwanza tumsikilize Robert naye atueleze ya kwake kama kuna maelezo yoyote”, Willy alisema.

Robert aliyekuwa amesimama alienda na kukaa chini halafu akasema.

“Nina mambo mengi sana ya kuwaelezeni, jana usiku mlipoondoka nilizungumza na Chifu nikamweleza yote kama tulivyokuwa tumeamua. Yeye alinieleza kuwa tuendele katika hali hii hii mpaka hapo atakapotupatia maelekezo mengine. Asubuhi hii niliondoka nikaenda ofisini ambako nilituma habari kwa Chifu juu ya matukio ya jana usiku kama Ozu alivyokuwa amenieleza kwa kifupi”, alinyamaza kidogo ili kupitisha mate halafu akaendelea.

“Baada ya kupeleka habari kwa Chifu nilimtafuta rafiki yangu wa C.N.D. nikazungumza naye ili nijue serikali ina msimamo gani juu ya matukio ya jana usiku. Habari alizonipa ni kuwa serikali inaendelea na uchunguzi mkali sana. Wale wenye magereji yaliyolipuliwa wameisha andika maelezo kwa kifupi kuwa wanafikiri wenye magereji wenzao ambao walikuwa wanawaonea wivu wa kibiashara ndio wamefanya uhalibifu huu.

Vile vile alinieleza kuwa hii Kampuni ya Sozidime Agence ambayo ndiyo wakala wa magereji haya yaliyolipuliwa imepiga makelele mengi sana, na kutaka serikali ichunguze tukio hili, na kuwakamata wanaohusika na kuwapeleka mbele ya mahakama. Alisema Mkurugenzi wa Sozidime ni mtu ambaye anaheshimiwa sana serikalini na ana nguvu nyingi sana kwa Serikali maana Mawaziri wengi ni marafiki zake. Amewahi kuwasaidia sana katika mambo yao ya kibiashara, hivi neno lake lolote lazima lishugulikiwe kikamilifu. Hivyo polisi na C.N.D wamo katika uchunguzi wa matukio yote ya jana, tokea ya Mwadi, Kabeya na wenzake mpaka yale ya usiku”, Robert alinyamaza tena kidogo ili kupumua halafu akamwangalia Willy na kuendelea.

“Juu ya mauaji ya Mwadi, Willy inasemekana unahusika. Watu wa pale hotelini wameeleza kuwa wewe ulikuwa na uhusiano naye, na kuwa tangu Mwadi ameuawa ulikuwa bado haujaonekana. Hivi sasa kuna polisi pale Hotelini Memling anakusubiri ili kukuuliza juu ya mauaji hayo, hivyo lazima uwe tayari kwa maswali. Baada ya kuachana na huyo rafiki yangu wa C.N.D nilikwenda kuangalia kama Kadima Kashimuka amerudi kutoka Zambia. Kwa bahati nimepata habari kuwa amerudi leo asubuhi, na kwa vile kutakuwa na mkutano saa sita Wizarani kwao atakuwa ofisini mchana mpaka saa tisa wakati wanapotegemea mkutano huo kwisha. Hayo ndiyo niliyopata katika uchunguzi wangu”, alimalizia Robert.

“Umefanya kazi nzuri sana. Sasa inaonyesha jinsi BOSS inavyoweza kujiingiza ndani kabisa ya Serikali ya Zaire na kujijenga thabiti. Hii inaonyesha kuwa kiungo hasa cha ujasusi katika eneo hili la Afrika ni hii Kampuni ya Sozidime. Kwa hivyo tukiiangusha Sozidime tutakuwa tumevunja kabisa mikondo ya kijasusi ya BOSS

katika Afrika. Ni imani yangu kuwa tukifikia hapo tutakuwa tumemaliza kazi yetu. Ninachowaomba ni kila mtu akae anafikiria jinsi gani tutaweza kuikamata ofisi hii bila kugombana na serikali ya Zaire kitu ambacho ndicho kinafanya kazi yote hii iwe ngumu”, Willy alieleza.

“Sasa unasemaje juu ya huyu Kadima?” Robert aliuliza.

“Hivi sasa mimi ninaondoka kwenda hotelini kwangu ili niweze kupambana na hao polisi ili niweze kujisafisha. Saa nane na nusu ningojee pale nje ya ofisi zenu nitakupitia hapo. Jaribu kufanya kila njia umfahamu kwa sura huyo Kadima, ili hiyo saa tisa tukamsubiri hapo ofisini kwake na tutajua la kufanya hapo hapo”, Willy alishauri.

“Sawa, nitajitahidi”, alijibu Robert.

“Sisi tunaondoka tukaiangalie hiyo Garage du Peuple ili tuwe na ramani yake kamili. Inaonekana huenda katika gereji hii ndiko kuna mkubwa zaidi wa hawa wengine, huenda ndiyo sababu tulikuwa bado hatujaigungua”, Ozu alieleza.

“Lakini mjiangalie sana, sababu watu hawa watakuwa kama Simba aliyejeruhiwa wanaweza kufanya lolote,” Willy alionya.

“Usiwe na wasiwasi tutajitahidi kujiangalia”, Ozu alijibu.

“Kwa hiyo saa ngapi tutaonana hapa?” Kofi aliuliza.

“Kiasi cha saa kumi tuwe wote hapa”, Willy alijibu.

Willy alienda kwenye simu akapiga simu. “Hapo ni STK?” aliuliza.

“Ndiyo, STK uwanja wa ndege,” alijibiwa.

“Naomba kuzungumza na Ntumba”.

“Subiri”. Alijibiwa. Baada ya muda kidogo aliitikiwa;

“Hallo Ntumba hapa”.

“Willy hapa, habari yako?”

“Nzuri Willy, habari yako?”

“Nzuri,” Willy alijibu, “Habari za Brazzaville?”

“Nzuri tu,” alijibu, “Ehe lete habari ninapewa miadi au vipi?” Ntumba alisema kwa sauti ya kejeli.

“Samahani Ntumba, nina tatizo naomba unisaidie.”

“Mwanaume wewe, kila siku wewe una tatizo tu, tatizo langu mimi hutaki”.

“Ukiweza kunisaidia tatizo hili tatizo lako nitalimaliza mara moja”.

“Haya sema tatizo lako, mimi niko tayari masaa ishirini na nne kukusaidia, shauri yako wewe unayeniponda!” Ntumba alijibu.

“Jana ulikwenda wapi toka ulipotoka kazini?” Willy aliuliza.

“Kwanini unauliza? Mimi nilikuwa nyumbani na sikutoka kabisa jana”, alijibu Ntumba.

“Sasa sikiliza kwa makini. Mimi nina tatizo kidogo na polisi, mimi nimewaambia kuwa tulikuwa wote toka jana kiasi cha saa kumi na moja mpaka leo asubuhi. Nimewaambia kuwa tulikuwa nyumbani kwako na kwamba hatukutoka mpaka asubuhi. Naomba wakikuuliza useme hivyo hivyo, tafadhali sana,” Willy aliomba.

“Umefanya nini, mwanaume wewe?” Aliuliza Ntumba.

“Usitake kujua tafadhali. Je utafanya hivyo?” Willy alitaka kuhakikisha.

“Siwezi kukuangusha nitafanya hivyo. Je jioni nitakuona?” Ntumba alisema.

“Asante sana”, alijibu Willy akikata simu. Alipomaliza kuzungumza kwenye simu, aliagana na wenzake na kuelekea mjini.

Katika ofisi za Pierre huko gereji Du Peuple, viongozi wa 'WP' walikuwa wamekusanyika tena saa nne hii kuelezana nini wafanye baada ya tukio la jana usiku. “Mmemaliza kuandika maelezo yenu polisi?” Pierre aliwauliza wenzake.

“Ndiyo tumemaliza, wote tumeandika maelezo mafupi tu kama tulivyozungumza. Tumeeleza tu kuwa sisi tunafikiria ni washindani wetu ambao wanaweza kuwa wamefanya maafa haya. Polisi hawakuonekana kuridhika lakini walichukua tu hivyo hivyo sababu Max alikuja akiwa ametumwa na Mkurugenzi, wewe mwenyewe unawajua polisi wanavyomuogopa Mkurugenzi,” alijibu Jean kwa niaba ya wenzake.

“Vizuri. Habari tulizozipata kutoka Boss kuhusu huyu Willy Chitalu ni kwamba mtu huyu ni Willy Gamba ambaye ni mpelelezi nambari moja Afrika. Mimi niliwahi kumsikia na kuna jarada lake katika makao makuu ya BOSS. Niliwahi kusoma jarada hili wakati wakiwa Johannesburg. Mtu huyu ni hatari sana. Ni mpelelezi mjanja sana na jasiri sana. Kwa hivi mambo yalivyofanyika jana usiku

yanadhihirisha kabisa ni yeye. Kwa hivi jamani tujue tuko katika upinzani wa hali ya juu”, Pierre aliwajulisha wenzake.

“Kijana huyo hata mimi nimekwisha wahi kumsikia. Jamaa mmoja wa CIA aliwahi kunieleza juu ya kijana huyu na kunieleza kuwa aliwahi kupambana huko Uganda na akanihakikishia kuwa hajawahi kuonana na mpelelezi kama huyu. Aliniambia kuwa kijana huyo angelimuua lakini alimuonea huruma na kumpeleka mikononi mwa serikali ya Uganda ambao walimfukuza nchini na kurudi Maerekani”, Papa alieleza.

Jean naye alieleza kuwa alikuwa amewahi kumsikia na kwamba hata yeye alisikia kwamba huyu mtu ni hatari sana.

“Lo, mimi tu ndiye sijawahi kumsikia. Itakuwa vizuri kupambana naye, maana na mimi siku moja nitakuwa na kitu cha kusimulia juu yake,” Muteba alisema.

“Si mtu wa kuomba kuonana naye”, alimjibu Papa.

“Kwa hiyo jamani nyinyi wenyewe mnajua ni upinzani gani tulionao kwa sasa hivi; Hawa watu watatu wakiwa sasa pamoja ni hatari kabisa. Mpaka sasa hivi agizo kutoka BOSS ni kwamba tuwakabili watu hawa mpaka hapo watakapoamua vinginevyo,” Pierre aliwajulisha.

“Lakini watu hawa wamejificha wapi? Maana hotelini kwao hawalali, na jana tulipowafuata walihakikisha kuwa wanatupoteza huenda tukipata wanakojificha mchana kutwa tunaweza kuwashambulia kwa urahisi”, Muteba alishauri.

“Kwa sasa hivi itakuwa vigumu maana watu wengi wameuawa. Kitu ambacho mimi nakifikiria ni kwamba leo lazima watashambulia gereji hii. Kama wameweza kuyajua magereji mengine yote lazima na hili wanalijua. Kwa hiyo sisi itatubidi tujitayarishe kuwakabiri; naamini watu hawa hawawezi kutushinda hata kama wana ujuzi wa namna gani. Nimezungumza na Mkurugenzi amesema atatuongezea ulinzi kwa kutupa watu na silaha za kutosha. Sisi wenyewe tukiwa tunaongoza kikosi hiki naamini wakithubutu kushambulia leo ndiyo mwisho wao...” Simu ililia ikamkata Pierre kauli, “Samahani,” aliwaeleza akaiendela simu. Alizungumza mara moja akakata simu akasema. “Jamani naitwa wakala haraka sana, kwa hiyo inatubidi tuvunja mkutano huu ili tuonane hapa kiasi cha saa tisa mchana wakati tutakapopanga mambo ya jioni. Kwa sasa hivi kajitayarisheni tayari kwa pambano la jioni maana leo ndiyo leo”. Walikubaliana kuwa wataonana saa tisa za mchana halafu wakatawanyika.

Willy alisimamisha gari lake kwenye maegesho ya Memling Hoteli. Alitoa kadi aliyokuwa amepewa na Ntumba akasoma anwani ya nyumbani kwake Ntumba na kujitayarisha kwa maswali. Aliingia pale hotelini kama kwamba hana habari yoyote. Alipotaka kupanda ngazi za kwenda juu akasimamishwa na meneja wa hoteli.

“Wewe unaitwa Willy Chitalu?”

“Ndiyo”, Willy alijibu.

“Samahani kidogo, ninakuhitaji ofisini”, Meneja alimwambia Willy. Willy bila kubisha alimfuata meneja huyo. Alipoingia ofisini mwa meneja huyo alikuta mna watu wawili. “Karibu Bwana Chitalu. Samahani sikukujulisha hapo nje, mimi ndiye meneja wa hoteli hii na hawa mabwana wawili wanatoka kwenye idara ya polisi”, Meneja alieleza. Willy alisalimiana na watu hawa kisha akavuta kitu akakaa. Wale jamaa wa polisi walitoa vitambulisho vyao kumhakikishia Willy kuwa kweli wao walikuwa polisi kutoka idara ya upelelezi ya makosa ya jinai.

“Bwana Chitalu, sijui kama una habari kuwa mfanyakazi wetu mmoja aliyekuwa anafanyakazi hapo mapokezi aitwaye Mwadi ameuawa?” Meneja aliuliza.

Willy alionyesha sura ya kushtuka sana na kushangaa kiasi kwamba hata polisi walidanganyika.

“Sina habari”, alijibu taratibu kabisa.

“Basi hawa mabwana wana maswali machache ya kukuuliza. Usiwe na wasiwasi kwani wapangaji wetu wote inabidi waulizwe. Wewe mwenyewe unajua wakati kitendo kama hiki kikitokea lazima mambo kama haya yatokee”. Meneja alijaribu kumtuliza.

“Hamna taabu”, alijibu Willy kwa unyonge.

Polisi mmoja alitoa daftari tayari kwa kuandika malezo na mwingine akajitayarisha kwa kuuliza.

“Bwana Chitalu kama alivyokueleza Meneja, maswali yetu ni jambo la kawaida tatizo kama hili linapotokea, hivi unaombwa kueleza ukweli mtupu”, yule polisi alimweleza.

““Hamna wasiwasi”, Willy alijibu.

“Bwana Chitalu umefika hapa mjini lini?” Polisi aliuliza.

“Jumatatu”, alijibu Willy.

“Ni mara yako ya ngapi kufika mjini Kinshasa?”

“Mara ya tatu”, alijibu Willy.

“Huyu msichana Mwadi ulikuwa unamfahamu?”

“Ndiyo”, alijibu Willy.

“Kwa muda gani umemfahamu?”

“Toka Jumatatu”, alijibu.

“Je mmewahi kuwa na uhusiano wowote toka siku hiyo?”

“Ndiyo”, alijibu Willy.

“Uhusiano wa namna gani?”

“Uhusiano wa kawaida tu wa mwanamke na mwanaume”, alijibu Willy.

“Je, umewahi kufika kwake ama kwenda naye mahali popote?”

“Ndiyo”, alijibu Willy.

“Lini na wapi mlitembelea?”

“Juzi usiku na tulitembelea Parafifi baa”, Willy alijibu.

“Je jana jioni mlionana?”

“Hapana”, Willy alijibu.

“Unaweza kutueleza jana kiasi cha saa kumi na moja jioni mpaka leo asubuhi ulikuwa wapi?”

“Nilikuwa nimekaribishwa mahali”, alijibu.

“Mahali gani?”

“Kwa msichana mmoja,” alijibu.

“Unaweza kututajia jina la huyo msichana?” Willy alisita kidogo kisha akasema, “Anaitwa Ntumba Akanda”.

“Anakaa wapi?”

“Anakaa huko Matonge barabara ya Inzia nyumba nambari 26B “, Willy alijibu.

“Anafanya kazi?”

“Ndiyo.”

“Wapi?”

“STK uwanja wa ndege”, alijibu Willy.

“Una maana jioni yote ulikuwa huko na hukuondoka hata mara moja mpaka asubuhi?”

“Ndiyo”, alijibu Willy.

“Una lolote unaloweza kutueleza juu ya mauaji ya Mwadi?”

“Nimesikitika sana”, alijibu Willy.

Yule polisi aliyekuwa anauliza maswali alimwangalia mwenzake na mwenzake naye akaonekana kuwa hakuwa na swali zaidi.

“Asante sana bwana Chitalu. Tunalokuomba ni kwamba usiondoke hapa mjini bila kupasha habari kituo cha polisi cha 'Brigede Mobile'. Vile vile tunakuomba usihame kutoka hoteli hapa mpaka sisi tuwe tumepata habari”, yule polisi alimweleza.

“Hamna wasiwasi”, Willy alijibu.

“Unaweza kwenda”.

“Asanteni sana,” aliaga Willy na kutoka nje.

Wale polisi walichukua simu na kupiga moja kwa moja STK uwanja wa ndege. Walimuulizia Ntumba na walipompata walimuuliza kama alikuwa anamfahamu Willy Chitalu. Baada ya mazungumzo marefu aliwathibitishia kuwa alikuwa na Willy tokea saa kumi na moja jioni mpaka asubuhi. Waliridhika wakaondoka.

Willy alipoondoka ndani ya ofisi ya meneja aliitwa na kijana aliyekuwa mapokezi.

“Kuna msichana mmoja anaitwa Tete amekupigia simu zaidi ya mara nne, anasema umpigie,” yule kijana alimweleza. Willy alimpa simu ya Tete na kumwambia. “Ukimpata niletee simu chumbani kwangu”, Willy alipoingia chumbani kwake alikuta chumba chake kimepekuliwa kwa ustadi sana kiasi cha kwamba mtu wa kawaida asingeweza kujua. Aliangalia vitu vyake akakuta vyote salama. Yeye naye akakipekua kile chumba kuona kama wangeweza kuwa

wameacha chombo chochote cha kunasa sauti hakukuta kitu. Mara kengere ya simu iliita.

“Halo”, Willy aliita.

“Zungumza na Tete”, yule kijana wa mapokezi alimwambia.

“Halo, Willy hapa”.

“Tete, habari yako?” Tete alijibu kwa sauti ya chini sana.

“Nzuri, je wewe?” Willy aliuliza.

“Bado moyo wangu mzito sana kwa ajili ya kifo cha Mwadi,” Willy alijibu.

“Tafadhali sana tuonane saa sita. Sasa hivi ni saa sita kasoro dakika ishirini, tafadhali fanya kila njia tuonane nina jambo la lazima,” Tete alisema kwa sauti ya wasiwasi.

“Wapi?” Willy aliuliza.

“Mahali popote utakapooni pana usalama hata kama ni hapo hotelini kwako”, Tete alijibu.

Willy alifikiria nini msichana huyu alikuwa anamtakia lakini, hakupata jibu. Alifikiria huenda akina Muteba walikuwa wamemuwekea mtego lakini akaamua ajaribu bahati yake. Hata yeye alikuwa na haja ya kuzungumza na msichana huyu lakini si kwa namna hii.

“Fanya hivi, ukitoka njoo na gari lako moja kwa moja na barabara ya 30 Juin halafu ingia kwenye maegesho ya Banque Commerciale Zairoise, mimi nitakukuta hapo, sawa?” Willy alieleza.

“Sawa, saa sita”, alijibu Tete.

“Saa sita”, alijibu Willy huku Tete akiwa tayari ameisha kata simu. Baada ya kuweka simu chini, Willy alibadilisha nguo zake haraka haraka, halafu akateremka chini mbio mbio. Aliingia ndani ya gari lake, akaondoka kuelekea kwenye ofisi za Agence Sozidime. Willy aliposimamisha gari lake katikati ya magari yaliyokuwa kwenye maegesho ya Cine Rac ilikuwa saa sita kasoro dakika tano.

Alitoka ndani ya gari na kuelekea upande mwingine wa barabara ambapo alibana kwenye sehemu ambapo alikuwa anaona moja kwa moja ndani ya lango la ofisi za Sozidime. Hakuwa hata hajajibanza vizuri alipomuona Tete akiwa anatoka ndani,

akaingia ndani ya gari lake, akawasha moto na kuondoka. Mlinzi wa pale alimfungulia lango na gari la Tete likapita.

SURA YA KUMI NA SABA

WILLY alisubiri kuona kama kulikuwa na gari lolote linamfuata Tete. Lakini hakuona dalili. Alikimbia mpaka kwenye gari lake na kuondoka kwa mwendo mkali alimfuata Tete. Ni kwenye barabara ya 30 Juin alipomuona, alimfuata pole pole mpaka walipofika B.C.Z. Tete akaingia kwenye maegesho ya pale kama Willy alivyokuwa ameagiza. Willy huku akiwa amehakikisha kuwa hakukuwa na mtu aliyekuwa anawafuata naye aliingia kwenye maegesho ya B.C.Z. akafunga gari lake akafuata pale Tete alipokuwa ameegesha. Alipofika kwenye gari la Tete alimwambia.

“Sogea huko, mimi nitaendesha,” Tete alisogea kwenye kiti cha abiria, Willy aliingia kwenye kiti cha dereva akawasha gari moto, wakaondoka.

“Mbona umeacha gari lako?” Tete alimuuliza.

“Napenda sana kuendesha gari aina ya sports”, alitania Willy.

“Tunakwenda wapi sasa?” Tete aliuliza.

“Mahali penye usalama kama ulivyokuwa umesema”, Willy alijibu. Willy alikuwa amekata shauri kuwa, mahali penye usalama pa kuweza kuzungumza na Tete palikuwa nyumbani kwa Robert tu, potelea mbali kama angegundua maficho yao, lakini alitumaini ya kwamba lilikuwa ni jambo la busara.

Walifika nyumbani kwa Robert na kukuta hakuna mtu. Willy alifungua gereji na kulificha gari la Tete ndani kwani alitegemea gari la msichana kama Tete lazima lingekuwa linafahamika mjini. Alimkaribisha ndani, akatayarisha kinywaji kwa ajili yao wote.

“Hapa ni nyumbani kwa nani?” Tete aliuliza.

“Kwa rafiki yangu” Willy alijibu.

“Mbona jana hukurudi nyumbani kwangu kama ulivyoahidi?” Tete aliuliza.

“Shughuli zilizidi”, Willy alijibu.

“Kwanza nataka kutoa shukrani zangu kwa kumlipizia rafiki yangu Mwadi kisasi”, alisema Tete.

“Umejuaje kama nililipiza?” Willy aliuliza.

“Si uliniambia kuwa ungelipiza, na nikapata habari toka kwa Muteba kuwa Kabeya ameuawa hivi nikajua umelipiza,” Tete alijibu.

“Muteba alikueleza saa ngapi?” Willy aliuliza.

“Alikuwa nyumbani kwangu kiasi cha saa kumi za asubuhi. Kwanza tuache hayo tafadhali Willy nataka unieleze bila kunificha chochote wewe ni nani na uko hapa Kinshasa kwa ajili gani, halafu na mimi nitakueleza mambo ambayo ninaamini yatakuwa na manufaa kwako. Mpaka sasa hivi ninauza maisha yangu kwa ajili yako, tafadhali usinifiche”, Tete alisema.

“Kwanini ujitolee kuuza maisha yako kwa ajili yangu?” Willy alimuuliza.

“Kwa sababu ile ile ambayo ilimfanya Mwadi auze maisha yake kwa ajili yako. Mwadi alikuwa rafiki yangu mpenzi sana, hivi niko tayari kuendeleza chochote alichocha bila kumaliza,” Tete alieleza.

“Mimi nitakuamini namna gani kukueleza mambo hayo unayotaka kuyajua?” Aliuliza Willy.

“Nafikiri itabidi uniamini au kama huniamini ubahatishe kuniamini, maana nadhani kama nilivyokueleza kuwa nina habari zinazoweza kuwa na manufaa,” Tete alijibu.

“Wewe unaaminije kuwa niliyokueleza ni ya kweli?” Willy aliuliza.

“Mimi ninaamini lazima mtu kama wewe si wa kusema uongo,” alijibu Tete.

Willy aliamua kujitosa na kumweleza msichana huyu kila kitu na ikiwa kama alikuwa ametumiwa kuja kumdadisi, hayo yalikuwa mambo ya kawaida katika kazi hivi angeweza kuyakabiri bila taabu.

“Nimeridhika Tete, hivi nitakueleza kwa kirefu. Mimi jina langu hasa ninaitwa Willy Gamba na kazi yangu mimi ni mpelelezi.” Willy alimweleza. Tete alimwangalia kwa macho makavu bila kuonyesha mshangao wowote. Akiwa anavutwa na uzuri na ukali wa macho ya msichana huyu. Willy alimweleza kwa ufasaha kabisa mambo yaliyokuwa yamemleta hapa pamoja na wenzake na mambo yote waliyokuwa wameyafanya mpaka wakati huo. “Ulitaka kujua sasa umeshajua, nimekueleza kila kitu sikuacha kitu,” Willy alimalizia.

“Sasa nimeelewa, nimeelewa kabisa kwanini mambo yako namna ile ofisini kwetu. Nilikuwa naona mambo mengi ya ajabu ajabu lakini sikuwa ninajua yana maana gani. Umenifumbua macho, nimekuwa kama kipofu ambaye amefumbuliwa

macho. Wamekuwa wananitumia kwa mambo mengi bila mimi kujua,” alieleza Tete akiwa kama anazungumza ndotoni.

“Uliniambia kuwa ungenieleza mambo ambayo yangukuwa na manufaa kwangu, nieleze”.

“Mambo mengi umeshayaelewa kutokana na ulivyonieleza. Ni kweli kabisa kuwa Kampuni yetu inashughulika na mambo ya kijasusi sasa nimeona kwanini mambo yako hivyo. Mkurugenzi wetu anaitwa Fernand Barbier anajiita kuwa ni Mbelgiji lakini ni kaburu. Huyu Mkurugenzi wa 'Gereji Du Peuple', Pierre Simonard naye si Mbelgiji ni kaburu hata Jean Vergeance. Mambo haya niliwahi kueleza na Muteba siku moja wakati mapenzi yetu yalipokuwa moto sana. Nilimuuliza hawa wazungu alifahamiana fahamiana nao namna gani akanieleza kuwa alikuwa ameonana nao huku Afrika Kusini alipokwenda huko na askari wa kukodiwa baada ya kupigana na askari hao upande wa majeshi ya Tshombe huko jimbo la Shaba”, Tete alinyamaza kidogo kuvuta pumzi kisha akaendelea.

“Nilipomuuliza kwa nini wanajiita kuwa ni Wabelgiji, alisema kuwa ingekuwa vigumu kwa makaburu kufanya biashara katika nchi huru ya Kiafrika kufuatana na siasa ya nchi za Kiafrika. Hii ndiyo alitoa kama sababu kwa nini watu hawa walikuwa wanatumia uraia wa bandia. Yule Maximilian leo uliyekuja kumuona, naye si Mbelgiji bali ni Mfaransa. Mpaka sasa nashindwa kujua kwa nini anatumia uraia bandia, Kwani Wafaransa hawakataliwi katika Afrika na wako chungu nzima hapa Zaire kwa shughuli mbali mbali”, Tete alitua tena kuvuta pumzi kisha akaendelea.

“Huyu Max kama tunavyomuita aliwahi kunieleza mwenyewe akijitapa mbele yangu kuwa si Mbelgiji bali ni Mfaransa kamili.” Tete alimwangalia machoni Willy, akasita kidogo kama kama kwamba anaona haya kueleza alichotaka kueleza, kisha akaangalia sehemu nyingine akaendelea. “Max ananipenda sana mimi, amekuwa ananitongoza kwa muda mrefu sana. Anamchukia sana Muteba kwa ajili yangu mimi. Katika kutaka kujionyesha alivyo na thamani kuliko Muteba na hawa watu wengine, amekuwa ananieleza mambo mengi sana. Anasema amewahi kuwa Meneja katika jeshi la Ufaransa kabla hajaweza kupewa kazi mbali mbali katika nchi mbali mbali zenye uhusiano na Ufaransa. Wakati fulani Fernand alikwenda Ulaya kwa likizo yeye akabaki ndiye Mkuu wa ofisi yetu. Siku moja Lucie alikuwa anaumwa mimi nikawa nafanya kazi ofisini kwake ilipofika saa za kufunga ofisi aliniambia nisiondoke kuna kazi. Wafanyakazi wengine wote

waliondoka tukabaki mimi na yeye tu. Kisha akafunga milango ya kutokea nje ya ofisi akanijia nimfuate.” Tete alitabasamu kidogo kisha akaendelea.

“Nilimfuata ingawaje kwa woga sana lakini nilitaka nijue nini nia yake. Tulienda mpaka kwenye ofisi ya Fernand akafungua tukaingia ndani akafunga. Akiwa sasa amenishika mkono tulienda mpaka kwenye ukuta ambao ulikuwa nyuma ya meza ya Fernand. Alinieleza kuwa nisiogope kwani alitaka kunionyesha milango inayoenda kwenye chumba cha siri ambako ndiko tungeweza kufanya mazungumzo yetu. Alienda kwenye pembe ya ukuta wa nyuma kulikuwa na kidude akakibonyeza mara ukuta ukaachana na kuwepo na mlango. Kumbe ukuta huo ulikuwa wa bandia ulikuwa wa mbao.

Chini ya mlango kulikuwa na ngazi zinateremka chini, aliwasha taa za kwenye ndazi hizi, na tulipokuwa kwenye uchochoro wa ngazi hizi za kuteremka chini alibonyeza kidude kingine, ukuta ule ukarudi sawa sawa. Tuliteremka chini tukakuta mlango akaufungua tukaingia ndani ya chumba kimoja kizuri ajabu, kilikuwa na kila kitu. Kitanda kikubwa, makochi mazuri, barafu, jiko la umeme, kusema kweli chumba hiki kilikuwa na kila kitu mtu anaweza kuhitaji. Vile vile mlikuwa na makabati mawili makubwa ya chuma. Max alinionya kabisa kuwa nisimweleze mtu yeyote juu ya chumba hiki na akasema ni yeye na Fernand tuu waliokuwa wanajua juu ya chumba hiki na kwamba mimi ndiye nilikuwa mtu wa tatu,” Tete alimwangalia Willy, kisha akaendelea. “Kusema kweli Willy sijawahi kumwambia mtu ila ni wewe leo. Nilipomuuliza kwa nini iliwabidi wawe na nyumba ya namna hii, alijibu kuwa kwa ajili ya usala wao yakitokea machafuko, kwani Zaire ni nchi yenye machafuko mara kwa mara.

Nilimuuliza chumba kama hiki kilikuwa na usalama gani. Akaniambia kuwa nyumba hii ilikuwa ya Jenerali mmoja wa jeshi la Kibelgiji ambaye alijijengea kwa usalama wake wakati wa msukosuko. Alisema Jenereli huyo alikuwa amekitengenezea chumba hiki mlango ambao ulikuwa unatokea sehemu nyingine kabisa. Alienda kwenye sehemu nyingine ya ukuta akabonyeza kidude kama kile alichokuwa amebonyeza ofisini kwa Fernand mara ukuta ukaachana na nikajikuta naangalia ndani ya uchochoro wenye giza kubwa.

Akaniambia kuwa uchochoro huu ulikuwa unatokea nyuma ya lile jumba refu liitwalo' Galleries Presidentielles', na kulikuwa na taa ndani ya uchochoro huu. Max alinieleza yote haya ili niweze kumtia maana kusudi niweze kumtimizia haja zake. Wanaume wana matatizo sana,” Tete alinyamaza na kumwangalia Willy, lakini Willy aliendelea kumwangalia katika hali ile ile;

“Sasa leo ndiyo nimejua kwa nini Sozidime ina ofisi za namna ile. Nimekubaliana kabisa Willy, ile ni ofisi ya majasusi ndiyo sababu iko vile”, Tete aliendelea.

Maelezo yote haya yalimwingia Willy kama nyali za moto. Alijiona mtu mwenye bahati sana katika safari hii kwani alikuwa ameweza kupata habari za muhimu sana bila matatizo makubwa. “Je umewahi kwenda kuona pale kwenye uchochoro huo unapotokea?” Willy aliuliza.

“Kwa bahati nimewahi. Nilitaka kuhakikisha kama maneno ya Max ni kweli kwani mimi sikuamini kama kungeweza kujengwa njia ya chini kwa chini mpaka mahali pale aliposema. Hivyo siku moja nilimtania na kumwambia kuwa alikuwa ni mwongo, ilikuwa haiwezekani kuwa na njia ya namna hiyo. Kwa vile alikuwa hataki kuniacha hata mara moja alinipeleka pale mahali na kunithibitishia kwa hivi ninapafahamu. Pamefunikwa na mfuniko kama ule unaofunika mashimo ya vyoo, lakini unaingia sawa sawa pale kwenye shimo la mlango na kufungwa kwa funguo,” Tete alijibu.

“Kwa hiyo na mimi utanionyesha hapo mahali?” Willy aliuliza.

“Bila wasiwasi”, Tete alijibu.

“Endelea na maelezo yako”, Willy alimwambia.

“Sasa tukiacha hayo mambo ya zamani, nataka kukueleza kuwa wao wameishagundua kuwa wewe si Willy Chitalu bali Willy Gamba mpelelezi hatari sana,” Tete alieleza.

“Wamejuaje?” Willy aliuliza.

“Zilikuja habari kwa telex, kutoka kwa hao wateja wao leo asubuhi zilizokuwa zinakuelezea wewe. Nilizipokea mimi lakini kama kawaida huwa zinafumbwa fumbwa zikiwa zinazungumzia mambo ya spea. lakini nilieleza kwa sababu niliona majina yako yote kwenye hiyo Telex. Nilipompelekea karatasi hiyo Max, alinieleza ya kwamba wewe ulikuwa mtu hatari sana katika mambo ya biashara na akanishukuru sana kwa kuweza kukufahamisha kwake”, Tete alijibu.

“Ahaa,” aliitikia Willy.

“Kisa hasa kilichonifanya nikate shauri kukuona na kuzungumza na wewe kinatokana na maneno aliyonieleza alipokuja leo asubuhi nyumbani kwangu. Muteba huwa haji kwangu wakati wa saa kama zile ila anapokuwa anakerwa na kitu.

Alikuja akionekana amechoka kabisa na akiwa amepoteza hata rangi ya sura yake. Aliniambia kuwa umemuua Kabeya na Charles na kwamba ulikuwa umelipua magereji yao yote isipokuwa gereji la Pierre. Alikulaani vikali sana na akaniapia kwamba lazima atakuua. Alinieleza pia kuwa Mwadi aliuawa na Kabeya sababu za kuficha siri zako na akanionya kuwa kama mimi ninajua kitu chochote juu yako ni afadhali niseme, maana kweli toka tufahamiane na Muteba sijamwona katika hali ile, na niliogopa hata kumuuliza swali lolote. Alilala kwa muda wa saa moja tu akaamka na kuondoka na kuaniambia tuonane naye mchana.

Maelezo haya yalinifanya nifikiri vitu viwili, cha kwanza wewe si mfanyabiashara kama ulivyosema, na pili kuwa Muteba naye alikuwa si mfanyabiashara tu kama alivyokuwa anafahamika ila alikuwa amejiingiza katika jambo fulani la kijambazi na wale wazungu na ndiyo sababu alikuwa katika hali aliyokuwamo. Tokea asubuhi nilikuwa nafikiria niwe upande upi, na baada ya kufikiria sana nikaona ikiwa Mwadi alikuwa anakufichia siri yako na kujitolea kufa basi wewe hukuwa mtu mbaya, Maana Mwadi ninamfahamu sana alikuwa msichana aliyejisitahi sana na hakuwa na uhusiano na watu hovy hovy. Hata mimi aliwahi kunionya juu ya urafiki wangu na Muteba, kwani alisema Muteba hakuwa anatembea na kundi zuri. Hivyo nikaona nikuone ili niweze kuwa na msimamo,” Tete alimalizia na kuvuta pumzi ndefu.

“Sasa umepata msimamo?” Willy alimuuliza.

“Ndiyo, nina msimamo kamili tokea sasa mimi niko upande wako. Nitaanzia pale marehemu rafiki yangu alipoachia”, alijibu Tete huku machozi yanamtoka.

Willy aliyekuwa amekaa karibu naye alimsogelea akatoa kitambaa akaanza kumfuta machozi. Tete alipitisha mikono yake mabegani kwa Willy na wakaanza kupeana busu moto moto, “Kazi na dawa”, Willy alibwabwata.

Ilikuwa saa nne unusu juu ya alama Willy aliposimamisha gari lake mbele ya ofisi za O.A.U. Robert naye alikuwa tayari ameishateremka pale chini, alipomuona Willy anaegisha gari alimfuata.

“Ingia twende”, Willy alimwambia.

“Gari langu niliache?” Robert aliuliza.

“Liache”, Willy alimjibu. Robert aliingia ndani ya gari wakaondoka.

“Vipi umeweza kufaulu kumuona Kadima?” Willy aliuliza.

“Ndiyo nimefanikiwa”, Robert alijibu.

“Sasa twende tubane mahali pale Wizarani kwao tumsabiri, akiteremka tu, tumteke nyara, ili tukamuulize vizuri,” Willy alishauri.

“Lakini pale Wizarani pana watu wengi, kumteka nyara patakuwa na kazi,” Robert alieleza.

“Si kitu tutafanya kila mbinu hata ikibidi tufanye ghasia ili tumchukue tutafanya,” Willy alijibu.

“Vipi mambo yako, yameenda namna gani?” Robert alimuuliza.

Willy alimweleza mambo yote yaliyotokea tangu alipofika Hoteli Memling na vile vile akamweleza juu ya mazungumzo yake na Tete. Alieleza yote haya wakiwa wameegisha gari lao kwenye nafasi ambayo walikuwa wanauona mlango wa mbele wa Wizarani ya mambo ya nchi za nje, na kuhakikisha kuwa kila mtu aliyetoka ndani wanamuona.

“Msichana huyu ameenda ofisini kwake lakini atakuja huko nyumbani kwako baada tu ya kutoka kazini,” Willy alimalizia kueleza.

“Hii sasa imeleta picha yote ya mambo ilivyo. Ninaweza kusema bila kusita kuwa huyu Maximillian ni jasusi wa Shirika la Ujasusi la Ufaransa 'SCEPE' maana SCEPE, BOSS na CIA zinafanya kazi zao kwa pamoja katika Afrika. Mimi kila siku nasema ningekuwa rais wa nchi yoyote huru ya Afrika lazima ningepiga kelele nchi za Afrika zisiwe na uhusiano wowote na Ufaransa.” Alisisitiza Robert.

“Siasa ni kitu kingine, utakuta Mkuu wa nchi hii ana sababu zake za kuhusiana na nchi fulani na Mkuu wa nchi nyingine ana sababu zake za kuhusiana na nchi nyingine ili mradi kila mtu apate maslahi yake. Umasikini wa nchi za kifaraka ndio tatizo kubwa linalozifanya zisiwe na msimamo thabiti wa kisiasa.” Willy alieleza. Ilikuwa imeishatimia saa tisa na nusu lakini Kadima alikuwa bado hajatokea. Watu walikuwa wanatoka lakini Kadima alikuwa hajatokea.

“Vipi huyu mtu hakuja nini?” Willy aliuliza.

“Habari nilizopata na ni za uhakika ni kwamba yupo ndani ya mkutano. Huenda mkutano haujaisha”, Robert alijibu.

Mara watu wawili walitokea wakiwa wamebeba mikoba yao. “Huyo wa upande wa kushoto ndiye Kadima,” Robert alimweleza Willy.

“Twende,” Willy alimweleza Robert. Waliteremka kama watu wa kawaida tu, wakaelekea kwenye maegesho ya magari hapo Wizarani huku wanajifanya kama kwamba wana mazungumzo kati yao. Kadima alisimama akizungumza na yule mwenzie. Willy na Robert nao walisimama.

“Nenda ukalete gari sehemu hii. Atakapomaliza mazungumzo yake mimi nitamfuata.” Willy alimweleza Robert.

Kadima aliagana na yule mwenzake na kila mtu akaelekea kwenye gari lake. Willy alimkatisha na kuonana naye kabla hajafika kwenye gari lake.

“Bwana Kadima nafikiri,” Willy alimsemesha.

“Ndiyo kijana nikusaidie nini?” Kadima alijibu baada ya kumwangukia Willy na kumuona kijana muungawana kabisa.

“Ningependa kuzungumza nawe kidogo”, alisema Willy na wakati ule ule Robert akasimamisha gari pembeni mwao. Willy alitoa bastola yake alikokuwa ameificha na akamwamrisha Kadima. “Ingia ndani ya gari na usipige kelele kwa usalama wako.”

Kadima ambaye tokea azaliwe alikuwa hajawahi kuonyeshwa bastola au silaha ya aina yoyote alikuwa karibia azimie. Bila kusema neno aliingia ndani ya gari na Willy akaingia pembeni mwake Robert akaondoa gari. Waliondoka naye moja kwa moja mpaka nyumbani kwa Robert. Njiani kila mtu alikuwa kimya. Kadima ambaye mawazo yake yalikuwa yakizunguka huku na kule ili kujua kwa nini ametekwa alikaa amezubaa kabisa. Walipofika nyumbani kwa Robert walimteremsha na kumuingiza ndani ambako walimkaribisha kitini. Robert alienda akachukua glasi tatu akaweka barafu halafu akaweka kinywaji na kuwakaribisha. Kadima alishangaa sana kujikuta ameletwa ndani ya nyumba nzuri na vile vile alijua nyumba za mtaa huu zilikuwa zimetengwa kwa ajili ya maafisa wa vyeo vya juu nchini na mabalozi. Alizidi pia kushangazwa na vijana hawa walioonekana waungwana sana. Woga wake kwa ujumla ulipungua.

“Bwana Kadima samahani sana kwa jinsi tulivyokuchukua kwa sababu hakukuwa na njia nyingine. Mimi naitwa Willy na mwenzangu anaitwa Robert. Ndugu Robert ni Katibu Mwenezi katika ofisi ya OAU iliyoko mjini hapa huenda utakuwa umewahi kumsikia kwani kazi zako na zake zinakaribiana”, Willy alimfahamisha.

“Sijawahi kumwona”, Kadima alijibu kwa mkato.

“Tuna maswali machache ambayo tungependa kukuuliza na tungeomba usitudanganye maana sisi tayari tunaielewa mambo mengi. Usishangae ukikuta tunabadilika na kuwa watu wabaya”, Willy alimwekea mikwala.

“Wewe ni nani? Maana umesema jina lako tu hukujieleza wewe ni nani?” Kadima aliuliza.

“Mimi utanijua muda si mrefu”, Willy alijibu.

“Haya kama ni maswali ninayoyajua nitayajibu kama siyajui sitaweza.” Kadima alieleza.

“Vizuri. Wewe ndiye unashughulika na mambo ya Ukombozi wa Kusini mwa Afrika Wizarani kwenu”, Willy aliuliza.

“Ndiyo”, alijibu Kadima.

“Siku chache zilizopita Mkuu mmoja wa vyama vya wapigania Uhuru Kusini mwa Afrika aliuawa mjini hapa sijui kama una habari hizi?” Willy aliuliza.

Jasho jembamba na baridi lilimtoka Kadima. Sasa ndipo alikuwa amegundua kwa nini amekamatwa na kuletwa hapa kwani asubuhi ile alikuwa amepata habari kutoka kwa Fernand wa Agence Sozidime kuwa kulikuwa na wasiwasi wa mambo, lakini alikuwa amemweleza ya kuwa wangezungumza baadaye.

“Siku za mwizi ni thelathini na tisa ya arobaini unakamatwa”, Kadima alifikiria.

Willy alihisi kuwa Kadima alikuwa amegutuka kutokana na swali hili kwa vile aliliona jasho lililomtoka na jnisi mikono yake ilivyotetemeka kiasi cha kutoweza kushika glasi.

“Habari hizo ninazo, na hivi leo nimetoka mjini Lusaka kupeleka mizigo ya marehemu.” Kadima alijibu taratibu.

“Kifo cha marehemu ni miongoni kati ya vifo vingi ambavyo vimetokea kwa wapigania uhuru katika nchi kadhaa za Afrika. Na kifo hiki ni cha pili katika Kinshasa kwa muda huu wewe ukishughulikia idara hiyo katika Wizarata ya mambo ya nchi za nje. Sijui unaweza kutueleza ni nini chanzo cha mauaji haya?” Willy alimuuliza huku amemkazia macho.

“Siwezi kujua, polisi na idara ya upelelezi ndio wanajua,” Kadima alijibu.

“Bwana Kadima sina haja ya kupoteza muda wako mwingi, hivi sina haja ya kuzunguka, au kusumbuana na huku mambo yanaeleweka waziwazi. Hivi nataka

utueleze uhusiano ulionao kati yako na Mkurugenzi wa Kampuni ya Sozidime Agence au wenye magereji ya G.A.D. Papadimitriou, Banninga na Du Peuple”, Willy alimuuliza.

Kadima alitetemeka kabisa, alitambua kuwa huu ndio ulikuwa mwisho wake na kwa sababu hakuwa mtu aliyezoea matatizo hivi hakuwa mtu mwenye moyo mgumu. Siku moja aliwahi kujifikiria kuwa kupenda pesa kulikuwa kunampeleka mbali. Alianza kukumbuka miaka mitatu iliyopita simu ya Pierre Simonard ambaye alikuwa ameunda urafiki kutokana na kupeleka gari lake kwenye gereji yake. Pierre alimuomba waonane Hoteli Intercintinental jioni hiyo kama yeye akikubali. Jioni ile walipoonana, Pierre alikuja na mtu mwingine aliyemjulisha kwake kuwa alikuwa Mkurugenzi wa Kampuni ya Agence Sozidime.

SURA YA KUMI NA NANE

NI JIONI hiyo ambapo uhusiano kati yake na Fernand ulipoanza. Na tokea hapo ndipo walipomshawishi na kumfanya kibaraka wao wa kuweza kuwapasha habari zote juu ya wapigania uhuru. Alikuwa amelipwa pesa nyingi sana na sasa hivi alikuwa kati ya maafisa tajiri sana katika Zaire. Alikuwa na pesa chungu nzima huko Geneva, na alikuwa na majumba na hoteli kubwa huko Paris. Sasa leo maji yalikuwa yamemfika shingoni, kwa sababu alikuwa hajui watu hawa wanajua kiasi gani, na kwa sababu alikuwa anaogopa kufa, na kwa vile alitambua vijana hawa lazima ni wapelelezi aliamua kuwaeleza ukweli. Lakini kabla ya hapo alitaka kujua ki ukweli huyu kijana ni nani.

“Kijana umeniuliza swali la maana kabisa. Lakini kabla sijakujibu naomba kitu kimoja unieleze wewe ni nani na unawakilisha nini. Halafu mimi nitakueleza kila kitu bila kuficha. Nimechoka kukaa na mzigo huu, moyoni mwangu, na kama wewe ndiye mtu mwenyewe unayefaa nikueleze nitakueleza. Lakini kwanza nieleze wewe ni nani?” Kadima alieleza. Willy alijua mtu huyu alikuwa anazungumza ukweli na alijua ataeleza ukweli akijibiwa swali lake. Maana Willy alikua ameishaona watu wengi wa namna hii kutambua kama mtu huyu atasema ukweli au vipi. Hivyo Willy aliamua kumweleza yeye ni nani, na alikuwa amekuja hapa kufanya nini. Vile vile alimweleza mambo juu juu ya kuonyesha kuwa tayari walikuwa wamepata habari za kutosha juu ya 'WP' kwa hivi Kadima kuficha kusema ukweli kusingemsaidia neno.

“Loh poleni sana, sasa nisikilizeni kwa makini, nikimaliza kueleza mnaweza kunifanya lolote”, Alianza Kadima. Kadima alieleza tokea siku ile Pierre alipomfahamisha kwa Fernand mpaka tukio hili la Mongo. “Mimi nimewasaliti ndugu zangu shauri ya pesa. Na katika nchi hii tuko wengi. Hiki kikundi cha 'WP' kimeotesha mizizi mirefu katika nchi hii na ina vibaraka wengi sana. Jambo hili limewezekana katika nchi kwa kufuatana na siasa ya nchi hii. Viongozi wote wa nchi hii wako tayari kufanya lolote ili kujaza tumbo lao. Mimi nimekuwa hivyo ingawaje jambo hili limekuwa linanikera moyoni. Sasa mnaweza kunifanya mnavyotaka mimi nimetubu yote niliyoyafanya nayajutia”, Kadima alimalizia machozi yanamtoka.

“Lo masikini Afrika”, Robert alilalamika.

“Tamaa ya viongozi ndiyo inaiangamiza Afrika. Mpaka hapo tutakapopata viongozi wenye kuipenda Afrika kwa dhati na siyo matumbo yao ndipo Afrika itakapoendelea”, Willy alisikitika.

“Ni viongozi wachache wanaoipenda Afrika kwa dhati” Kadima alithibitisha.

“Kwa sasa hivi bwana Kadima utakaa hapa mbapa hapo tutakapokuruhusu. Tutakupa mwanya upige simu nyumbani kwako uwaeleze umepata safari ya ghafla. Tutakata shauri juu yako baadaye”, Willy alimweleza Kadima.

Kadima ambaye roho yake ilikuwa imechoka kabisa alijibu, “Lolote mtakaloniambia, nitafanya ili mradi tu mtakapomaliza kazi zenu mnisikilize mambo yangu, Fernand na Pierre ni watu wabaya sana ndio wamenifanya mimi nikatumbukia katika maovu haya, mkiwakamata wapeni salamu zangu”, Willy alimuongoza katika chumba kimojawapo baada ya kupiga simu na kumfungia ndani. Chumba hiki kilikuwa kidogo na dirisha dogo ambalo Kadima asingeweza kupita.

Robert alimwita Willy akamweleza, “Unajua nilitaka kusahau, Nilipata habari kutoka kwa Chifu anaeleza kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ukombozi ya OAU anaingia mjini hapa leo jioni. Ameeleza sisi tuendele kama kawaida yeye anakuja na mipango kamili.”

“Ahaa vizuri, kama akitutaka atatujulisha, nafikiri Chifu atakuwa amemweleza jinsi ya kutupata. Sasa hivi tuwangojee akina Ozu, tupange mipango ya leo jioni”. Willy alieleza.

Pierre na wenzake walikuwa wamekutana tena mchana huu kama walivyokuwa wameahidi.

“Nilipokwenda kuonana na Mkurugenzi huko Sozidime wakati nilipowaacha hapa nilipata habari nzuri sana kutoka BOSs. Boss imeamua kuwa baada ya kuhakikisha kuwa tumewateketeza wapelelezi hawa wa Afrika tutaruhusiwa kustaafu na kuchangua nchi yoyote tunayotaka kwenda kuishi kazi tuliyoifanya ni nzuri ya kutosha,” Pierre aliwaeleza wenzake kwa tabasamu kwa mara ya kwanza tangu wafahamiane. Pierre siku zote alikuwa mtu ambaye hatabasamu wala hacheki. Kisha aliendelea. “Tayari Mkurugenzi ameishatufanyia mipango ya usafiri kiasi kwamba tukimaliza shughuli hii iliyobaki tunaondoka bila kuchelewa kwani wakati mwingine itatubidi kuondoka mjini hapa kwa haraka.

“Kwa hivi jamani tuwateketeze wapelelezi hawa mapema ndiyo itakuwa raha yetu,” Pierre aliwaeleza. Kila mmoja wao waliingiwa na mawazo ya kupanga wapi pa kwenda. Muteba alimfikiria Tete.

“Sijui kama Tete atakuwa tayari kuondoka na mimi, nitaenda kumshawishi nikitoka hapa,” Muteba aliwaza.

Jean naye alikuwa na haja ya kwenda kukaa Ufaransa na alikuwa siku zote anaota kwenda kuishi huko. Aliamua kuwa angemchukua Lucie aende naye kwani walikuwa wanapendana sana.

Papa yeye alikuwa anafikiria kwenda Hong Kong, kwa vile alikuwa ameziwekea pesa nyingi sana katika benki za nchi za nje basi alikuwa hana wasiwasi. Alifikiria kuwa kweli muda ulikuwa umefika kwake kustaafu ili akafaidi utajiri aliokuwa ameziwekea.

Pierre yeye alikuwa na mipango ya kwenda Marekani ambako alikuwa na marafiki aliokuwa amefanya nao kazi wakati walipokuwa amepolekwa C.I.A. kufanya kazi kwa muda, ambao sasa amestaafu.

“Loo mpango mzuri sana. Hii kazi iliyobaki ni kidogo sana naamini tutaimaliza usiku wa leo”, Papa alieleza. Kisha walianza kupanga namna watakavyoweka ulinzi wao tayari kwa kuwakabili adui zao.

“Tuna walinzi wapatao thelathini ambao ni wazuri sana sidhani tutapata matatizo yoyote hasa ikiwa sisi wenyewe ndiyo tunawaongoza. Lililobaki ni kutayarisha silaha za kutosha,” Pierre alishauri.

Mara kengere ya simu ililia, Pierre aliangalia saa yake ilikuwa saa tisa na nusu, akaondoka kwenda kuijibu. Alisikiliza mara moja akajibu kwa sauti. “Tunakuja”, akakata simu. Wenzie wote walimkodolea macho kwani nywele zake zilisimama.

“Vipi?” Muteba aliuliza.

“Vijana wetu wamewaona Kofi na Ozu wanaingia Hoteli Intercontinental hivi wanaomba msaada. Naamini hawatategemea kuwashambulia mchana na mbele za watu, Hivyo twende sisi wenyewe, nafikiri hii ndiyo nafasi nzuri sana,” Pierre alishauri.

“Lo, tusiipoteze nafasi hii,” alijibu Muteba akasimama tayari kwenda kwenye mapambano. Kundi zima la watu wanne, wakiwa ni majasusi wenye ujuzi wa hali ya juu waliondoka.

Kofi na Ozu baada ya kuchukua plani yote ya gereji Du Peuple, pamoja na maelezo yote waliyoyataka tayari kwa mashambulizi ya jioni. Waliondoka na kuelekea Hoteli Regna ambako Ozu alikuwa amefikia. Ozu alibadilisha nguo na kuchukua silaha zingine alizokuwa amezitayarisha kwa mapambano zaidi.

Chakula cha mchana walipatia hapa hapa, na baada ya hapo waliondoka kuelekea Hoteli Intercontinental ili Kofi naye akajiweke tayari kwa ajili ya jioni.

Ilikuwa saa tisa na nusu walipoingia Hoteli Intercontinental baada ya kuridhika kuwa hakuna mtu aliyekuwa amewafuata. Lakini kwa bahati mbaya vijana wa 'WP' waliokuwa wakiwangojea hapo Hoteli Intercontinental walipowaona bila wao kujua. Ozu alienda kwenye bar wakati Kofi alipanda juu kwenda kubadilisha nguo zake. Ilikuwa saa kumi kasoro dakika kumi Kofi alipompitia Ozu kwenye bar. “Niko tayari kabisa, twende zetu tukawawahi Willy na Robert wasije wakatungoja sana. Maana tulikubaliana kuonana saa kumi”, Kofi alimweleza Ozu.

“Twende zetu,” alijibu Ozu. Ozu alilipa bia yake na wakaondoka.

Nje ya Hoteli Intercontinental kundi la 'WP' lilikuwa limekaa tayari likiwasubiri, Pierre na Jean pamoja na vijana wao wawili walingojea kwenye mlango unaotokea pembeni mwa hoteli upande wa barabara ya 8E Armie. Papa na Muteba pamoja na vijana watatu walingojea kwenye mlango wa mbele, Makundi haya mawili yalikuwa kila moja likiwa linajifanya linashughulikia gari lililoharibika na kwa jinsi hii hakuna mtu aliyewajali. Pierre, Jean, Papa na Muteba walibaki wamekaa ndani ya gari tayari tayari huku vijana wao wakijifanya kushughulika.

Kofi na Ozu walikata shauri kutokea mlango wa mbele bila kujua kuwa wanangojewa, walitembea katika tahadhari yao ya kawaida tu. Walipotokea mlangoni waliangaza kwa mara moja. Na wakati huo huo Papa na Muteba walibonyezwa kuwa tayari walikuwa wameshatoka nje. Papa na Muteba waliruka mara moja na kupiga risasi. Ozu aliwaona mara moja wakati Kofi aliangaza sehemu nyingine, hivi Ozu akapiga kelele “Kofi” yeye akajitupa nyuma ya gari wakati ule ule risasi zikamiminika pale alipokuwa amesimama. Kofi aliposhituliwa na Ozu aliruka kama umeme kwa bahati mbaya risasi zikampata kifuani na kuanguka ndani ya mlango wa hoteli na kujiviringisha mle ndani. Ozu alipiga risasi kuwazuia wale watu, lakini waliruka ndani ya gari na kuondoka mwendo mkali sana. Ozu alisimama akakimbia ndani ya hoteli ambako watu wote walikuwa wamelala chini kwa kuogopa risasi na huku kelele za vilio zikisikika huku na huko. Alienda akamwangalia Kofi akakuta tayari ameishakata roho. Alikuwa

amechanwa na risasi kifuani kwani watu wale walikuwa wametumia 'Sub Machine Gun'

“Kofi Kofi,” Ozu aliita huku machozi yanamtoka. Watu walikusanyika na simu ikapigwa polisi.

“Sijaona kitu kama hiki kwa muda mrefu sana hapa Kinshasa. Kumshambulia mtu mchana mchana mbele ya watu wengi namna hii na mbele ya hoteli kubwa namna hii,” mtu mmoja katika hilo kundi alilalamika.

“Tena aliyekuwa na bunduki ile kubwa alikuwa Mhindi”, mtoto mmoja mdogo alisema, lakini mama yake akamfinya na kumvuta kutoka hapo. Kwa sababu ya uchungu mwingi. Ozu hakujua la kufanya ila alijua hawezi kufanya jambo lolote kwa sasa ila kwenda kuwaarifu akina Willy tayari kwa mapambano na watu hawa. Vile vile kama polisi watamkuta hapo wangepoteza muda mwingi wa kumuuliza maswali. Hivi aliangalia mwili wa Kofi akasema moyoni. “Kofi umekuwa kama mdogo wangu tangu tulipofahamiana, Mungu yupo damu yako haitamwagika bure. Nitahakikisha,” kisha akapotea ndani ya kundi lililokuwa pale kama umeme. Pierre na kundi lake walirudi gerji Du Peuple na furaha kubwa sana kwa sababu walijua wamepunguza adui mmoja hivyo upinzani jioni yake ungekuwa kidogo sana.

“Watu wawili kwa watu thelathini, hawatuwezi” Papa alidiriki kusema.

Ilikuwa saa kumi na nusu Ozu alipowasiri nyumbani kwa Robert. Alipoingia aliwakuta Willy, Robert pamoja na msichana mmoja mzuri sana ambaye alitambua kuwa msichana huyu atakuwa ndiye Tete. Alimwalia Willy na Robert machozi yalianza kumtoka tena, mara Willy na Robert wakatambua kuwa Kofi ameuawa. Robert alikimbia akaweka Whiski ndani ya glasi akampa Ozu ambaye alikuwa bado machozi yanammiminika.

“Tueleze imetokea vipi?” Willy alimwambia.

Ozu alikunywa glasi yote ya Whiski kwa mara moja halafu akawaeleza ilivyotokea, “Kofi amekufa mbele ya macho yangu mimi ninaona hivi hivi, Watu hawa ni wanyama watakufa kwa mkono wangu, Mungu anisaidie,” Ozu alimalizia machozi yalianza kumtoka tena.

Willy alitambua uchungu Ozu aliokuwa nao akamwambia, “Ozu, hata sisi jambo hili limetushitua sana, sasa lililopo ni kutulia na kupanga jinsi ya kupambana na watu hawa,” Willy alieleza taratibu.

Tete aliyekuwa amekaa pembeni kidogo alimwambia Ozu na ghafla naye akaanza kulia. Jambo hili lilimshitua Ozu na kumfanya atulie na kuelekea maliwatoni.

Mimi sasa namchukia Muteba na wenzake kiasi ambacho sijawahi kumchukia mtu maishani mwangu. Tokea sasa mimi nitachukua nafasi ya Kofi,” Tete alisema bila kutania.

“Kazi hiyo haikufai mama, kazi uliyokwishaifanya inatosha kabisa “Willy alimjibu.

“Mimi najua kitu nitakachowasaidieni. Mimi ni dereva stadi sijui kama kati yenu kuna dereva kama mimi. tafadhali sana msiniache mtakapokwenda kwenye mapambano ya leo. Tafadhali naomba mniridhishe nafsi yangu. Kule kuwaendesha tu nitajiona nimelipa deni kubwa kwa Mwadi, maana ni mimi niliyefanya akina Muteba wamfahamu. Hivyo Willy mpenzi usiniache,” Tete aliomba akaanza kulia tena.

Ozu aliporudi kutoka maliwatoni alikuwa na hali nzuri kidogo. Alipofika alianza kuwaeleza plani yote ya gereji Du Peuple na jinsi alivyokuwa amefikiria wanaweza kuiingilia.

“Hata wakiwa watu hamsini, tukiwashambulia hivi tunaweza tukawapenya, ili mradi tu, tuwe na silaha za kutosha. Mimi naona 'machine gun' na bastola tulizonazo zinatosha kabisa,” alimalizia Ozu. Willy naye alimwelezea Ozu juu ya Kadima. “Na jambo jingine ni kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ukombozi ataingia hapa usiku”, Willy alimweleza.

“Nafikiri atafika wakati unaofaa kabisa, maana leo mimi nataka kuona mwisho wa watu hawa,” Ozu alisisitiza. Waliendelea na mipango ya siku ile na mwishowe hata ombi la Tete lilikubaliwa.

“Yeye anazifahamu ofisi za Sozidime vizuri sana hivi anaweza kuwa wa msaada sana kwetu ingawaje ni jambo la hatari”, Ozu alisema.

“Mimi siogopi hata kidogo hiyo hatari nataka niipate. Mimi naomba mnihesabu kama mmoja wenu,” Tete alizidi kuomba. Baada ya kukubaliwa. Willy na Tete waliondoka kwenda chumbani ambako Willy alikuwa analala. Huko alitoa silaha zake huku akiwa anaongea na Tete, alizitia mafuta. Robert na Ozu nao walishughulikia silaha zao kuziweka tayari.

SURA YA KUMI NA TISA

USHINDI NI DHAHIRI

Ilikuwa saa nne za usiku na hapo gereji Du Peuple huko Limete kulikuwa na pilika pilika nyingi sana. Kundi zima la 'WP' lilikuwa limewasili isipokuwa Muteba. Pierre alizunguka kila sehemu kukagua ulinzi ulivyokuwa umepangwa. Alikuta kila mtu ameshika nafasi yake. Baada ya kuridhika na ulinzi uliopangwa alirudi ofisini mwake ambamo Jean na Papa walikuwa wanamsubiri.

“Muteba amepatwa na maafa ama vipi?” Pierre aliuliza.

“Sijui, Patron, alikuwa ameniambia kuwa atakuwa hapa kabla ya saa tatu lakini ninashangaa mpaka sasa bado hajafika,” Alijibu Papa. Alipomaliza kusema hivyo tu walisikia mlango unagongwa halafu ukafunguliwa na Muteba akaingia. Wote wakapumua walipomuona. Muteba alikuwa amechelewa kwa sababu alipokuwa ameachana na wenzake baada ya shambulio lile la Hoteli Intercontinental, alienda moja kwa moja nyumbani kwake na kubadili nguo. Baada ya kubadilisha nguo aliondoka kwenda nyumbani kwa Tete ambako alitarajia kumweleza mipango ya kuondoka naye kama BOSS ilivyokuwa imewaletea habari. Alipofika nyumbani kwa Tete hakumkuta. Akaanza kumtafuta kila mahali alipofikiria kuwepo asiweze kumuona. Jambo hili lilikuwa karibu limtia Muteba wazimu. Alitumia zaidi ya masaa manne akimtafuta Tete bila kumuona kabisa mwishowe akajikuta ameishachelewa kufika gereji Du Peuple kama alivyokuwa anatakiwa ndipo akaondoka na kuja moja kwa moja gereji Du Peuple.

Wenzake walipomwangalia walijua kulikuwa na kitu kinamsumbua rohoni. “Vipi, mbona hivi?” Pierre alimuuliza bila kuficha jinsi alivyokuwa amemtafuta Tete. “Sahau hayo mambo ya mwanamke tukimaliza shughuli hii salama, mambo haya yatanyooka tu. Bila shaka anashughuli zake” Pierre alimshauri.

“Huenda huyu Willy amemkamata baada ya kujua kwa kikamilifu juu ya uhusiano wangu na wake”, Muteba alilalamika.

“Achana na mawazo hayo, sasa hivi tuna kazi muhimu kuliko kufikiria matatizo ya mwanamke.” Pierre alisema kwa ukali. Muteba alijigundua kuwa alikuwa kweli amefanya kosa la kikazi kuwa na mawazo mengine wakati mbele yao kuna kazi muhimu kabisa. Hivi alijisahihisha akasema. “Samahani Patroni, tuendelee”.

Pierre alieleza tena ulinzi ulivyokuwa umepangwa na wote wakaridhika nao kabisa. “Vijana tayari, wameishashika sehemu zao,” alisema akimwangalia Muteba.

“Nimewaona wakati naingia, hakika ulinzi umepangwa vizuri kabisa”. Muteba alikubaliana. Papa ataongoza ulinzi wa mbele, Jean utaongoza wa nyuma na Muteba utaongoza sehemu zilizobaki,” Pierre aliwaeleza. “Sasa twendeni wote tukakague sehemu zenu, na ikiwa kuna marekebisho turekebishe halafu tuwangojee washenzi hawa kama watathubutu kuja,” Pierre alieleza.

Willy na Robert ambao walikuwa wameondoka jioni ile na kuelekea mjini walirudi kiasi cha saa tatu na kumkuta Tete na Ozu wakiwa wameishatengeneza chakula. Willy alikuwa amepitia hotelini kwake ambako alichukua vifaa fulani fulani ambavyo vilikuwa vya lazima katika shughuli ya usiku huo. Pamoja na silaha zaidi alizokuwa amechukua, alichukua na fulana mbili ambazo zilikuwa haziingiwi na risasi. Fulana hizi Willy alikuwa mara kwa mara anazitumia alipokuwa karibu kukabili pambano kali sana. Na mara nyingi zilikuwa zimemsaidia, hivi alikuwa akisafiri nazo mara kwa mara. Fulana hizi zilikuwa ni zawadi alizokuwa amepewa na Mkuu wa kikosi cha Scotland Yard wa huko Uingereza alikokuwa amepolekwa kwa mafunzo ya miezi sita na kujitokeza kuwa mtu aliyefuzu vizuri kuliko watu wote waliokuwa wamepitia kwenye kikosi hicho cha mafunzo. Kwa furaha ya Mkuu wa kikosi hicho alimpa fulana hizo kama zawadi.

Robert alikuwa amemwacha Willy Hoteli kwake akijitayarisha, na yeye akaenda nyumbani kwa rafiki yake yule aliyekuwa Afisa wa juu katika Shirika la Upelelezi la Zaire C.N.D. Alimkuta huyu rafiki yake na wakazungumza vitu vya manufaa kati yao. Akiwa na furaha kubwa baada ya kuwa na mazungumzo yaliyofanikiwa kati yake na huyu rafiki yake alirudi hoteli Memling akampitia Willy na bila kumueleza Willy wapi alikuwa ameenda, walirudi nyumbani.

“Chakula tayari”, Tete aliwaeleza.

“Ooh, safi sana mimi nina njaa sana”, Robert alidai.

“Vipi Bwana Kadima mmempa chakula?” Willy aliuliza.

“Tayari kabisa”, Ozu alijibu. Walikaa kwenye meza wakala chakula cha jioni ambacho kilikuwa kimepikwa vizuri sana. Wakati wakila Tete alieleza.”

“Wakati mmeondoka alikuja msichana mmoja hapa anaitwa Ebebe, alikuwa anamtafuta Robert. Tulimwambia Robert ametoka amsubiri lakini hakutaka, akaondoka akaenda zake. Alionekana amechukia”.

...”Shauri yake nitamwona kesho. Rafiki yangu sana, lakini ana wivu mwingi.” Robert alieleza.

“Nafikiri alipomkuta Tete anapika alifikiri kuwa amepinduliwa serikali yake ya hapa nyumbani,” Willy alitania wote wakacheka.

“Hasa alipoona mapinduzi yenyewe yamefanywa na msichana chuma namna hii”, aliongeza Ozu. Walipomaliza kula walianza kujiandaa.

“Tunasubiri tukashambulie sehemu hii usiku, ili kama watakuwa wanatusubiri wawe wameshakata tamaa na kuchoka. Unajua mtu wa kawaida tu kuwa katika hali ya tahadhari kwa muda usiopungua masaa manne ni vigumu sana”, Willy aliwaeleza.

“Hizo ndiyo saa zenyewe, wengine watakuwa wameanza kusinziasinzia. Hata mimi zamani kabla sijazoea, nilikuwa na ubovu huo”, alieleza Ozu.

Willy alitoa fulana zake ndani ya mfuko akaeleza. “Hapa ninazo fulana hizi mbili ambazo haziingiwi risasi. Sasa kati yenu sijui nani atachukua moja,”

“Mpe Robert mimi sina taabu,” Ozu aliamua.

“Hapana mpe Ozu. Mimi nina ujuzi wa hali ya juu sana katika kareti na Kung-Fu, sitahitaji kabisa fulana hiyo. Na kwa taarifa yenu ni mara chache, natumia silaha, mpaka iwe lazima sana,” Robert alieleza. Willy alikubaliana na Robert kwani alikuwa amemuona siku ile walipopambana na akina Mulumba.

“Ozu chukua hii. Wewe una ujuzi mwingi katika kutumia bunduki hasa hizi kubwa kubwa hivyo naamini utahitaji”. Willy alimshauri.

“Huenda tumpatie dereva wetu.” Ozu alisema huku anamwangalia Tete.

“Wacha matani, mimi sina haja nayo”, Tete alijibu kwa ukali.

“Wengi wape,” alijibu Ozu na kuichukua ile fulana.

“Sasa ni saa nne twendani tukapumzike lakini saa nane tuwe tumejiweka tayari kwa kuondoka hapa.” Willy alishauri. Kila mmoja alienda chumbani kwake, Willy na Tete wakaandamana chumbani kwa Willy. “Tete unajua unachukua mzigo mzito sana usiokuwa kiasi chako,” Willy alimweleza Tete.

“Wewe niache, mimi mwenyewe ndiye nimekata shauri na wala sikushawishiwa na mtu yeyote. Tuzungumzie jambo jingine Willy, jambo hili tuliache hivyo lilivyo, mimi nitakwenda pamoja nanyi,” Tete alijibu kwa ukali, Willy bado alikuwa hajakuwa na imani kabisa na msichana huyu. Maana yeye Willy huwa hawaamini sana wasichana wenye sura nzuri kwani kila wakati mambo yao hayaeleweki. Lakini hata hivyo aliamua kuyaacha mambo yalivyo aangalie huko mbele ya safari.

Ilipotimia saa nane simu ililia ofisi kwa Pierre. “Hallo”, aliitikia alipoinua simu.

“Fernand hapa, vipi mambo bado?” Aliuliza Mkurugenzi.

“Bado, huenda hawatakuja na kama hawatakuja watakuwa wamvuruga mambo maana mimi nimechoka. Kama tutamaliza shughuli hii mimi kesho nitaondoka.” Pierre alieleza kwa unyonge.

“Usiwe na wasiwasi mambo yote yako tayari, ukimaliza shughuli za hapo tu njoo moja kwa moja hapa ofisini, mimi nipo tu mpaka mwisho”, alijibu Fernand na kukata simu.

Pierre aliangalia tena saa yake, akiwa na mashaka makubwa kama mambo yangekwenda kama walivyopanga. Wenzake nao ambao walikuwa nje na vijana wao walikuwa nao wamechoka. Kwani walikuwa sasa wamesimama wakisubiri zaidi ya masaa manne. Wale vijana wengi walikuwa wameanza kusinzia sinzia. Kwa ujumla jeshi zima lilikuwa limeshikwa na uchovu, na mawazo ya kwamba “Hakuna kitu” ndiyo yalikuwa yamewajaa wote.

Ilikuwa saa tisa kasoro robo wakati KIKOSI CHA KISASI kilipokuwa tayari kuondoka nyumbani kwa Robert ili kuelekea Limete. Kila mtu alivaa mvao wa kazi. Tete naye alivaa dingirizi na T'shati, na akaweka jaketi juu. Miguuni alivaa raba na nywele zake akawa amezifunga, kwa ujumla alionenana mmoja wao kabisa. “Loo utafikiri tunaenda kuteka ndege nyara. Kwa kawaida wateka nyara wasichana wa Kipalestina huwa ni wazuri sana kama Tete” Ozu alitania.

“Na wewe na maneno yako”. Robert alijibu na kuingia stoo. Aliporudi alikuwa na kamba akampatia Willy. Ilikuwa kamba ndefu. Willy akaikata akampa Robert kipande akamwambia aiweke wataondoka nayo. Willy alienda akafungua mlango wa chumba ambamo Kadima alikuwa amelala. Alimkuta Kadima amelala akamwamsha.

“Samahani Bwana Kadima itabidi nikufunge kwa usalama wako,” Willy alimwambia. Kadima alimwambia tu bila kumjibu, Willy akamfungia kwenye kitanda. Alimfunga miguu na mikono kwa ustadi kabisa, “Samahani sana”, Willy alimwambia tena Kadima na kuondoka, na kuufunga mlango vizuri kabisa. “Sasa twende zetu,” Willy aliwaambia wenzake. Wakiwa wameweka silaha zao tayari walipanda ndani ya gari Willy alilokuwa akitumia. Tete akapiga moto na kuondoka pale nyumbani kwa Robert kama risasi.

“Tete ukifika Limete kwenye barabara ya P.E Lumumba ingia barabara ya tisa inayoingia viwandani, nenda moja kwa moja na usimamishe gari mbele kidogo na Kampuni ya BISCO, sisi tutateremka hapo. Wewe utarudi mpaka kwenye njia ndogo inayounganisha mabarabara yanayoingia viwandani, na egesha gari mbele ya nyumba ya pili kutoka barabara ya nane. Nyumba hii wenyewe wamekwenda Brazzaville na haina mlinzi bali lango lake limefungwa. Wewe utaegesha gari mbele ya lango la nyumba hiyo na nina imani hakuna mtu atakutilia mashaka yoyote. Utatungoza hapo ukiwa tayari tayari, kama itapita zaidi ya saa moja na nusu hujaona hata mmoja wetu, jua mambo yameharibika ondoa gari uende zako. Lakini nina imani nusu saa itatutosha. Umenielewa?” Willy aliuliza.

“Nimeelewa hamna wasiwasi kabisa” Tete alimjibu kwa sauti kavu kabisa.

Kutokana na taarifa Ozu aliyokuwa ameleta, kampuni ya Bisco ambayo hutengeneza biscuti inafanya kazi masaa ishirini na nne. Na inafanyakazi kwa zamu na kwa bahati kulikuwa na zamu iliyokuwa inaingia saa tisa za usiku. Kufuatana na taarifa hii ndiyo sababu walikuwa wameamua kushukia mbele ya Kampuni hii ili ionekane kama kwamba gari ile ilikuwa imeleta watu wa zamu. Jengo la gereji Du Peuple likuwa jengo la tatu mkono wa kushoto kwenye barabara ya tisa kama unatoka barabara ya Patrice Emiry Lumumba. Kulikuwa na majengo mengine matatu makubwa kabla hujafika kwenye jengo la kampuni ya BISCO kutoka gereji Du Peuple.

Tete ambaye aliwadhihirishia abiria wake kuwa alikuwa dereva stadi sana aliongoza gari kama alivyokuwa ameelezwa. Alipofika kwenye kona ya P.E. Lumumba na barabara ya tisa. alionyesha taa na kuingia barabara ya tisa. Alivuta gari katika mwendo mkali sana na kusimama mbele kidodo ya Kampuni ya BISCO. Alimvuta kidogo Willy aliyekuwa amekaa naye kwenye viti vya mbele ya gari na kumbusu haraka haraka.

“Bahati njema aliwaambia kwa ujumla huku akiwarushia busu”.

“Na wewe vile vile.” Ozu alijibu kwa niaba ya wenzake.

Vijana wa Kikosi cha Kisasi wakateremka kuelekea kwenye mapambano ambayo yangeamua mwisho wa kazi yao unakuwa vipi. Tete aliondoa gari lake, huku watu wote walioona mwendo wake wakahisi kuwa alikuwa taksi dereva aliyekuwa amelea wafanyakazi wa BISCO waliokuwa wamechelewa zamu. Wazo hili ndilo lilimpata hata Papa aliyeliona gari hili na kulishuku lakini baada ya kusimama mbele ya kampuni ya

Bisco akaondoa wasiwasi wake.

Baada ya kuteremka tu Willy na wenzake walipotelea ndani ya uchochoro uliokuwa ukipita kati ya BISCO na jengo lililokuwa linafuata. Kulikuwa na giza katika uchochoro huu lakini kwa vile Ozu alikuwa amepita aliwaongoza. Walienda mpaka wakatokea kwenye uchochoro uliokuwa nyuma ya majengo haya yaliyokuwa yanatazama barabara ya nane. Walipokaribia jengo la gereji Du Peuple kwa nyuma, walianza kutembea kwa kunyata na katika tahadhari kubwa.

“Sii” Robert aliyekuwa mbele aliwasimamisha wenzake, “Nimeona mtu amepita”, aliwanong'oneza, “Nisubirini” Robert alienda akinjongwajongwa, na alipofika kwenye pembe ya mwisho ya jengo jirani na gereji Du Peuple alisimama. Alianganza akaona kuna walinzi watatu kwenye ukuta uliokuwa umepakana na jengo hili jingine na walikuwa wanazungumza. Walikuwa hatua chache tuu na alipokuwa. Alipoangalia juu ya ngome ya ukuta uliozunguka gereji Du Peuple aliona kulikuwa na walinzi wanatembea kwa juu. Mmoja alitembea juu ya ukuta wa nyuma na mmoja kwenye ukuta wa pembe ya upande waliyokuwa. Alipokwisha kuona mambo haya alirudi pale wenzake walipokuwa akawaeleza.

“Kwa hiyo hawa wanaozungumza nafikiri ndiyo walinzi wa nje”. Willy alisema.

“Sawa kabisa”, Robert alikubaliana, “Na ninafikiria kuna mlinzi mwingine juu ya ukuta wa upande mwingine lakini amezuiwa na paa la nyumba hatuwezi kumuona”, aliongeza wote watatu wakiwa wamefichwa na kivuli cha majengo haya walinyata mpaka kwenye pembe ya mwisho ya kutokea gereji Du Peuple. Wale walinzi waliokuwa wanazungumza walimaliza na wakamuacha mmoja wao anaelekea mbele ya jengo. Watu hawa walipitia karibu kabisa na pale akina Robert walipokuwa wamejibanza.

“Hawa watu hawaji tunasumbuka bure, mle ndani watu wameishachoka wanasinzia ovyo”, mmoja wao alisema.

“Hata mimi najisikia kuchoka kabisa katika siku hizi tatu sijalala vizuri”, yule mwenzake alijibu na wakaendelea. Walipoenda hatua chache kidogo Robert alinyata mpaka kwenye ukuta wa ngome bila kuwagutua walinzi hawa. Aliangalia juu akamuona yule mlinzi aliyekuwa juu ya ukuta alikuwa amekwenda upande mwingine, hivyo hakuwa na wasiwasi wa kuonekana.

Wale walinzi wawili walisimama, mmoja wao akamuomba mwenzake sigara Robert alichukua hii nafasi wakati mawazo yao yako kwenye sigara akawanyatia. Yule mmoja alitoa sigara akampa mwenzake na akatoa kiberiti ili kumwashia sigara. Robert alikuwa ameishafika bila wao kujua, akatoa kiberiti chake haraka akamwashia yule mlinzi aliyekuwa tayari ameweka sigara yake mdomoni akingojea moto. Yule mlinzi mwingine aliyekuwa amewasha kiberiti akagutuka, moto mwingine unatoka wapi. Walipotaka kugeuka tu Robert akawapiga kareti wote wawili kwa mara moja na pigo alilokuwa ametoa lilikuwa kali sana akiwa amewapiga shingoni, wote walianguka chini na kufa pale pale bila kelele.

Aliangalia tena juu ya ukuta yule mlinzi wa juu alikuwa haonekani. Akawafanyia ishara wenzake wamfuate. Wakiwa wamezuiwa na kivuli cha majengo waliruka mpaka nyuma ya majengo ya gereji Du Peuple ambako Robert alikuwa bila kuonwa na walinzi wa pembeni kwao. Waliwavuta hawa watu wakawalaza chini ya ua wa michongoma mtu asiweze kuwaona kwa urahisi. Willy alimuona yule mlinzi wa juu ya ukuta wa upande ule wa nyuma akirudi akiwabonyeza wenzake ambao walijibanza. Ozu alijificha chini ya michongoma. Robert na Willy wakajifanya kama kwamba wao ndio wale walinzi waliokuwa wameuawa. Kwa vile wote walivaa nguo nyeusi nyeusi ilikuwa vigumu kutambuana usiku namna hii. Yule mlinzi wa juu hakuweza kuwatilia mashaka kwani aliamini ni wenzake.

Yule mlinzi alipokaribia Robert alimwita kwa kumfanyia, “Sii” yule mlinzi alikuja akauliza, “Unasemaje?”

“Inama nikueleze”, Robert alimwambia akawa anajua ni mwenzake akadanganyika akainama. Robert aliruka kama umeme akampiga kareti ya katikati ya paji la uso na kumpasua kabisa. na wakati huo huo alimvuta wakamdaka na kumlaza chini akiwa ameisha kufa. Naye alikufa bila kelele. Upesi upesi wakampandisha Ozu akachukua nafasi ya yule mlinzi, akaanza kulinda sehemu hii ya nyuma. Kitendo hiki kilifanyika bila kufahamika ndani ya ngome.

Willy alizunguka mpaka pembe nyingine akakuta hakuna mlinzi wa chini ila yule wa juu ya ukuta alikuwepo. Willy alikohoa yule mlinzi wa juu aliyekuwa anaangalia upande mwingine akageuka, akampungia mkono. Akiwa anafikiri kuwa

ni yule mwenzake alikuja. Ozu aliyekuwa tayari akijifanya kulinda sehemu hii ya nyuma aliona ishara ya Willy akajua Willy alikuwa anataka kufanya nini, hivi naye akasogea upande ule. Yule mlinzi akiwa na uhakika na uhakika kuwa wote walikuwa walinzi wenzake alikuja mbio mbio. Alipofika pale Willy alipokuwa amesimama Ozu naye akawa amefika.

“Huyu anasemaje”, yule mlinzi alimuuliza Ozu.

“Inama msikilize,” Ozu alimweleza kwa sauti ya chini chini. Alipoinama tuu Ozu alimkata mkono wa shingo na kumtua chini. Robert alikuja wakamficha. Robert akampandisha Willy kwenye ukuta akachukua nafasi ya huyu mtu.

Ozu alimfuata yule mlinzi wa chini wa upande ule waliokuwa wametokea. Mlinzi huyu alikuwa amesimama tu karibu na kona ya kwenda upande wa nyuma.

“Hallo” Ozu alimwita kwa sauti ya chini chini, yule mlinzi akaangalia juu. Ozu akamuonyesha ishara kuwa anaitwa kule nyuma. Robert alikuwa amebana kabisa kwenye kona akiwa anaona mambo yote yaliyokuwa yanafanyika. Yule mlinzi naye akiwa hana wasiwasi wowote akijua kuwa hawa ni walinzi wenzake alienda haraka haraka. Alipojitokeza tu kwenye kona Robert alimrukia akamkaba kabari mpaka akamuua na kumvuta mpaka pale wenzake walipokuwa wamelazwa.

Ozu akamuonyesha ishara Willy kuwa amebaki mmoja. Bila kujua nini kinatokea yule mlinzi wa juu ya ukuta wa upande ule waliotokea alikuwa anaendelea na shughuli zake za ulinzi bila wasiwasi. Robert alijifanya kuwa yeye ni mlinzi wa chini wa upande ule alimwendea akamwita;

“Sii” Yule mlinzi alipogeuka kumwanguka alimuonyesha ishara amfuata nyuma. Yule mlinzi akiwa hana wasiwasi naye alimfuata. Alipofika kule kwenye ukuta wa nyuma Ozu naye alikuwa yuko tayari.

“Inameni niwaeleze” Robert aliwaambia wote. Ozu alijifanya anainama na yule mlinzi naye akadanganyika akainama. Ozu akamkata mkono wa shingo na kulivunja, akamsukumia Robert akamdaka na kumvuta chini. Kisha Ozu akainama akampa Robert mkono akapanda na yeye juu ya ngome.

Willy ambaye alikuwa ameishazunguka na kuona jinsi ulinzi ndani ya gereji ulivyokuwa alipita kwa wenzake akiwaeleza huku wakijifanya kama kwamba wanabadilishana sehemu,

“Sehemu ambayo bado wako macho ni kule mbele, sehemu hizi zote wengine wamelala na wengine wanasinziasinzia.” Willy alimnong'oneza Robert.

“Basi mimi ninateremka kwa huku nyuma. Nitajaribu kushambulia kwa kadri niwezavyo nikitumia mikono yangu, nyinyi muwe tayari kunichunga kama watagutuka,” Robert alisema.

“Kuna walinzi karibu ishirini humu ndani,” Willy alimweleza. Kisha Willy aliendelea akamweleza Ozu. Walipokuwa wameshika nafasi sawa sawa na kuweza kumchungu. Robert kama nyani alitumbukia ndani ya gereji kwa nyuma bila kishindo. Jean ambaye alikuwa analinda sehemu ya nyuma pamoja na vijana wapatao sita alikuwa amelala ndani ya gari moja bovu, na akiwa amewaamrisha vijana wake kumwamsha kukitokea tatizo lolote. Alikuwa amekaa macho, mpaka saa tisa lakini akawa amekata tamaa kuwa hawa watu hawawezi kuja tena. Na kwa vile alikuwa hajalala vizuri kwa muda wa siku tatu alisikia usingizi mzito sana.

Ilikuwa sasa imepita miaka mingi bila Jean kujiweka katika hali ya kuweza kukabili hali ya namna hii. Zamani alipokuwa hajaletwa Zaire angeweza kukaa hata juma moja bila kulala asichoke kama alivyokuwa amechoka siku hii, hivyo Robert alipotumbukia ndani Jean alikuwa amelala kabisa.

Baada ya Robert kutumbukia ndani aliwanyatia walinzi wawili waliokuwa wameegemea kwenye gari, aliwatokea nyuma akawapiga kareti za katikati ya vichwa vyao wakafa pale pale kwani alivipasua kabisa. Akatoa ishara kwa Willy kuwa ameua wawili. Kisha akamuona mlinzi mmoja anatokea sehemu ya kushoto kwake akajiegemeza kwenye gari kama mmoja wao, na kutoa sigara. Yule mlinzi alipomuana alimfuata akidhani ni mwenzake akamwomba sigara. Robert akampa halafu akatoa kiberiti kumwashia, na akatelemlsha kiberiti chini. Yule mlinzi alipotelemlsha mdomo chini ili kuwasha sigara.

Robert alimkata mkono wa shingo na kulivunja. Akamchukua taratibu akamuegemeza kwenye gari. Alipozunguka kutokea ule upande wa kushoto, Willy alimfanyia ishara kumuonyesha kuwa kuna watu ndani ya gari alilokuwa karibu kulipita. Alichungulia ndani akakuta kuna walinzi wawili wamelala, alifungua mlango taratibu kabisa akatoa bastola yake yenye sailensa akawapiga risasi kimya kimya.

Ni wakati alipokuwa amemaliza kuwaua hawa ndipo mlinzi mwingine aliyekuwa amelala ndani ya gari ambapo Robert alikuwa amewaegemeza wale watu wawili aliokuwa amewaua kwanza alipoamka. Kufungua mlango, alipojitokeza na kuwagusa wale wenzake aliokuwa anafikiri wamelala akakuta wamekufa. Kwa hifu akafyatua risasi ovyo. Gereji nzima ikawa katika vurugu, walinzi waliokuwa wamelala wakaanza kukimbia ovyo, hii iliwapa nafasi nzuri Willy na Ozu kujua ni

wapi washambulie. Ozu alirukia ndani katikati ya kikundi kilichokuwa kinaongozwa na Papa na akaanza kushambulia. Willy naye alirukia katikati ya gereji ambako Muteba ndiko alikuwa akiongoza. Robert akabaki kule kule kwenye kikundi cha Jean.

Jean aligutushwa na mlio wa bunduki, akaamka na kupiga kelele, “Shambulia shambulia”, Robert aliwahi kumpiga risasi yule kijana aliyekuwa anapiga risasi na kutahadharisha gereji nzima. Jean alijikuta hana mtu ila yeye peke yake kwa upande huu. Robert alimuona, akamsubiri kwani alikuwa anakwenda ovyo katika woga mkuu. Kisha akakata shauri kurukia kwenye ukuta na kujitupa nje. Robert alihisi mawazo yake, na kwa vile alikuwa ameelekeza mgongo wake kwa Robert, Robert alimnyemelea akapiga bastoka kutoka mikononi mwa Jean, Jean kwa hofu aligeuka akajikuta uso kwa uso na Robert.

“Nitakuua kwa mikono yangu kulipiza vifo vya wazalendo wa Afrika ambao umewaua”. Robert alimtishia Jean naye alikuwa mjuzi sana wa kareti, hivi hakusita kuzianzisha moja kwa moja akifikiri Robert hakuwa na ujuzi kiasi chake. Jean alipeleka pigo la kwanza akapoteza la pili akapoteza la tatu akapoteza, akabadilisha. Robert alikuwa anatabasamu. Jean alipobadilisha alikuja na ufundi wa hali ya juu sana. Mapigo haya yalimpata Robert na kumpandisha mori.

Robert alimwingilia Jean kwa Kung-Fu ya hali ya juu kabisa ambayo Jean alikuwa hajawahi kuona. Robert alimpiga Jean mapigo matatu mfululizo. Jean akaona hamwezi akageuka kutaka kukimbia. Robert akamvuta shati, akamgeuza na kumpiga mapigo mengine matatu ya haraka haraka. Jean alijaribu kwa kadri ya ujuzi wake lakini wapi. Jean aliruka juu ya gari, halafu akamrukia Robert. Robert akamkwepa halafu yeye Robert akamrukia Jean akampiga teke kali kali ajabu kifuani, likamuua Jean pale pale.

Willy aliporukia ndani ya gereji alikuwa ameshikiria 'machine gun'. Aliwaua walinzi kama mchezo maana walikuwa wanapigana bila mpango, Muteba alipoona walinzi wake wanakwisha alichukua 'machine gun' akaanza kushambulia yeye mwenyewe. Alikumbuka ujuzi wake aliokuwa ameupata vitani na katika makambi ya mafunzo ya BOSS, Willy akiwa anadonga huku anaruka hapa na pale aliwaua walinzi wa Muteba wote. Ikawa wamebaki yeye na Muteba.

Ozu naye alishambulia vibaya sana kundi la Papa. Hili ndilo kundi lililokuwa kali sana. Lakini Ozu alipigana kwa ujuzi wa hali ya juu, Akitumia magari kama ngao yake aliua mmoja mmoja akitumia bastola. Walipoanza kutumia bunduki kubwa na yeye akakamata 'machine gun' na hapa ndipo hakuwakawiza, akawa amebaki yeye

na Papa. Pierre aliyekuwa anachungulia mapigano yalivyokuwa yanakwenda, aliogopa alipoona walinzi wake walivyokuwa wameteketewa. Hivyo akatambua kuwa mwisho wa mapigano haya ungekuwa mbaya.

Alirudi ofisini kwake haraka haraka akachukua mkoba wake aliokuwa ametayarisha, akachukua bastola yake akaijaza risasi akatoka ndani ya ile ofisi. Alipofika nje ya ofisi alikuta mapambano kati ya Muteba na Willy. Ozu na Papa yanaendelea, Robert alikuwa naye ndiyo anaondoka nyuma ya ofisi baada ya pambano lake na Jean. Hivi Pierre aliweza kukimbia bila upinzani mkubwa. Wote waliokuwa wanapambana walimuona lakini hawakuwa na nafasi ya kumfanyia lolote. Hivyo alipata nafasi ya kuondoka gereji Du Peuple salama. Ozu alipokumbuka sura ya Papa wakati anampiga Kofi risasi alijawa na hasira na uchungu mpya hasa ALIPOTAMBUA KUWA MTU HUYU NDIYE ALIYEKUWA ANAPIGANA naye sasa.

“Papadimitriu?” Ozu aliita. Papa hakujibu ila alitupa risasi nyingi pale sauti ilipokuwa inatokea.

“Mchana umemuuu ndugu yangu Kofi nikikuona sasa utalipa, utalipa madeni yote” Ozu alimpigia kelele. Ghafla Ozu aliruka juu ya gari, Papa akamimina pale risasi nyingi. Ozu aliruka tena kabla na kumuwahi na kuupiga mkono wake risasi, bunduki ikaanguka upande. Papa aliinuka na kujaribu kuirukia tena bunduki yake Ozu akampiga risasi ya kiuno akaanguka chini na kupiga kelele. Ozu alimfuata mpaka pale chini.

“Umeua watu wengi sana katika maisha yako, watu wasio na makosa. sasa mimi ninawalipizia wote. Nitakupiga risasi tatu kifuni, kumlipizia ndugu yangu Kofi, na zile zitakazofuata ni kuwalipizia ndugu zangu wana mapinduzi wa Afrika uliowaua”, Ozu alimsomea risala.

“Nisamehe...,” kabla hajamaliza Ozu alimpiga risasi zaidi ya kumi.

Willy na Muteba walipambana vikali sana. Muteba alitumia ujuzi wake wote aliokuwa nao, lakini alimkuta Willy yuko tayari kabisa. Willy alitupa 'machine gun' akachukua bastola. Muteba aling'ang'ania 'machine gun' lakini Willy aliruka hapa na pale kumhangaisha mpaka risasi zikamuishia, hapo ndipo Willy aliporuka mpaka pale Muteba alipokuwa kabla hajachukua silaha nyingine, Muteba alisimama wakaangalia na Willy ana kwa ana.

“Wewe ndiye Willy Gamba?” Muteba alimuuliza.

“Ndiyo mimi, na wewe ndiye Muteba Kalonzo?” Willy naye alimuuliza.

“Tete yuko wapi?” Muteba alimuuliza Willy.

“Yupo hapo nje ndani ya gari langu”. Willy alimjibu taratibu huku bastola imemlenga Muteba kifuani.

“Umemkamata kwa nguvu?” Muteba alisema.

“Amenitafuta kwa hiari yake. Hana nafasi na watu waovu kama wewe” Willy alimtibia Muteba, jambo hili lilimtia uchungu akapandisha mori. Kama umeme aliruka na kupiga teke bastola ikatoka mikononi mwa Willy.

“Muongo...” alipiga kelele. Hapo hapo alichomoa bastola yake nyingine kwa upesi sana na kupiga risasi pale Willy alipokuwa lakini Willy naye alikuwa ameisharuka kabla risasi hazijatua pale. Akiwa ameruka kabla hajatua chini alichomoa bastola yake nyingine akampiga Muteba risasi iliyompata katikati ya paji la uso na kumuua. Willy aliangalia chini akajiviringisha aliposimama akamuona Robert amesimama karibu naye akiwa ameshikilia bastola.

“Umemuwahi vizuri sana, sikutegemea, mimi nilikuwa tayari tayari”, Robert alimweleza Willy.

“Asante sana, mtu huyu alikuwa hatari sana,” Willy alijibu. Ozu alikuja anakimbia.

“Tayari?” aliuliza. Wenzake walimjibu tayari. Wote walitoka pale mbio kwani walitegemea polisi kufika wakati wowote. Walipofika pale Tete alipokuwa ameegea gari walipanda Willy akasema.

“Moja kwa moja SOZIDIME”.

Tete ambaye alikuwa anawasubiri kwa wasiwasi sana alifurahi kuwaona wote wamerudi salama. Alitia gari moto na kuondoka kuelekea sehemu za Gombe.

“Nimeona gari la Pierre linaelekea mjini”, Tete aliwaeleza.

“Ndiyo hata sisi tumemuona”, Willy alimjibu. Tete alienda na kusimamisha gari pale “CINE RAC”

“Sasa utatusubiri hapa,” Willy alimweleza Tete, wakateremka wote watatu.

“Robert utatupandisha sisi turuke juu ya michongoma tukiishaingia ndani tutakufungulia wewe lango”, Willy alimweleza Robert. Walienda kwenye uchochoro uliokuwa unatenganisha Cine Rac na ua wa Sozidime. Walipofika

pembeni mwa ua huu wa michongoma Robert alimpandisha kwanza Willy ambaye alirukia ndani ya ua wa ofisi hii na kuwa tayari kwa pambano lolote. Kisha Robert alimpandisha Ozu na wote wawili wakawa wametumbukia ndani. Kwa mshangao wao walikuta ile ofisi shwari kabisa na hakukuwa na dalili ya kuwepo mtu. Lakini hata hivyo walikaa tayari tayari na walitembea katika tahadhari kubwa. Robert alizungukia kwenye lango Willy akamfungulia,

“Inaonekana hakuna mtu hapa lakini wanaweza kuwa wamefanya mtego, hivyo wewe Robert utabaki umejibanza nje, wakati sisi tutakapoingia ndani, kama lolote likitokea unajua la kufanya”, Willy alimweleza Robert.

“Sawa”, Robert alijibu.

Robert alinjongwajongwa na kubana kwenye ukuta wa ile. Willy na Ozu walienda kwenye mlango wa mbele. Willy akatoa funguo zake malaya na kuanza kufungua huku Ozu akiwa tayari tayari analinda kwa lolote. Lakini kinyume na walivyotegemea, walifungua mlango ule bila kupambana na kitu chochote. Waliingia ndani wakarudisha mlango na wakajikuta wako mapokezi ya ile ofisi mahali ambapo Willy alipokuwa amefika.

Ghafla taa zikawaka, na wakajikuta wote wanaangalia ndani ya midomo ya bunduki ya watu wanne waliokuwa wamewalenga huku wamelala chini.

“Tupeni silaha zenu”, walielezwa. Kuona walivyokuwa wamesakamwa walitupa silaha zao. Mmoja wa wale watu alisimama akaanza kuwapekua na kuwanyang'anya silaha zilizobaki. Mara Max akatokea.

“Oh Willy, mbona umekuja namna hii, wafanyabiashara hawavunji ndani ya maofisi ya watu, karibuni”, Max alisema huku akitabasamu.

“Haya tembeeni”, walamrisha na mlinzi mmoja aliyekuwa ameshikilia 'machine gun'. Willy na Ozu walijua hapa wasingeweza kuanza lolote ila kufuata amri ili waweze kununua muda, kwani walikuwa wamejiingiza ndani ya mtego wao wenyewe kama wajinga.

“Lukamba, nenda ukafunge lile lango na kufuli na fikiri watu tulio kuwa tunawangojea wamefika,” Max alimwamru Lukambo akiwa ameshika silaha yake sawa sawa alifungua mlango na kutoka nje. Willy na Ozu waliongozwa huku wanamfuata Max.

Robert aliona mambo yote yalivyotokea. Hivyo Lukamba alipotoka nje Robert alimvizia. Lukamba akiwa anaenda bila wasiwasi Robert alimnyemelea na

alipofika pale langoni Robert alimkaba kabari kwa nyuma na kumuua halafu akamlaza chini. Robert alifungua lile lango kakimbia mpaka pale Tete alipokuwa ameegesha gari. Alitoa kikaratasi kilichokuwa na jina na anuani akampa Tete halafu akamweleza.

“Nenda pale kwenye kibanda cha simu kiko hapo kwenye kona ya upande ule wa Cine Rac. Mpigie huyu Umba Kitete ni rafiki yangu, na ni afisa wa C.N.D. mwambie Robert anasema mambo tayari, aje hapa Sozidime na atakukuta wewe na wewe utaingia naye ndani, afanye haraka maana mambo tayari. Yeye anaelewa nilikuwa nimezungumza naye wakati tulipokuacha na Ozu, tukaondoka na Willy saa zile zajioni. Hivi utamkuta yuko tayari, fanya haraka”.

“Usiwe na wasiwasi”, Tete alijibu, Robert aliweka bastola yake sawa sawa haraka haraka akarudi ndani ya ua wa Sozidime akajifanya yeye ndiye Lukomba. Kwa vile Max na watu wake walikuwa wanajua kuna Willy na Ozu tu, hivyo walipowakamata wale wawili walijua hakuna mtu mwingine. Jambo hili lilimpa faida sana Robert kuingilia ofisi za Sozidime bila kipingamizi kikubwa.

Willy na Ozu waliongozwa mpaka ofisini kwa Fernand ambako Max alifungua ule mlango wa siri, na kuwatelemsha kuelekea chumba cha siri. Jambo hili halikuwashangaza sababu walikuwa na habari nalo kabla. Max aliwaongoza mpaka katika chumba cha siri ambako walimkuta Pierre na Fernand wamekaa wanakunywa kahawa.

“Nimewaleta hawa watu ambao wametupa taabu nyingi sana.” Max aliwaambia Fernand na Pierre.

“Ohooo, karibu Willy Gamba pamoja na Kapteni Petit Osei, nashukuru sana kuwaona. Lazima nitoe heko zangu kwenu kwani kazi yenu mmeitekeleza vizuri sana ingawaje hamtaweza kuimaliza kabisa. Kwani hapa ndipo mmefika mwisho wenu,” alijigamba Fernand halafu akatoa kicheko cha dharau kisha akaendelea; “Nchi huru za Kiafrika, nchi huru za Kiafrika... zitaweza nini?”

“Haziwezi kamwe,” alijibu Pierre.

“Unajua bwana Gamba mimi nasikitika sana kuwaueni vijana shupavu na jasiri kama nyinyi, lakini itabidi nifanye hivyo maana hiyo ni amri kutoka kwa wakubwa zangu. Lakini kabla sijawaueni nitawaeleza kwanini nchi za Kiafrika hazitaweza kamwe kuishinda Afrika Kusini”, alinyamaza kidogo kupitisha mate halafu akaendelea.

“Nchi za Kiafrika hazina umoja. Nchi za Kiafrika viongozi wake wengi ni watu wapenda pesa wala siyo viongozi wanaopenda nchi zao kwa dhati, OAU ikipiga kelele Afrika Kusini iwekewe vikwazo vya uchumi na jambo hili likipitishwa kwenye kikao cha viongozi wa nchi huru za Kiafrika, kesho yake viongozi wengine wanatupigia simu na kutuambia tusijali hayo yaliyopitishwa, hiyo ilikuwa ni siasa tu. Uhusiano wetu utaendelea hapo hapo ulipokuwa. Kwa hivyo nchi za Kiafrika zinakosa umoja na hili ndilo tatizo lake kubwa. Kwa mfano utakuta BOSS inasaidia viongozi wengi wa nchi huru za Kiafrika wasiweze kuangushwa. Wewe unafikiri mtu uliyemsaidia namna hiyo ukimuomba msaada wa kukupa siri za OAU atakataa. Kwa taarifa yenu BOSS itasonga milele, na itaendeleza shughuli zake bila shida katika Afrika. Hao wapigania uhuru tutahakikisha tutawateketeza, kiasi mlichotuchafulia sisi hatukijali ni kama mtu aliyejikwaa tu na kuumiza kidole. Lakini akishakiangalia na kukifunga anaendelea na safari yake.” Fernand aliangua tena kicheko.

“Lakini ujuwe siku zaja, wapo vijana wanamapinduzi wa Kiafrika ambao watateketeza kabisa udhalimu wa makaburu na Afrika nzima itakuwa huru. Kitu ambacho lazima ujuwe ni kwamba utafika wakati vijana wa Afrika watakuwa wamekandamizwa sana na hawatakubali lazima watafanya mapinduzi makubwa ambayo yataangusha serikali zote za vibaraka, na kuua ukoloni mamboleo na kujenga serikali za kizalendo. Mapambano bado yanaendelea, ushindi ni dhahiri”, Willy alizungumza kishujaa kabisa.

“Wapige risasi hawa, wananieleza siasa inayonuka, ambayo sitaki kui...” kabla Fernand hajamaliza kusema, mlango wa hiki chumba ulifunguliwa ghafla na Robert akajitupa ndani bastola mbili mkononi na kuwashambulia walinzi wa Fernand ambao walishtuliwa bila kutegemea, hivi hawakuwa tayari kwa tukio. Kule kufunguliwa tu mlango Willy na Ozu waliruka upande mwingine, na kumpa Robert nafasi ya kuwapiga risasi wale walinzi. Bastola za hawa walinzi zilidondoka na moja ikarukia karibu na Willy alipokuwa akaidaka na kumsaidia Robert katika mashambulizi ambayo yalichukua chini ya nusu dakika na kuweza kuwa wameua walinzi wote pamoja na Max. Pierre alikuwa amejeruhiwa sana, Fernand ndiye alikuwa mzima akiwa anatetemeka ovyo.

“Vijana wa C.N.D. watafika sasa hivi. Tete atakuja nao”, Robert alisema huku Willy na Ozu wanamwangalia kwa mshangao mkubwa. Willy alimwendea Fernand akamfunga mikono na miguu na akamweleza;

“Huu ndio mwanzo wa kuwasafisha majasusi wa nchi zinazopinga maendeleo ya Muafrika, wewe ndiwe utakuwa mfano”. Ozu alimwendea Pierre lakini alikuwa mahututi sana lakini akatambua kuwa angeweza kufa dakika yoyote.

“Muteba, Jean na Papa wamekufa sasa wewe”, alimweleza. Willy alifungua mkoba wa Fernand uliokuwa pale kwenye meza, na ndani yake akakuta makaratasi yenye habari za kijasusi zilizonaswa katika nchi nyingi za Kiafrika.

“Karatasi hizi ndizo zitakuwa kielelezo”, Willy alisema. Mara wakasikia nyayo zinateremka ndazi. Haraka haraka Tete akiwa anaongoza msafara wa watu sita aliingia.

“Oh Willy nilifikiri tutakuta mambo yamesharibika”, Tete alisema akamrukia Willy, akaning'inia shingoni mwake na kumbusu.

“Kazi na dawa” Ozu aliwatania.

“Kazi imekwisha. Bwana Umba huyu mtu wako. Mfuko huu umejaa karatasi ambazo ni vielelezo. Nyumbani kwangu kuna shahidi mwingine twende ukamchukue. Hadithi kamili nitakueleza baadaye”, Robert alimweleza Umba afisa wa juu wa C.N.D.

Huko sehemu za Nsele ambayo ni sehemu inayotumiwa na wakazi wa Kinshasa kwenda kupumzika wakati wa siku za mapumziko, na ambayo iko kando kando ya mto Congo. Jumapili hii palijaa watu. Sehemu hii ambayo iko kilomita 60 kutoka Kinshasa ni sehemu nzuri sana. Katika watu waliokuwa wamefika hapa kulikuwa na kundi la wavulana watatu na wasichana watatu ambao walivutia sana watu wengine kwa jinsi walivyokuwa.

Siku tatu baada ya kusafisha kikundi cha 'WP' Willy na wenzake walikuwa wanapumzika hapa Nsele. Willy akiwa katika nguo za kuogelea alilala kando kando ya bwawa la kuogelea lililoko sehemu hii linaloitwa 'Bassin Olympic' na huku Tete ambaye naye alikuwa katika nguo za kuogelea, alijilaza ubavuni mwake huku akimpapasa kifuni kwa mkono laini wakiota jua. Mara Ozi akiwa ameshikana mikono na Ntumba na Robert akiwa amemshikilia Ebebe kiunoni na wote wakiwa katika nguo za kuogelea walikuja mpaka pale Willy na Tete walipokuwa wamelala. Ozu akiwa amebeba gazeti mkononi.

“Willy umeshaona gazeti la 'Salongo' leo” Ozu alimuuliza.

“Bado”, Willy alijibu.

“Haya soma habari hizi hapa”, Ozu alimuonyesha. Willy alichukua gazeti, yeye na Tete wakaanza kulisoma. Lilikuwa limeandikwa kama ifuatavyo.

“Wapelelezi wa OAU juzi usiku waligundua na kuteketeza maofisi yaliyokuwa yanatumiwa na majasusi wa Shirika la Ujasusi la Afrika Kusini 'BOSS'. Ofisi hizi ambazo zilikuwa mjini hapa zilijidai ni za biashara na kumbe za majasusi zimeteketezwa kabisa na wapelelezi hao. Hili limekuwa onyo kali sana kwa Afrika Kusini kuacha mbinu zake za kishenzi inazotumia katika Afrika huru.

Wakati huo huo Mwenyekiti wa Kamati ya Ukombozi ya OAU, ambaye naye yuko mjini hapa tokea juzi amezitaka serikali zote za Kiafrika zenye mikataba na uhusiano wowote na Afrika Kusini kuvunja mara moja mikataba hiyo vinginevyo afadhali zijitoe katika umoja wa nchi huru za Kiafrika, ili harakati za Ukombozi wa Kusini mwa Afrika ziweze kupata nguvu kamili. Na huko Algiers Algeria. Umoja wa Chama cha umoja wa vijana wa Afrika (PAYM) ambacho kina makao yake makuu nchini humo, kimeitisha maandamano kwenye ofisi zake zote zilizoko katika nchi mbali mbali za Kiafrika ya kuzitaka nchi za Kiafrika zenye uhusiano wa kiuchumi na Afrika Kusini kuvunja uhusiano na nchi hiyo baada ya kugundulika mbinu zake”, gazeti hilo lilieleza. Willy aliweka gazeti kando.

“Tutaenda wote Dar es Salaam?” Tete alimuulza Willy alipomuona amemaliza kusoma gazeti. Willy aliwaangalia wenzake waliokuwa wamesimama kando wakingojea atoe maelezo yake juu ya habari zilizoandikwa kwenye gazeti hilo lakini akainuka na kumlalia Tete kifuani akamjibu.

“Tutaangalia”, huku akimbusu.

MWISHO